

20 APRILI, 2012

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Tisa – Tarehe 20 Aprili, 2012

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

MHE. MARTHA M. MLATA (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII): Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA MAENDELEO YA JAMII: Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MHE. IGNAS A. MALOCHA (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA SHERIA NDOGO): Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI: Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MHE. JADDY SIMAI JADDY (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA): Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MHE. SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE VIWANDA NA BIASHARA): Taarifa ya Kamati ya Bunge

20 APRILI, 2012

ya Viwanda na Biashara ya Bunge Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA: Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Atakayeuliza swali la kwanza ni Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla.

Na. 106

Mgogoro wa Ardhi Kinyenze

MHE. AMOS G. MAKALLA aliuliza:-

- (a) Je, Serikali inashughulikiaje mgogoro wa ardhi kati ya mwekezaji na Kitongoji cha Kinyenze kilichopo Kipera unaohusu uhalali wa umiliki, mipaka na unyanyasaji mbalimbali?
- (b) Kwa nini kuna tofauti ya ramani ya sasa na ya awali ya mwaka 1950 kuhusiana na mipaka?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla, Mbunge wa Mvomero, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inatambua kuwepo kwa mgogoro wa ardhi baina ya mwekezaji na wakazi wa Kitongoji cha Kinyenze kilichopo Kipera katika Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero. Mgogoro huo wa ardhi unahusu shamba Na.296 lenye ukubwa wa hekta 97.7 lililopo katika Kijiji cha Kipera.

Shamba hili linamilikiwa na Badrudin Dharams Walji wa Morogoro tangu mwaka 1959 bila Hati. Upimaji wa shamba hilo ulifanyika mwaka

20 APRILI, 2012

1997 na kupewa Hati ya kumiliki Na.48836 ya miaka 99 tangu tarehe 1 Oktoba, 1997.

Mheshimiwa Spika, baada ya mmiliki wa kwanza wa shamba hili kufariki mwaka, 2008 warithi wa mmiliki huyu walihamisha miliki ya shamba hilo kutoka kwa Badrudin Dharams Walji kwenda kwa *Tanbreed Poultry Limited* wa Morogoro.

Mgogoro huu ulijitokeza baada ya eneo hilo kupimwa na mwekezaji kufunga njia zote zilizokuwa zinakatiza ndani ya shamba hili ikiwemo kuwaondoa baadhi ya wananchi waliokuwa wakilima ndani ya shamba hilo. Lalamiko lingine limekuwa ni baadhi ya wananchi kulalamikia mipaka ya shamba la mwekezaji huyo ambalo lilimeza maeneo yao waliyokuwa wakiyalima kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri imeshughulikia mgogoro huu kwa kuwakutanisha mwekezaji na wananchi ambapo maazimio yaliyofikiwa ni kufanyika kwa uhakiki wa mipaka ya shamba hilo ili kundoa utata uliyopo na mwekezaji kuridhia pendekezo la kufunguliwa kwa njia inayokatiza katika shamba hilo.

(b) Mheshimiwa Spika, shamba hili halikuwahi kupimwa kutoka mwaka 1959 hadi mwaka 1997 lilipopimwa na kupatiwa ramani Na. E/357/2 iliyoidhinishwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani wa Wizara ya Ardhi. Kwa maelezo hayo eneo hilo halijawahi kuwa na ramani mbili tofauti.

MHE. AMOS G. MAKALLA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ambayo hayajatoa matumaini sana juu ya tatizo hili, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Serikali inakiri hapa kwamba vipo vitendo vya unyanyasaji ikiwemo kufunga njia na kuwanyanyasa wananchi walioko katika eneo hilo vinavyofanywa na huyu *Tanbreed Poultry Limited* na kusababisha sasa kuweza kuwepo na umwagikaji wa damu; Serikali inatamka nini sasa kuharakisha suala hili kuona kwamba tatizo hili linamalizwa kuwepo kwa usalama na wananchi wapate haki yao na mwekezaji apate haki yake?

Pili; kwa kuwa Serikali inakiri kwamba shamba hili halijawahi kupimwa toka mwaka 1959, limekuja kupimwa mwaka 1997; na wananchi wa eneo hilo, nimeenda mara mbili, wanalalamika kwamba eneo lao limemegwa na hata uhalali wa kumiliki huyu Badru unakuwa wa mashaka kwani halikuwahi kupimwa.

20 APRILI, 2012

Je, kwa nini mimi na wananchi wangu tusiamini kwamba ramani iliyoko sasa imechakachuliwa, siyo kama ile ya awali ambayo wananchi walikuwa na haki na eneo hili?

SPIKA: Asante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Naomba maswali yenu ya nyongeza yawe mafupi na majibu ya nyongeza yawe mafupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa mimi nataka niliweke vizuri hapa, nataka nimthibitishie Mheshimiwa Amos Makalla kwamba sisi kama ofisi tuko tayari pia kushirikiana na yeye. Tumelifuatilia jambo hili kwa karibu sana na nimeeleza hapa mambo yaliyojitokeza hapa.

Mheshimiwa Spika, mimi ninachoweza kushauri kwa hatua hii tuliyofikia sasa hivi, iko haja ya Mheshimiwa Mbunge pamoja na Halmashauri, kwa sababu wameanza mazungumzo haya, na wanazungumza vizuri na ninavyoona mazungumzo na maelezo niliyopata yanavyotiririka, mimi naona muafaka unaweza ukapatikana katika hali ya amani kabisa bila kuingiza mgogoro wa aina yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wananchi hawa walizoea kulima pale, lakini sasa baada ya umilikaji huu ambao nimezungumzia, mmilikaji akaenda akafunga njia na akafunga eneo lote lile.

Kwa hiyo, wale watoto wa shule waliokuwa wanapita katika eneo lile, hawawezi kupita tena. Nadhani ndhicho hiki Mheshimiwa Amos Makalla anachokitafsiri kama ni kunyanyaswa. Pia watu waliokuwa wanalima katika eneo lile nao wamezuiwa katika sehemu fulani ya hilo eneo wamezua.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nataka niseme tu kwamba tuko tayari sisi kusaidiana na Mheshimiwa Amos Makalla pamoja na Halmashauri kuhakikisha kwamba tatizo hili linaondoka.

Sasa hili la kupimwa eneo kwamba limepimwa vibaya, halikukaa... ndicho ninachojibu hapa na Mkurugenzi nimemwagiza pamoja na wenzake na Wapima wote waende wakahakiki. Swali lilikuwa linaulizwa kwamba kuna ramani mbili, nimethibitishiwa kwamba pale hakuna ramani mbili.

20 APRILI, 2012

Lakini hiki anachosema Mheshimiwa Mbunge, tunakubaliana naye na tumeagiza Halmashauri pamoja Wapima waende wakapime pale ili kuhakikisha kwamba kilichopo katika ramani ndicho kilichoko katika ardhi. Hayo ndiyo ambayo naweza nikashauri kwa sasa hivi. *(Makofi)*

MHE. SUSAN L. A. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Suala la migogoro ya ardhi limejikita sana ndani ya Mkoa wa Morogoro, hata hivi nina *document* nimeletewa kutoka Kijiji cha Mkangawaro kule Mgeta ambapo Wenyeviti wa Vijiji wameshiriki sana kuuza ardhi ya wananchi bila ridhaa ya wanavijiji wenyewe; na limejikita Wilaya zote Mkoa wa Morogoro.

Je, Waziri sasa yuko tayari nikimletea orodha ya maeneo yote yenye migogoro ndani ya Mkoa wa Morogoro Wilaya mbalimbali na kuishughulikia haraka bila kupoteza muda ili wananchi wapate maendeleo yao? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi. Naomba maswali yawe mafupi kusudi tuweze kuwa na watu wengi wanaochangia.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kama yeye anavyo vielelezo na kama anavyoeleza, Morogoro nimefika kule. Tunamwomba atuletee halafu tutashughulikia.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Hivi karibuni kulikuwa na mgogoro wa ardhi katika mapori ya Kagera Nkanda kule pamoja na Vijiji vya Mvinza ambapo mgogoro huu tuliweza kuishughulikia na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

Moja ya mambo ambayo tulikubaliana ilikuwa ni pamoja na kuweza kuwashughulikia watumishi wa Idara ya Maliasili na Mazingira ambao waliwaacha wananchi wa Wilaya ya Kasulu kuendelea kwenda kulima katika mapori hayo. Lakini mpaka leo hii watu hao hawajaweza kuchukuliwa hatua. Naomba kuuliza.

Je, Serikali iko tayari kuweza kuwawajibisha wale maafisa wa Maliasili ambao waliwaacha wakulima kwenda kulima kwenye maeneo ya Hifadhi kwa mujibu wa Serikali na hivyo kuweza kuondolewa katika maeneo yale bila kufuata utaratibu?

20 APRILI, 2012

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ni kweli tulikubaliana kwamba uchunguzi ufanyike na hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa wale ambao wataonekana wamefanya makosa.

Watumishi walioko kwenye Halmashauri wako kwenye mamlaka ya nidhamu ya Halmashauri kama ambavyo jana ilielezwa kwamba ukiachia Mkurugenzi, watumishi wengine wote wanasimamia tu sekta lakini mamlaka yao ya nidhamu ni pale pale kwenye Halmashauri. Walioko kwenye sekretarieti ya Mkoa, mamlaka yao ya nidhamu iko kule kule Mkoani.

Tumekwishakutoa maelekezo ya kitalaam sisi kama Wizara kueleza ni namna gani wanapaswa kufanya kazi zao na tayari tumekwishakuwasiliana na Mkoa kwamba taratibu za nidhamu kwa pale ambapo watakuwa wamekosea, zifuatwe na zichukuliwe haraka.

Na. 107

Wajibu wa Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA aliuliza:-

Msingi mkubwa wa maendeleo ya jamii huanzia kwenye ngazi ya Mitaa na Vijiji ambapo hutegemea ubunifu na utendaji wa viongozi wa ngazi husika.

Je, Serikali inawezaje kuwahakikishia wananchi kwamba Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji wanajua wajibu wao?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kwamba msingi wa maendeleo ya jamii unaanzia katika ngazi ya chini ya Serikali za Mitaa. Wasimamizi wa maendeleo katika ngazi hiyo ni Wenyeviti wa Vitongoji, Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Mitaa.

Aidha, ni kweli kwamba ili viongozi hao waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi ni lazima wapatiwe mafunzo ya kuwajengea uwezo. Kwa kuzingatia hilo, mara baada ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2009, kila Halmashauri ilitoa mafunzo kwa viongozi hao ili kuwawezesha kufahamu majukumu yao.

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara (Mikindani) katika mwaka 2009 kwa kutumia vyanzo ya ndani vya mapato ilitoa mafunzo kwa Wenyeviti wote wa Vijiji na Mitaa.

Aidha, Halmashauri kupitia Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GTZ) viongozi hao walipatiwa mafunzo ya siku tatu yenye lengo la kuwajengea uwezo katika majukumu yao.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza kabisa, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Nne inafanya mabadiliko makubwa mawili:- La kwanza ni hili la Mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini la pili ni hili la Utoaji wa Vitambulisho vya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, katika mazoezi haya, Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa ni wadau wakubwa ambao wanaweza wakahakikisha kwamba mazoezi haya yanaenda vizuri.

Je, Serikali imeandaa utaratibu gani kwa Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji ili kuhakikisha kwamba wanaotunga Katiba ni raia wa Tanzania na pia utaratibu wa kutoa vile Vitambulisho vya Kitaifa unafuatwa kwa makundi yanayotakiwa, wale raia ambao siyo Watanzania na raia ambao ni Watanzania?

Mheshimiwa Spika, la pili; jana Mheshimiwa Waziri Mkuu alituhidi hapa kwamba katika bajeti ya mwaka huu, posho kwa Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji itazingatiwa sana sana.

Je, Serikali itakubali sasa kuhakikisha kwamba suala hili linatekelezwa katika kipindi cha bajeti ya mwaka huu na haitakuwa kigeugeu? Asante.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, hili la sensa na hili la vitambulisho, wala hatuna matatizo. Miradi yote inayokwenda katika Halmashauri, na hili ni vizuri Waheshimiwa Wabunge wakajua, miradi yote tunayoipeleka kule, ya maji, ya afya, kwanza kabisa lazima tufanye suala la kuwajengea uwezo Wenyeviti wetu.

20 APRILI, 2012

Kwa hiyo, mimi nina hakika kabisa kwamba kupitia Sekretarieti za Mikoa na kupitia katika Halmashauri zetu, hao Wenyevidi wetu wa Vijiji watakuwa wamejua utaratibu mzima unaotumika.

Hili la vitambulisho na hili la sensa, hayana tatizo, watakuwa wanaelimishwa *as we go along*. Na miradi yote inayokwenda kule ya maji, ya MEMEM, ya MMES, yote, kabla ya kufanya hii miradi na kuitekeleza, tunahakikisha kwamba wamepata mafunzo walau ya kujua ni nini kinachotakiwa kufanyika kule.

Je, Serikali imeandaa utaratibu gani kwa Wenyevidi wa Mitaa na Vijiji ili kuhakikisha kwamba wanaotunga Katiba ni raia wa Tanzania na pia utaratibu wa kutoa vile Vitambulisho vya Kitaifa unafuatwa kwa makundi yanayotakiwa, wale raia ambao siyo Watanzania na raia ambao ni Watanzania?

Mheshimiwa Spika, la pili; jana Mheshimiwa Waziri Mkuu alituhidi hapa kwamba katika bajeti ya mwaka huu, posho kwa Wenyevidi wa Mitaa na Vijiji itazingatiwa sana sana.

Je, Serikali itakubali sasa kuhakikisha kwamba suala hili linatekelezwa katika kipindi cha Bajeti ya mwaka huu na haitakuwa kigeugeu? Asante sana.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, hili la sensa na hili la vitambulisho, wala hatuna matatizo. Miradi yote inayokwenda katika Halmashauri, na hili ni vizuri Waheshimiwa Wabunge wakajua, miradi yote tunayoipeleka kule, ya maji, ya afya, kwanza kabisa lazima tufanye suala la kuwajengea uwezo Wenyevidi wetu.

Kwa hiyo, mimi nina hakika kabisa kwamba kupitia Sekretarieti za Mikoa na kupitia katika Halmashauri zetu, hao Wenyevidi wetu wa Vijiji watakuwa wamejua utaratibu mzima unaotumika.

Hili la vitambulisho na hili la sensa, hayana tatizo, watakuwa wanaelimishwa *as we go along*. Miradi yote inayokwenda kule ya maji, ya MEMEM, ya MMES, yote, kabla ya kufanya hii miradi na kuitekeleza, tunahakikisha kwamba wamepata mafunzo walau ya kujua ni nini kinachotakiwa kufanyika kule.

Mheshimiwa Spika, hili swali la pili analoniuliza dada yangu Anastazia Wambura kuhusu posho ya Wenyevidi wa Mitaa itatekelezwa, Waziri Mkuu jana alisimama hapa tena alitumia msamiati wa 'piga geuza'

20 APRILI, 2012

lakini ni lazima tuhakikishe kwamba kwa hali itakavyokwenda tutahakikisha kwamba posho hizi nazo tunaziangalia, sasa siwezi kujibu zaidi ya hapo kile alichosema Mkuu hapa ndicho hicho alichosema.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika nashukuru sana, nilitaka kufahamu je, Serikali licha ya kuwa na Wenyeviti wa Vitongoji na vijiji hawapati malipo au posho zozote. Wanafahamu kwamba vifaa na vitendea kazi havipatikani kwa watendaji hawa ambao tunawategemea watusaidie kazi?

SPIKA: Vifaa kama nini?

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, vifaa kama *stationeries* na vinginevyo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kuna hela ambazo zinaitwa hela za kujenga uwezo zinapofika pale kwenye Halmashauri sehemu ya hizo hela zinachukuliwa moja kwa moja zinapelekwa pale kwenye kijiji Ndizo zinazotumika kwa ajili ya kuwasaidia hawa wenyeviti wa vijiji kupata posho hizo, na kwa ajili pia ya kitu kinaitwa *retooling* yaani kwa ajili ya kuhakikisha kwamba vifaa hivi vinapatikana pale.

Kwa hiyo, ni suala la kufuatilia sasa katika Halmashauri zao kuona kwamba hizo hela zinapokuwa *allocated* hazienidi kwenye maeneo mengine zinafanya kazi hii ya *retooling*, *retooling* ni pamoja na mashine, kompyuta, kalamu, *stationary* na kila kitu kinafanyika pale.

Na. 108

Ufumbuzi wa Tatizo la Watoto wa Mitaani na Ombamba

MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMED aliuliza:-

Ongezeko la Watoto wa mitaani ni kubwa na wengi wao wanakosa haki yao ya kielimu na kiafya na kwamba suala hili bado halijapatiwa ufumbuzi:-

Je, Serikali ipo tayari kukubali kuwa imeshindwa kutatua suala la watoto wa mitaani na ombamba?

20 APRILI, 2012

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Thuwayba Idris Muhamed, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna ongezeko la watoto wanaoishi mitaani na ombaomba ambao wanakosa haki zao za kielimu na kiafya, watoto wanaoishi mitaani ni moja kati ya makundi walio katika mazingira hatarisha, takwimu za utambuzi wa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi ulifanyika Halmashauri 95 hapa nchini zinaonesha kwamba asilimia 4 ambayo ni sawa na watoto 33,962 ni kati ya watoto wote 849,054 waliotambuliwa kuwa wako katika mazingira hatarishi ni watoto wanaoishi mitaani.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi zinaonesha ukubwa wa tatizo hili ambalo Wizara imeshaliona. Katika kukubaliana na hali hiyo Serikali imeunda kikosi kazi kinachohusisha wadau mbalimbali wa masuala ya watoto, kikosi kazi kiliundwa Mwezi Aprili, 2011 na kinatakiwa kutoa ripoti yake kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha kumalizika.

Mheshimiwa Spika, Serikali itahakikisha itayafanyia kazi mapendekezo na ushauri utakaotolewa na kikosi kazi hicho, Aidha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wamefanya jitihada zifuatazo katika kutatua tatizo hili:-

(i)Kupitia mpango wa utambuzi wa watoto walio katika mazingira hatarishi, jamii imewezeshwa kutambua watoto wanaoishi mitaani na kuweka mikakati ya kuwahudumia.

(ii)Kufanya uchambuzi yakinifu wa makao au vituo vya kuhudumia watoto hao katika makao yanayolea watoto walio katika mazingira hatarishi wakiwemo wanaoishi mitaani kwa lengo la kuboresha huduma kwa watoto hao.

(iii)Ugatuaji wa huduma za ustawi wa jamii katika mamlaka za tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuboresha huduma kwa makundi maalum wakiwemo watoto wanaoishi mitaani.

(iv)Kushirikiana na *UNICEF* Wizara ya AFya na Ustawi wa Jamii imeandaa mradi ambao umewashirikisha Halmashauri zote za Manispaa za Dar es Salaam pamoja na ofisi kuu ya Mkuu wa Mkoa ambapo mradi huu unatafuta mbinu za kutatua tatizo la watoto wa mitaani na ombaomba, matokeo ya mradi huu wa Dar es Salaam yataiwezesha Wizara kutatua matatizo ya aina hii katika Miji mingine.

20 APRILI, 2012

MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMED: Mheshimiwa Spika ahsante, pia namshukuru Waziri kwa kujibu vizuri zaidi, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa kuna wawekezaji wengi hapa nchini ambao wanachangia mfuko wa *CSI* na kwa kuwa kuna makampuni kama ya bia na simu ambayo yanachangia fedha nyingi sana katika michezo.

Je kwanini Serikali hamuwasajihishi kampuni hizi zikaweza kujenga majengo na shule ambazo zitaweza kuwasaidia watoto hawa kwa kuwaweka na kuwasomosha kama vile alivyofanya Marehemu Abeid Karume kule Zanzibar?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kwamba wazo lako ni la msingi sana na ni hoja ambayo kwa kweli iko wazi, na italeti tija sana endapo tutawashirikisha wadau hawa katika sekta binafsi.

Mojawapo ya jukumu ambalo wanalifanya ni kuboresha ustawi wa jamii ya Watanzania. Nami basi naomba nichukue nafasi hii tena kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba tutalifanyia kazi. Tutawasiliana na taasisi hizi kama ulivyozitamka na zingine nje ya hapa ili tuone namna gani nao wanaweza wakashiriki katika kusaidia kutatua tatizo hili la ustawi wa watoto hawa.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Spika watoto wengi wa mitaani ni zao la wazazi kuachana au wazazi kufariki, mara nyingi jukumu hili huachiwa Bibi au Babu ambao hali zao za kiuchumi zimekuwa duni.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuharakisha zoezi la kuwapa pensheni wazee wote walio na umri kuanzia miaka 60 na kuendelea ambao ndiyo wenye jukumu kubwa la kulea watoto hawa wa mitaani?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, Serikali tunaona umuhimu wa kutoa pensheni kwa wazee na kupitia Wizara ya ajira na kazi, Serikali kuna kipindi tulitoa dhamira kwamba tunaweka utaratibu ambao tutaona ni namna gani tutaweza kutoa pensheni kwa kundi hili ambalo kwa kweli linahitaji kupewa nguvu za ziada na kuwa *supported* ili waweze nao pia kwa sababu tunaamini na wengi tunashuhudia wengi wa wazee hawa ndiyo walezi wa watoto.

Sasa kama hawatahudumiwa ipasavyo siyo tu wataathirika hawa Wazee lakini kadhalika na watoto ambao tunawalenga wataathirika.

20 APRILI, 2012

Na. 109

Kuongeza Idadi ya Dawa kwa Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe

MHE. SELEMANI S. JAFO aliuliza:-

Kutokana na wingi wa wagonjwa wanaotibiwa kwenye hospitali ya Wilaya ya Kisarawe, wakitokea Wilaya ya Ilala, hasa maeneo ya Gongolamboto, Pugu, Chanika na Majohe wakitokea Wilaya ya Ilala, husababisha upungufu wa dawa mara kwa mara kutokana na idadi hiyo kubwa ya wagonjwa:-

Je, Serikali ina mapango gani wa kuongeza kiwango cha dawa kwa hospitali hiyo kukidhi idadi ya watu wanaokwenda kupatiwa matibabu hospitalini hapo.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Seleman Said Jafo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na upungufu wa dawa, vifaa vifaa tiba na vitendanishi, Wizara ya Afya na Ustawi wa jamii imechukua hatua ya kusambaza dawa na mahitaji mengine hadi katika zahanati na vituo vya Afya vya Umma.

Aidha, Wizara kupitia Bohari Kuu (MSD) inagawa dawa na vifaa tiba kwa kuzingatia vigezo mbalimbali, vikiwa ni pamoja na idadi ya wananchi wanaopata huduma katika vituo vya Umma, vifo vya watoto chini ya miaka mitano na kiwango cha umaskini wa wananchi katika Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, hospitali za Umma nchini, ikiwemo hospitali ya Wilaya ya Kisarawe, zinapata mgao wa fedha za dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kulingana na vigezo nilivyotaja hapo juu.

Ili kurekebisha hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika hospitali ya Wilaya ya Kisarawe, Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, ameagizwa kuwasilisha idadi ya wananchi wanaotibiwa kuiwezesha Wizara kuchukua hatua zinazostahili.

Kwa kuwa fedha zinazotolewa na Serikali na wadau wa maendeleo kwa ajili ya dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi hazikidhi mahitaji, hospitali za umma nchini zinahushauriwa kutumia fedha za

20 APRILI, 2012

uchangiaji wa huduma za afya kwa ajili ya kununua dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi pale panapokuwa na upungufu wa vifaa au dawa zinazohitajika.

MHE. SELEMAN S. JAFO: Mheshimiwa Spika ahsante, pamoja na majibu ya Waziri, kabla sijauliza maswala mawili ya nyongeza ningependa kulishukuru shirika *ICAP International* ambalo limetujengea bohari kubwa ya madawa pale Kisarawe.

Hali kadhalika ningependa kuwashukuru shirika la *Plan International* ambao wametuletea *mobile clinic* kwa ajili ya kuwahudumia wananchi katika Wilaya yetu ya Kisarawe, sasa napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana niliuliza swali hapa kuhusiana na tatizo la miundombinu katika hospitali ya Wilaya ya Kisarawe ambayo inatibu Wagonjwa wengi sana wa Wilaya ya Kisarawe na wale wa Jiji la Dar es Salaam.

Ninamshukuru Naibu Waziri wa TAMISEMI aliahidi kwamba katika bajeti ya mwaka huu wa fedha Wilaya ya Kisarawe itapewa kipaumbele katika eneo hilo, Naomba *commitment* ya Serikali hapa wanakisarawe leo hii wanaisikia Serikali yao kwamba kwa ahadi ya mwaka jana itakubali maombi yetu, ombi maalum kwa kuhakikisha kwamba Wilaya ya Kisarawe mwaka huu Bajeti yake ya ombi maalum la ukarabati wa Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe ikiwemo *mortuary* na chumba cha madaktari na maeneo mengine kama miundombinu ya maji litakubaliwa katika bajeti ya mwaka huu wa fedha 2012/2013. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Spika, wahudumu wangu pale Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe na Zahanati zake wanafanyakazi katika mazingira magumu sana hata vitendeakazi hawana, japokuwa Waziri ameahidi hapa kwamba kutokana na utaratibu wa Serikali umepanga utaratibu gani kutumia mifuko.

Je, Serikali inaonaje kuhakikisha kwamba Wilaya ya Kisarawe inapewa kipaumbele cha kuhakikisha kwamba kwa sababu ina mzigo mkubwa wa kuwahudumia wananchi wengi sana, ipewe fungu maalum ili mradi kununua vitendea kazi na wahudumu wafanyakazi katika maingira mazuri?

20 APRILI, 2012

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Jafo kwa bidii na jitihada kubwa ambazo anazifanya kwa wananchi wake wa Jimbo la Kisarawe, mara kadhaa amekuja kwangu binafsi kuja kufuatilia ni namna gani huduma za jamii zinaweza zikaboreshwa ikiwemo huduma ya afya. Nampongeza sana Mheshimiwa Jafo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kukarabati miundombinu pamoja na chumba cha kuhifadhi maiti mimi namshauri kwamba awasiliane na kwa sababu yeye mwenyewe ni member wa baraza la madiwani katika mpango wa Bajeti wa mwaka huu muioanisha hiyo na mkishaoanisha hiyo katika mipango yenu basi TAMISEMI nao watachukua hiyo wataweka na ninahakika Bunge letu Tukufu litapitisha Bajeti hiyo wananchi wa Kisarawe watafanyiwa marekebisho yao ya miundombinu katika hospitali yao kama wanavyohitaji.

Mheshimiwa Spika, naomba nafasi hii kutoa taarifa kwamba Serikali imefanikisha kuboresha chumba kile ambacho kilikuwa kinatoa huduma za xray na sasa hivi tayari tumeweka mashine ya x-ray na leo hii wataaamu wetu watakwenda kuweka betri na wiki ijayo wakishahakiki kama inafanyakazi wananchi wa kisarawe kuanzia wiki mbili zijazo huduma za x-ray zitarudia kama ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Spika, suala la mazingira magumu na vitendeakazi, Mheshimiwa Jafo hili ni suala ambalo nimekuwa nikilizungumzia kwa muda ni suala linalotokana na Bajeti finyu lakini bado tutumie vema vyanzo vingine ambavyo vipo kama ulivyobuni wewe, umewasiliana na *Plan International* na taasisi nyingine.

Lakini vile vile nilikuwa naomba nitoe ushauri, katika hivi vifaa tiba bado Halmashauri wana nafasi ya kuwasiliana na mfuko wa bima ya afya wa Taifa, mfuko ule nao tumewaelekeza wawa-support hospitali zote, vituo vya afya ikiwezekana mpaka zahanati waweze kutoa mkopo ulio na masharti nafuu ili angalau kujazia au kuziba ile *gap ya financing* ambayo tunayo ndani ya Serikali. *(Makofi)*

MHE. LOLENSIA M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa katika maeneo ya uchimbaji wa madini yana mvuto kwa watu wengi sana ambao wanatokea sehemu mbalimbali za nchi hii.

20 APRILI, 2012

Kwa mfano pale Nyarugusu unakuta watu wanatokea Singida, wengine Kisarawe na sehemu mbalimbali na hii inasababisha upungufu wa madawa katika zahanati na vituo vya afya, pia katika hospitali yetu ya Wilaya ya Geita.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua ni nini hasa mpango wa Serikali kuweza kuongeza madawa ili wananchi waweze kunufaika kwa huduma za afya katika maeneo ya Geita? *(Makofi)*

SPIKA: Katika maeneo ya machimbo, haya Mheshimiwa Waziri naomba ujibu kwa kifupi tafadhali, muda unakula kwetu. *(Makofi)*

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuongeza mahitaji ya vifaa na dawa katika Halmashauri mbalimbali ikiwemo ya Halmashauri ya Geita, vigezo nilivyovitaja ni kama vya mwanzo kwamba tunatoa mgao ule kutegemea na vigezo vya idadi ya wananchi wanapata huduma katika hospitali ile husika, kigezo kingine tunachokifanya ni kuangalia idadi ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano na hali ya umaskini.

Lakini hiyo tu haitoshi bado tunaangalia vile na hata utumiaji wa hizo huduma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Bukwimba ufuate vigezo hivyo, uwasilishe katika sehemu husika tutavifanyia kazi.

SPIKA: Umechukua dakika nane hapo kwa hiyo naenda swali linalofuata la Wizara ya Maliasili na Utalii.

Na. 110

Kutangaza Mlima Kilimanjaro na Njia zake.

MHE. JOSEPH R. SELASINI aliuliza:-

Mlima Kilimanjaro kijiografia upo katika Wilaya ya Rombo ambako njia ya kufikia kilele cha mlima huo kwa upande wa Rombo ni fupi na rahisi kuliko njia nyingine.

Je, kwa nini Serikali haitangazi njia hiyo inapotangaza mlima huo?

20 APRILI, 2012

WAZIRI WA MALIASILI NAUTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge, wa Rombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utalii wa kupanda mlima Kilimanjaro ni moja ya zao linalovutia watalii wengi kutembelea nchini. Kijiografia, mlima huu una maajabu mengi na uamuzi wa njia gani itumike kuupanda hadi kufika kileleni hutegemea vitu vingi, mazingatio muhimu huwa ni utashi wa mtalii mwenyewe kutumia njia ngumu au njia rahisi kutegemea muda wake, hali ya kiafya na pia vitu anavyotaka kuviona.

Vilevile, uamuzi huo wakati mwingine hutegemea makubaliano yanayofikiwa baina ya mtalii na wakala anayemtumia kuandaa safari ya mgeni huyo.

Mheshimiwa Spika, uzoefu umeonesha kuwa, mtalii anapopanda mlima kwa siku nyingi ndivyo anavyojiweka katika nafasi nzuri zaidi ya kufika kileleni. Hii ni kwa sababu anapata muda wa kutosha kwa mwili wake kuzoea mazingira ya mlimani.

Aidha, kadri mtalii anavyotumia muda mwingi kupanda mlima ndivyo mapato yanaongezeka. Kwa mantiki hiyo, ufupi au urahisi wa njia ya upande wa Rombo kufikia kileleni siyo kigezo pekee cha kuifanya itangazwe kuwa njia ya kutumia zaidi.

Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumika kutangaza vivutio vya kitalii unalenga kuhamasisha wananchi na wageni wote kwa ujumla kutembelea vivutio vilivyoko nchini.

Kwa upande wa Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro njia za kupanda na kushuka kwenye kilele zimeainishwa kitalaam katika mpango wa jumla. Njia zote zilizoainishwa katika mpango huo wa hifadhi, hutangazwa bila ya upendeleo kwa wadau wote na wao hubaki na uamuzi wa mwisho wa njia ipi itumike.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ningependa kuuliza maswali mawili ya yongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa faida ya moja kwa moja ya wananchi wanayoipata kutoka mlimani inatokana na huduma wanazotoa kwa watalii. Na kwa kuwa eneo kubwa kama nilivyosema liko upande wa Rombo ambako njia za kwenda mlimani hazipo.

(a)Je, wananchi hao wanafaidika namna gani moja kwa moja na mapato yanayotokana na utalii wa mlima ambao uko upande wao? (Makofi)

(b)Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mlima Kilimanjaro hivi sasa kwa kiasi mkubwa msitu unaozunguka unavamiwa na majangili wakikata miti ya asili iliyo ndani ya Hifadhi pamoja na uvunaji wa asali na kwa kuwa wananchi wanaozunguka mlima Kilimanjaro ni walinzi wa uhakika sana wa hifadhi hii. Je, Serikali haioni kwamba sasa imefika wakati Halmashauri zizozunguka Mlima Kilimanjaro zikapewa mrahaba kwa niaba ya wananchi ili kutoa motisha ya kutosha waweze kulinda hifadhi hii kwa sababu bila kufanya hivyo sasa hasara ambayo tunaiona ya moja kwa moja theluji iliyoko katika mlima inapungua na miti ikiendelea kukatwa hata maji yatapotea? (Makofi)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwanza kabla ya kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Selasini naomba nimpongeze sana kwa ushirikiano na msaada mkubwa ambao amekuwa akitupa wa kimawazo. Nilipotembelea Rombo tulizungumza naye mengi sana kuhusu kuendeleza utalii hasa upande wa Rombo. Mengi ya mambo aliyoyauliza yako katika majadiliano tuliyoyafanya.

Moja ni kwamba tulikubaliana kwamba kwa sababu wenzetu wa upande wa Kenya wanajenga uwanja wa ndege jirani njia pekee itakayoweza kutusaidia sisi kunufaika ni kuweka hoteli upande ule ili wageni kabla ya kupanda au baada ya kushuka waweze kulala kwenye hoteli zetu kwa sababu *practically* inakuwa siyo rahisi mtu atoke kwenye uwanja ndege kule aje upande moja kwa moja siku hiyo. Jambo hili tumekwishaanza kulifanyia kazi na njia hii itarahisisha sana wananchi wa Rombo kuweza kupata mapato.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ambalo tumekuwa tukilifanya ni kutoa miradi ya ujirani mwema kwenye Wilaya zote zinazozunguka mlima kupitia mpango wa ujirani mwema wa TANAPA. Lakini kwa sasa hivi kuna majadiliano ambayo yanaendelea baina ya wadau wa mlima huu na Wizara ya Maliasili na Utalii kuziruhusu Halmashauri zinazozunguka mlima kutoza ushuru maalum kwa ajili ya uhifadhi kwa sababu bila kushirikisha wananchi jambo hili linaweza lisifanikiwe. Majadiliano yamekuwepo muda mrefu sana na Mheshimiwa Aggrey Mwanri amekuwa akiongoza majadiliano hayo. Nimhakikishie tu kwamba Mheshimiwa Selasini kwamba sisi tuko pamoja na wananchi wa Kilimanjaro. Watakapokamilisha sisi hatuna matatizo tutaweza kushirikiano nao kuruhusu waanze kutoza. (Makofi)

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mlima wa Kilimanjaro uliingia katika kushindanishwa kuingia katika vivutio 7 vya dunia. Matokeo yake *Table Mountains* ya Afrika Kusini ndio ilishinda. Lakini tukiangalia sababu za wazi ni sababu zipi ambazo zilisababisha Mlima wa Afrika Kusini kushindwa, wenzetu walikuwa wamejipanga na waliutangaza mlima wao takribani miaka minne iliyopita. Sasa nina swali kwa Wizara. Je, Serikali inatoa maelekezo gani katika Bunge hili na Watanzania kuhusiana na mlima wetu kutokuingia, ingawa kwamba wamejipanga vizuri wangeweza kushinda. Je, Wizara iliwatendea haki Watanzania, na Waziri kabisa una *right* ya kuendelea kuitwa Waziri wa Maliasili na Utalii? (*Makofi*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa dada yangu Ester Bulaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala hili liliwahi kujitokeza hapa Bungeni na tukatoa maelezo. Niseme tu kwa kifupi sana kwamba ni kweli sisi tuna changamoto kubwa sana na hasa ya kushirikisha sekta binafsi katika utangazaji wa utalii. Suala hili lilipojitokeza tulipata kwanza upinzani hata ndani ya vyombo vya habari vya nchi. Tulipoomba kwa mfano tuanze kutangaza au kuomba kupiga kura kwa kutumia kampuni zetu za simu tuliambiwa tulipie. Bodi ya Utalii haikuwa na fedha za kulipia, majadiliano yalifanyika na hadi yakakubalika dakika za mwisho sana. Kwa kifupi ni kwamba kulikuwa na changamoto ya kimaandalizi. Kwa hiyo, niseme kwamba pamoja na changamoto hizi tunazozipata tumekwisha kujifunza, tumekwisha kujipanga tunaamini kwamba fursa zingine zitakapokuja kujitokeza tutaweza kuzifanya vizuri zaidi.

MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupewa nafasi. Kwa kuwa Wizara hii imekuwa ikitangaza vivutio vya utalii nchi za nje kupitia *CNN* na kutumia fedha nyingi na kwa kuwa sayansi ya teknolojia ya habari imekua hivyo kuwezesha vyombo vya ndani vikiwezesha kutangaza vizuri biashara hii. Je, Serikali sasa itakuwa tayari kuanzisha Kituo cha Utangazaji kupitia shirika la *TBC* kitakachokuwa kinatangaza vivutio hivi kwa lugha za kigeni kama vile Kingereza, Kijerumani, Kirusi, Kiarabu na nyinginezo ili kupanua uwigo wa watalii?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Binilith Satano Mahenge, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la kutangaza utalii ni jambo muhimu. Zimekuwepo mbinu mbalimbali ambazo tumekuwa tukizifanya lakini

20 APRILI, 2012

changamoto kubwa ambayo tumekuwa nayo kwa kweli ni fedha kwa *TTB* Bodi ya Utalii imekuwa ikipata Bajeti isiyoziidi bilioni 5 kwa mwaka. Tumehangaika sana na suala hili baadaye tumefikia uamuzi wa Kiwizara kwamba tufanye mchakato wa kubadilisha sheria ya *TTB* ili iweze kuwa inakusanya ushuru kutoka kwenye biashara hii ya utalii ndivyo wanavyofanya nchi zingine na wamefanya hivyo kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, uwezekano huu ukishakamilika tutakuwa na uwezo mzuri wa kifedha wa kufanya kazi hizi ambazo Mheshimiwa Mbunge ameshauri. Hata hivyo wakati haya yakiendelea tayari tumekwisha kuanza kuvishirikisha vyombo vya ndani katika kutangaza utalii.

Televisheni ya *Channel Ten* wamekuwa wakitangaza utalii kwa kutumia mpango wao wanaita Utalii wa Ndani wana kipindi maalum. Lakini *TBC* pia wamekuwa wakitangaza kwa kuonyesha vivutio, Radio ya *TBC* nao wamekuwa wakitangaza vivutio vyetu kwa kuwa na kipindi maalum ambacho kilifadhiliwa na kulipwa na *TANAPA*.

Nishukuru kwa wazo hili alilolisema Mheshimiwa Mbunge, nimhakikishie kwamba tutalifanyia kazi lakini changamoto ambayo imekuwepo ni fedha, lakini naamini tutakaporekebisha suala hilo tutaweza kufanikiwa. (*Makofi*)

Na. 111

Wanawake Kuwezeshwa Kiuchumi

MHE. SUSAN A. LYIMO aliuliza:-

Historia ya kweli ya nchi yetu inaonyesha uwezo mkubwa wa wanawake wa kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za ujenzi wa Taifa. Lakini kikwazo kikubwa ni ukosefu wa uwezeshwaji kiuchumi kutokana na mila na desturi zilizowafanya wasipelekwe shule kama kaka zao.

Serikali pamoja na juhudi zake za kutoa mikopo kwao bado ni asilimia ndogo mno wanayopata huku makundi yenye uhitaji yakiachwa:-

Je, Serikali ina mikakati gani sasa inayotekelezeka ya kuwasaidia walengwa?

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaaliana na Mheshimiwa Susan Lyimo, kuwa mila na desturi kandamizi zimekuwa ni kikwazo kwa wanawake kupatiwa mikopo hususan katika Benki za Biashara. Aidha, ni kweli kuwa wanawake wengi hawajapata fursa ya kujiendeleza kielimu katika baadhi ya jamii. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha jamii kupiga vita mila na desturi kandamizi ambazo ni kikwazo katika kuwaendeleza wanawake.

Mheshimiwa Spika, katika suala la elimu, Serikali imefanya jitihada kubwa katika kuhamasisha jamii kuwaandikisha watoto wa jinsia zote shuleni bila ubaguzi na kuweka sheria ndogo za kutekeleza jitihada hizi. Aidha, Serikali imejenga shule za msingi kila kijiji na sekondari kila kata ili kuwawezesha watoto wote kupata elimu karibuni na mazingira ya karibu nyumbani.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama vile taasisi za kifedha ikiwemo Benki ya Wanawake, Asasi za Kiraia, Asasi za Kidini na watu binafsi wamekuwa wakiwapatia mikopo inayowawezesha wanawake kuanzisha biashara ndogondogo kwa lengo la kuwawezesha kiuchumi.

Aidha, wanawake wamekuwa wakijengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo ya ujasiriamali ili waweze kuendesha biashara zao kwa faida na kurejesha mikopo wanayopatiwa. Mafunzo haya pia huwawezesha kujiunga pamoja kuanzisha vikundi vya ujasiriamali kama vile SACCOS na Vikoba.

MHE. SUSAN A. LYIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba mila na desturi kandamizi zimekuwa kikwazao kikubwa sana kwa akina mama kupata mikopo. Je, kwa kuwa Wizara imeshaligundua hilo na kwa kuwa kuna mila kwa mfano suala zima la mirathi, lakini vile vile suala zima la watoto wa kike wanapopata mimba kutorejeshwa shuleni.

(a)Je, ni lini sasa Mheshimiwa Waziri ataleta Muswada hapa Bungeni ili sisi Wabunge tuweze kuhakikisha kwamba akina mama hawa wanafaidika na sheria mpya itakayoundwa? (*Makofi*)

20 APRILI, 2012

(b)Kwa kuwa Benki ya Wanawake imekuwa ni suluhisho kubwa kwa wanawake hususan wa Dar es Salaam na Mheshimiwa Waziri mara kwa mara amekuwa akisema kwamba Benki za Wanawake zitafunguliwa matawi mengine katika nchi nzima ikiwemo pamoja na Zanzibar. Je, Mheshimiwa Waziri anatuambia nini sasa Serikali ina mikakati gani kuhakikisha kwamba matawi mengine ya Benki ya Wanawake yanafunguliwa nchi nzima ili kuwapatia akina mama hawa mikopo na waweze kunufaika nayo ambapo sasa hivi ni wanawake wa Dar es Salaam tu?

SPIKA: Maswali marefu mno.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu maswali yake ya nyongeza Mheshimiwa Susan Lyimo, kama ifuatavyo:-

Ni kweli wanawake wengi wamekuwa wakikoseshwa kujiendeleza kiuchumi kutokana na sheria kama ya mirathi ambayo mpaka sasa sheria ya mirathi inafanyiwa kazi na iko katika stage nzuri ya kuweza kuletwa na kujadiliwa hapa Bungeni. Sheria hii imechukua muda lakini kwa sababu inahusu mirathi ambayo ilikuwa ikitumia zaidi mila ni vizuri tuwe waangalifu zaidi katika kutunga sheria kama hii kwa sababu inawagusa sana wananchi wote. Lingine alilouliza ni kuhusu watoto waliopata mimba kurudishwa majumbani. Pia Serikali ilianza mchakato wa kuwauliza wananchi tufanyeje kuhusu wasichana wanaopata mimba warudi shuleni au wasirudi shuleni. Mchakato huu haukwenda vizuri kwa sababu kumekuwa na mabishano makubwa wengine wakasema kwa nini warudi shuleni, wengine kwa nini wasirudi shuleni. Lakini bado sisi kama Wizara tunasema pale inapowezekana msichana ambaye amepata mimba na wazazi wake wapo tayari kulea yule mtoto apate nafasi ya kuendelea na shule. Tutashukuru kama Waheshimiwa Wabunge, nao wakiliona hilo umuhimu wa huyu msichana ambaye amepata mimba arudi shuleni.

Swali lake la pili anazungumzia kuhusu Benki ya Wanawake. Ni kweli Serikali inajitahidi sana kuiwezesha Benki ya Wanawake na imeahidi kutoa bilioni 2 kila mwaka kuhakikisha benki hii inakuwa na kwa sasa Benki Kuu imeiruhusu kama nilivyojibu katika swali langu lingine hapa wiki iliyopita kwamba Benki Kuu imeruhusu Benki ya Wanawake kuweza kuuza hisa na hivyo mtaji utakua na hivyo kuweza kufungua matawi maeneo mengine. Kwa Zanzibar pia nilizungumza kwamba tayari tumeshapata eneo, tumeshapata ofisi jengo ambalo tunaweza tukaanzisha tawi la benki pale. Ahsante sana.

20 APRILI, 2012

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mfuko wa mabilioni ya Kikwete ulianza vizuri na kuwapatia mikopo na misaada mbalimbali wananchi wa Tanzania wakiwemo wanawake. Na kwa kuwa ukimpatia msaada mwanamke huwa unasaidia yeye mwanamke na unasaidia jamii na watoto. Lakini kwa kuwa sasa hivi mfuko huu sasa naona kama haufanyi tena kama haupo haupo.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha mfuko huu wa Kikwete ili kuweza kusaidia wananchi wa Tanzania wakiwemo Wanawake? Ahsante sana.

SPIKA: Sasa ilikuwa ile benki ya wanawake huo mfuko uko Wizara nyingine. Sijui Mheshimiwa Waziri jibu. Huo mfuko uko kwingine na siyo swali la msingi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, ni kweli mfuko huu uliwawezesha sana vijana na wanawake ambao walijitokeza na kwamba mfuko huu sisi kama Benki ya Wanawake tumeomba kwamba fedha zitakapotolewa tena kwa mfuko haya mabilioni mengine yaingie kwenye benki ya wanawake kwa sababu benki ya wanawake inajadili zaidi wale wanawake ambao hawana hata dhamana na vikundi mbalimbali vikiwemo vikoba na SACCOS mbalimbali za wanawake.

Kwa hiyo, ni kweli mfuko huu unaweza ukaisaidia sana benki na tutashukuru sana kama mkitupigia debe kwamba mfuko wote huu ukija uingie katika Benki ya Wanawake na hivyo itatusaidia kukuza Benki ya Wanawake.

Na. 112

Ujenzi wa Barabara ya Manyovu – Kasulu

MHE. ABERT OBAMA NTABALIBA aliuliza:-

(a)Je, ni lini barabara ya Manyovu toka Mnanila mpaka Kasulu itajengwa kwa kiwango cha Lami?

(b)Je, Serikali haioni umuhimu wa kuunganisha barabara za Mkoa wa Kigoma na Mikoa mingine ili wananchi hao waweze kufanya shughuli za uchumi kama watu wengine nchini?

20 APRILI, 2012

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Manyovu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kutokana na na ufinyu wa Bajeti Serikali haina mpango kwa sasa wa kujenga barabara ya Mnanila – Kasulu kwa kiwango cha lami. Kipaumbele cha Serikali kwa sasa ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara kuu kwanza.

Barabara ya Mnanila – Kasulu itaendelea kutengenezwa kwa kiwango cha changarawe ili iendelee kupitika vizuri kwa kipindi chote cha mwaka.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaona umuhimu wa kuunganisha Mkoa wa Kigoma na Mikoa mingine kwa barabara za lami na tayari kazi hii imeanza kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi wa barabara ya Kigoma – Kidahwe (km. 36) inayounganisha Mkoa wa Kigoma na Mikoa ya Tabora, Kagera, Shinyanga, Mwanza na Rukwa ulikamilika tarehe 8 Juni, 2010 kwa gharama ya shilingi bilioni 33.754.

(ii) Upembezi yakinifu na utayarishaji wa nyaraka za Zabuni kwa barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi yenye urefu (km. 310) itakayounganisha Mkoa wa Kigoma na Mikoa ya Kagera, Shinyanga na Mwanza ulikamilika mwezi Julai 2009 kwa gharama ya shilingi bilioni 1.365 ikiwa ni maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

(iii) Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara Mwandiga – Manyovu (km. 60) inayounganisha Mkoa wa Kigoma na nchi ya Burundi ulikamilika mwezi Oktoba, 2010 kwa gharama ya shilingi bilioni 55.13.

(iv) Mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kidahwe – Uvinza (km. 76.6) inayounganisha Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Tabora ulisainiwa tarehe 24 Juni, 2010 na kwa sasa kazi za ujenzi zinaendelea na zimepangwa kukamilika mwezi Oktoba, 2013.

(v) Mkataba wa ujenzi wa daraja la Malagarasi (*Kikwete Bridge*) na barabara zake (km. 48) linalounganisha Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Tabora ulisainiwa tarehe 21 Oktoba, 2010 na kwa sasa kazi za ujenzi zitakazogharimu jumla ya dola za Kimarekani milioni 57.248 zinaendelea na zimepangwa kukamilika mwezi Desemba, 2013 na mwisho.

(vi) Upembezi yakinifu, usanifu na utayarishaji wa nyaraka za zabuni kwa barabara ya Kanyani – Uvinza – Mpanda (km 252) inayounganisha Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Rukwa ulikamiika mwezi Desemba 2011 kwa gharama ya shilingi bilioni 1.548 ikiwa ni maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niweze kumwuliza maswali mawili Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi kwa majibu aliyoyatoa:-

(a)Kwa kuwa barabara hii ya kutoka Mnamila Manyovu ni barabara kubwa ambayo itaunganisha nchi ya Burundi kuja Kasulu na kuelekea Kibondo mpaka Nyakanazi. Lakini barabara hii hii vile vile ina umuhimu wa kuunganisha masoko matatu ya Kimataifa yanayojengwa na Serikali hii ya Mnanila, Kibande na Kilelema. Lakini barabara hii hii tena itaunganisha kutoka Mnanila kupitia Wilaya mpya ya Buhigwe kwenda Heru Juu mpaka Kasulu. Je, Serikali haioni sasa umuhimu wa kuiona hii barabara ni muhimu kwa kuleta huduma kwa wananchi na kupunguza gharama za huduma?

(b)Kigoma sasa ni Mkoa ambao Mtanzania yeyote kama anasafiri kama kwenda kule lazima alale njiani. Usafiri wetu wa kutoka hapa mpaka kwenda Kigoma lazima ulale Kahama na gharama za sasa za wasafiri imekuwa sasa gharama kati ya laki moja kwa sababu usafiri ni elfu 60, kulala elfu 20, kula elfu 20 ni laki moja kufia Kigoma na Watanzania walio wengi sasa, wote mlioko hapa mnaifika majumbani mwenu mapema. Je, Serikali sasa haioni umuhimu wa kuharakisha barabara hii ya Kidawe-Nyakanazi?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, kama ifuatavyo:-

(a)Kwanza naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua sana umuhimu wa hii barabara ya Mnanila kwenda Kasulu, lakini kama tulivyokwishasema katika Bunge hili maana swali hili alishaliuliza kama miezi minane iliyopita tena, jibu letu ni lile lile kwamba kwa sasa Serikali kwa kweli haina uwezo wa kubeba mzigo mwingine tena wa ziada, lakini hatusemi hatutaweza kuijenga tena hii barabara hapana, mzigo utakapopungua tutajitahidi kuiangalia hii barabara.

20 APRILI, 2012

Pengine nichukue fursa hii kutoa wito kwa *Manager* wa *TANROADS Kigoma* na vile vile uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kuwa wabunifu kwa hii pesa tunayowatumia kila mwaka kwa ajili ya utengenezaji wa barabara hizi za changarawe, wanaweza kabisa wakaanza polepole ujenzi wa lami nyepesi na sisi baadaye tukaweza kuwapokea huo mzigo, lakini sio kusubiri Serikali ifanye kila kitu.

(b)Mheshimiwa Spika, la pili kuhusu usafiri mgumu Kigoma. Hili tunalielewa lakini naomba Mheshimiwa Mbunge atambue kwamba Serikali ya awamu ya nne ndiyo ambayo kwa kweli imefungulia milango Mkoa wa Kigoma. Nimeelezea miradi yote sita hapa sasa hivi ambayo inayoendelea na mingine tunatafutia pesa kwa sasa ni jumla ya shilingi bilioni 259.208 ambazo tumezi-commit kwa ajili ya Mkoa wa Kigoma kwa ajili ya kufungua miundombinu.

Mheshimiwa Spika, nakuhakikishia tukishamaliza barabara ya Kanyani-Uvinza-Mpanda ya kilomita 252, tukamaliza barabara ya Kidawe inapita tena kwa Mheshimiwa Obama, Kasulu, Kibondo mpaka Nyakanazi kilomita 310 sura ya Kigoma itakuwa imebadilika kabisa katika miaka hii mitatu, minne, mitano ijayo. (*Makofi*)

Na. 113

Miundombinu ya Barabara- Kibaha Vijijini

MHE. ABUU HAMOUD JUMAA aliuliza:-

Miundombinu ya barabara kwenye Wilaya mpya ya KibahaVijijini ni duni sana kwani hakuna barabara ya lami kuharakisha maendeleo ya wananchi, hasa barabara ya Makofia-Mzenga ambayo inategemewa sana na wananchi wengi kwa shughuli zao za maendeleo na kusafirisha mazao yao:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara za Wilaya ya Kibaha Vijijini, kwa kiwango cha lami hasa ile ya Makofia-Mzenga?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Barabara za Wilaya ya kibaha Vijijini zina jumla ya kilomita 355.9, kati ya hizo kilomita 66 zipo chini ya Wizara ya Ujenzi na zinahudumiwa na

20 APRILI, 2012

Wakala wa Barabara nchini TANROADS. Kilomita 289.9 ziko chini ya TAMISEMI na zinahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kati ya kilomita 66 za barabara zinahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Mkoa wa Pwani, kilomita 16.86 zipo katika kiwango cha lami, urefu wa barabara uliopo katika kiwango cha lami na barabara zinazohusika ni kama ifuatavyo:-

(a) Barabara ya Pugu-Vikumburu	- km 12
(b) Barabara ya Mlandizi- Manerumango	- km 0.32
(c) Barabara ya Makofia-Mlandizi	- km 2.81
(d) Barabara ya Mkuranga- Kisiju	- km 0.77
(e) Barabra ya Kibiti- Utete	- km 0.96

Mheshimiwa Spika, barabara ya Makofia- Mlandizi-Maneromago (km 100.4) inayojumuisha sehemu ya Makofia-Mzenga imeainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 (Uk. 76) kuwa itafanyiwa upembuzi yakinifu na wa kina, kazi ambayo ni maandalizi ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Wizara imepanga kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hizo, Wizara yangu inahudumia barabara ya Morogoro ambayo inapitia Wilaya ya Kibaha. Barabara hii huchangia sana katika maendeleo ya Wilaya ya Kibaha. (Makofi)

MHE. ABUU HAMOUD JUMAA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri ambayo yana masikitiko makubwa ameanisha barabara ambazo hazipo katika Jimbo langu, lakini majibu haya ya upembuzi yakinifu tumechoka nayo sasa.

Tunahitaji utekelezaji wa barabara hii ya Makofia –Mzenga ni barabara ambayo inategemewa na wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini katika kunyanyua uchumi wa Jimbo lao. Ni lini sasa barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abuu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hatutaweza kuijenga hiyo barabara bila kufanya upembuzi yakinifu na pia usanifu wa kina. Tuko kwenye kipindi cha sayansi na teknolojia, hatuwezi kurudi tena enzi zile za kuweka kamba na kuanza

20 APRILI, 2012

kulima barabara bila hata kufanya upembuzi yakinifu. Tumepanga kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na pesa tutakuwa tunayo katika kipindi cha mwaka 2013/2014.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Barabara ya kutoka Isyonje kwenda Makete amabyo ni kiunganishi cha Mkoa wa Mbeya na Njombe ni barabara ambayo sasa hivi imeharibika vibaya sana na haipitiki. Naomba aniambie Waziri kwamba barabara hiyo wataiwekea lami au wataitengeneza kwa sasa hivi wakati haipitiki? Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tulishajibu katika Bunge lako hili Tukufu kwamba barabara hiyo Isyonje ni barabara kweli inayosimamiwa na *TANROADS*, lakini kwa sasa Serikali haina mpango kuijenga kwa kiwango cha lami kutokana na ufinyu wa Bajeti.

Lakini kwa kusema hivyo hatuna maana kwamba hatutakuja kuijenga kwa kiwango cha lami, hapana ni kwamba kutokana na mzigo tulionao sasa hivi, tutaendelea kuisimamia hiyo barabara katika hali iliyopo ya changarawe, lakini kuna kitu amenieleza Mheshimiwa Mbunge sasa hivi kwamba barabara hii kwa sasa imeharibika sana, napenda kutumia fursa hii kutoa wito kwa *Manager* wa *TANROADS* Mkoa wa Mbeya akaiangalie barabara haraka iwezekanavyo kama hajafanya hivyo mpaka sasa.

Na. 114

Elimu ya Juu Zanzibar

MHE. WARIDE BAKARI JABU aliuliza:-

Licha ya kuwa elimu siyo suala la Muungano, Elimu ya juu inaendeshwa Kimuungano.

(a)Je, ni utaratibu gani unaotumika katika uendeshaji wa Elimu ya juu ambao unakidhi mahitaji ya Tanzania Zanzibar?

(b)Je,Serikali ya Muungano inatenga kiasi gani cha fedha kila mwaka kwa ajili ya uendeshaji wa Elimu ya Juu upande wa Tanzania Bara?

20 APRILI, 2012

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mbunge wa Kiembesamaki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uendeshaji wa Elimu ya juu Tanzania Bara na Zanzibar husimamiwa na vyombo vinavyomiliki Vyuo hivyo. Kwa Tanzania Bara, Vyuo Vikuu husimamiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Vyuo Vikuu vilivyoko Zanzibar husimamiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Masuala ya uendeshaji ikiwa ni pamoja na Bajeti za vyuo hufanywa na vyombo vinavyomiliki Vyuo hivyo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, wanafunzi wa vyuo vikuu vya Zanzibar wana fursa sawa ya kupata mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa wanafunzi wanaotimiza vigezo vya kukopeshwa kutoka Bodi hiyo. Vile vile, kupitia mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya juu, Vyuo Vikuu vya Serikali vya Zanzibar vina fursa sawa ya kupata fedha za kuimarisha miundombinu na kuwajengea uwezo wanataaluma wake.

Aidha, vyuo Vikuu vya Zanzibar vinanufaika pia kwa uwepo wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*) ambapo wanataaluma katika Vyuo Vikuu hivyo, wanayo fursa ya kupata fedha za utafiti kutoka taasisi hiyo iwapo wameandaa andiko linalokubalika.

Mheshimiwa Spika, katika masuala ya skolashipu, ipo Kamati ya Ushari ya Elimu ya Juu na Mafunzo (*Sub-Advisory Committee on Higher Education and Training (SACHET)*) ambayo pia Wajumbe kutoka pande zote mbili za Muungano wanakuwa ni Wajumbe. Mfano; Mkurugenzi wa Ofisi ya kuratibu shughuli za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar-Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Elimu ya Juu-Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mkurugenzi wa Elimu ya Juu Sayansi na Teknolojia-Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali- Zanzibar, Baraza la Mitihani, Tume ya Taifa ya Vyuo Vikuu (*TCU*), Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya juu, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na wawakilishi wawili kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kazi ya Kamati hii ni kupitia na kuratibu maombi ya skolashipu zinazotolewa na nchi rafiki au Mashirika ya Kimataifa yanayotoa fursa hizo kwa Tanzania.

MHE. WARIDE BAKARI JABU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na amjibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kumwuliza maswali mawili ya nyongeza:-

20 APRILI, 2012

- (a) Ni mambo gani au Idara zipi katika Wizara yake inayoshirikiana Kimwungano?
- (b) Je, Idara hizo ziko Zanzibar? Na kama hazipo ni lini ofisi hizi zitafunguliwa kwa upande wa Zanzibar? Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mbunge wa Kiembesamaki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi zipo taasisi na baadhi ya mambo ambayo tunashirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kama tunavyosema kila wakati Baraza la mitihani limekaa Kimuungano na baadhi ya walimu wanaosahisha Mitihani wanatoka Zanzibar na ofisi ipo, yupo mtumishi mmoja pale Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali –Zanzibar, tunamtumia katika shughuli za Baraza la Mitihani.

Lakini vile vile taasisi nyingine kama *TET* yaani Taasisi ya Elimu Tanzania tunashirikiana nao katika masuala ya mitahala kwa upande wa elimu ya Sekondari na Vyuo vya Uwalimu. Lakini taasisi nyingine ni Bodi ya mikopo kama ambavyo tunasema kila siku, Bodi ya Mikopo inakopesha wanafunzi vile vile kutoka Zanzibar na Ofisi ya Bodi ya Mikopo ipo na mwezi huu wa nne tayari tumefungua imeanza kufanya kazi. Lakini vile vile Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi yaani *NACTE* tunashirikiana nao, baadhi ya vyuo vya ufundi na mafunzo *study* wanakuja Dar es Salaam pale Wizara ya Elimu kwenye Baraza la Taifa hilo kuja kupata *accreditation* ili vyeti vyao viweze kutambulika. Lakini bado taasisi ya Tanzania Commission of Universities (*TCU*) wanatoa huduma katika Vyuo vyote vya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani katika kuangalia ubora wa vyuo na kutoa *accreditation*.

Lakini vile vile iko miradi mbalimbali ya Vyuo Vikuu kwenye elimu ya juu kama *COSTECH*, hii Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia kuna mambo mbalimbali ya skolashipu tunashirikiana pamoja na watu wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka tu nimhakikishie Mbunge kwamba Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania haijasahau Serikali ya Zanzibar, tunashirikiana nao vizuri sana katika mambo ya elimu ya juu. (*Makofi*)

20 APRILI, 2012

Na. 115

Kujenga Mabweni kwa Ajili ya Wanafunzi wa Kike Nchini

MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA aliuliza:-

Malengo ya Milenia ni pamoja na kuhakikisha watoto wa kike wanapata elimu. Lakini taarifa za sasa zinaonesha kuwa watoto wengi hushindwa kumaliza elimu ya sekondari kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo upataji mimba.

Je, ni lini Serikali itatenga fedha za kujenga mabweni kwa ajili ya wanafunzi wa kike kote nchini?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa wapo wanafunzi wa shule za Sekondari za kutwa ambao wanaishi katika mazingira yasiyo rafiki.

Mheshimiwa Spika, makazi stahili ya wanafunzi yanachangia kupunguza mdondoko shuleni (*drop out*), makazi yasiyostahili. Makazi hayo na mfumo huo unatokana na sababu mbalimbali ikiwemo tatizo la mimba.

Katika kuondoa tatizo hilo, awamu ya pili ya mpango wa maendeleo ya elimu ya sekondari (*MMES II*) imeweka mikakati mbalimbali na mikakati ya ujenzi wa hosteli katika shule za sekondari. Matarajio ni kujenga hosteli 20 kwa kila mwaka zenye uwezo wa kulaza wanafunzi 48 kila moja. Mpango huu unatekelezwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kutoa stadi mbalimbali za maisha na ushauri nasaha mashuleni ikiwa ni sehemu ya kukabiliana na changamoto ya wanafunzi kupata mimba na kuwasaidia wanafunzi hao kuweza kujiamini na kutafuta ushauri kabla ya kufanya maamuzi ambayo siyo sahihi kwa maendeleo ya masomo yao.

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa wananchi wote kuwa tushirikiane katika kuwalinda wanafunzi wetu wa kike ili waweze kuzifikia ndoto zao za kupata elimu na baadaye kulitumikia Taifa letu.

MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri kabisa ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kumwuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa katika Mkoa wa Kanda ya Ziwa hususani Mkoa mpya wa Geita tatizo la ukosefu wa mabweni ni kubwa na ni kubwa kweli kweli. Watoto wetu na hasa watoto wa kike wamekuwa wakipata elimu yao katika mazingira magumu na hatarishi kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, watoto hawa wamekuwa wakilazimika kupanga kwenye nyumba za watu binafsi na kibaya zaidi wamekuwa wakipata mimba na magonjwa mbali mbali mabaya kama UKIMWI na kadhalika.

Je, Serikali haioni kuna haja ya kunusuru maisha ya watoto hawa kwa kutumia hata Mashirika ya Umma kama vile *National Housing Corporation (NHC)* kuweza kujenga mabweni katika shule zetu za Sekondari? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema katika awamu ya kwanza, Serikali inayo nia ya kuendeleza elimu nchini, lakini kikubwa hapa ni ufinyu wa bajeti. Kama tulivyosema pia kwamba, tumetenga fedha kwenye mpango wa MMES wa kujenga hosteli *20 at least* kwa kila mwaka. Naomba labda nimweleweshe Mheshimiwa Mbunge jambo moja, tunaposema shule za bweni na tunaposema kujenga hosteli ni kitu tofauti kabisa. Shule za bweni maana yake wanafunzi wote kutoka *Form One* ama mpaka *Form Six* maana yake wanakaa shuleni hapo hapo, wavulana au wasichana, wanakula hapo, wanalala hapo na wanachaguliwa kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, hosteli ni nyumba tunazojenga kwa kushirikiana na Halmashauri ama Baraza la Madiwani kule kwenye Kata, zile *Ward C's*, wanakaa pamoja wanakubaliana kwamba tujenge hosteli kwa ajili ya watoto wanaokaa mbali na kituo cha shule kilipo, maana wanatoka kwenye vijiji mbali kidogo. Kwa hiyo, hosteli ni nyumba tu ambayo tunakuwa tumeweka pale kwa ajili ya wanafunzi wanaotoka mbali lakini inakuwa ni mchanganyiko, wanafunzi wanaokaa hosteli na wengine wanatoka mbali. Tunazo shule za mfano huo kama vile Lugalo, Mbeya Day, hata pale Azania na Tambaza.

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kunakuwa na wanafunzi wanatoka *day* na wengine wanakaa pale hosteli, lakini shule za bweni ni kwa ajili ya bweni tu na watoto wanatoka katika *different dejects* kama vile *Songea Boys, Tabora Boys* na shule zingine za mfumo huo. Kwa hiyo, kwa upande wa Geita, ukosefu wa hosteli, namwomba Mheshimiwa Mbunge kwa sababu na yeye ni Mjumbe kwenye Halmashauri ya Wilaya, wakae, wapange, waone ni namna gani wataweza kusaidia. Lakini bado Serikali sisi tutachangia mfumo mwingine kama nilivyosema kwamba tutajenga hosteli 20 na kila mwaka tunaweka bajeti hiyo.

SPIKA: Mheshimiwa uandae semina ya kutosha peke yenu. Mheshimiwa Moza swali lingine la nyongeza, liwe fupi.

MHE. MOZA A. SAIDY: Nashukuru Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi ya kuweza kumwuliza Mheshimiwa Waziri swali la nyongeza. Pamoja na nia njema ya Serikali kujenga mabweni ya wasichana; je, Serikali inajipangaje na changamoto ya utandawazi ya wanafunzi wasichana kupata ujauzito kwenye mabweni? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa naomba ujibu kwa kifupi sana, maana yake muda kwa semina hautoshi.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kidogo teminoloji hiyo imeniacha hoi kidogo ya utandawazi wa masuala ya mamba, lakini kwa ujumla suala la mimba lina changamoto nyingi. Naomba hapa niseme kwamba Waheshimiwa Wabunge sisi wenyewe kama wazazi na wazazi wengine kule wanaolea watoto na wanafunzi kwa ujumla, ipo sheria inayokatiza masuala ya mimba shuleni. Nazo ni Sheria ya mwaka 1978, kifungu cha 25 ambacho kinasema, mwanafunzi atakayepata mimba ataachishwa shule na yule aliyempa mimba atafungwa kwa sheria za kawaida ya miaka kumi jela.

Mheshimiwa Spika, lakini ninaposema kuna changamoto ni nini? Wanafunzi hao wanapeana mimba huko shuleni au huko hosteli, lakini baadaye tunapeleka hizi kesi Polisi. Wakosaji wanakamatwa, lakini ushahidi wa kwenda Mahakamani kama mnavyojua Sheria inafuata mkondo wake, unakuta wazazi sisi kwa lugha ya kule Mbeya tunasema '*Kayemba na kayemba*', wanakaa huko wanapeana ng'ombe. Basi unakuta ile kesi mpaka Hakimku anakuja kuifuta, maana yake watu hawafiki Mahakamani kutoa ushahidi. Huyu mwanaume na mwanamke waliopeana mimba, unakuta mwanaume anakimbia. Msichana hataki kutoa ushahidi Mahakamani. Kwa hiyo kidogo pana changamoto kubwa. Kumbeni rai yangu ni kwamba, sisi wenyewe Wabunge

20 APRILI, 2012

tunapokuwa kwenye mikutano ya hadhara tuendeleo kuielimisha jamii kwa masuala ya mimba mashuleni.

Na. 116

Ruzuku ya Pembejeo za Kilimo Kutowafikia Wakulima

MHE. CATHERINE V. MAGIGE aliuliza:-

Mwaka 2011 Serikali ilitoa ruzuku za pembejeo za kilimo kwa wakulima wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, lakini hazikuwafikia wakulima na hivyo kuathiri uzalishaji wa mazao ya chakula kwa sababu wakulima hawakuweza kumudu gharama za pembejeo:-

(a) Je, Serikali ina habari juu ya kitendo kilichofanywa na watendaji wa Halmashauri ya Wilaya huku ikijua kuwa mawakala walilipwa?

(b) Je, ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya watendaji hao?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Valentino Magige, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ni moja ya Halmashauri zinazoshirikishwa katika mpango wa Taifa wa ruzuku katika pembejeo za kilimo kwa wakulima. Ruzuku hiyo inatolewa katika mbolea na mbegu bora za mazao ya chakula, hususan, mahindi kwa kutumia utaratibu wa vocha. Katika mwaka 2010/2011 Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ilipokea jumla ya vocha 60,300 zikigawiwa katika Vijiji vyote 71 zikiwemo vocha 20,100 za mbegu bora za mahindi; 20,100 za mbolea ya kupandia na kiasi kama hicho cha mbolea ya kukuzia. Vocha hizo ziligawiwa kwa wakulima kwa kufuata maelekezo na mwongozo wa utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa utaratibu wa vocha uliotolewa na Wizara yangu.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu mawakala wa pembejeo waliolipwa bila ya kutoa huduma, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika imewasiliana na uongozi wa Mkoa Arusha na Wilaya ya Arusha kupata maelezo kama kulikuwa na hujuma katika utaratibu huo. Taarifa zilizoletwa na Mkoa na Wilaya hiyo hadi sasa zinaonesha kwamba hakukuwa na hujuma iliyofanyika. Hata ninamwomba Mheshimiwa

20 APRILI, 2012

Magige ananipatie taarifa na nyaraka alizonazo kuhusu tatizo hili tuchukue hatua stahiki. Aidha, pamoja na taarifa kutoka Mkoani na Wilayani, ukaguzi maalum unafanywa na watakaothibitika kuhusika na hujuma katika mpango huu watachukuliwa hatua za kisheria.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa yapo malalamiko mengi juu ya suala hili kwa nini isiundwe Tume Maalum kwa ajili ya kwenda kuchunguza suala hili badala ya kumtuma mtu mmoja ambaye ni Rais kudanganywa? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa taarifa hiyo iliyotolewa imeandaliwa na Halmashauri ya Wilaya ambao ni watuhumiwa wakuu katika suala hili. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuongozana na mimi mpaka kwa wananchi hao kwenda kusikiliza kero zinazohusiana na Wizara yake? *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, naomba nawe ujibu kwa kifupi *time is not in our side.*

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, sioni kama kuna sababu ya kuunda Tume Maalum wakati ambapo Mkaguzi na Mdhhibiti Mkuu wa Serikali ameshaandaa ukaguzi maalum katika jambo hili. Hatua ya kwanza ya ukaguzi huo yaani ile *preliminary audit* imeshakamilika na wanajiandaa sasa kwenda kufanya ukaguzi wa pili. Kwa hiyo, tungoje taarifa yake ili tuweze kuchukua hatua stahiki.

Pili, nitafuatana na Mheshimiwa Mbunge kwa furaha kabisa ili kusikiliza malalamiko ya wananchi. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 117

Kupitia Upya Mikataba ya Wawekezaji wa Mashamba ya Kahawa Moshi Vijijini na Hai

MHE. BETTY E. MACHANGU aliuliza:-

Serikali ilikabidhi mashamba 41 ya Kahawa katika Wilaya za Moshi Vijijini na Hai yalikabidhiwa na Serikali kwa Vyama vya Ushirika ambavyo navyo vilitafuta wabia ambao kwa bahati mbaya walikuwa sio waaminifu, kati ya hayo mashamba 15 tu ndio yaliyofanya vizuri, mashamba 12 yana hali ya wastani na mashamba 14 yana hali mbaya sana na uzalishaji umesitishwa kutokana na ukosefu wa fedha na utawala kwa wawekezaji hao na kwamba vyama vinapotaka kuwaondoa

20 APRILI, 2012

wawekezaji hao kama Silvdale, Mbono, Kindi, Kindi Kale na Despo kwa sababu ya kushindwa kutoa pato kwa wanachama na kodi kwa Serikali hukimbilia Mahakamani ambako kesi hukaa kwa zaidi ya miaka kumi:-

Je, Serikali haioni kuwa, kuna haja ya kuwasiliana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili Mahakama iruhusu mikataba hiyo isiyokuwa na tija kupitiwa upya au kuvunjwa ili ufumbuji upatikane?

WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Kilimanjaro kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 1971 Serikali ilitaifisha mashamba makubwa ya kahawa 41 katika Wilaya za Moshi, Hai na Siha. Mwaka 1982, mashamba hayo yalikalidhiwa kwa Vyama vya Ushirika ambavyo navyo viliamua kutafuta wawekazaji.

Katika mwaka 2007, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro aliteua Kamati iliyokagua mashamba yote 41 yalikalidhiwa kwa Vyama vya Ushirika na mashamba ya Serikali yaliyopo *West Kilimanjaro (NAFCO, NARCO* na mashamba yaliyokuwa chini ya *TALIRO*).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini upungufu mkubwa katika uwekezaji unaofanywa na Vyama vya Ushirika ambavyo:-

(1) Ni pamoja na maeneo ya vyanzo vya maji yamevamiwa na kuharibiwa kwa shughuli za kibinadamu;

(2) Mikataba iliyopo kati ya Vyama vya Ushirika na wawekezaji ina kasoro nyingi na haina faida kwa vyama hivyo;

(3) Kuna kampuni zisizokuwa na uhalali wa kisheria zilizoingia mikataba na Vyama vya Ushirika; na

(4) Wawekezaji wengi hawalipi kodi ya pango ya ardhi wala hawaendelezi zao la kahawa.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla kuna upungufu mkubwa katika uwekezaji na matumizi ya mashamba hayo na baadhi ya wawekezaji wameshindwa kuyaendeleza na kubadili matumizi yake.

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, pamoja na udhaifu huo katika uwekezaji, tathmini ilionesha pia kuwa uendelezaji umekuwa mzuri katika mashamba 15. Aidha, Serikali sasa itamwomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia upya mikataba yote ya uwekezaji katika mashamba hayo na kuishauri Serikali juu ya hatua za kuchukua ili kurekebisha kasoro hizo.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali imekiri kwamba wawekezaji wengine wa mashamba hayo wamebadili matumizi na biashara ambayo wanafanya ni uzaji wa mbaao za miti iliyoko huko je, Serikali iko tayari sasa kuwazuia kufanya biashara hiyo, TRA kuwadai kodi na Wizara ya Ardhi kudai kodi la pango la ardhi kwa pato la Taifa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, uwekezaji huo ulisimamiwa na Serikali na makubaliano yalikuwa ni asilimia 60 irudi kwa jamii na asilimia 40 irudi kwa Vyama vya Ushirika. Je, Serikali iko tayari sasa kuvinusuru Vyama hivi vya Ushirika kwa kuwalipa hiyo asilimia 40 kwa sababu ya mikataba isiyokuwa na tija?

WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, jambo hili lina matatizo na ndiyo maana tumeona tuombe ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Vyama hivi vya Ushirika na wawekezaji hawa walipewa mashamba haya kisheria. Kwa hiyo, tutangoja Mwanasheria Mkuu wa Serikali aangalie jambo kwa undani kabla hatujachukua hatua. Tutakapopata ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali hatua stahiki zitachukuliwa.

Pili, Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mashamba haya yalitolewa kwa makubaliano kwamba jamii itapata asilimia 60 na Vyama vya Ushirika vichukue asilimia 40. Lakini katika utekelezaji wa uwekezaji huu Vyama vya Ushirika vilitafuta wawekezaji binafsi. Kwa hiyo, kama nilivyosema ni vizuri tumngoje Mwanasheria Mkuu wa Serikali atushauri juu ya jambo hili ili tukichukua hatua tuchukue hatua ambazo zina msingi wa kisheria.

SPIKA: Ahsante. Nataka kumwita kati ya Nassari na Mdee lakini kwa sababu hawajafunga ndoa, basi nitamwita Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa suala la ardhi ni suala *sensitive* sana katika Mkoa wa Kilimanjaro na ni kweli mashamba haya katika Wilaya za Siha, Hai na Moshi Vijijini, mengi yana migogoro mikubwa mno ambayo yanaweza hata kuhatarisha usalama wa raia na mali zao. Kabla ya hatua ya Waziri

20 APRILI, 2012

kulipeleka jambo hili kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waziri haoni ni muhimu zaidi kulipanua kwa kuanza kuwa na kikao cha kwanza na Wabunge wa Mkoa wa Kilimanjaro ili wamueleze kwa kina na upana matatizo haya kisha ndiyo apeleke kwa Mwanasheria Mkuu?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, tuko tayari kuzungumza na Wabunge wa Mkoa wa Kilimanjaro na kuwasikiliza ili tukimwomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliangalie tuwe tumepata mawazo kutoka kwa wadau mbalimbali. *(Makofi)*

Na. 118

Fidia kwa Wananchi Waliopisha Mgodini – Geita

MHE. MKIWA A. KIMWANGA aliuliza:-

Wananchi wa eneo la Nyakabale walitakiwa kuhama ili kupisha shughuli za uendelezaji na uchimbaji madini katika mgodi wa GGM, ambapo tathmini ya nyumba na maeneo yao ulifanyika tangu mwaka 2004 kwa ajili ya malipo. Hata hivyo, fidia waliyolipwa wananchi hao ni ndogo na hailingani na tathmini iliyofanyika:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kurekebisha kasoro zilizojitokeza ili wananchi hao walipwe malipo sahihi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Binti Adamu Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika eneo linalomilikiwa na mgodi wa GGM, lipo eneo dogo la Nyakabale ambalo mgodi ulitaka kulichukua kwa ajili ya matumizi yake, hivyo kutakiwa kulipa fidia kwa mujibu wa Sheria. Wakati mchakato wa tathmini unaendelea wananchi wa eneo hilo waliamua kupanda migomba mingi kinyume na taratibu za kilimo kwa lengo la kupata fidia kubwa itakavyolipwa. Baada ya mgodi kuona hali hiyo ulisitisha zoezi hilo la ulipaji wa fidia wa eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mgodi huo haujawa na uhitaji wa eneo hilo kwa sasa, hakuna mwananchi wa Kijiji cha Nyakabale aliyelipwa fidia. Hivyo, umuhimu wa kuhamasisha wanakijiji hao na kuwalipa fidia stahiki ili kupisha shughuli za mgodi huo haukuwepo tena. Endapo eneo hilo litahitajika tathmini itafanywa upya kwa viwango vya

sasa hivi na fidia stahiki kwa wakati huu italipwa kwa wananchi wa eneo hilo.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Swali langu ni kutohitaji au kwa kuhitaji eneo hilo la mgodi si suala langu. Suala langu ni kwamba, kwanza kabisa napenda Mheshimiwa Naibu Waziri afahamu eneo hilo limeshatathminiwa, nyaraka ninazo hapa na wananchi wamekwishalipwa pungufu au mapunjo. Swali langu ni kwamba, ni lini wananchi watalipwa haki zao za msingi? Naomba Serikali iweze kuwasimamia kupata haki zao kutoka kwenye mgodi huo kwa sababu tathmini tayari na wananchi hao wamelipwa mapunjo kama Mheshimiwa Naibu Waziri huna taarifa, tayari tathmini imeshafanyika. (*Makofi*)

Swali la pili, kwa kuwa tangu tathmini ifanywe ni muda mrefu kuanzia mwaka 2004 mpaka leo hii. Eneo hilo halijaendelezwa, wananchi wamekaa bila kueleza shughuli zao za kijamii. Je, Waziri sasa yupo tayari kuongozana na mimi kwenda kwenye eneo hili na kuhakiki kwa haya ambayo tayari Mkuu wa Wilaya amethibitisha kwamba wamelipwa mapunjo?

Mheshimiwa Spika, Katibu Tarafa amehakikisha kwamba wamelipwa mapunjo, Katibu Kata amehakiki kwamba wamelipwa mapunjo, Katibu Mtendaji wa Kijiji amehakiki kwamba wamepunjwa mapunjo, ili tukakae na wananchi hawa kujua nini hatma ya haki yao ya msingi? (*Makofi*)

SPIKA: Yaani mapunjo kwamba wamelipa kidogo kuliko walivyostahili? Haya! Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, eneo la Nyakabale lina leseni mbili, kuna upande mmoja wa Nyakabale una leseni ya *Special Mining License*; kuna upande mwingine wa leseni wa Nyakabale hiyo hiyo Kijiji hicho hicho kina eneo la *Prospecting License*. Hili swali tulikuwa tumelijibu mwaka 2010, Februari kwenye kikao chako cha wakati huo na Waziri wa Nishati na Madini alikuwa amelitolea maelezo ya kina tu.

Sasa Mheshimiwa Spika, tunachosema ni kwamba, kuna hatua mbalimbali za ulipaji wa fidia. Kwa yale maeneo ambayo tunasema kama wanayahitaji kuyatumia, tatizo la fidia ambalo ni kubwa ni kwamba, watu wanapoona kwamba kuna uwezekano wa kulipwa fidia, anaweka mazingira ya kupata zaidi ya kile ambacho kingetathminiwa. Sasa baada ya kuona uwezekano kwamba, pale ile hali ingekuwa

20 APRILI, 2012

kidogo ndivyo sivyo, wale mabwana wakasema kwamba basi eneo hilo sisi kwa sasa hivi hatutalitumia tena. Kwa hiyo kama kulikuwa na mpango au kuna mapunjo yalikuwa yamelipwa na kadhalika, lakini kwa sababu eneo lile halihitaji kutumika kwa sasa hivi, ndiyo maana *process* haikuendelea.

Mheshimiwa Spika, nilichosema, kwa kuwa yale maeneo yana leseni zote mbili, liko eneo la *special mining license* na liko eneo lenye *prospecting license*. Watakapoingia kutumia maeneo yale siyo fidia ya 2004 tena. Itabidi ifanyiwe tathmini ya leo 2012 tena kwa Sheria Mpya ya 2010, siyo tena ya 1998 na wapate pesa yao stahili kwa mujibu wa viwango vya sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, lile la pili la kusema kwamba labda kama Mheshimiwa twende pamoja *Inshallah* mimi nimekubali tutakwenda pamoja Geita. (*Makofi*)

SPIKA: Na maelezo yako haya, inabidi mwende pamoja.

Tunaendelea na swali la mwisho. Waheshimiwa Wabunge, msidhani kama ni tabia ya kuongeza muda bila utaratibu; huu muda tuliutumia ni ule tuliowaruhusu Wenyeviti kuwasilisha nyaraka zao. Swali letu la mwisho litakuwa la Mheshimiwa Kangi Lugola, aulize swali.

Na. 119

Kuvipatia Umeme Vijiji vya Jimbo La Mwibara

MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA aliuliza:-

Njia ya umeme kutoka Bunda Mjini kwenda Ukerewe imepitia katika Jimbo la Mwibara:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Rais ya kuvipatia umeme Vijiji vya Buzimbwe, Bulamba, Kasuguti, Mahyolo, Nyamitebili, Kasahunga, Namibu, Kitengule, Busambara, Bunere, Nambaza, Nansimo, Mwitende, Makwa, Masahunga, Nambubi na Bwanza?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo:-

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, kutokana na tathmini iliyofanywa na Shirika la Umeme TANESCO kuhusu upelekaji umeme kwenye Vijiji 12 vya Mwibara, Bulamba, Kasuguti, Mahoyolo, Kasahunga, Namibu, Busambara, Dodoma, Nambaza, Nansimo, Genge, Mwitende, Nyamitebili na Masahunga, gharama za kupeleka umeme katika maeneo ya vijiji hivyo yalikadiriwa kuwa kama shilingi milioni 936. Gharama hizi zinahusisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 33 umbali wa kilometa 14.3, ufungaji wa vituo 12 vya kupozea umeme kwa wateja na ujenzi wa njia ya msongo wa kilovolti 400 (*Low Voltage Line*) yenye urefu wa kilometa kama 18. Umeme katika vijiji hivi utatoka katika njia kubwa inayotoka Bunda kwenda Ukerewe.

Mheshimiwa Spika, makadirio haya ni makisizo ya awali yaliyofanywa kipindi cha nyuma na hivyo maombi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu yameshawaliwa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na vijiji hivi vimeingizwa kwenye Awamu ya Pili ya Mradi unaotarajiwa kutengewa fedha katika bajeti ya mwaka 2012/2013. Hatua iliyofikiwa hadi sasa ni maandalizi ya manunuzi ya Wakandarasi, watakaotekeleza Mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine kubwa inayofanywa ni kuboresha upatikanaji wa umeme kwa kiwango cha ubora zaidi, kwa Kanda yote ya maeneo ya Mkoa ya Mara, Mwanza, Kagera, Geita, Shinyanga na Simiyu, ambayo ina mahitaji ya umeme yanayoongezeka kila siku, lakini miundombinu haijaboreshwa kukidhi upana wa mahitaji haya. Hivyo basi, pamoja na Miradi inayofanyiwa kazi na inayopangwa kutekelezwa ni vyema kusisitiza kazi kubwa itakayojumuisha kukamilika kwa Kituo cha Uzalishaji cha Nyakato, Jijini Mwanza. Naomba niliahidi Bunge lako kwamba, Wizara yangu itaandaa Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi hii na kuiwasilisha humu ndani.

MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniruhusu niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, nashukuru sana Serikali kwa kutenga fedha kwenye bajeti itakayoletwa hapa Bungeni na kwamba, wameanza maandalizi ya manunuzi kwa ajili ya kupata Mkandarasi.

(i) Kwa kuwa Bunge hili tumekuwa tukipitisha fedha za Miradi mbalimbali kwenye maeneo yetu na baadhi ya Miradi pesa zimekuwa haziendi; na kwa kuwa Sheria ya Manunuzi inazitaka Taasisi za Serikali na Idara zake kuandaa Mpango wa Manunuzi wa Mwaka (*Annual Procurement Plan*). Je, ili isione kwamba haya majibu ni hewa; Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kunionesha au kunipatia *Annual Procurement Plan* nione kweli haya manunuzi yamo? (*Makofi*)

(ii) Nguzo za umeme kwenye Vijiji vya Kibara Stoo, Kibara A, Kibara B, Mwibara na Kisolya, wamewekewa *line* moja tu ya umeme au *line* mbili na vile vijiji ni vikubwa na ni umeme wa vijijini. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari sasa kuhakikisha miundombinu kwa maana ya *line* zingine za umeme wanasogezewa karibu hawa wananchi ambao kipato chao ni kidogo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Kangi Lugola, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, labda nifafanue; hili jambo la kukosekana, *REA* wanaweka Mipango, Wabunge wanaomba, tunakuja hapa tunapitisha kiasi fulani cha fedha, siyo kwa sababu ya ukosefu wa *Annual Procurement Plan*. Mwaka 2010/2011 tuliwapa *REA* shilingi bilioni 50 kwa ajili ya kutekeleza Miradi mbalimbali, lakini mpaka mwaka ulipoisha *REA* wakawa wamepata shilingi bilioni 13. Kwa hiyo, *not withstanding Annual Procurement Plan*, kama pesa hazikutoka Hazina kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ile itakuwa haitekelezeki.

Mheshimiwa Spika, na kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu, suala siyo *Annual Procurement Plan* tu, suala ni kuomba pesa zinazotengwa kwa ajili ya Miradi ya Nishati Vijijini na hasa kufikisha huduma ya umeme kwenye vijiji vilivyotengwa na *REA*. Tumeshakubaliana na wenzetu wa Hazina kwamba, pesa hizi zitakuwa zimetengwa kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Tutakuwa hatuna matatizo haya tena ya kujua kama pesa hizo zitapatikana au hazitapatikana. Kwa hiyo, nadhani hili tatizo tumeshalipatia ufumbuzi mzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, hili la pili la maeneo ya Kibara, Mwibara Kisolya, hili ni tatizo la *distribution* kwa maeneo hayo kwa maana ya kwamba ni usambazaji tu. Nadhani *TANESCO* walipopoleka umeme, makadirio ya mwanzo yalikuwa ni kwa usambazaji wa mwanzo uliofanyika wakati ule.

Mheshimiwa Spika, sasa kama mahitaji yameongezeka, hili ni tatizo ambalo linaonekana kwenye maeneo mengi tu kwamba, umeme ukishafika mahitaji yanaongezeka na hivyo kuna mahitaji ya usambazaji. Kwa hiyo, tunalazimika kuongeza nguzo, nyaya na *transformer* zaidi.

Naomba nimhakikishie kwamba, tutaiagiza *TANESCO* iende ikafanye tathmini ya mahitaji haya yaliyoongezeka ili huduma hii iweze kuwafikia wananchi wengi zaidi Mwibara. Nakushukuru.

20 APRILI, 2012

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita, lakini kama ninavyosema, bado tujifunze kuuliza maswali kwa kifupi na kujibu kwa kifupi, tutumie muda wetu kufuatana na Kanuni.

Tunao wageni ambao wapo katika Bunge letu hili hivi sasa. Tunao Marais 40 wa Vyuo Vikuu vya Tanzania Bara na Zanzibar, wakiongozwa na Mwenyekiti wao wa TAHILISO, Ndugu Paul Makonda. Kwanza, Ndugu Paul Makonda asimame. Nafikiri ndiyo Rais Mkuu wa Shirikisho, ahsante. *(Makofi)*

Sasa Marais wengine wote 40, wasimame; ahsante sana, tumefurahi kuwaoneni. *(Makofi)*

Ombi langu kwa ninyi Marais, naomba mkae. Tunalo tatizo kubwa bado halijapata jibu la mikopo kwa wanafunzi; inaelekea kwamba, wanafunzi ambao wazazi wao wana uwezo mara nyingi unakuta wao ndiyo wanaopata mikopo na wale ambao wazazi wao hawana uwezo, ndiyo mara nyingi wanakosa. Mimi ningewaomba ninyi Marais na Mabaraza yenu, kwa nini msifanye kazi moja ya ku-*identify* kati ya wanaopata mikopo ni wepi ambao wazazi wao wanaweza na ni wepi ambao wazazi wao hawawezi, kwa sababu *you are in the kitchen*, mnaweza kujua. Acheni kufumbia mambo kama haya, maana sasa hivi maskini wanakosa, wenye uwezo wanafanikiwa.

Marais wangu nawaombeni hii kazi muifanye, tuweze kuboresha mfumo mzima wa mikopo, uwanufaishe wale ambao hawawezi. Hilo ni ombi langu kwenu, ningekuwa na muda ningengea na ninyi, lakini bahati mbaya tumebanwa. Nafurahi sana mmekuja, naomba hili mkalifanyie kazi.

Tunao Wakurugenzi na Wafanyakazi watano wa Studio Mpya ya Kisasa, inaitwa *Image For You Photo Studio* ya Mjini Dodoma; hebu simameni wapo wapi hawa?

Okay, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, kuna hiyo *Photograph Centre* hapo inaitwa *Image For You Photo Studio*. Karibuni sana.

Tuna kikundi cha akina mama kinachoitwa *Tanga Rafiki Women Group*, wakiongozwa na Ndugu Diana Bendera, Katibu wa Kikundi. Wasimame hao akina mama wako wapi? Ahsanteni sana, karibuni sana. Tunafurah sana kwa mfano wenu huo mzuri. *(Makofi)*

20 APRILI, 2012

Tuna wageni wengine wanne kutoka Chama cha Wasafirishaji wa Viumbe hai Nje, wakiongozwa na Mwenyekiti wao, Ndugu Henry Kashangaki. Hebu simameni huko, ahsante nashukuru. Nadhani kwa sababu walijua hawa Kamati yao itawasilisha, lakini tutatoa maelezo baadaye.

Tunao pia Wanasemina 41 wa Huduma za Afya ya Akili kutoka Magereza Makuu 15 ya Tanzania Bara, wakiongozwa na Dkt. Joseph Mbatia, Mkurugenzi wa Mafunzo ya Akili. Naomba Dkt. Joseph Mbatia asimame; yuko wapi? Pia tunaye Dkt. Juma Mallewa; sijui wako wapi? Na wale wengine 41 tunaomba wasimame. Najua kazi yenu ni ngumu sana, lakini inahitaji wito na uvumilivu, ahsanteni sana kwa kuja. (*Makofi*)

Tuna wanafunzi 54 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, *UDOM*. Popote walipo wasimame wanafunzi wetu wa *UDOM*. Ahsante sana, Chuo kipo kwenu hapa, mnaweza kuja kwa kutoa taarifa tu kwa sababu ya kukosa nafasi, lakini wakati wote mnakaribishwa. (*Makofi*)

Tuna wageni wengine tisa kutoka Tarime, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Mheshimiwa Amos Sagala Nyabikwi. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri, Amosi Sagala Nyabikwi asimame, halafu na wengine wote sijui Madiwani simameni. Ahsante sana, tunawatakiwa kazi njema huko mnakofanya kazi yenu. (*Makofi*)

Tuna wanafunzi 28 kutoka *Emarx Training Centre Dodoma*; hawa nao wasimame. Mimi siifahamu *Emarx*, wasimame walipo; ahsante sana. Bahati mbaya sijaifahamu hiyo *Emarx* ni nini; basi karibuni sana. (*Makofi*)

Ninao wageni wengine, Waheshimiwa Wabunge, bado utaratibu wetu ni kuandika na kupeleka kwenye Ofisi ya Mawasiliano, siyo kuleta vikaratasi hapa. Yupo Ndugu Abdul Abdi Madabida kutoka *Tanzania Pharmaceutical Industry, Arusha*; sijui yuko wapi? Ahsante sana.

Shughuli za kazi; kwanza kabisa, nimeombwa na Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, huyu ni Katibu wa Wabunge wanaotoka Majimbo yanayolima Pamba, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote wanaotoka kwenye maeneo yanayolima pamba kuwa, watakuwa na Kikao chao leo saa saba mchana katika Ukumbi wa Msekwa B na mnaombwa kufika kwa wakati ili kumaliza Kikao mapema. Kwa hiyo, wale wanaolima pamba.

Pia kuna tangazo kutoka Ofisini kwangu pale; Katibu wa Bunge, anawatangazia Wabunge wote kuhudhuria Semina kuhusu Marejesho ya Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika tarehe 12 Aprili, 2012. Lengo la

20 APRILI, 2012

Semina hiyo ni Wabunge kupatiwa yaliyotokana na Kikao hicho na ratiba ya uhamasishaji kwa Wabunge kuanzia mwezi Mei mpaka Septemba, 2012. Semina hiyo itafanyika leo tarehe 20, kuanzia saa saba mchana hadi saa tisa alasiri katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Kwa hiyo, Wabunge wote, mnaombwa kuhudhuria hiyo semina bila kukosa kwa sababu mtakuwa na maelekezo ya kufanya kazi kule mnakokwenda.

HOJA ZA KAMATI

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, jana Wenyeviti waliwasilisha Taarifa zao hapa Mezani zikasomwa na nyingine zimewasilishwa asubuhi hii zikasomwa. Kamati zangu hizi zipo zaidi ya 15, kwa hiyo, siyo kweli kwamba, tunaweza kufanya hii kazi katika muda wa siku moja, leo na kesho.

Kwa hiyo, ningependa kusema hivi; Kamati zitakazohusika leo kwanza ni Kamati ya Nishati na Madini. Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini tumempa *priority* ya kuanza kwa sababu anayo safari ya kuondoka leo baada ya kuwasilisha Taarifa. Kamati nyingine zitakazohusika leo ni Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Kamati ya Miundombinu na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Tutashughulikia Kamati hizi nne tu. Kamati nyingine zote, tutakapoanza Kikao cha Bajeti, tutaanza na wao. Tutakuwa na muda kama wa siku mbili kushughulikia Taarifa za Kamati hizi nyingine zilizobaki. Kwa hiyo, mtakapokuwa mnajiandaa, mtajiandaa kwa Kamati ya Nishati na Madini, Kamati ya Fedha na Uchumi, Kamati ya Miundombinu na Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Kwanza Kabisa, nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini. Mtatumia nusu saa kuwasilisha Taarifa zenu; tutawasilisha zote kwa nusu saa nusu saa.

Kamati ya Nishati na Madini

MHE. JANUARY Y. MAKAMBA – MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wabunge wenzangu, Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Taarifa yetu ya shughuli za mwaka za Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 114 (15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, kwa niaba ya Wajumbe wenzangu, naomba kuwasilisha Taarifa ya shughuli ambazo Kamati ya Bunge ya Nishati na

20 APRILI, 2012

Madini imezifanya katika kipindi cha kuanzia Februari 2011 hadi Aprili 2012.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini uliowateua kwa mujibu wa Kanuni ya 113 (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, ambao kwa niaba yao nawasilisha Taarifa hii ni hawa wafuatao:-

Kwanza ni mimi Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla, Mheshimiwa Khalfan Hilaly Aesh, Mheshimiwa Abia Muhama Nyabakari, Mheshimiwa Charles Poul Mwijage, Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir, Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole Sendeka, Mheshimiwa Dkt. Festus Bulugu Limbu, Mheshimiwa Shafin Amedal Sumar, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagulla, Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mheshimiwa Suleiman Nchambis Suleiman, Mheshimiwa Kisyeri Werema Chambiri, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mheshimiwa Sarah Ali Msafiri, Mheshimiwa Munde Abdallah Tambwe, Mheshimiwa Vicky Kamata na Mheshimiwa John John Mnyika.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Nishati na Madini imepewa majukumu yafuatayo:-

- (i) Kushughulikia Bajeti za Wizara ya Nishati na Madini.
- (ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara hiyo.
- (iii) Kushughulikia Taarifa za kila mwaka za utendaji wa Wizara hiyo.
- (iv) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hiyo kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Februari 2011 hadi Aprili 2012, Kamati ilishughulikia mambo yafuatayo na ambayo tunayatolea taarifa na mapendekezo: Tatizo la Umeme Nchini; Biashara ya Nishati ya Mafuta; Sekta ya Madini; Sekta Ndogo ya Gesi; utafutaji wa Gesi na Mafuta; Bajeti ya Wizara; na utendaji wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, ulipoiunda Kamati hii, hapo mwezi Februari 2011, taifa lilikuwa kwenye tatizo kubwa la umeme. Bunge lako Tukufu litakiri na Watanzania kwa ujumla watakubali kwamba, Kamati imefanya kazi kubwa kuisukuma na kuisimamia Serikali kushughulikia tatizo la umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, mara tu baada ya Kamati kuundwa, ulitoa kibali kuiruhusu Kamati kuanza kazi mara moja kushughulikia tatizo la umeme. Kamati ilikaa na Wizara, TANESCO, Hazina, Shirikisho la wenye Viwanda (CTI), Mfuko wa Taifa wa Sekta Binafsi nchini (TPSF), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kuitisha mkutano wa wadau pale Karimjee Hall. Matokeo ya kazi hii yalikuwa ni mapendekezo 29 tuliyoyotoa, ambayo tuliamini yakitekelezwa, tatizo la umeme nchini litakwisha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka uliopita, Kamati imekutana na wadau karibu wote wa umeme nchini, imetembelea karibu vyanzo vyote na mitambo yote ya kuzalisha umeme na imekutana na TANESCO na Wizara mara kwa mara kufuatilia tatizo la umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi, hali ya umeme nchini bado siyo nzuri. Tatizo la umeme linasababisha kuongezeka kwa gharama za uzalishaji wa viwandani na hatimaye bei ya bidhaa zinazozalishwa zinaongezeka (*cost push inflation*). Aidha, kuongezeka kwa gharama ya uzalishaji wa bidhaa za ndani zinasababisha bidhaa zinazozalishwa nchini kushindwa kushindana na bidhaa za nje katika soko la ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia na Taasisi ya Jalbuena (2010), unaonesha kuwa mgao wa umeme unaigharimu Tanzania zaidi ya asilimia tano ya Pato la Taifa kwa mwaka. Kukosekana kwa umeme wa uhakika nchini kunaathiri uwekezaji ambapo uzalishaji husimama kwa wastani wa mara 63 kwa mwaka na kupunguza tija viwandani kwa asilimia sita.

Mheshimiwa Spika, mgawo wa umeme umeendelea kuathiri ukusanyaji wa mapato yatokanayo na kodi za ndani na ushuru wa forodha kwa kuwa matumizi ya teknolojia ya kompyuta (mfumo wa *Asycuda* na *ITAX*) katika jitihada za kuboresha ukusanyaji wa mapato zinategemea upatikanaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba, wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, mwezi Julai 2011, Serikali ililazimika kuiondoa bajeti hiyo kutokana na kutojumuisa mipango dhahiri na thabiti ya kumaliza tatizo la umeme nchini.

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, katika mkutano huo huo, Serikali ililazimika kuleta Mpango wa Dharura wa Umeme wenye awamu mbili; kuanzia Agosti hadi Disemba 2011, ambapo kiasi cha Megawati 572 zilitarajiwa kuzalishwa kwa gharama ya shilingi bilioni 523. Awamu ya pili kuanzia Januari 2012 hadi Disemba 2012, ambapo kiasi cha Megawati 310 zilitarajiwa kuzalishwa kwa gharama ya Dola za Kimarekani milioni 314.5 na Euro milioni 48.7.

Mheshimiwa Spika, kama Bunge lako lilivyoagiza, Kamati iliomba kuletewa na ilipatiwa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa dharura.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, katika kushughulikia tatizo la umeme nchini, ikiwemo kufuatilia utekelezaji wa mpango wa dharura, tumebaini mambo yafuatayo:-

(i) Bado tatizo la upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini halijaisha, licha ya nafuu ya muda iliyopatikana katika miezi ya Disemba hadi Februari.

(ii) Katika miezi ya hivi ya karibuni, kumekuwa na ongezeko kubwa la kuharibika mara kwa mara kwa transfoma na miundombinu mingine ya umeme, kutokana na uchakavu au ubora wake, jambo ambalo limechangia kukatika umeme mara kwa mara na kusababisha adha na usumbufu kwa watumiaji wa umeme.

(iii) Mpango wa Umeme wa Dharura haujatekelezwa kwa kasi na kiwango kama ilivyoahidiwa hapa Bungeni mwaka jana. Katika megawati 572 zilizoahidiwa kuzalishwa kati ya mwezi Agosti 2011 hadi Disemba 2011 ni megawati 342 tu ndizo zilizoweza kuzalishwa. Vilevile, fedha shilingi bilioni 408 ambazo Serikali iliahidi kuidhamini TANESCO kukopa kugharamia awamu hii ya kwanza ya mpango wa dharura, fedha ambazo ziliahidiwa na zilipaswa kupatikana kabla ya Disemba 2011, Mheshimiwa Spika, fedha hizi hazijapatikana hadi leo hii tunapokaribia mwishoni wa Aprili 2012.

(iv) Zipo tuhuma za rushwa na ufisadi kwenye ununuzi wa mafuta ya kuendesha mitambo ya dharura. Serikali imekiri kwamba, uchunguzi juu ya suala hili unafanyika hususan kwenye mafuta yanatotumika kuendesha mitambo ya IPTL. Kutokana na ufinyu wa muda, Kamati imeshindwa kukutana na wahusika wa suala hili na tunapenda kuahidi kuwa tutatafuta muda na kuwaita wahusika ili kushughulikia suala hili.

(v) Shirika la TANESCO lipo kwenye hali mbaya ya kifedha na kiuendeshaji. Hadi tarehe 10 Aprili, Shirika lilikuwa linadaiwa shilingi bilioni

296.8 na wadaiwa mbalimbali, ikiwemo makampuni yanayozalisha umeme wa dharura. Baadhi ya makampuni hayo, yamesimamisha mitambo yao kabisa kutokana na kutolipwa au kutokana na TANESCO kushindwa kununua mafuta ya kuiendesha. Ikumbukwe kwamba, licha ya kuzima mitambo hii, makampuni haya bado yanaendelea kudai *capacity charges*. Kuzimwa kwa mitambo hii, kunasababisha TANESCO kutumia zaidi maji kidogo yaliyopo kwenye mabwawa ya kufulia umeme. Hali hii inaliweka Taifa katika hatari ya kurudi kwenye mgawo mkubwa wa umeme wakati wa kiangazi, ikizingatiwa kwamba hadi kufikia tarehe 17 Aprili, kina cha maji katika Bwawa la Mtera kilikuwa kimefikia mita 691.37, ambacho ni mita 1.37 juu ya kiwango cha chini kabisa kinachoruhusiwa cha mita 690.

(vi) Kutokana na kuchelewa kwa mradi wa ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara, ipo hatari kwamba, katika kipindi cha zaidi ya miezi kumi na nane ijayo, Taifa litaendelea kutegemea kwa kiasi kikubwa umeme huu aghali unaozalishwa kwa kutumia mafuta.

(vii) Kutokana na kukabiliwa na hali mbaya ya kifedha, baadhi ya wagavi (*suppliers*) wa TANESCO wanatishia kusimamisha huduma mbalimbali kwa shirika hilo. Aidha, kutokana na kukosa fedha na kutumia fedha zote kulipia madeni na umeme wa dharura, Shirika linashindwa kufanya ukarabati wa uhakika wa mifumo na miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme na hivyo kuongeza tatizo la upatikanaji wa umeme hata pale kiwango cha uzalishaji kinapokuwa cha kutosheleza mahitaji. Vilevile, kutokana na uchakavu wa miundombinu, kiwango cha umeme kinachopotea njiani kinaongezeka hivyo kusababisha hasara kubwa kwa TANESCO kutokana na umeme unaonunuliwa kwa gharama kubwa kuishia kupotea njiani.

(viii) Licha ya kuongezewa bei ya umeme kwa asilimia 40.29, mapato ya TANESCO bado yameendelea kuwa madogo na hivyo Shirika limelazimika kufuta Miradi yote ya kuwaunganishia umeme wateja. Kama mnavyofahamu, lengo la Serikali ni kufikia walau asilimia 30 ya watu waliouganishiwa umeme itakapofika mwaka 2015.

(ix) Ili kufikia lengo hili, TANESCO walikadiria kwamba wangeweza kuwaunganishia umeme wateja wapatao 137,000 kwa mwezi kuanzia Machi 2012. Kutokana na hali hii mbaya ya kifedha na kiundeshaji ya Shirika, lengo hili halitaweza kufikiwa kwani TANESCO imeitaarifu Kamati kwamba inashindwa kulipia vifaa vya kutosha na kwa wakati.

(x) Kwa kifupi, Shirika kwa sasa linaelemewa na mzigo mkubwa na hali hii ikiendelea litashindwa kutimiza majukumu yake. Kama hali hii

haitarekebishwa haraka, ipo hatari nchi kuingia kwenye mgawo mkubwa wa umeme wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto katika upatikanaji wa umeme, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Pamoja na kwamba fedha za mkopo wa shilingi bilioni 408, karibu zote zitaingia kwenye kulipa madeni ya *TANESCO*, Serikali ikamilishe dhamana ya mkopo huo haraka iwezekanavyo, kama ilivyoahidi hapa Bungeni ili kulinusuru Shirika. Katika kutoa dhamana hiyo, maslahi ya Taifa yazingatiwe. Kwa maana ya masharti ya mikopo.

(ii) Vilevile Kamati inapendekeza kuwa uchunguzi wa Kibunge ufanyike kuhusu tuhuma za rushwa na ufiisadi kwenye ununuzi wa mafuta ya kuendeshea mitambo ya dharura.

(iii) Pamoja na kutegemea chanzo cha maji ambacho ni bei nafuu, Kamati inarudia tena ushauri iliutoa mara kwa mara huko nyuma kwamba, Serikali kuanzia sasa iwekeze kwenye vyanzo vingine vya kuzalisha umeme kama gesi, makaa ya mawe, urani, upepo na joto ardhi na jua.

(iv) Kutokana na transfoma nyingi kuungua na kupelekea maeneo mengi kukosa umeme mara kwa mara na kusababisha adha na usumbufu kwa watu, Kamati inashauri Serikali ilishughulikie tatizo hili haraka iwezekanavyo.

(a) *TANESCO* ihakikishe kwamba kuna akiba ya transfoma za kutosha nchini ili pindi kunapokuwa na hitilafu kusiwepo na muda mrefu wa kusubiri.

(b) *TANESCO* ihakikishe inanunua transfoma zenye ubora.

(c) *TANESCO* itoe taarifa kwa wananchi kuhusu matatizo ya miundombinu mibovu likiwemo tatizo sugu la kuungua transfoma ili wananchi waelewe tatizo halisi linalopelekea kukosa umeme. Hii itasaidia umma kuelewa kama ukosefu wa umeme unatokana na uwezo wa kuzalisha au mfumo wa usambazaji.

(d) *TANESCO* ianzishe ushirikishaji wa umma katika ulinzi wa miundombinu yake hasa transfoma na kwa siku zijazo teknolojia ya kutumia transfoma zisizo na mafuta itumike kama *TANESCO* ilivyoahidi.

(v) Serikali ihamasishe Sekta Binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa umeme kwa kuhakikisha inaweka vivutio.

(vi) Kwa kuzingatia unafuu wa bei ya umeme utakaozalishwa katika Mradi wa Umeme wa Maji wa Ruhudji (Megawati 358) na Kiwira (Megawati 400), Kamati inashauri *TANESCO* ndiyo iwekeze katika Miradi hiyo kwa kiwango kikubwa kuliko wawekezaji binafsi. Kamati inashauri Serikali ikope pesa za kutekeleza Miradi hii kwa kuzingatia vipaumbele ilivyojiwekea.

(vii) Kamati inarudia ushauri iliowahi kuutoa huko nyuma kwamba, Serikali iachane kabisa na utaratibu wa kukodi mitambo ya kuzalisha umeme. Uzoefu umeonesha mitambo ya kukodishwa kwa dharura ni ya gharama kubwa na matatizo kwa Taifa ikiwemo mikataba isiyofaa. Ili kuepuka ukosefu wa umeme siku za usoni kutokana na matatizo ukame au sababu nyingine, Kamati inashauri Serikali ijiandae kununua mitambo yake sasa kwa matumizi ya siku zijazo.

(viii) Serikali ianze kupitia upya mikataba ambayo imekuwa ni mzigo mkubwa kwa *TANESCO* na Taifa kwa ujumla.

(ix) Kwa kuwa Serikali imetumia muda mwingi na rasilimali nyingi katika kuandaa *Power System Master Plan*, Kamati inashauri Serikali katika mipango na bajeti zake izingatie mipango iliyomo kwenye *Power System Master Plan* hiyo ili kuweza kutekeleza kwa wakati miradi ya uzalishaji wa umeme na kuondokana na tatizo la mgawo wa mara kwa mara.

(x) Katika kukabiliana na upotevu wa umeme unaosababishwa na kuchakaa kwa miundombinu, Serikali itengeneze Mpango Maalum na itafute fedha za kutosha za kukarabati miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme.

(xi) Serikali ipunguze gharama za kuwaunganishia wananchi umeme ili wananchi wengi zaidi waweze kuunganishwa. Aidha, Serikali ipitie utaratibu wa sasa ambao wananchi wanagharamia wenyewe miundombinu ya umeme, zikiwemo nguzo, lakini miundombinu hiyo inabaki kumilikiwa na *TANESCO*. *TANESCO* itafute njia nzuri ya kuwarejeshea gharama zao sawia bila kuathiri ustawi wa *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, nishati ya mafuta jamii ya petroli ni nyenzo muhimu sana kwa uchumi na usalama wa nchi. Mafuta jamii ya petroli huchangia karibu asilimia 40 ya makusanyo ya ushuru na kodi inayokusanywa na *TRA*. Pamoja na umuhimu wake, Kamati imebaini

20 APRILI, 2012

kwamba biashara hii ina changamoto nyingi ambazo ni muhimu zikafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi tunachokitolea ripoti, Kamati ilifanya mikutano kadhaa na wadau wote wa mafuta nchini, ikiwemo *TIPPER, TPDC, TRA, TPA, EWURA, TBS, TAOMAC* (Chama cha Wafanyabiashara wa Mafuta) na Wizara, kujadili kwa kina kuhusu sekta hii muhimu nchini. Kamati pia ilipata fursa ya kutembelea Kampuni ya Hifadhi ya Mafuta TIPER Kigamboni, Eneo la Upakuaji Mafuta la Kurasini (KOJ), Ghala la Mafuta ya BP na kufanya ziara ya kushtukiza kwenye kituo cha kuuza mafuta huko Tabata eneo ambalo lilisemekana uchakachuzi wa mafuta unafanyika.

Kamati iliandaa taarifa ya kina ambayo iliwasilishwa Serikalini. Katika taarifa hiyo, Kamati ilieleza kwa kina na kutoa mapendekezo na ushauri katika masuala yanayohusu bei ya mafuta, miundombinu ya mafuta, ubora wa mafuta na mfumo wa uagizaji kwa wingi (*Bulk Procurement*).

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba Serikali iliamua kuanzisha Mfumo wa Uagizaji kwa Pamoja (*Bulk Procurement*) kama njia ya kupunguza bei ya mafuta na kudhibiti ubora wa mafuta na mapato ya Serikali. Wakati wa kuanzishwa kwa utaratibu huu, kulizuka mjadala mkubwa kuhusu utayari na manufaa ya mfumo huu ukizingatia hali ya sasa ya ufinyu wa miundombinu ya ushushaji na upokeaji mafuta.

Kulingana na Taarifa za *EWURA* na *PIC*, takwimu sahihi za uingizaji wa mafuta zimeanza kupatikana. Kutokana na takwimu hizo inaonesha kuwa, mara baada ya kuanzishwa kwa mfumo huu, kiwango cha mafuta yanayohitajika nchini ni kikubwa kuliko ilivyokuwa inaonekana awali. Kulingana na takwimu hizo, mwezi Novemba 2011 kiasi cha mafuta yaliyoingizwa nchini ni lita 212,094,130, wakati mwezi Februari 2012 ilikuwa lita 243,376,016. Hata hivyo, lipo kundi linalodai kuwa ongezeko hilo ni ishara ya makampuni kuwa na imani na mfumo wa Serikali kupanga bei chini ya mfumo wa uagizaji kwa wingi (*Bulk Procurement System*). Hoja hapa ni kuwa matatizo ya upangaji bei ya mwezi Agosti na Septemba yalipelekea makampuni mengi kusita kuagiza mafuta kwa wingi kwa ajili ya matumizi na hifadhi. Baada ya kuwa na uhakika wa kurudisha mtaji na kupata faida ndiyo sababu ya ongezeko la uagizaji. Kamati yetu inajipangia eneo hili kama sehemu ya kufuatilia kwa karibu.

Katika kipindi hiki cha uagizaji kwa wingi, miezi miwili iliyopita, Kamati imebaini manung'uniko makubwa miongoni mwa washiriki wa utaratibu huu na lawama dhidi ya *PIC* na kwa Kampuni iliyoshinda *tender*.

20 APRILI, 2012

Mnamo tarehe 16 Machi 2012, *EWURA* iliandika barua kwa *PIC* kushughulikia kero hizi. Mnamo tarehe 5 Aprili 2012, Chama cha Wafanyabiashara ya Mafuta Nchini (*TAOMAC*), kiliwasilisha malalamiko rasmi dhidi ya Kampuni ya Augusta Energy ambayo imeshinda *tender* hii mara tatu, kuhusu ubora wa mafuta yanayoingizwa nchini. Baada ya hapo kumekuwa na barua na *emails* za kushutumiana baina ya wadau wakuu wa sekta hii. Kwa kifupi, Kamati imebaini kwamba, hali ya mahusiano siyo nzuri na ikiachwa kuendelea hivi, nchi itaingia tena kwenye janga la uhaba wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia sekta hii, Kamati imebaini mambo kadhaa:-

(i) Serikali imeshindwa kutimiza ahadi yake ya kuanzisha Kampuni ya Taifa ya Biashara ya Mafuta *COPEC*. Kampuni imepatiwa leseni lakini haijawezeshwa kufanya biashara hiyo na hadi sasa haina ofisi wala watumishi.

(ii) Licha ya kuondoa msamaha wa kodi kwenye mafuta ya taa, tatizo la uchakachujaji wa mafuta bado linaendelea na sasa zimezuka mbinu mpya za uchakachujaji. *EWURA* bado inahitaji uwezo zaidi wa kusimamia suala hili. Vilevile, teknolojia ya vinasaba inayotumika sasa, pamoja na gharama yake kubwa, gharama ambayo inaenda kwa mlaji, haijaweza kuleta ufanisi unaotarajiwa.

(iii) Matarajio ya mfumo wa uagizaji kwa wingi (*Bulk Procurement system*) bado hayajafikiwa kwani bei ya mafuta kwa mlaji wa mwisho bado ipo juu. Pamoja na kudhoofu kwa shilingi na kupanda kwa bei ya mafuta katika Soko la Dunia, matumizi ya mfumo wa uagizaji kwa wingi hayajakidhi matarajio ya mlaji wa mwisho, yaani unafuu katika bei. Kamati imeitaka *EWURA* itoe vielelezo kwa tarakimu kuonesha kuwa kuna manufaa ambayo yamepatikana.

(iv) Miundombinu ya kushusha mafuta bado ni finyu hali ambayo haiwezi kuleta ufanisi katika uagizaji kwa wingi kama Kamati ilivyoshauri mwanzoni.

(v) Hakuna mahusiano na ushirikiano mzuri baina ya wadau wakuu wa katika shughuli za mafuta nchini. Mpaka sasa tunapotegemea uboreshaji wa miundombinu ulete ufanisi, hakuna makubaliano ya dhati na wazi kati ya *TPA*, Makampuni ya Mafuta na Serikali itakayoleta tija tegemewa.

(vi) Usimamizi na udhibiti wa sekta hii bado haujaimarika.

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu biashara ya mafuta:-

(i) Kanuni za Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (*Public Procurement System Regulations*) zipitiwe upya na kurekebisha vipengele vinavyoelekea kuzorotesha na kuleta upenyo wa malalamiko kwenye mfumo huu.

(ii) Muundo wa *PIC* uangaliwe upya, kwani hali iliyopo sasa Wanabodi wa *PIC* ni washiriki wa *tender* na wakati huo huo ndiyo waamuzi wa *tender* hizo za kuagiza mafuta, siyo sahihi na imeleta malalamiko mengi.

(iii) Hali ya mahusiano baina ya wadau kwenye sekta irekebishwe kwa sababu ina hatari ya kuathiri sekta nzima.

(iv) Kufuatia ongezeko la kodi katika mafuta ya taa ambalo kwa kiasi kikubwa limechangia katika kusitisha uchakachujaji wa mafuta, inapendekezwa matumizi ya vinasaba yasitishwe. Hii itasaidia kuokoa shilingi sita kwa kila lita ambayo inatozwa kwa mafuta yanayouzwa sokoni sasa. Aidha, tunashauri *TRA* kwa kushirikina na *EWURA* waanzishe mfumo wa kudhibiti mafuta yanayokwenda nchi jirani bila kuwasukumia gharama walaji wa nchini.

(v) Ili kuongeza ufanisi wa ushushaji mafuta kwa mahitaji ya sasa na baadaye kupitia Bandari ya Dar es Salaam, Serikali ihakikishe mfumo wa kushusha mafuta (*SBM*), ambao unapangwa kujengwa, unahusisha ujenzi wa matenki makubwa ya kupokelea na kuhifadhi mafuta kulingana na meli zinazotegemewa kutumika.

(vi) Makampuni ya mafuta pamoja na Mamlaka ya Bandari, chini ya Uongozi wa *EWURA*, watekeleze maelekezo ya kurekebisha mfumo wa kupokea na kuhifadhi mafuta ili kuweza kuleta ufanisi katika mpango wa uagizaji na ushushaji wa mafuta kwa wingi.

(vii) Ujenzi wa miundombinu hususan hifadhi na vituo vya kuuzia mafuta lazima vizingatie sheria za usalama na hifadhi ya mazingira.

(viii) *EWURA* na *TBS* wahakikishe mzabuni anayeleta mafuta kwa wingi anazingatia kuleta mafuta yenye viwango vya juu na hatua kali zichukuliwe pale itakapobainika ameleta mafuta yasiyokidhi viwango.

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilishughulikia kwa kina masuala yanayohusu Sekta ya Madini. Sekta hii imekuwa ikikua kwa kasi kwa miaka ya hivi karibuni. Kasi ambayo inahitaji usimamizi makini na thabiti ili nchi yetu inufaike. Kamati inakiri kuwepo kwa jitihada mbalimbali, lakini pia imebaini udhaifu kwenye usimamizi wa Sekta hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na rasilimali hii kubwa tuliyonayo, bado nchi haijanufaika ipasavyo kwani uchumi wa nchi hauendani na mapato yatokanayo na wingi wa madini tuliyonayo. Aidha, migogoro ya wawekezaji na wananchi imeendelea kuongezeka na hivyo kuhatarisha usalama wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanikiwa kutembelea migodi iliyopo Kanda ya Ziwa na maeneo ya wachimbaji wadogo yanayozunguka migodi hiyo. Migodi iliyotembelewa ni pamoja na Mgodu wa Dhahabu wa African Barrick North Mara – Nyamongo, Mgodu wa Dhahabu wa Geita (*Geita Gold Mine*) na Mgodu wa Almasi wa Williamson & Diamonds Ltd wa Shinyanga. Kamati pia ilikutana na wadau wote wa Sekta ya Madini nchini wakiwemo *TCME, TANSORT, STAMICO, GST, TMAA* na *TEITI*, kujadili kwa kina changamoto na fursa zilizopo kwenye Sekta hii.

Kamati pia ilifanya semina kuhusu Sera na Sheria za Madini na Nishati, pamoja na mkutano mahususi wa wadau wa urani nchini, ikiwemo makampuni yanayotafuta madini hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia Sekta hii, Kamati imebaini yafuatayo:-

(i) Kwa ujumla, mahusiano ya wananchi na wawekezaji siyo mazuri hasa katika migodi karibu yote, kutokana na wananchi kutotengewa maeneo ya kuchimba, kutokana na wananchi kutolipwa ama kutoridhika na fidia mara baada ya kuachia maeneo yao kwa ajili ya kupisha uwekezaji mkubwa.

(ii) Migodi ya Golden Pride, Geita, Tulawaka na Tanzanite One imeanza kulipa kodi ya mapato jambo ambalo ni jema.

(iii) Makampuni karibu yote yanayochimba madini hayajaanza kulipa mrabaha mpya wa asilimia nne.

(iv) Muunganiko kati ya Sekta ya Madini na Sekta nyingine za uchumi bado ni mdogo.

(v) Bado kuna malalamiko kwenye suala la utoaji leseni za utafutaji madini na zipo leseni nyingi zinazoshikiliwa na watu bila kufanyiwa kazi yoyote huku watu wengi wakiendelea kuomba leseni mbalimbali.

(vi) Hakuna mawasiliano na uratibu wa kutosha kati ya mamlaka ya kutoa leseni za madini na Serikali za Mitaa, hali inayosababisha migogoro ya umiliki wa maeneo kwani leseni hutolewa hata kwa maeneo ambayo tayari yanamilikiwa na watu au yana matumizi mengine ya kijamii kama mashule na zahanati.

(vii) Kutokana na elimu ndogo kwa umma kuhusu madini ya urani, kuna uelewa mdogo na hofu kubwa miongoni mwa wananchi kuhusu uchimbaji wa madini hayo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa madini katika nchi yetu, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Kampuni zote zinazochimba madini nchini zianze kulipa mrabaha uliokubaliwa kwa mujibu wa Sheria mpya ya Madini ya Mwaka 2010.

(ii) Kwa kuwa tayari kuna migodi ambayo imeanza kulipa kodi, ambayo inakwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina, mrabaha unaotokana na uchimbaji madini uingizwe kwenye Mfuko Maalum kwa ajili ya kujenga miradi mikubwa kama vile Vyuo Vikuu na miradi mikubwa ya maji ambayo wananchi wataweza kuiona na kuihusisha moja kwa moja na uvunaji wa rasilimali yao.

(iii) Kwa kuwa shughuli za uchimbaji wa madini zinahusisha kuwaondoa wakazi wa maeneo husika ili kupisha shughuli za uchimbaji, Serikali ihakikishe kwamba wakazi wanaohamishwa wanapewa fidia stahiki kabla shughuli za uchimbaji madini hazijaanza. Aidha, kwa nia ya kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo wanaokutwa katika maeneo hayo, Serikali iweke utaratibu utakaowezesha wachimbaji hao kunufaika.

(iv) Ili kuwaunga mkono wachimbaji wadogo wadogo nchini, Serikali ihakikishe inawatengea fedha za kutosha ambazo zitawawezesha kununua vifaa vya kisasa zaidi ambavyo ndiyo nyenzo muhimu katika shughuli yao.

(v) Kutokana na uchimbaji wa Madini ya Tanzanite kuwa unatofautiana na uchimbaji wa madini mengine, kwa maana ya jiolojia

ya kipekee ya madini hayo, Serikali itunge kanuni mahususi kwa ajili ya uchimbaji wa madini hayo.

(vi) Serikali ikague matumizi ya ajira ya watoto katika migodi ambao hujulikana kama nyoka na itoe adhabu kali kwa makampuni au watu wanaotumia watoto.

(vii) Serikali iandae mpango na mkakati maalum ambapo kabla ya madini kuchimbwa wananchi wataelimishwa juu ushiriki na manufaa ya migodi ili kujenga mahusiano mazuri kati ya wananchi na wawekezaji.

(viii) Kwa kuwa Watanzania wengi hawashiriki katika kutoa huduma za ugavi kwenye migodi na kwa kuwa huduma hii ina faida sana hasa katika kukua kwa Pato la Taifa, Kamati inashauri Serikali kwa kushirikiana na makampuni ya madini, ianzishe taasisi na mfuko maalum wa kutoa taarifa na mafunzo kwa wajasiriamali wazalendo kuhusu fursa zilizopo kwenye Sekta ya Madini na kuwawezesha kwa mikopo maalum kufikia viwango vinavyohitajiwa kutoa huduma hizo.

(ix) Serikali iongeze kasi ya kuipitia upya mikataba yote kwa maslahi ya Taifa na Bunge lipewe taarifa ya utekelezaji huo.

(x) Serikali iongeze kasi ya kushiriki katika umiliki wa Makampuni ya Madini badala ya kuwaachia wawekezaji kutoka nje pekee. Aidha, Serikali ihakikishe inasomesha wataalam wa kutosha ili waweze kusimamia madini ya vito hususan almasi ambayo yanahitaji utaalum wa kutosha kuweza kujua thamani yake.

(xi) Serikali ihakikishe inatoa elimu kwa wananchi kuhusu faida na madhara yatokanayo na uchimbaji wa madini ya urani kwani uelewa kwa wananchi ni mdogo na hofu kwao ni kubwa.

(xii) Serikali iwe na Jengo Maalum (*One stop Centre*) ambalo Wadau wa Sekta ya Madini watakutana kujielimisha, kuuza, kutunza na kununua madini mbalimbali yanayopatikana nchini Tanzania

(xiii) Serikali ianze kutekeleza Maazimio ya Bunge ya kutaka mikataba yote mikubwa na yenye maslahi kwa Taifa iwe inapitiwa na Bunge ili kuweza kujiridhisha kuwa maslahi ya Taifa yanazingatiwa.

(xiv) Mikataba yote inayoandaliwa lazima iainishe kifungu ambacho mfuko wa kurekebisha mazingira unaanza kulipwa tangu mgodi unapoanza kuzalisha badala ya kulipa wakati mgodi unafungwa.

(xv) Mikataba ya uchimbaji madini iwekewe kifungu ambapo rasilimali zote zinazoondosheka na zisizoondosheka zitahesabika kuwa ni rasilimali za nchi hii na endapo Kampuni inayochimba madini nchini itauzwa kokote duniani, mamlaka za Tanzania zipate kodi za mauzo (*Capital Gain Tax*) kulingana na thamani ya rasilimali zilizopo nchini.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia sekta ndogo ya gesi, tunazungumzia gesi ya Songo Songo na Mnazi Bay ambayo tayari inachimbwa na kutumika kuzalisha umeme na matumizi mengine. Aidha, taarifa hii haihusishi gesi nyingi iliyopatikana kwenye bahari ya kina kirefu. Eneo la Songo Songo linakadiriwa kuwa na akiba ya gesi yenye futi za ujazo trilioni mbili (2Tcf) na kati ya hizo, futi za ujazo zilizohibitishwa ni bilioni 880; Mnazi Bay ina futi za ujazo Trilioni 5 (5Tcf) na kati ya hizo, futi za ujazo zilizohibitishwa ni bilioni 262, ugunduzi wa bahari ya kina kirefu unakadiriwa kuwa na gesi futi za ujazo Trilioni 15 na kazi ya uchimbaji bado inaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa nyakati tofauti, Kamati ya Nishati na Madini imekuwa ikiifuatilia Sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. Katika vikao vilivyoanza tarehe 21 Machi - 1 Aprili, 2011, Kamati iliwasilisha taarifa yake iliyohusu masuala ya mafuta na gesi asili.

Kamati ilieleza kwa kina umuhimu wa gesi asili kwani ni sekta ambayo ilionekana kuwa na matatizo mengi na hivyo kuleta mashaka kwa ustawi wa Uchumi wa Taifa. Aidha, Kamati ilifanya kazi ya uchunguzi ili kufuatilia uendeshaji wa Sekta ndogo ya gesi nchini na tuliwasilisha taarifa yetu katika Mkutano wa Tano wa Bunge. Bunge lako Tukufu liliyapokea, kuyaridhia na kuyaazimia maoni 26. Katika Mkutano wa Sita wa Bunge, Serikali iliwasilisha Taarifa yake ya kwanza ya utekelezaji wa Maazimio hayo ambayo mengi bado utekelezaji wake unaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta hii ndogo ya gesi Kamati imebaini yafuatayo:-

(i) Shughuli za utafutaji na uchimbaji wa gesi zinaendelea kwa kasi nchini na mikataba mingi mipya inaendelea kusainiwa, wakati nchi haina Sera ya Gesi, Sheria ya Gesi, wala Mpango-Mkakati wa Uwekezaji na Matumizi ya Gesi; hali ambayo inaleta mashaka kwa Taifa.

(ii) Utekelezaji wa ujenzi wa bomba la gesi unachelewa sana, hali ambayo inahatarisha uhakika wa upatikanaji wa umeme nchini. Hadi sasa, mkopo wa ujenzi wa bomba hilo haujasainiwa. Kamati imeelezwa kwamba, moja ya sababu za kuchelewa kwa Mradi huu ni mashaka waliyoyapata Wachina kutokana na kampeni chafu iliyofanywa na

20 APRILI, 2012

Kampuni ya Pan-African Energy na SONGAS juu ya haja na umuhimu wa Mradi huu, ambao ulionekana na mwarubaini wa ukiritimba wa kampuni hiyo kwenye Sekta ya Gesi.

(iii) Bado ukiritimba katika Sekta ndogo ya gesi nchini unaendelea ambapo Kampuni moja ya Pan-African Energy ndiyo mwendeshaji na mwamuzi mkuu kuhusu uhakika wa upatikanaji na matumizi ya gesi inayotumika sasa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa nchi hainufaiki kama inavyopaswa kutokana na kuwepo kwa gesi inayopatikana katika maeneo ya Songo Songo na Mnazi Bay ikiwemo unafuu wa bei, uharaka wa upatikanaji wa gesi na kujenga uwezo kwa Watanzania katika uwekezaji na utaalumu katika masuala ya gesi. Licha ya kwamba, gesi ni maliasili muhimu kwa uchumi na usalama wa nchi, biashara na utaratibu mzima wa uchimbaji, usafishaji, usambazaji na uuzaji vyote vimehodhiwa na Sekta Binafsi ambapo bei hata ile anayouziwa TANESCO na maamuzi ya upatikanaji na usambazaji yameachwa sana kwa kampuni binafsi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uendeshaji wa Sekta ndogo ya gesi, Kamati inashauri:-

(i) Kwa kuwa utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sekta ndogo ya gesi umepelekwa kwenye *Government Negotiating Teams (GNT)*. Kamati inashauri kwamba utaratibu wa kuunda *GNT* kushughulikia masuala yaliyoainishwa wazi kwa mujibu wa mikataba na kwa sheria na kanuni za Serikali uangaliwe upya.

(ii) Serikali iingilie kati na kuondoa mkanganyiko uliopo kuhusu haki, majukumu na wajibu wa wadau mbalimbali ili nchi inufaiki na kuwepo kwa gesi nchini na uwekezaji wa miradi ya kuzalisha umeme kwa gesi uongezeke.

(iii) Kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli (*TPDC*) na Wizara ya Nishati na Madini, Serikali iweke mkakati maalum kuanzia sasa wa kuandaa kada ya wataalamu wa kusimamia Sekta hii muhimu.

(iv) Kutokana na faida kubwa inayoendana na shughuli hii, Serikali lazima ihakikishe inao uangalizi na usimamizi wa kina katika maeneo muhimu kama Mikataba (*PSA*), umiliki wa mabomba ya kusafirisha gesi/mafuta na mitambo ya kusafisha gesi.

(v) Kutokana na miradi ya majaribio ya matumizi ya gesi asili majumbani na kwenye magari iliyoendeshwa na *TPDC* kuonesha mafanikio, basi Serikali iwezeshe *TPDC* kupanua miradi hii na kuisimamia ili manufaa hayo yaonekane kwa jamii. *TPDC* iwezeshe kukopa ili kujenga mtandao wa usambazaji wa gesi kwenye viwanda na majumbani.

(vi) Ili kusimamia majukumu yaliyotajwa hapo juu kwa ufanisi, wakati umefika sasa wa Kampuni ya Taifa ya Gesi (*GASCO*) kuanza kazi zake ili isimamie majukumu hayo.

(vii) Kwa kuzingatia umuhimu wa nishati ya gesi kwa uchumi na usalama wa nchi, Serikali iharakishe ujenzi wa Bomba jipya la gesi.

(viii) Ili kuimarisha mahusiano na kuonesha manufaa ya rasilimali hii, Kamati inashauri mahali husika inapochimbwa gesi lazima wapewe mrabaha na gawiwo ambalo lipo wazi kimkataba. Aidha, wananchi wa maeneo hayo wawezeshwe ili waweze kutoa huduma za ugavi kwenye miradi husika.

(ix) Kutokana na kuwepo kwa maeneo mengi yenye utata ndani ya mikataba hii yanayosababisha migogoro na kuhatarisha maslahi ya nchi, Kamati inaishauri Serikali kuagiza wadau wote wanaohusika na mikataba hii kurekebisha vipengele vyenye utata ili kuleta ustawi wa sekta.

Mheshimiwa Spika, utafutaji wa gesi na mafuta; pamoja na kwamba nchi yetu imekuwa na gesi katika maeneo ya Songo Songo na Mnazi Bay kwa muda mrefu sasa, Taifa letu limeingia kwenye ramani ya nchi zenye hazina kubwa ya gesi duniani baada ya kupatikana kiasi kikubwa cha gesi kwenye bahari ya kina kirefu. Makampuni makubwa ya mafuta na gesi duniani tayari yapo nchini au yako mbioni kuja Tanzania. Kwa sasa kuna takriban makampuni 18 ambayo yamepewa leseni 26 za utafiti, utafutaji na uchimbaji wa gesi na mafuta nchi kavu na kwenye bahari ya kina kirefu.

Kamati ilipata fursa ya kufanya mkutano na Umoja wa Makampuni ya Mafuta na Gesi Tanzania (*OGAT*) na kutembelea eneo la uchimbaji wa gesi la bahari ya kina kirefu na kujionea jinsi shughuli za uchimbaji zinavyofanywa na Kampuni ya Petrobras ya Brazil.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa utafutaji wa gesi na mafuta Kamati imebaini yafuatayo:-

(i) Taifa bado halijajiandaa ipasavyo kiseru, kisheria, kitaasisi na kirasilimali watu kupokea na kunufaika na uwekezaji mkubwa unaotarajiwa kufanywa kutokana na upatikanaji wa gesi nyingi nchini. Kampuni ya British Gas, ambayo imepata kiasi kikubwa cha gesi, inatarajiwa kuwekeza kiasi cha kati ya dola bilioni 15 hadi 20 nchini kuanzia mwaka 2015, kama tutakuwa tupo tayari. Kampuni nyingine ya Statoil ya Norway, nayo inapanga uwekezaji mkubwa kama huo. Huu ni uwekezaji mkubwa kuwahi kufanyika katika historia ya nchi yetu na Afrika ya Mahshariki. Ni dhahiri yote haya yanategemea maandalizi yetu kama Taifa, siyo tu kupokea uwekezaji huu bali kunufaika nao.

(ii) Watanzania, ikiwemo Wabunge na Viongozi wengine, hawajapewa taarifa rasmi, kamili na sahihi kuhusu nini hasa kinaendelea, nini kimepatikana, tafsiri yake ni nini, manufaa yake ni yapi na maandalizi gani yanahitajika.

(iii) Mikataba mingi ya utafutaji na ugawanaji wa mapato (*PSA*) haijafanyiwa ukaguzi kwa kipindi kirefu, kama ambavyo sheria inahitaji. Kati ya mikataba 26 iliyopo ni mikataba minne tu ndiyo iliyofanyiwa ukaguzi. Kufanya ukaguzi wa mikataba ni muhimu sana, kwani hata udanganyifu na dhuluma iliyoonekana kwenye Mikataba wa Pan-African Energy uligundulika baada ya ukaguzi uliofanyika ukiwa umechelewa kwa miaka mitano.

(iv) Taifa halina wataalam wazalendo wa kutosha kuweza kushiriki na kuisimamia shughuli za utafiti, utafutaji na uchimbaji wa gesi na mafuta.

(v) Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*), ambalo ndilo msimamizi mkuu, mdhibiti mkuu na mbia wa uwekezaji huu kwa niaba ya Taifa, halijawezeshwa vya kutosha kifedha, utaalum, vifaa na kwa rasilimali watu kusimamia vizuri sekta hii kwa manufaa ya Taifa. Vilevile, muundo wa *TPDC* kwa sasa haukidhi mazingira haya mapya.

(vi) Serikali haijaweka dhahiri kama kuna mpango wowote wenye kusudi la kuwanda wananchi na Idara za Serikali kufuatia ujio wa chanzo kingine na kikubwa cha mapato kwa Taifa.

(vii) Maeneo ya utafutaji na uchimbaji mafuta katika nchi yetu yamepata mvuto kwa kasi baada ya uvumbuzi mkubwa wa gesi katika bahari ya kina kirefu upande wa Tanzania na Msumbiji. Hali hii inawavutia wawekezaji wenye uhakika waje kuwekeza katika nchi yetu kwa faida ya Taifa letu.

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu Utafutaji Gesi na Mafuta:-

(i) Serikali iandae mapema iwezekanavyo, Sera ya Gesi, Sheria ya Gesi na Mpango-Mkakati wa Gesi.

(ii) Serikali isimamishe kusaini mikataba mipya ya mafuta na gesi hadi Sheria mpya ya Gesi itakapopitishwa. Kwa kadiri mikataba mingi inavyosainiwa, Sheria itakayotungwa itakuwa haina shughuli ya kusimamia kwa sababu haiwezi kutumika *retrospectively*.

(iii) Serikali itoe fedha, kama jambo la dharura, kuwezesha kufanyika haraka ukaguzi wa mikataba ya utafutaji na uchimbaji mafuta kama mikataba inavyotaka kabla muda mrefu haujapita na kufanya kazi hiyo kuwa ngumu au kushindikana kabisa.

(iv) Mfumo wa fedha (*Fiscal Regime*) kwenye Sekta ya Gesi na Mafuta unategemea kiwango cha uhakika wa upatikanaji wa rasilimali hizo (*risk*). Tanzania sasa siyo nchi tena yenye uhakika mdogo katika utafutaji wa gesi. Kwa msingi huo, mfumo wa fedha katika utafutaji gesi ubadilishwe na baadhi ya vivutio, ikiwemo misamaha mingi ya kodi kwenye shughuli za utafutaji, iondolewe.

(v) Kufuatia ujio wa makampuni mengi ya Kimataifa yakiwinda kutafuta na kuchimba gesi nchini kwetu, Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa kwa kiasi cha hali ya juu shughuli za utengaji na ugawaji wa maeneo ya uchimbaji yanakuwa na uwazi na haki ya hali ya juu. Mfumo wa kutoa leseni uwe kwa zabuni na kampuni inayopata eneo itoe *signature bonus* (Kilemba) kwani mfumo huu unatumika katika nchi nyingi duniani.

(vi) Serikali iandae wataalam wa kutosha nchini watakaoweza Taifa kunufaika na fursa hii mpya. Fedha za mafunzo zinazotolewa na makampuni yenye leseni, ambazo zinazidi shilingi bilioni tatu kwa mwaka na ambazo zimekuwa zinatumiwa zaidi kwa safari, posho na semina, sasa ziwekwe kwenye akaunti maalum na Bodi ya Mfuko iundwe ili kila mwaka ichague vijana wa Kitanzania waliofanya vizuri mashuleni kwenda kusomea masuala ya gesi na mafuta katika nchi na vyo vilivyobobea katika masuala hayo.

(vii) Vyo vikuu na hasa vyo vya ufundi ikiwemo VETA Mtwara viimarishwe ili kuandaa wataalamu watakaoweza kutengeneza rasilimali watu inayohitajika katika Sekta hii muhimu.

(viii) Maeneo ambayo gesi na mafuta vinapatikana hapa nchini yawekewe mipango na mikakati maalum ya maendeleo ili wananchi wa maeneo hayo waone manufaa ya uwekezaji na washiriki kwenye kuilinda miundombinu ya gesi na mafuta, ikiwemo mabomba.

(ix) Katika mazingira haya ya sasa, Taifa linahitaji *TPDC* iliyo madhubuti. Kutokana na bajeti ndogo, uchache wa wafanyakazi na kutokana na haja ya kuomba kibali Utumishi kuajiri ambacho huchukua muda mrefu kupatikana, Shirika linashindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kuanzia mwaka ujao wa fedha, Shirika hili liruhusiwe kubakiza fedha yote (*retention*) na liruhusiwe kuajiri kwa kadri akidi na utaalum unavyohitajika bila kufuata mlolongo mrefu wa Utumishi. Aidha, Kamati inapenda kuona *TPDC* likiwa Shirika huru na lisiloingiliwa na Serikali kwa kuagizwa lifanye nini kila uchao.

(x) Muundo wa *TPDC* pia ubadilishwe. Shirika hili lina majukumu ya kutoa leseni, kushiriki kwenye uwekezaji wa uchimbaji wa mafuta na gesi (*upstream*), kudhibiti shughuli hizo, kushiriki kwenye biashara ya usambazaji na uzaji gesi na mafuta rejareja (*downstream*). Majukumu haya yanaingiliana. Iwepo *TPDC* Mdhubiti (*Regulator*), *TPDC* inayoshughulikia shughuli za biashara ya gesi (*GASCO*) na *TPDC* Mwekezaji kwa niaba ya Serikali kwani huwezi kuwa mdhibiti na kushiriki kwenye shughuli hiyo hiyo unayoidhibiti.

(x) Ipo hatari ambayo imekwishaonekana katika baadhi ya nchi zenye gesi na mafuta, kwa Serikali kutegemea kupita kiasi mapato ya gesi katika kujiendesha na wananchi kubweteka kwa mawazo kuwa nchi yao ina gesi/mafuta mengi. Mara rasilimali hizi zinapokwisha au kushuka bei, uchumi wa nchi huyumba na wananchi kukimbillia kufanya vurugu. Serikali lazima iendelee kuimarisha maeneo mengine ya uchumi kama kilimo, utalii na viwanda licha ya mapato makubwa yatakayokuwa yanapatikana kwenye gesi. Kamati inapendekeza kwamba, mapato yatakayopatikana kutokana na gesi na mafuta, yasitumike kabisa kwa matumizi ya kawaida ya Serikali kama mishahara, posho, vikao, magari, ruzuku mbalimbali na kadhalika (*consumption*), bali yawekewe matumizi maalum yanayolenga kuchochea sekta nyingine za maendeleo kama kilimo, umeme, viwanda, miundombinu, elimu, afya, maji na kadhalika.

(xi) Kutokana na eneo la nchi yetu sasa kuwa na mvuto kwa makampuni ya utafutaji na uchimbaji wa gesi na mafuta, Kamati inapendekeza *tender* za ugawaji wa maeneo ya utafutaji na uchimbaji zitakazotangazwa hivi karibuni ziwe na kifungu kinachoitaka Serikali kumiliki asilimia 12.5 ya hisa za kampuni yoyote itakayotafuta na kuchimba gesi katika eneo husika na hisa hizo zitolewe bure (*Free Carry Interest*).

(xii) Ujio wa makampuni haya uwekewe kifungu katika mikataba ambapo rasilimali zote zinazoondosheka na zisizoondosheka zitahesabika ni rasilimali katika nchi hii na endapo kampuni inayochimba gesi au mafuta nchini itauzwa kokote duniani, mamlaka za Tanzania zipate kodi za mauzo (*Capital Gain Tax*) kulingana na rasilimali zilizopo nchini. Aidha, Kamati inapendekeza kipengele hiki kihusishe sekta nyingine zinazohusisha Makampuni ya Kimataifa na kama Sheria Mama ni kikwazo basi Muswada Maalum uletwe Bungeni.

(xiii) Serikali, kwa kushirikiana na makampuni ya gesi na mafuta, ianzishe taasisi mahususi ya kutoa taarifa, mafunzo na uwezeshaji kwa makampuni ya kizalendo kuweza kushiriki na kunufaika na uchumi wa gesi kwa kutoa huduma na kufanya biashara katika maeneo ya bima, ujenzi, ulinzi, ukodishaji magari, huduma za vyakula na nyinginezo katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kwamba umeme ndiyo nguzo ya maendeleo ya nchi yetu na kwamba ni muhimu huduma hii ikasambazwa sehemu zote za nchini ili kujenga usawa katika kasi ya kupata maendeleo. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana kwa kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya, bado ni asilimia tatu tu ya Watanzania wanaoishi vijijini ndiyo wanaopata huduma hiyo ya umeme. Kiasi hiki ni kidogo sana. Kama Serikali inatumia mabilioni ya fedha kuhakikisha umeme unapatikana, kama tulivyoeleza hapo juu, basi ni lazima manufaa ya matumizi ya fedha hizi nyingi za umma yawe kwa wengi.

Mheshimiwa Spika, Kamati haijaridhishwa na kasi ndogo ya usambazaji wa umeme vijijini ikizingatiwa kuwa tuliongeza kodi kwenye mafuta ya taa kwa matarajio kuwa bilioni 50 zilizokuwa zinaibiwa kwa mwezi kwa mtindo wa uchakachujaji, sehemu kubwa ingepelekwaa REA ili kusambaza umeme kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na gharama kubwa na urasimu na ucheleweshaji mkubwa katika kuwaunganishia umeme wananchi majumbani na kwenye shughuli za biashara.

Mheshimiwa Spika, katika kuharakisha kasi ya usambazaji wa umeme vijijini, Kamati inapendekeza ifuatavyo:-

(i) Serikali itenge na kutoa fedha za kutosha ili REA iweze kufikisha umeme kwa wananchi wengi wa vijijini. Katika mwaka huu fedha, Serikali imetenga shilingi bilioni 104, kwa kuzingatia kiasi

kilichookolewa na zoezi la kudhibiti uchakachujaji kwa kuongeza kodi ya mafuta ya taa (Tsh 600 Bilioni) kwa mwaka, basi *REA* ingepewa angalau Shilingi bilioni 250.

(ii) Serikali iangalie vyanzo vipya vya fedha kwa ajili ya Miradi ya Umeme Vijijini. Pia Serikali itekeleze Azimio la Bunge na mpango wake wa kupata fedha za umeme vijijini kutoka kwenye matumizi ya simu za mikononi.

(iii) Ili kuleta manufaa na mwonekano wa haraka katika kusambaza umeme vijijini, Serikali ianze na maeneo ya huduma za umma ambazo zinawanufaisha wengi kama vile Shule, Vituo vya Afya, Zahanati na sehemu nyinginezo.

(iv) Kwa kuwa ajenda ya umeme vijijini ni ajenda itakayodumu kwa miaka zaidi ya 50 ijayo, Serikali iangalie uwezekano wa kuweka vivutio vya kuanzishwa kwa viwanda vingi zaidi vya kutengeneza bidhaa zinazotumika kwa usambazaji wa umeme. Vifaa hivyo ni kama nyaya, transfoma, Mita za LUKU na kadhalika. Kuendelea kuagiza nje ya nchi vifaa hivi ambavyo siyo vya teknolojia kubwa, kutaendelea kuchelewesha usambazaji wa umeme vijijini, kuongeza matumizi ya fedha za kigeni ambazo ni haba na hatimaye kuongeza gharama za kuunganisha umeme.

(v) Kamati inapendekeza maeneo ya umma kama shule, hospitali na zahanati gharama za uunganishaji umeme zibebwe na *REA*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Nishati na Madini ilijadili utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Wizaa ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011. Katika kujadili utekelezaji wa Mpango huo, ilionekana ya kuwa Wizara na Taasisi zake bado zinakumbana na changamoto ya kutengewa fedha kidogo ikilinganishwa na mahitaji yake. Aidha, fedha hizo zimekuwa zikichelewa kutolewa na mara nyingine hazitolewi zote na hivyo kuathiri utendaji na ufanisi wa kazi za Wizara.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilichambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 na kutoa maoni yake ili yazingatiwe hasa kuhusu ufinyu wa bajeti kwa Wizara hiyo hususan Sekta ya Nishati (Umeme), kama ambavyo maoni hayo yalivyowasilishwa katika taarifa yake Bungeni Julai 2011 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge.

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Serikali kwa kufanya *reallocation* na kuiongezea fedha bajeti ya Wizara. Hata hivyo, bado changamoto ya bajeti ndogo na ucheleweshwaji wa mafungu ya fedha kwa Wizara na Taasisi zake bado upo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inawashukuru wafadhili kwa moyo wao wa kuisaidia nchi yetu katika Sekta ya Nishati. Hata hivyo, kasi ya kupatikana kwa ahadi za fedha wanazotoa imekuwa ndogo. Jedwali hapa chini linaonesha hali hiyo.

AINA YA MATUMIZI	BAJETI	ZILIZOPOKELEWA	SALIO	%
Matumizi ya Kawaida	155,953,934,000/=	129,673,343,858/=	26,280,590,141/=	83.1
Miradi ya Maendeleo				
Fedha za ndani	293,423,391,000/=	266,612,000,000/=	26,811,390,999/=	90.8
Fedha za nje	89,136,746,000/=	11,361,245,783/=	77,775,500,217/=	12.7
JUMLA KUU	538,514,071,000/=	407,646,589,641/=	130,867,481,358/=	75.6

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilipata wasaa wa kupitia shughuli mbalimbali zinazofanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati na Madini. Taasisi ambazo Kamati ilipitia shughuli zake ni pamoja na *TANESCO, TPDC, REA, STAMICO, TMAA, EWURA* na *TEITI*.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*), lilianzishwa mwaka 1964 likiwa na jukumu kuu la kuzalisha au kufua, kusafirisha, kusambaza na kuuza umeme. *TANESCO* ndiyo kila kitu katika suala zima la umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jukumu kuu lililopewa *TANESCO* la kuhakikisha kuwa inazalisha au kufua, kusafirisha, kusambaza na kuuza umeme nchini, inashindwa kutimiza majukumu hayo kikamilifu kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo:-

(i) Ufinyu wa Bajeti unaosababisha Shirika lishindwe kutekeleza Miradi yake.

20 APRILI, 2012

(ii) Ukosefu wa umeme wa kutosha kutokana na Serikali kushindwa kuwekeza kwenye mitambo ya kuzalisha umeme kwa muda mrefu licha ya ukuaji wa mahitaji ya umeme nchini.

(iii) Uchakavu wa miundombinu unaosababisha umeme mwingi kupotea njiani na hivyo kupunguza kiwango cha umeme kinachowafikia wananchi.

(iv) Mabadiliko ya tabia nchi na ukame wa muda mrefu unaosababisha ukosefu wa mvua na hivyo kuathiri mitambo mingi ambayo ilikuwa inatumia maji na hivyo kujikuta nchi inaingia gharama kubwa katika kukodi mitambo ya dharura ambayo ni ghali kuiendesha na inatumia dizeli, mafuta ya ndege na mafuta mazito ambayo bei yake ipo juu katika Soko la Dunia.

(v) Wateja wengi zikiwemo Wizara na Taasisi nyingi za Serikali kutolipa ankara zao kwa wakati.

(vi) Mpangilio wa bei ya umeme ambapo mteja hulipa chini ya gharama halisi za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Maendeleo ya Petroli (*TPDC*) linajihusisha na kazi za msingi za utafiti, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asili nchini. Pia Shirika hili linalo jukumu la kusimamia shughuli za utafutaji na uchimbaji unaofanywa na makampuni mbalimbali ya uwekezaji. Kwa ujumla *TPDC* ndiyo msimamizi wa Sekta ya mafuta na gesi kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wake, *TPDC* imekuwa ikikumbana na changamoto zifuatazo:-

(i) Idadi ndogo ya wataalamu na watumishi.

(ii) Pamoja na uchache wa wataalamu, wengi wao wana umri mkubwa na wanastaafu wakati wowote kutoka sasa, hali ambayo itapelekea Taifa kukosa wataalamu ambao imetumia muda mwingi na gharama kubwa kuwaelimisha.

(iii) Bajeti ndogo, hali inayopelekea Shirika lishindwe kutekeleza majukumu yake muhimu kwa Taifa.

(iv) Utaratibu wa Serikali kuchukua mapato yote yanayotokana na gesi na kuwarejeshea asilimia 50 bila kujali umuhimu wa miradi waliyonayo na changamoto ya uendelezaji wa sekta.

(v) Ufinyu wa ofisi na mazingira yasiyofaa kwa kazi za mafuta katika Jengo la Mkapa Tower.

(vi) Pamoja na ujuzi na uzoefu katika Sekta ya Mafuta waliyonayo, *TPDC* hawahusishwi kikamilifu katika shughuli za uagizaji, uhifadhi na usambazaji wa mafuta jamii ya Petroli nchini.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) ana jukumu la kuwezesha, kuratibu na kuhamasisha uendelezaji wa Miradi ya Nishati bora vijijini ili ichangie ipasavyo katika ukuaji wa uchumi na hivyo kuboresha hali ya maisha ya wananchi. Tangu kuanzishwa kwake, *REA* imefanikiwa kutoa ruzuku kwa kwa ajili ya kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya mbalimbali nchini, kuhamasisha matumizi ya nishati bora vijijini na kujenga uwezo kwa waendelezaji wa Miradi ya Nishati vijijini. Pamoja na malengo mazuri ya kuanzishwa *REA*, bado changamoto kadhaa zimekuwa kikwazo katika utekelezaji wa majukumu yake. Baadhi ya changamoto wanazokumbana nazo ni pamoja na:-

(i) Ufinyu wa Bajeti, hali inayowafanya washindwe kusambaza umeme katika maeneo yote ya vijijini kwa upande mmoja na matumaini makubwa ya wananchi kuwa *REA* angewafikishia umeme watu wote kwa wakati mmoja.

(ii) Kuchelewa kutolewa fedha kwa wakati na kupata pungufu ya bajeti iliyopitishwa na Bunge.

(iii) Kasi ndogo ya utekelezaji wa Miradi ya Gridi (*Grid Extension*), ambayo imekwishapewa fedha za utekelezaji kutoka Mfuko wa Nishati Vijijini. Tatizo hili linatokana na mchakato wa ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa miundombinu ambao kwa mujibu wa kanuni za ununuzi huchukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (*EWURA*), inasimamiwa kiutawala na Wizara ya Maji na kiutendaji inasimamiwa na Wizara zote mbili kwa maana ya Wizara ya Maji na Wizara ya Nishati na Madini kupitia Sheria ya Umeme ya Mwaka 2008 na Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya *EWURA* ni pamoja na kutoa na kusimamia leseni, kuweka na kusimamia viwango vya ubora wa huduma zinazodhibitiwa, kudurusu na kusimamia bei kwa huduma zinazodhibitiwa na kutunga sheria ndogo au kanuni.

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwake *EWURA* imeweza kudhibiti upandaji holela wa bei za mafuta ya petroli kwa kutoa bei elekezi kila baada ya wiki mbili kuanzia mwaka 2009 na kudhibiti uchakachuzi wa bidhaa za mafuta.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, Kamati imebaini kwamba, *EWURA* inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Tabia mbovu ya uchakachuzi wa bidhaa za mafuta ina vivutio vingi na inafanyika katika eneo kubwa la nchi yetu.

(ii) Ukosefu wa miundombinu ya kutosha ya kupokelea mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam hali inayosababisha mrundikano wa meli bandarini na hivyo kusababisha bei kubwa kwa mtumiaji wa mwisho wa mafuta.

(iii) *EWURA* kutokuwa na ofisi mikoani hali inayofanywa washindwe kuwafikia wananchi.

(iv) Kupanda kwa bei ya mafuta kusikokoma katika Soko la Dunia kukiambatana na kudhoofu kwa Shilingi ya Tanzania.

(v) Kutokuwepo miundombinu ya kusafirisha bidhaa za mafuta kwa gharama nafuu nchini (reli, meli na mabomba), kunakosababisha bei kuwa kubwa kwa mlaji wa mwisho na kutoa fursa kwa wachakachuzi wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*), lilianzishwa kwa madhumuni ya kujihusisha na shughuli zote zinazohusu madini ambazo ni pamoja na utafutaji, uchunguzi, uchimbaji, uchenjuaji, utunzaji, usafirishaji, biashara na uongezaji thamani. Katika Sheria ya Madini iliyopitishwa Mwaka 2010, *STAMICO* imepewa jukumu la kuwa Msimamizi Mkuu wa Rasilimali ya Madini nchini.

Mheshimiwa Spika, tangu Shirika hili liondolewe katika Mashirika yaliyopangwa kubinafsishwa, *STAMICO* imetekeleza yafuatayo:-

(i) *STAMICO* imeingia ubia na Kampuni ya Tanzania Royalty Exploration Corporation Ltd ya Canada katika uendelezaji wa Mgodu wa Buckreef kwa hisa 45 kwa 55.

(ii) *STAMICO* imekamilisha utaratibu wa kuzichukua hisa asilimia 70 zilizokuwa zinamilikiwa na Tan Power Resources Ltd katika Mgodu wa Makaa ya Mawe Kiwira.

(iii) STAMICO imepewa leseni ya utafutaji wa madini katika Mgodu wa Buhemba.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba, *STAMICO* inakabiliwa na changamoto kuu ya ukosefu wa fedha hasa ikizingatiwa kuwa Shirika lilisimama kwa muda mrefu. Kwa kuwa tumefanya uamuzi wa kutoibinafsisha tena stamico basi Serikali iliwezeshe Shirika hili kuwa ndiyo mbia wa shughuli za madini kwa niaba ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Ukaguzi wa Almasi (*TANSORT*) kiliundwa mwaka 1966 na ofisi zake zilikuwa London hadi mwaka 2010 zilipohamishiwa nchini. Kitengo kina jukumu la kuchambua na kutathmini almasi zote nchini, kutetea na kupigania bei ya almasi nchini. Tangu kuanzishwa kwake, Kitengo kimesaidia kupandisha thamani ya almasi ya Tanzania, kuwa na wataalam wa viwango vya Kimataifa katika uchambuzi na uthamini wa almasi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba, *TANSORT* pia inakumbana na changamoto mbalimbali zifuatazo:-

(i) Usalama kutokana na thamani ya madini haya hivyo kuvutia wezi wengi na watu wasio waaminifu kujiingiza katika masuala ya utapeli.

(ii) Elimu duni kwa wazalishaji na imani potofu kuwa madini haya yanahusiana na nguvu za giza.

(iii) Ukosefu wa soko la ndani kwani hamna jengo au eneo maalum la kuuzia almasi. Nchi nyingine kuna jengo maalum na lenye ulinzi kutokana na thamani ya madini hayo.

(iv) Uhaba wa wataalam wa kutosha kusimamia kitengo hiki muhimu.

(v) Ukwepaji mkubwa wa ushuru na kodi za Serikali

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ukaguzi wa Madini (*TMAA*) ulianzishwa Novemba, 2009 kwa ajili ya uimarishaji, ufuatiliaji na ukaguzi wa shughuli za uchimbaji madini ili kuongeza maduhuli ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wake, Kamati imebaini kwamba, Wakala unakumbana na changamoto zifuatazo:-

20 APRILI, 2012

(i) Kushamiri kwa biashara haramu (magendo) ya madini nchini, hususan dhahabu na madini ya vito yanayozalishwa na wachimbaji wadogo na wa kati.

(ii) Ukosefu wa jengo la kudumu la Ofisi za Wakala

Mheshimiwa Spika, Tasnia ya Uziduaaji (*Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative - TEITI*) ni sehemu ya Asasi ya Kimataifa inayohamasisha Uwazi na Uwajibikaji katika mapato yatokanayo na Sekta za Madini, Gesi Asili na Mafuta. Utekelezaji wa *TEITI* unasaidia Vyama vya Kijamii, vyombo vya habari na jamii kwa ujumla kuhoji na kutathmini kiasi cha kodi na mrabaha kinacholipwa Serikalini na makampuni ya uwekezaji

Tangu kuanzishwa kwake, *TEITI* imefanikiwa kutoa taarifa yake moja ambayo inaonesha ulinganisho wa malipo ya kodi zilizolipwa na makampuni ya uwekezaji na mapato yaliyopokelewa na Serikali. Katika Taarifa hiyo kampuni zimeonesha kulipa jumla ya shilingi bilioni 174.9 wakati Serikali imeonesha kupokea jumla ya shilingi bilioni 128.4 na hivyo kuwepo tofauti kati ya malipo na mapato kiasi cha shilingi bilioni 46.5 kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yetu tumekuwa tukishirikiana na Watendaji wa Wizara ya Nishati na Madini na Taasisi zake kama *TANESCO, TPDC, EWURA, STAMICO, REA, GST, TEITI, TANSORT, TMAA* na *TIPER*. Kwa ujumla Kamati inayo maoni yafuatayo juu ya utendaji wa Wizara na Taasisi zake:-

(i) Wizara hii imekuwa inalaumiwa na Wananchi na Wabunge, hasa kutokana na tatizo la umeme na matatizo kwenye Sekta ya Madini. Hata hivyo, baadhi ya malalamiko haya yanatokana na kukosekana kwa taarifa sahihi na kwa wakati. Kutokana Wizara na Taasisi zake kutokuwa wepesi wa kuzungumza masuala yanayohusu sehemu zao za kazi, Kamati inashauri Idara za Mawasiliano ya Umma ziimarishwe na inapotokea jambo lenye maslahi kwa umma wawe wepesi wa kuyasemea kabla wananchi kulalamika.

(ii) Kamati imebaini mashirika mengi yaliyopo chini ya Wizara ya Nishati na Madini hayako huru katika utendaji yakionekana kama ni Idara badala ya kufanya kazi kama Mashirika. Pamoja na kuwa ipo haja ya kufanya kazi chini ya Wizara, Kamati inashauri Mashirika yapewe uhuru zaidi ili kuvutia uthubutu na ubunifu utakaopelekea ufanisi katika utendaji.

(iii) Wizara hii ina fursa nyingi ambazo zinaweza kutumika na watu wasio waaminifu kuliibia Taifa letu, lakini pia kuna vishawishi vingi vya rushwa. Kamati inapendekeza kwa Serikali kuchunguza mara kwa mara tuhuma zinapojitokeza na kuchukua hatua za haraka ili kujenga uaminifu wa wananchi kwamba Serikali inasimamia vizuri rasilimali zao.

(iv) Kamati imebaini Wizara ya Nishati na Madini na Taasisi zake zinakabiliwa na upungufu wa rasilimali ikiwemo rasilimali watu. Kutokana na fursa kubwa inayoangukia chini ya Wizara hii, Kamati inashauri Serikali itenge rasilimali za kutosha ili tuweze kuvuna na kusimamia rasilimali hizi muhimu.

(v) Kamati imebaini kuna mwingiliano wa kiutendaji na kiusimamizi katika kuendesha hifadhi ya mafuta ya *TIPER*. Kamati inashauri Wizara ya Nishati na Madini na Msajili wa Hazina wawe na mikakati ya pamoja itakayoweza Taifa kunufaika na hifadhi ya mafuta ya *TIPER*.

(vi) Kutokana na uhaba wa fedha unaoikabili *TPDC* unaoathiri utekelezaji wa miradi muhimu, Kamati inapendekeza *TPDC* iruhusiwe kubaki na fedha zote zinazotokana na mapato yake ya gesi.

(vii) Kamati inashauri kwamba Serikali ilete Bungeni haraka iwezekanavyo Sheria ya Uzidujaji (*TEITI*) kama ambavyo makubaliano ya kujiunga na taasisi hii yalivyoridhiwa kwenye Mkataba.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, napenda kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii ili kuweza kuwasilisha Taarifa ya Kamati. Aidha, nakupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu vizuri.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii pia kuwashukuru Mawaziri wafuatao; Mheshimiwa William M. Ngeleja (Mb), Waziri wa Nishati na Madini na Mheshimiwa Adam K. Malima (Mb), Naibu Waziri wa Nishati na Madini, kwa ushirikiano wao waliutoa kwa Kamati katika kipindi chote ilichokuwa kazini. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru pia Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Ndugu Eliakim Maswi na Watendaji wote wa Wizara za Nishati na Madini, kwa kuwa tayari kutoa ushirikiano pale ulipohitajika. Kamati inatumaini ushirikiano huo utaendelea katika kipindi kijacho.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, kwa ushirikiano anaonipa. Aidha, naomba

20 APRILI, 2012

kuwashukuru kwa dhati na kuwapongeza Wajumbe wa Kamati, kwa uvumilivu, busara na ushirikiano mzuri wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuipongeza Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge, Ndugu Thomas D. Kashililah, kwa ushirikiano anaoipa Kamati. Aidha, namshukuru Katibu wa Kamati hii, Ndugu Ndugu Pamela E. Pallangyo, kwa kuihudumia Kamati vizuri kwa kipindi chote na kuratibu kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwa Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati yetu imepata mwaliko kutoka Serikali ya Norway kwenda kujifunza masuala yanayohusu udhibiti wa mapato yanayotokana na gesi na mafuta. Kesho nitaongoza Ujumbe wa Wanakamati 11 kwa ajili ya shughuli hiyo na tunaahidi kwamba, Kamati yetu itatoa Uongozi thabiti kwa niaba yenu ili kuhakikisha nchi yetu inanufaika katika shughuli ya gesi na mafuta ambayo inakuja nchini na tutaleta taarifa ya safari yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba Bunge lako Tukufu lipokee mapendekezo yetu, kuyajadili na kuyaridhia kama maazimio. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. YUSUPH A. NASSOR: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA – MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na. 114 (15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Fedha na Uchumi kwa kipindi cha Aprili 2011 hadi Aprili 2012.

Mheshimiwa Spika, katika kutimiza majukumu yake, Kamati hii inahusika kikamilifu katika kutekeleza majukumu ya msingi yafuatayo:-

(i) Kusimamia shughuli zote zinazohusu masuala ya fedha na ukuaji wa uchumi, unaofanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji na Uwezeshaji), Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango.

(ii) Kushughulikia Bajeti za Wizara ya Fedha, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji na Uwezeshaji) na Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu).

20 APRILI, 2012

(iii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge ambayo chanzo chake ni Wizara hizi.

(iv) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizi kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(b) ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeendelea kutoa michango, ushauri, mapendekezo na maelezo ambayo Serikali imekuwa ikiyazingatia katika kuboresha utekelezaji wa majukumu yake ya kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera na Mikakati ya Uchumi; kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani na nje na matumizi ya Serikali; utekelezaji wa MKUKUTA; Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na kupanga Mipango ya Maendeleo kupitia Tume ya Mipango; kusimamia Sheria, Kanuni na Taratibu za Uhasibu na Manunuzi ya Umma; na usimamizi wa mali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha utekelezaji cha mwaka mzima, Kamati ilitekeleza majukumu yake ya ujumla kama ifuatavyo:-

(a) Ilijadili na kuchambua Taarifa ya Serikali kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2010 na Mwelekeo katika kipindi cha muda wa kati (2010/2011 - 2012/2013) na makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2011/2012.

(b) Ilijadili na kutoa ushauri kuhusu Mwongozo wa Utayarishaji na Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012 na 2012/2013.

(c) Ilijadili utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji na Uwezeshaji), Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu), Tume ya Mipango, Wizara ya Fedha kwa Mwaka 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2011/2012.

(d) Ilichambua na kujadili taarifa mbalimbali zilizohusu uboreshaji wa Uchumi wa Nchi, uwezeshaji na uwekezaji, zilizowasilishwa na Wizara husika.

(e) Ilijadili utendaji kazi wa Taasisi na Mashirika mbalimbali yaliyo chini ya Wizara husika.

(f) Ilijadili Miswada na Maazimio mbalimbali yaliyohusu masuala ya fedha na uchumi na kuwasilisha taarifa zake Bungeni.

20 APRILI, 2012

(g) Ilifanya ziara mbalimbali kuangalia shughuli za kukuza uchumi na kuboresha uchumi katika mikoa mbalimbali na imewasilisha mapendekezo yake katika taarifa hii.

(h) Ilishiriki semina na warsha mbalimbali ambazo zimesaidia kuongeza ufahamu na upeo kwa Wajumbe kuweza kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya msingi yanayohitaji utekelezaji wa haraka kwa Serikali: Tunapoangalia maendeleo ya Uchumi wa Nchi yetu, kipimo kikubwa ni kuangalia jinsi Uchumi Jumla (*Macro-Economy*), unavyofanya kazi kwa mwingiliano na Uchumi Mdogo (*Micro-Economy*). Kwa mantinki hii, utulivu wa Uchumi Jumla (*macro-economic stability*) ndiyo kigezo kikubwa cha kujua hali ya uchumi wa nchi ikoje. Uchumi jumla unajengeka chini ya msingi, ifuatayo: Kwanza, viwango vya bei ambavyo vina-*determine* mfumko wa bei; pili, biashara ya nje ambayo *hu-determine* viwango vya thamani ya kubadilisha fedha yetu (*exchange rate*); tatu, fursa za ajira kupitia mikakati ya uwekezaji (*employment and investment*); nne, Mapato na Matumizi ya Serikali; tano, uwiano wa malipo yetu nje (*balance of payments*); na hatimaye sita ni kukua kwa Uchumi wetu (*GDP Growth Rate*).

Mheshimiwa Spika, vichocheo vikubwa vya kuimarisha misingi ya Uchumi Jumla ni Sera za Kifedha zinazojumuisha viwango vya riba na kadhalika na Sera za Kodi zinazojumuisha aina za kodi zinazotowazwa, Bajeti za Serikali Kuu na Mitaa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi tulichonacho sasa, Hali ya Uchumi wa Nchi yetu ni dhaifu na haijatengemaa vizuri. Tatizo la mfumko wa bei ni kubwa kufikia kiwango cha asilimia 20 na kasi yake ya kupungua bado ni ndogo. Bado lipo tatizo la uwiano kati ya mapato na matumizi ya Serikali na uwezo mdogo wa mauzo yetu nje kukidhi mahitaji yetu ya fedha za kigeni. Hivi sasa mauzo nje yanakidhi asilimia 60 tu ya mahitaji ya fedha za Kigeni.

Mheshimiwa Spika, inawezekana zikawepo sababu nyingi zinazopelekea uchumi jumla kutokuwa tulivu, lakini Kamati imebaini kuwa, lipo vile vile tatizo kubwa la usimamizi na uendeshaji hafifu wa uchumi (*economic mis-management*). Kwa hiyo, Taarifa ya Kamati imejikita katika eneo la nini kifanyike ili kuboresha hali ilivyo sasa na kuwa bora.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu, Uchumi wa Tanzania umeendelea kukua. Mwaka 2010, Pato halisi la Taifa lilikua kwa kiwango cha asilimia 7.0 ikilinganishwa na asilimia 6.0 mwaka 2009. Katika kipindi

cha robo mwaka wa 2011 (January - Septemba), Pato la Taifa limekua kwa asilimia 6.3 ukilinganisha na asilimia 7.0 kwa mwaka uliopita na limechangiwa na Sekta ya Utaaji Huduma (asilimia 8.0), Sekta ya Viwanda na Ujenzi (asilimia 8.7), Sekta ya Uvuvi asilimia 4.1 na Sekta ya Kilimo (asilimia 4.0). Ukuaji huu wa uchumi bado haujasaidia kuondoa umaskini wa kipato kwa wananchi kwa kuwa sekta zinazochangia zaidi kwenye ukuaji wa Pato la Taifa zinahusisha idadi ya watu wachache. Sekta ya Kilimo ambayo inahusisha idadi kubwa ya Watanzania imeendelea kukua pole pole. Kilimo inawahusisha (asilimia 73.7 ya watu wote), yaani Wananchi takriban 32,000,000 wanaoishi Vijijini. Sekta ya Uvuvi nayo imekua kwa asilimia moja tu, licha ya fedha nyingi kuelekezwa huko kupitia programu mbalimbali kama vile *MANCEP* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, siyo jambo geni hivi sasa kusikia wananchi wengi wakiuliza kukua kwa uchumi maana yake ni nini, wakati hali ya maisha inaendelea kuwa ngumu. Kamati inaitanabahisha Serikali kuwa, pamoja na kupata mafanikio katika kukuza uchumi (*economic growth*), bado ukuaji huo haujatengeneza ajira ya kutosha wala kupunguza umaskini hasa wa Kipato. Uchumi wa Vijijini haujakua na takwimu zinaonesha hivyo kwa muda wa miaka kadhaa iliyopita. Pamoja na kukua kwa uchumi, Mipango na Bajeti zetu ni lazima sasa zielekezwe kutegua kitendawili (*paradox*) hiki na lazima zijibu changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sasa tukajielekeza kwenye maendeleo ya Uchumi Vijijini hasa tukilenga kuboresha Kilimo na Miundombinu ya vijijini ili isaidie Kilimo. Programu za kupeleka umeme Vijijini, kujenga barabara Vijijini, kuboresha upatikanaji wa maji Vijijini, upatikanaji wa huduma za fedha (Mikopo na Akiba), upatikanaji wa pembejeo za kutosha na kadhalika, zitasaidia kukuza Kilimo kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi kutekeleza hatua zifuatazo:-

(i) Upungufu uliobainishwa katika Mkakati/Programu ya KILIMO KWANZA urekebishwe na kutekelezwa mapema hasa huu ufuatao: Kilimo kiwe cha Kisayansi; Serikali iongeze Bajeti ya Kilimo; kuboresha *Contract Farming System (CFS)*; kuanzisha Vivutio vya Sera na Sheria ili kukuza uwekezaji kwenye kilimo, kama kupunguza *Corporate Tax* kwa Makampuni yanayowekeza vijijini ili kuboresha kilimo; kuharakisha kutenga Ardhi kwa ajili ya kilimo kila Wilaya; kuboresha mfumo wa masoko ya mazao ya kilimo na taarifa zake; kuwezesha mtaji wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (*NFRA*) ili wakala awe na fedha ya kutosha kununua mazao; na kuboresha miundombinu (barabara) maeneo ya uzalishaji yote.

(ii) Uanzishaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) uharakishwe na uwe na mtaji wa kutosha.

(iii) Kodi ya mafuta kwa matumizi ya kilimo, kwa mfano, utayarishaji wa ardhi, umwagiliaji, usindikaji ipunguzwe kutoka asilimia 20 ya hivi sasa mpaka asilimia 10. Punguzo hili litachochea Wawekezaji kwenye Sekta ya Kilimo.

(iv) Kodi kwenye vifungashio vya mazao ya Kilimo iondolewe.

(v) Kodi kwenye vifaa vya umwagiliaji na vipuri vyake visitozwe, kodi mfano, kilimo cha mazao ya chakula, chai, miwa, mboga, matunda na kadhalika. Pili, kutokana na utitiri wa kodi nyingi zinazotozwa na kuathiri tija ya uzalishaji katika Sekta mbalimbali za Uchumi, Serikali ibadilishe mfumo wa kodi kwa kufanya marekebisho makubwa ya Mfumo wa Kodi (*Major Tax Structure Reform*) kwa kuiga mfano wa Nchi ya Mauritius na Brazil.

(vi) Kuwa na Sera thabiti na ya uwazi kuhusu uuzaji wa chakula nje ya nchi. Ili kuepusha wakulima wasibabaishwe na msimamo wa Serikali, Serikali iweke sera ya wazi inayoruhusu Wakulima kuuza mazao nje ya nchi. Hata hivyo, Serikali ijandae mapema kununua mazao ya wakulima kwa bei ya soko na kinachobaki ndicho kitakuwa kwa ajili ya kuuza nje ya nchi.

(vii) Kuwepo sera zinazotabirika kwa ajili ya uwekezaji endelevu. Sera zinazohusu uwekezaji katika Sekta ya Kilimo zisiwe zinabadilika mara kwa mara. Kama Sera zinabadilika kila mwaka humfanya mwekezaji yeyote yule kushindwa kuweka mipango yake ya muda mrefu.

(viii) Kujenga uwezo wa sekta binafsi kitaaluma, kimuundo na kifedha kwa kutenga mfuko maalumu. Kamati inasisitiza Serikali isaidie kuboresha upatikanaji wa Mikopo kupitia Vyama vya Ushirika, SACCOS, VIKOBA na vikundi vingine vya uzalishaji.

(ix) Kulinda mazao yanayotoa mafuta ya kula. Tanzania inaagiza kutoka nje mafuta ya kula nchini takriban tani 300,000 kwa mwaka. Hii ni sawa na asimilia 55 ya mafuta yote tunayotumia. Kwa hiyo, tunatumia fedha nyingi za Kigeni kuingiza bidhaa hii wakati nchi hii tunalima mazao ya Alizeti, Pamba, Karanga, Mawese na kadhalika, ambayo ni vyanzo vikubwa vya mafuta ya kula. Serikali itoze ushuru mkubwa mafuta yanayotoka nje ili mafuta yetu yashindane kwa bei na yanunulike.

20 APRILI, 2012

(x) Serikali iweke msisitizo wa uanzilishaji wa viwanda vya usindikaji wa mazao ya kilimo (*Agro-Based Processing Industries*) na ihamasishe watu binafsi kupitia Sheria na Programu ya *Public Private Partnership (PPP)*.

(xi) Uanzishwe utaratibu wa zamani wa kutoa motisha kwa wakulima wazuri toka kila Kata, Wilaya na Mkoa. Utaratibu huu utahamasisha ushindani katika kilimo na hivyo kuwa kichocheo cha uzalishaji.

(xii) Serikali iimaarishe miundombinu (barabara) kwenye maeneo yote yanayozalisha chakula kingi ambacho kinategemewa na Taifa na soko la nje ya nchi.

(xiii) Serikali ibuni na iweke Sera na Mkakati wa Uwezeshaji inayolenga kundi la vijana nchini ili wavutiwe na shughuli za Kilimo.

Mheshimiwa Spika, Takwimu zinaonesha kuwa mfumko wa bei umekuwa ukiongezeka kutoka asilimia 13.0 mwezi Julai 2011 hadi asilimia 16.8 mwezi Septemba, 2011 na kuendelea kuongezeka hadi kufikia asilimia 19.8 mwezi Desemba 2011. Ongezeko la bei nchini lilichangiwa na mambo kadhaa yakiwemo; kuporomoka kwa thamani ya shilingi, kupanda kwa bei ya mafuta, upungufu wa nishati ya umeme, uwepo wa ukame katika baadhi ya maeneo ya nchi na kupanda kwa bei ya bidhaa za vyakula. Mfumko wa Bei za vyakula umechangia mfumko wa bei kwa kasi kubwa kwa asilimia 14.8 mwezi Julai hadi kufikia asilimia 24.7 mwezi Novemba 2011. Bei ya mchele imekua kwa asilimia 50, sukari asilimia 50, nyama asilimia 30 na Samaki kwa takriban asilimia 40.

Mheshimiwa Spika, Kamati imekuwa ikipata maelezo kuwa mfumko wa bei unatokana na sababu zilizo nje ya uwezo wetu; kwa mfano, bei za mafuta, viwango vya mfumko wa bei na nchi jirani na kadhalika. Hata hivyo, maeneo yote haya yanachangia takriban asilimia 30 tu ya mfumko, wakati asilimia 70 inatokana na kupanda kwa bei ya vyakula. Je, hili nalo haliwezi kudhibitiwa na Uchumi wetu? Ushauri wa Kamati kwa Serikali ni huu ufuatao:-

(a) Ijiweke na iwe tayari (*preparedness*) katika programu zake za kuhakikisha kuwa chakula kinasambazwa kutoka kwenye maeneo ya ziada ya chakula kama vile Ruvuma, Rukwa na kadhalika kwenda kwenye maeneo yenye upungufu kwa wakati. Pia hatua hii itapunguza *economic waste* katika uchumi wetu.

(b) Katika kutekeleza hili Serikali iimarisha mipango yake ya Hifadhi ya Chakula na ielewe kuwa suala la usalama wa chakula halisimamiwi na wakulima bali ni la Serikali. Wakulima wakishavuna mazao yao waachwe huru wauze katika soko lolote pamoja na Hifadhi ya Taifa kulingana na bei za soko zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imekuwa ikiisitiza sana Serikali kupambana na changamoto ya kupunguza hali ngumu ya maisha inayowapata Wananchi, kutokana na kupanda gharama za maisha zinazokabili hata mahitaji muhimu ya kila siku (*basic necessities*). Ushahidi ni ushauri toka Kamati kwa Serikali kupunguza tozo za mafuta ili kupunguza ughali wa maisha.

(c) Usambazaji wa pembejeo ufuatane na misimu ya kupanda na ufanyike kwa wakati.

(d) Kodi zinazotowwa kwenye mahitaji muhimu kwa mfano vyakula kama vile mchele, unga na sukari zifutwe, kupunguza ughali wa bidhaa hizi muhimu. Sukari Kiwandani Kilombero huuzwa Sh.1,300 ambapo pamoja na VAT bei ya Sukari inakuwa Sh. 1,534 na hadi ifike kwa mlaji inauzwa kwa Shilingi 2,200 hadi 2,500 kwa kilo. Gharama hizi hazihimiliki.

(e) Upo utitiri mwingi wa kodi ambao umeathiri viwango vya uzalishaji katika kilimo na uzalishaji Viwandani. Vilevile hata kuathiri mikakati ya kulinda viwanda vyetu vya usindikaji wa mazao ya kilimo kwa mfano mafuta ya kula, maziwa na kadhalika. Serikali ichukue hatua za makusudi za kupunguza kodi hizi zinazotowwa kwenye mazao na bidhaa za kilimo kama vile kodi ya mazao, kodi ya ardhi, kodi za vifungashio, ushuru wa forodha asilimia 20 na VAT ya asilimia 18 inayotowwa kwenye mbegu na miche zinazoagizwa kutoka nchi za nje. Hatua hii itaongeza tija na ufanisi katika uzalishaji kwenye Sekta hizi muhimu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza Serikali kuendelea kusimamia ipasavyo bei ya mafuta ikiwemo kupunguza tozo zilizopo katika bei za mafuta ili kupunguza gharama za uzalishaji Viwandani na gharama za usafirishaji. Aidha, ununuzi wa mafuta wa jumla (*bulk procurement*) usimamiwe kikamilifu ili kuleta ahueni kwenye bei ya mafuta. Kamati inashauri Serikali kubadilisha utaratibu wa kumiliki *SBM* na *KOJ*, kwa maana miundombinu yote ya uingizaji mafuta iliyopo Baharini iwe chini ya Mamlaka ya Bandari (*TPA*). Mabomba yanayoleta mafuta chini ya bahari yanamilikiwa na *TPA* hadi nchi kavu hadi kwenye matanki ya mafuta na yale ya nchi kavu hadi kwenye matanki ya mafuta yanamilikiwa na *TIPPER*. Mabomba yote haya yanahitaji ukarabati

mkubwa ili kufanya huduma ziwe za kisasa pamoja na kupokea mzigo mkubwa wa mafuta. Hivi sasa *TIPPER* inauza hisa zake asilimia 50. Serikali inunue hisa zote hizo ili suala la kuagiza na kupokea mafuta (*bulk procurement*) liwe chini ya Serikali moja kwa moja. Hatua hii itapunguza gharama za mafuta, itaongeza usalama wa kuwepo mafuta nchini na *TIPPER* sasa itakuwa ni Hifadhi ya Taifa hata kwa matumizi ya Nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, mfumko wa bei umedumu kwa muda mrefu sasa (*persistent inflation*), hivyo kuleta hisia kuwa Sera za Kifedha (*Monetary Policies*) na zile za Kodi (*Fiscal Policies*) zimeshindwa kutatua tatizo hili na kuufanya mfumko huu uwe sugu (*stagflation*). Kamati inaishauri Serikali ichukue changamoto hii kwa kuifanyia kazi kwa haraka ili uchumi wa nchi uwe tulivu.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha makusanyo ya ndani kwa kipindi cha mwaka 2010/11 yamefikia Shilingi 5,698.5 bilioni wakati matumizi yalifikia Shilingi 10,202.6 bilioni katika kipindi hicho. Matumizi ya kawaida yalikuwa Shilingi 7453.6 bilioni na yale ya maendeleo yalikuwa shilingi 2749 bilioni. Uwiano huu unaonesha wazi kuwa Serikali ina matumizi makubwa, zaidi ya takriban ya mara mbili ya makusanyo. Hali hii inaonesha kuwa uchumi wetu unakula zaidi badala ya kuzalisha (*net consumer economy nation*). Mwelekeo huu ni kikwazo katika jitihada za kuzalisha na kukuza Uchumi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii Kamati inaishauri tena Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Ipanue wigo wa kukusanya kodi ili ongeze mapato kupitia sekta isiyo rasmi, kurekebisha Sheria ili kuzifanya Wakala wa Serikali (*Executive Agencies*) kupitisha fedha zao katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Ingawa Serikali iliamua kuondokana na utaratibu wa Mashirika ya Umma, utaratibu huu unajirudia tena kwa mlango wa nyuma. Serikali ianze mara moja utaratibu wa kutoza kodi Kampuni zote za simu ambazo hivi sasa kwa ujumla wake zinahudumia Wateja takriban 22,000,0000 nchi nzima. Serikali iimarisha utaratibu wa kutoza kodi za majengo (*property tax*) hasa ikizingatiwa kuwa sasa kuna mwamko mkubwa wa ujenzi wa nyumba hasa mjini na bado Serikali haijaweka mfumo mzima wa usimamizi wa ujenzi huo.

(b) Serikali ichukue haraka hatua za kupunguza matumizi makubwa yanayoweza kuepukika (*cost cutting measures*). Katika eneo hili, matumizi makubwa yatofautishwe na matumizi mabaya yanayoambatana na ubadhirifu na wizi. Tukijenga shule nyingi tutahitaji walimu; tukijenga Zahanati nyingi tutahitaji dawa nyingi na kadhalika; ipo

haja kwa Serikali kudhibiti matumizi mabaya na ufujaji wa fedha ili kuzingatia dhana ya thamani ya fedha (*value for money*) inavyotumika na matokeo yake. Kamati inasisitiza sasa Serikali kuanza utekelezaji wa hatua hii.

(c) Ipo haja kwa Serikali kutumia sasa Sheria mpya ya Madini ikijumuisha mapendekezo ya Tume ya Bomani ili kupata mapato mengi kutokana na shughuli za madini. Tokea Mwaka 2007 hatujawa na Miradi mipya ya Madini na Sheria Mpya ya Madini hadi sasa bado haijatumika. Hakuna Mgodji wowote unaofanya kazi chini ya utaratibu wa Sheria Mpya. Wakati umefika sasa wa kutumia Sheria hii ili kuongeza mapato ya nchi. Miradi iliyomaliza Mikataba ya awali iingie kwenye Sheria Mpya ili Serikali ipate takriban asilimia 15 – 20 ya Mapato ya Madini. Miradi mipya ya Mgodji wa *Barrick*, kwa mfano na ule wa Nyanzaga ambao utajiri watu 3,000 na ule wa *Kabanga Nickel*, ianze chini ya Sheria mpya. Migodji mingi ina Viwanja vya Ndege ambavyo si vya kuingia wala kutoka nchini. Ndege zinazotua huko zidhibitiwe na *TRA* wawepo katika maeneo hayo, kuepusha utoroshaji wa madini unaosemekana upo.

(d) Maoteo ya Mapato ya Mpango wa Mwaka 2012/13 ni Shilingi 13.4 trilioni wakati makusanyo ni shilingi 7.5 trilioni tu. Uwiano wa Mapato yetu na Pato la Taifa ni asilimia 16.7 tu, Serikali ijizatiti ni vipi tutafikia asilimia 20 na kuwa endelevu ili kukuza uchumi wetu.

(e) Serikali ijitahidi kukamilisha Mradi wa Bomba la Gesi. Hivi sasa tuko hatua gani hasa ikizingatiwa kuwa Mradi huu ungekamilika na kufika Dar es Salaam mwishoni mwa mwaka 2012. Hali hii itatufanya kutokutumia Miradi ya Umeme ya Dharura ya Kukodisha ambayo inatumia fedha nyingi mno. Utekelezaji wa Mpango wa dharura wa kuwezesha Nishati hii kupatikana umeigharimu Serikali takriban shilingi bilioni 288 katika Mwaka wa Fedha 2011/12. Serikali iepuke matumizi ya umeme ghali. Utaratibu huu uendane sambamba na ukarabati ya Reli yetu ya kati na Bandari zetu Kuu. Kamati inashangaa kuwa katika Mwongozo wa Mipango na Bajeti ya Mwaka 2012/13 hakuna maelezo yoyote kuhusu uendelezaji wa Bandari za Mwambani Tanga, Mtwara na Bagamoyo na Reli ya Tanga, Moshi, Arusha hadi Musoma. Je, Programu hizi zimeahirishwa?

(f) Serikali hivi sasa ijiulize kwa nini mapato yasiyo ya Kodi yanapungua. Kwa mfano, katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2011/12, Serikali ilikusanya Shilingi 172.1 bilioni badala ya Shilingi 247.6 bilioni iliyolengwa, wakati Mapato ya Serikali za Mitaa yalifikia Shilingi 120.0 bilioni badala ya Shilingi 175.2 zilizolengwa. Huu ni udhaifu katika eneo hili. Utafiti unaonesha kuwa mapato mengi yanavuja kutokana na

biashara haramu ya kukata magogo, mbaao na mavuno mengine ya misitu. Aidha, vile vile upo upotevu mkubwa wa mapato kutokana na uvuvi haramu hasa kwenye maeneo ya Bahari Kuu (*Deep Sea*) na umeshindwa kudhibitiwa. Uwezo wa Serikali za Mitaa katika ukusanyaji wa mapato ni dhaifu na pale yanapopatikana usimamizi wake ni mdogo na hivyo kuongeza matumizi mabaya ya fedha. Serikali ijizatiti kusimamia maeneo hayo na kufanya ufuatiliaji wa matumizi (*expenditure tracking*) ili kuongeza mapato. Kamati inaishauri Serikali kuona uwezekano wa *TRA* kupanua majukumu yake ili iweze kutoza kodi hizi na hatimaye mapato yaingie Mfuko Mkuu wa Serikali.

(g) Kamati iliishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kufuta au kupunguza misamaha ya kodi kutoka asilimia mbili na zaidi hadi kufikia asilimia moja ya Pato la Taifa. Eneo hili bado linahitaji kufanyiwa kazi. Taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali inaonesha kuwa misamaha ya kodi katika kipindi cha 2010/11 imefikia asilimia 18 ya makusanyo ya Pato la Taifa. Kenya na Uganda imefika asilimia 11. Uwiano wa Misamaha na Mapato ya Uchumi wetu ni vyema urekebishwe haraka ili kulinda mapato yanayokusanywa na *TRA* na yaelekezwe kwenye maeneo ya kukuza na kuimarisha Uchumi.

Mheshimiwa Spika, thamani ya fedha ya Tanzania imeshuka kwa kiwango cha asilimia 10.4 ukilinganisha na dola moja ya Kimarekani, kutoka Tsh.1449.5 kwa Mwaka 2010 mpaka 1599.98 kwa Mwaka 2011. Hili limesababishwa na mahitaji makubwa ya dola kwa ajili ya manunuzi ya mafuta ya mitambo ya umeme, malighafi za viwandani, kununua bidhaa kutoka nje na kadhalika. Sababu nyingine ni kuwa Mataifa kama vile China, India na Nchi za Ulaya, hivi sasa yanatumia sana Sarafu ya Dola ya Kimarekani badala ya *EURO* kutokana na anguko la Uchumi kwa Nchi ya Ulaya; hivyo, kufanya mahitaji ya dola duniani kuwa makubwa na hivyo kuongeza thamani yake maradufu. Hali hii imeathiri kwa kiwango kikubwa thamani ya sarafu yetu.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa mauzo yetu ya nje yanaweza kugharamia asilimia 60 tu ya mahitaji yetu ya bidhaa kutoka nje ya nchi na hivyo bakaa ya asilimia 40 haina chanzo maalum, hali ambayo inachangia katika kuporomoka kwa shilingi. Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ipo haja ya kuongeza jitahada zetu za kuongeza mauzo nje kwa kuimarisha uzalishaji wa bidhaza zetu za asili na zile zisizo za asili. Aidha, mipango ya masoko inabidi irekebishwe kuepukana na matatizo yanayoyakuta mazao yetu muhimu kama vile Korosho na Pamba, kukosa masoko ya uhakika na hivyo kuwaathiri Wakulima.

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua za kupunguza athari za upungufu kadhaa zinazochukuliwa na Benki Kuu, bado lipo tatizo la ulanguzi au kuotea katika soko (*Market Speculation*) wa fedha za Kigeni. Tatizo hili linaandamana na utaratibu mgumu wa malipo ya Dola za Kimarekani kwa huduma na bidhaa ndani ya Nchi yetu (*dollarization*). Matatizo yote hayo yanachangia kuzorota kwa thamani ya Sarafu yetu na hivyo kuleta shinikizo kubwa la fedha za Kigeni katika uchumi wetu. Kamati ingependa kujua yapo maduka mangapi ya fedha za Kigeni nchini na yanadhibitwa vipi?

Takwimu zinaonesha kuwa Tanzania ni nchi pekee ambayo ina utitiri wa maduka ya fedha za kigeni katika Ukanda wa Afrika Mashariki, Kusini na Kati, ambayo udhibiti wake haujulikani. Kamati inaishauri Serikali kuangalia eneo hili. Maeneo haya yakidhibitwa, pamoja na kuongeza mauzo yetu nje, yataimarisha thamani ya Sarafu yetu. Aidha, Serikali ni vyema ikajifunza uzoefu wa Afrika Kusini, Ethiopia na kadhalika katika mkakati wa kulinda thamani ya fedha zao na jinsi zinavyodhibitwa ununuzi na uuzaji wa fedha za kigeni katika nchi zao.

Mheshimiwa Spika, tatizo la Nishati ya Umeme limekuwa ni la muda mrefu na limekuwa likiathiri Uchumi wa Tanzania katika upande wa uzalishaji viwandani na utoaji wa huduma na kadiri siku zinavyozidi kwenda, tatizo hili limekuwa likiigharimu Serikali fedha nyingi kukabiliana na tatizo hili kwa kutekeleza miradi ya dharura na yenye gharama kubwa. Kamati inasisitiza kuwa nishati za makaa ya mawe na gesi ndiyo vyanzo vya umeme wa gharama nafuu. Serikali inatakiwa kuhakikisha inatekeleza haraka Miradi iliyopo ya kuzalisha nishati ya gesi na makaa ya mawe. Umeme wa dharura (*emergency*) ambao Serikali imekuwa ikiutumia mara kwa mara gharama yake ni *40 - 43 US\$ cents/KWh* ikilinganishwa na umeme wa makaa ya mawe ambao ni *10 - 11US\$ cents/KWh*.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Shirika la *TANESCO* lina hali mbaya ya kifedha. Linadaiwa na Makampuni ya kufua umeme wa dharura kiasi cha Shilingi bilioni 105 na wadeni wengine Shilingi bilioni 164. Hivyo, kufanya jumla ya madeni hadi kufikia tarehe 21 Machi 2012 kuwa Shilingi bilioni 269. Shirika hili limeendelea kukopa kiasi cha Shilingi bilioni 408 kutoka katika Benki za ndani, itakayotumia kuzalisha umeme kwa kutumia mitambo ya dharura ikiwa ni kulipia mitambo ya IPTL, Symbion, Aggreko na wadeni wengine wanaotoa huduma.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona gharama kubwa ya mkopo huu pamoja na ulipaji wa riba utafanya gharama za uzalishaji kuwa za juu, kwa matumizi ya kaya na viwanda na hivyo kuathiri Uchumi wa Tanzania.

20 APRILI, 2012

Malipo haya yanaongeza matumizi ya Serikali yenye ukusanyaji mdogo wa mapato.

Mheshimiwa Spika, moja ya eneo linalohitaji kuzingatiwa katika sekta hii ni utamaduni wa makusudi wa ukarabati wa njia za kusambaza umeme na vifaa katika mitambo ya kufua umeme. Mikakati ya sasa ya Serikali ya kuongeza umeme haitaleti tija ikiwa Gridi ya Taifa itaendelea kama ilivyo sasa. Ukarabati na ubadilishaji wa baadhi ya laini ni muhimu ili umeme wa ziada utakaopatikana utumike katika kujenga uchumi. Aidha, Serikali ijandae na kujitayarisha (*preparedness*), usimamizi wa nishati hizi kwa kuwa na Sera na Sheria zinazoendeleza matumizi ya faida ya rasilimali hizi kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kutumia fursa ya kijiografia ya nchi yetu hasa kwenye uboreshaji na uimarishaji wa miundombinu ambayo ndiyo nguzo kuu ya kukuza uchumi wetu. Uwepo wa Bandari ya Tanga, Dar es Salaam na Mtwara na Reli, unatupa fursa ya kutoa huduma endelevu za usafirishaji wa watu na mizigo kwa nchi zote za Afrika Mashariki. Kwa sasa fedha nyingi za Serikali zinatumika katika ukarabati wa barabara ambazo ndizo zimekuwa nguzo kuu ya usafirishaji na zinaharibiwa na mizigo mizito. Kamati inashauri mipango iliyotolewa na Serikali katika kufufua Reli na upanuzi wa Bandari zote itekelezwe mara moja ili kusaidia kuibua uchumi wetu kwa kuhudumia usafirishaji wa bidhaa na watu kwenye maeneo ya ndani ya nchi na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ili kukuza uchumi ni lazima kuwepo na juhudi za makusudi za kuendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji. Eneo hili bado lina changamoto kubwa na bado msukumo wa uwekezaji (*Investment Drive*) haujawa wa kutosha. Kutokuwa na uhakika wa mwelekeo wa sera ulio endelevu, urasimu, ucheleweshwaji wa utoaji wa maamuzi, kutokuboreshwa ipasavyo kwa mazingira ya biashara na uwekezaji katika kuboresha barabara zetu, reli, bandari upatikanaji wa umeme, maji na kadhalika ni maeneo yanayohitaji mwendelezo wa kasi wa kufanyiwa kazi.

Mahusiano yaliyoanzishwa Kisheria baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi chini ya utaratibu wa *PPP*, hauna budi kuimarishwa ili kusaidia Serikali kupata mitaji ya kutosha katika yale maeneo au ile Miradi inayohitaji fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, eneo la uwezeshaji; katika eneo hili Serikali imefanya jitihada ya kutosha ya kuanzisha Mifuko mbalimbali ya uwezeshaji na kuwepo kwa Baraza la Taifa la Uwezeshaji. Kamati inaamini kuwa, eneo hili muhimu litasaidia sana katika azma ya Serikali ya

kutekeleza malengo mawili ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato wa wananchi walio wengi hususan wale wenye vipato vya chini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza programu na mikakati takriban 15 inayolenga kuwawezesha wananchi wenye vipato vya chini. Programu hizi ni pamoja na Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Mfuko wa Wajasiriamali Wananchi, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, Mfuko wa Uwezeshaji wa Wajasiriamali Wadogo na kadhalika. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuzingatia kwa makini suala la walengwa (*targeting*) ili kuwasaidia wanaohusika. Mifuko hii isipokuwa na uratibu mzuri, fedha nyingi zinaweza kupelekwa kwa makundi machache badala ya kuhudumia makundi au watu wengi. Lazima wenye vipato vya chini wahudumiwe na nyanzo mbalimbali vya mikopo, vile rasmi na visivyo rasmi ili viweze kujiwekea akiba na mikopo nyenzo muhimu za kuendeleza shughuli zao za uchumi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa Mabenki mengi nchini, takriban 45, bado wananchi wengi vijijini na mijini hawajafaidika na huduma hii. Viwango vikubwa vya riba na masharti magumu imefanya Watanzania, chini ya asilimia 13, kufaidika na huduma za fedha. Hili ni changamoto.

Mheshimiwa Spika, ni asilimia 12.4 ya Watanzania wote wanaohudumiwa na vyombo vya fedha. Asilimia 56 hawapati huduma hizi kabisa. Vijijini ni asilimia tatu tu. Shughuli za kibiashara za mabenki ni asilimia 8.7 tu (*Banking out reach and market issues*), Mabenki matatu yanadhibiti asilimia 48 ya soko la dhamana na mikopo wakati ni mabenki manane yanadhibiti (*control*) asilimia 76 ya masoko ya kibenki. Matokeo yake ni kuwa ni asilimia 12 ya Watanzania wanapata huduma hizi.

Ukilinganisha na nchi nyingine, hali ya Tanzania ni ya chini, Afrika ya Kusini ni asilimia 60, Namibia asilimia 45, Botswana asilimia 41, Kenya asilimia 30, Nigeria asilimia 21, Malawi asilimia 19, Uganda asilimia 18, Zambia asilimia 12 na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa utaratibu wa *Microfinance* unavyoendeshwa nchini bado haujawekewa *Legal and Regulatory Framework* inayoweza kuboresha na kupanua shughuli zake. Kwa mfano, nchi ya Kenya wana *Microfinance Act, 2006, SACCOS Act, 2009* na *Banking and Financial Institution Act, 2006*. Kanuni zilizopo sasa zinazoziongoza Taasisi na *Microfinance* ni kikwazo:-

Kwanza, haziruhusu vyombo hivi vya fedha kuingiliana kiutendaji. Pili, zinadumisha *restructure lending* kwa taasisi hizi ndogo. Tatu, utaratibu

20 APRILI, 2012

wa utoaji leseni ni mgumu. Nne, vikwazo vya utawala (*administrative sanctions*) ni vingi. Kamati inashauri ifuatavyo:-

(i) *Microfinance Act* iandaliwe haraka.

(ii) Uandaliwe utaratibu mpya wa kanuni na usimamizi wa *Microfinance Institutions* zitakazosimamia ngazi ya kwanza, *VICOBA, ROSCAS, ASCAS*; ngazi ya pili, *Credit Only Non Deposit taking MFIs*; ngazi ya tatu, *Deposit taking MFIs*. Lengo liwe ni kuandaa mawanda ya kisheria, usimamizi na udhibiti bora kwa sekta nzima ya *Microfinance* kwa zile zinazochukua dhamana na zile zisizochukua dhamana.

(iii) Lazima sasa itungwe Sheria ya *SACCOS*, yaani *SACCOS Act* na isiwe chini ya *Cooperative Act* kama ilivyo sasa na iundwe Mamlaka ya Udhibiti (*Regulatory Authority*) ya *SACCOS*.

(iv) Lazima ianzishwe wakala wa kudhibiti na kusimamia Benki za Maendeleo za Wananchi (*Community Banks*). Kamati ya Fedha na Uchumi itatoa changamoto ya kuanza mchakato wa uandaaji wa Sheria hizi kwa niaba ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuanzisha utaratibu wa *Mortgage Financing* na *Financial Leasing*, bado utaratibu huu haujaanza kuondoa kero ya ukosefu wa nyumba za gharama za chini kwa wananchi wenye kipato kidogo. Msisitizo wa Serikali uwekwe kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa uchumi wa nchi hauwezi kuondoka bila ya kupata msaada wa huduma za Sekta ya Fedha. Uchumi vile vile hauwezi kuendelea bila ya Wananchi wengi kuingia katika biashara. Utendaji wa Sekta ya Fedha nchini na Masoko ya Fedha, ndiyo inayopelekea tija na ufanisi wa kuweka bei katika masoko ya msingi na yale ya mengine (*primary and secondary markets*). Kamati inajiuliza kuwa ni kwa kiasi gani ukubwa wa sekta hii unakidhi matakwa ya maendeleo ya nchi yetu?

Tunahitaji kukua kwa asilimia kumi tukitegemea *fiscal sector* na je, Sekta ya Fedha inachangiaje katika hili kwa maana ya uwekezaji nchini na kadhalika. Kamati inadhani Sekta ya Fedha ni ndogo au ni ndogo kwa makusudi (*artificially small*). Ukuaji wa Sekta ya Fedha ni lazima usaidie ukuaji wa uchumi. Tunayo Mabenki 45 ya kibiashara lakini mtaji wa uwekezaji bado ni mdogo. Utitiri wa Benki uliopo hauendani na mahitaji (*demand*) halisi ya huduma za Kibenki katika uchumi. Eneo hili linahitaji kuimarishwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa kunakuwepo na uendeshaji na usimamizi bora wa uchumi (*Better Economic Management*), eneo la uratibu wa Wizara na Taasisi mbalimbali za kiuchumi ni lazima liimarishwe. Bado Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha, vyombo nyeti vya kuendesha uchumi, havijaweka utaratibu wa uratibu unaowezesha maingiliano (*intergration*) na mashirikiano kiutendaji. Matokeo yake ni kila Kitengo kufanya kazi peke yake na kukosa ni wapi maamuzi ya mwisho yanafanyika. Kamati inaendelea kushauri Tume ya Mipango ni lazima ipewe nguvu juu ya Wizara zote (*Super Ministry*) kwa kupitia marekebisho ya Sheria iliyoionda ya Mwaka 1989. Tume ya Mipango katika nchi nyingine imepewa mamlaka makubwa ndani ya Katiba ikiwa inajitoshesha.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kuwa unapokosekana usimamizi na uendeshaji bora wa uchumi, utengemavu wa misingi mikuu ya uchumi mkubwa utakuwa dhaifu. Matumizi ya Sera za Kifedha na zile za Kodi zitapata wakati mgumu kutatua na kuondoa vikwazo vya kinfumo (*structural rigidities*) ambavyo siyo tu vitapunguza kasi ya kukuza uchumi bali vile vile zitashindwa kuendana pamoja na mikakati ya kupunguza umaskini baina ya wananchi. Hakuna atakaekataa kuwa swali kubwa linaloulizwa hivi sasa ni kama uchumi unakua mbona hali ya maisha bado ni ngumu? Nadharia na modeli za uchumi mkuu kushuka kwa wananchi (*trickle down theory*) na ile ya kujenga usawa hivi sasa hazitaweza kupunguza matatizo yetu ya kujenga uchumi na kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nadharia ya kwanza itaendelea kuendeleza ukuaji wa uchumi unaoambatana na kupanuka kwa tofauti kubwa ya mapato kati ya matajiri na umaskini na ile ya pili inayotoa kipaumbele katika kugawana rasilimali za nchi (*redistribution*), badala ya kutoa kipaumbele kwenye masuala ya uzalishaji na biashara na hivyo kutaka usawa bila kukua kwa uchumi au usawa katika umaskini itaendelea kudumaza uchumi wa nchi. Mfumo wa uchumi unaohitajika sasa ni ule utakaoleta maendeleo ya kiuchumi na jamii wenye lengo la kukuza uchumi na upunguzaji wa umaskini kwa wakati mmoja.

Kamati inaishauri Serikali ijitathmini inafuatiliaje utekelezaji wa Mipango inayowekwa kushughulikia changamoto hizi mbili. Ipo haja ya chombo kinachosimamia Mipango kufuatilia utekelezaji wa Mipango ya Taifa katika utekelezaji wa maamuzi ya Serikali. Nchi kama Brazil na nyinginezo, zina vitengo kama hivi pamoja na kuwa na Mahakama inayoangalia matumizi ya rasilimali za nchi katika kuleta maendeleo.

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwa, Wizara ya Fedha haiwezi kupanga Mipango ya Nchi, kazi yake kubwa ni kukusanya mapato na kusimamia mfumo wa matumizi. Mpango unakuwa *determined* na uwezo wa kifedha. Wizara kazi yake ni kutafuta fedha za kugharamia Mipango.

Wakati huo huo Serikali inabidi ijiepushe na matumizi makubwa kwa kigezo cha ufanisi juu ya matumizi ya bajeti ya Serikali; wapi tunapata fedha na wapi tunatumia; lakini vile vile tukitumia lazima tujiulize mapato tunapata wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa ushauri uliotolewa katika taarifa hii, ili kuboresha Mipango na Bajeti ya Nchi, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu, kupitia taarifa hii, liazimie kuwa Bunge lianzishe Kamati ya Bajeti, kupitia kutungwa kwa Sheria ya Bajeti kama ilivyo katika nchi nyingine za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Kamati yangu katika kutekeleza shughuli zake katika mwaka 2011/2012 yametokana na ushirikiano wa karibu sana wa Wizara ya Fedha, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji na Uwezeshaji), Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu); Tume ya Mipango pamoja na Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hizi, Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa na Wadau wetu wote. Napenda kuwashukuru wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani nyingi kwa ushirikiano tulioupata kutoka kwenye Ofisi yako Mheshimiwa Spika. Napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Dkt. Thomas Kashillillah na Katibu wa Kamati hii, Ndugu Michael Kadebe, kwa kazi nzuri waliyofanya ya kuratibu shughuli zote za Kamati kwa kipindi chote cha mwaka 2011/2012 na Wafanyakazi wote wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, nachukua fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi, kwa kutoa maoni, ushauri na ushirikiano wa kutosha kwenye Kamati, hali ambayo imewezesha kutekeleza na kufanikisha kazi nyingi za Kamati yetu. Aidha naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati hii kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omari Kigoda - Mwenyekiti, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Eustas Osler Katagira, Mheshimiwa Maulidah Anna Valerian Komu, Mheshimiwa Dkt. Binilith Satano Mahenge, Mheshimiwa Devotha Mkuwa Likokola, Mheshimiwa

20 APRILI, 2012

Martha Jachi Umbulla, Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Alhaji Mohamed Hamisi Missanga, Mheshimiwa Andrew John Chenge na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Ahsante. Kamati hii ya Nishati wamealikwa na Serikali ya Norway kwenda kuangalia *industry* ya mafuta na gesi.

Tumepewa pia mwaliko mwingine ambao Wajumbe wawili wawili kutoka Kamati ya Nishati na Madini, Kamati ya Fedha na Uchumi na Kamati ya *POAC*; ni Kamati tatu, watakwenda pia Trinidad and Tobago kwa sababu wale nao pia wana uzoefu mkubwa wa masuala ya gesi na mafuta, angalau kujifunza jinsi watu wanavyopanga bei za mafuta na zinavyoweza kuwasaidia wananchi. Kwa sababu wenzetu nchi zote wameshapata mafuta, si haba pengine na sisi tunaweza kuyapata, lakini ni vizuri kujiandaa kupokea kitu kikubwa kama hicho kabla hatujaingia huko na kugongana hovyoy. Kwa hiyo, nao pia watakwenda Trinidad na Tobago katika kipindi kinachofaa.

Tunaendelea, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu.

MHE. PETER J. SERUKAMBA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 114 (15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kazi za Kamati ya Bunge ya Miundombinu zilizofanywa kuanzia Februari, 2011 mpaka Aprili, 2012.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Kamati hii ilifanya kazi zifuatazo:-

(1) Kero ya Msongamano wa Magari Jijini Dar es Salaam;

- (2) Utendaji wa Kampuni za Reli Tanzania;
- (3) Utendaji Kazi wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL);
- (4) Utendaji wa Mamlaka ya Bandari Tanzania;
- (5) Kufanya ziara ya kukagua miradi mbalimbali iliyo chini ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati;
- (6) Kupitia na kujadili Maazimio yaliyowasilishwa mbele ya Kamati; na
- (7) Kupitia makadirio na matumizi ya Bajeti ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, kuhusu msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Usafiri katika Jiji la Dar es Salaam kama ilivyo katika miji mingine nchini unasimamiwa na mamlaka nyingi ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Mambo ya Ndani, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji. Hali hii inasababisha urasimu katika kufikia maamuzi na migongano ya kimamlaka na kimaslahi baina ya wadau.

Mpango wa Serikali wa kuanzisha usafiri wa reli Jijini Dar es Salaam utekelezwe haraka. Reli iliyopo kuanzia Stesheni ya Dar es Salaam hadi Ubungo Maziwa ifufuliwe na itumike kusafirisha abiria. Aidha, reli ya TAZARA itumike kusafirisha abiria kutoka Stesheni ya Mwakanga hadi Dar es Salaam. Taarifa zinaonesha kuwa usafiri wa treni kutoka Stesheni hadi Ubungo Maziwa utabeba kiasi cha abiria 9,600 kila siku. Idadi hii ni kubwa kiasi cha kupunguza kero ya usafiri Jijini Dar es Salaam. Aidha, gharama ya kuanzisha usafiri huu si kubwa sana kwani mpaka mwezi Septemba, 2010 gharama ilikuwa ni Tsh. 4,728,011,702/= tu kiasi ambacho kiko ndani ya uwezo wa Serikali, kinachotakiwa ni utashi wa kisiasa tu.

Mheshimiwa Spika, kuwe na hamasa na ushawishi kwa wawekezaji binafsi kujenga barabara mijini ili watumiaji wa barabara hizo wazitumie kwa malipo kama inavyofanyika katika nchi nyingi za mashariki ya mbali kama Singapore, Malaysia, Thailand na kadhalika. Utaratibu huu utapunguza ama kuondoa kabisa msongamano katika miji yetu hasa Dar es Salaam. Hii ni pamoja na ujenzi wa barabara zitokazo nje ya Dar es Salaam kwenda Mikoani (*Express roads*).

20 APRILI, 2012

Utoaji wa vibali vya kujenga majengo makubwa uzingatie ukubwa wa kiwanja husika ili kutoa nafasi kwa jengo husika kuwa na eneo la kutosha kwa ajili ya kuegesha magari ya watumiaji wa jengo hilo. Aidha, sheria zinazosimamia uwekaji wa maegesho kwenye majengo makubwa zifuatiliwe.

TANROADS wapewe jukumu la kujenga na kusimamia barabara zote za mijini kwani Halmashauri za Manispaa zina majukumu mengi kiasi cha kushindwa kujenga na kusimamia barabara hizo ipasavyo.

Suala la barabara za juu limekuwa likizungumzwa na Serikali kwa muda mrefu. Ni vema sasa Serikali itekeleze ujenzi wa barabara hizi kwenye makutano ya barabara kuu ufanywe haraka. Aidha, kasi ya kujenga mradi wa mabasi yaendayo kasi Jijini Dar es Salaam iongezwe ili kupunguza tatizo la msongamano.

Kamati inaamini kuwa barabara za mchepuo na za mitaani zikiimarishwa zitasaidia sana kupunguza msongamano wa magari kabla hata miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara na *flyovers* haijaanza.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa reli katika uchumi wa nchi unafahamika duniani kote. Warren Buffett, Mwekezaji na bilionea maarufu nchini Marekani, wakati ananunuaKampuni kubwa ya reli duniani. *BNSF*, alisema:-

Nanukuu: "Railroads represent the future. They're best-positioned to haul the raw material and finished goods for a nation and economy. Unlike trucks, trains don't have to compete on congested highways. Nor do railroads depend on strapped Governments to maintain infrastructure." (Mwisho wa kunukuu)

Tafsiri isiyo rasmi ya kauli hiyo ni kwamba: "Njia ya reli inamaanisha mustakabali mzuri. Ni njia bora zaidi kusafirisha malighafi kwa ajili ya Taifa na uchumi wake. Kinyume na malori, usafiri wa garimoshi hauhitaji kushindana katika msongamano kwenye barabara kuu. Aidha, usafiri wa reli hautegemei sana ukarabati unaofanywa na Serikali yenye uwezo mdogo kifedha."

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo, ni dhahiri kuwa katika uchumi wa Tanzania, sekta ya usafirishaji na uchukuzi inategemea usafiri wa reli kwa kiasi kikubwa. Ni usafiri unaosaidia kusafirisha mizigo mingi kwa wakati mmoja. Kulithibitishia Bunge lako Tukufu, utafiti umebaini kuwa mizigo inayosafirishwa na treni mara moja, ikisafirishwa kwa njia ya

barabara, itahitaji wastani wa malori 62 kuisafirisha. Hali hii ndio hasa iliyomfanya Mwekezaji huyu wa Kimarekani niliyemnuuu awali kusema:-

Nanukuu: *"The rail business is actually in tune with the future. Trains move goods using far less fuel than alternatives."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, maana ya maneno hayo ni kuwa, biashara ya reli inakubaliana kabisa na dhana ya kuzingatia mustakabali wa baadaye. Garimoshi husafirisha mizigo mingi zaidi kwa kutumia mafuta kidogo ikilinganisha na njia nyingine za uchukuzi na usafirishaji. Hali hii huwezesha bidhaa zinazosafirishwa kwa treni kuwa na bei nafuu katika soko na hivyo kuzuia mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Spika, ni kutokana na umuhimu wa reli katika uchumi ndiyo sababu nchi nyingine zinatilia mkazi ujenzi na matumizi ya reli. Kwa mfano, nchi ya Angola inajenga reli kuanzia bandari ya Benguela hadi Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ambayo inatarajia kukamilika mwaka huu wa 2012. Nayo Kenya inajenga reli kutoka Lamu kwenda Sudan Kusini. Aidha, nchi ya Msumbiji inajenga reli kuanzia bandari ya Nacala kwa ajili ya kuhudumia nchi za Malawi, Zambia na Zimbabwe.

Tafsiri yake ni kwamba, reli zetu hazitakuwa na mizigo ya kutoka na kwenda nchi ya Zambia, Malawi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo au kutakuwa na ushindani mkubwa kutokana na kujengwa kwa reli hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, reli zetu zote zina matatizo makubwa na hivyo kutokidhi matarajio ya wananchi na nchi jirani zinazohudumiwa na reli hizo. Tukiendelea na mwenendo tulionao, nchi yetu itaachwa nyuma sana kimaendeleo, kwani nchi jirani zinajenga na kuimarisha reli zao kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ushindani unaotarajiwa Kamati inashauri Serikali kuharakisha ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge* na pia kuimarisha reli ya TAZARA kwa ajili ya kuhimili ushindani huu na kuinua uchumi wa nchi yetu. Aidha, ni dhahiri kuwa katika suala la kuimarisha reli zetu Serikali haina nia thabiti wala utashi wa kisiasa na kama upo ni wa maneno zaidi kuliko vitendo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imesikitishwa sana na taarifa ya udhamini wa Serikali kwa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) mwaka 2007 ili liweze kukodi Ndege aina ya *Air Bus 420 – 214* kutoka kwa Kampuni ya *Wallis Trading* ya Lebanon kwa muda wa miaka sita.

20 APRILI, 2012

Hata hivyo, Ukodishaji wa Ndege hiyo ulifanyika Oktoba mwaka 2007 wakati dhamana ya Serikali kwa ATCL ilitolewa tarehe 2/4/2008. Hivyo ni wazi Ndege ilikodiwa kabla ya kutolewa dhamana ya Serikali.

Mkataba wa ukodishaji ndege ulilingiwa na kutiwa saini kinyume na ushauri wa wataalam wa ATCL ambao Katika Taarifa yao walisema sio sahihi kukodi Ndege ambayo baada ya miezi sita itatakiwa kufanyiwa matengenezo makubwa 12 years check.

Baada ya Ndege kukodiwa ilibaki mikononi mwa mkodishaji kwa kipindi cha miezi saba toka Mkataba usainiwe mwezi Oktoba 2007 hadi Mei, 2008 kutokana na kuchelewa kwa dhamana ya Serikali.

Ndege hiyo iliwasili nchini mwezi Mei, 2008 na kufanya kazi kwa miezi sita tu na kutakiwa kupelekwa nchini Ufaransa kufanyiwa matengenezo makubwa yaitwayo 12 year check kwa gharama za ATCL.

Mheshimiwa Spika, mwezi Julai 2009 ndege ilipelekwa Ufaransa na kukamilika matengenezo lakini haikurudishwa kwa sababu ATCL walikosa fedha za kulipia matengenezo USD 3,009,495. Dhamana ya Serikali iliyotolewa ilikuwa na thamani ya USD 60,000,000 na hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011. Kutokana na ATCL kushindwa kulipa deni hilo, Serikali italazimika kulipa deni la shilingi bilioni 121,000,000,000/= ikiwa ni dhamana pamoja na riba.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na mwenendo huu wa utendaji ndani ya Serikali kwani unaitia hasara nchi yetu na inashauri walihusika wote wachukuliwe hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa iwapo Serikali imeshindwa kuliendesha Shirika hili iliache kabisa kwani pamoja na kulipatia fedha kidogo sana kwa miaka miwili iliyopita halina hata Bodi ya kulisimamia.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuwepo kwa msongamano mkubwa wa mizigo katika bandari ya Dar es Salaam pamoja na meli kubwa kushindwa kuingia bandarini kwa sababu ya kina kifupi cha bandari hiyo. Kuanzia mwaka 2008 kumekuwa na mikakati kadhaa ya kuondoa tatizo hilo. Moja kati ya mikakati hiyo ni kupanua lango la kuingilia bandarini na kujenga Gati namba 13 na 14. Hata hivyo, ujenzi wa gati hizo umekuwa ukikwamishwa kutokana na Mamlaka ya Bandari kuingiliwa na Waziri wa Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, ili kujenga gati hizo Mamlaka ya Bandari baada ya kufanya utafiti imeamua kuomba mkopo wa Dola za Kimarekani

20 APRILI, 2012

milioni 523.1 kutoka *Exim Bank* ya China ambao riba yake ni 2% na utalipwa kwa miaka 12 na utanza kulipwa miaka mitatu baada ya kukamilika ujenzi na kuanza kutumika gati hizo. Aidha, katika mkopo huo Mamlaka itapaswa kuchangia 15% ya mkopo kiasi ambacho kiko ndani ya uwezo wake. Mchakato kupata mkopo huo umekamilika ikiwa ni pamoja na kupata dhamana ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kujenga kwa mkopo una faida zifuatazo:-

Kuiwezesha Mamlaka kumiliki miundombinu ya gati hiyo mpya na kuwa huru kufanya maamuzi ya uendeshaji wake na mapato yote yatakayopatikana yatakuwa ni mali ya Mamlaka.

Kwa kuwa Mamlaka ina uwezo wa kulipa deni hilo katika kipindi cha Mkopo na kubakiwa na faida, itaweza kuendeleza miundombinu ya bandari nyingine ambazo hazina uwezo wa kujiendesha ambalo ndiyo jukumu la mamlaka hiyo. Mkopo una masharti nafuu sana na Mamlaka itapata tozo lote la *Wharfage*. Mamlaka ina uzoefu katika kuhudumia mikopo kwani hata kitengo cha Makontena kilijengwa kwa mkopo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri na manufaa ya kujenga gati hizo kwa mkopo, Kamati inasikitishwa na maamuzi ya Waziri wa Uchukuzi kutaka gati hizi zijengwe na mwekezaji binafsi. Makubaliano baina ya Waziri wa Uchukuzi na Mwekezaji ambaye ni *China Merchants Holdings (International) Company Limited* hayajazingatia maslahi ya Mamlaka na Taifa kwa ujumla kwani baadhi ya vipengele vya makubaliano (*Memorandum of Understanding*) hayo vinasema:-

Ni mwekezaji huyo tu (*exclusively*) ndiye atakayejenga, kumiliki, kuendesha gati hizo na kuzikabidhi kwa Wizara ya Uchukuzi baada ya miaka 45.

Mwekezaji hatawajibika kwa lolote kutokana na hasara ambayo Wizara ya Uchukuzi itapata kutoka kwa mdau mwingine yeyote (*third party*) kutokana na shughuli zitakazokuwa zinafanywa na mwekezaji huyo.

Wizara ya Uchukuzi itatoa mamlaka ya kisheria (*Power of Attorney*) kwa mwekezaji ya kufanya shughuli hizo yeye peke yake (*exclusively*).

Vipengele vyote vilivyopo kwenye Makubaliano vitakuwa ni siri, mbali na walioingia makubaliano hayo, havitatakiwa kujulikana na mtu mwingine yeyote isipokuwa iwapo vitatakiwa Mahakamani au na Soko la Hisa la Hong Kong.

20 APRILI, 2012

Baada ya makubaliano hayo kukamilika iwapo kuna majadiliano mengine yakayohitajika baada ya hapo, majadiliano hayo lazima yapate kibali kutoka kwenye Bodi ya Mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, vipengele hivyo vinampendelea mwekezaji kwa dhahiri. Aidha, hasara zingine ambazo Mamlaka itapata kutokana na maamuzi ya Waziri wa Uchukuzi ni:

Kwamba, baada ya miaka 45 ya mwekezaji kutumia gati hizo miundombinu yake itakuwa imechakaa na hivyo kuhitaji uwekezaji mpya.

Mamlaka itakosa mapato kwa miaka yote 45 ya umiliki wa mwekezaji.

Mwekezaji itabidi amilikishwe ardhi ya eneo atakalolitumia kwa shughuli zake.

Iwapo mkopo utasitishwa kama anavyotaka kuamua Waziri wa Uchukuzi itabidi kuanza mchakato upya na hivyo kuendelea kuwa na msongamano wa mizigo bandarini. Aidha, washindani wa bandari ya Dar es Salaam (Mombasa, Beira na Durban) wanapanua bandari zao hivyo bandari yetu itakosa soko.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mazingira ya uwekezaji kwenye gati hizo Kamati inashauri Serikali ichukue huo mkopo mapema iwezekanavyo ili kazi ya ujenzi ianze. Aidha, kwa kuwa mkopo unapitia Hazina, Kamati inashauri upelekwe kwenye ujenzi wa mradi bila kuupunguza kwani ukipunguzwa utachelewesha ujenzi wa mradi na hivyo kutofikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka inao uwezo wa kulipa deni hilo kwani kwa mwaka 2010/2011, ilipata ziada ya sh. bilioni 111,494.94 na mapato yamekuwa yakiongezeka kwa 35.7% kila mwaka na hivyo kukamilika kwa ujenzi wa gati hizo kutaongeza mapato hayo kwa kiasi kikubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inamshauri Waziri wa Uchukuzi kutoingilia maamuzi ya Mamlaka ya Bandari hasa yanapofanywa kwa nia njema na kwa maslahi ya nchi yetu. Aidha, Mamlaka ya Bandari ni Mamlaka kamili yenye uwezo wa kununua (*Procurement Entity*) na kuingia mikataba na Taasisi au chombo kingine, hivyo kuingilia mchakato wa ujenzi wa Gati hizo ni kuvunja sheria.

20 APRILI, 2012

Mfumo unaopigiwa chapua na Waziri wa Uchukuzi wa kujenga, kumiliki, kuendesha na kuhamisha (*Build, Own, Operate and Transfer-BOOT*) unapingwa kote duniani na hata Taasisi za Kimataifa ikiwemo *International Trade Organisation (ITO)* na *World Trade Organisation (WTO)* kwani unazigandamiza nchi maskini na kunufaisha wawekezaji.

Mhesimiwa Spika, kwa kuwa mchakato wa kupata mkopo umekamilika Kamati inashauri ujenzi wa gati hizi uanze mara moja ndani ya mwaka huu wa fedha. Kamati inampongeza Waziri wa Fedha kwa kukubali kuidhamini mamlaka ili iweze kujenga gati. Aidha, inampongeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Menejimenti ya Mamlaka ya Bandari Tanzania pamoja na Bodi kwa umakini na uzalendo wao katika kuchukua njia muafaka za kujenga gati husika.

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Dar es Salaam inakimbiwa na wateja kwa sababu ya kukosekana kwa usafiri wa reli wa kuaminika na hivyo kulazimika kutumia usafiri wa malori. Hata hivyo, usafiri wa malori kuwa ni ghali bado kuna matatizo ya kusimamishwa njiani mara kwa mara. Kwa mfano, kutoka Dar es Salaam mpaka mpakani mwa Tanzania na Rwanda, malori yanasimamishwa mara 45 wakati kutoka Mombasa mpaka Kigali (Rwanda) yanasimamishwa mara tano tu. Hali hii inakatisha tamaa wafanyabiashara kwa sababu ya kuchelewa njiani. Aidha, bandari bado inalalamikiwa kutokana na msongamano wa mizigo pamoja na wizi hasa vifaa vya magari yanayoshushwa kutoka melini.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara nchini unufaishe zaidi wakandarasi wa ndani kwani kufanya hivyo kunaongeza uzoefu kwa wakandarasi, fedha zote zinabaki ndani ya nchi na ukarabati wa barabara hizo unakuwa rahisi kwani wajenzi wake wanakuwa hapa hapa nchini. Aidha, kuwe na utaratibu utakaowalazimisha wakandarasi wa nje kuwa na ubia na wakandarasi wa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Wakandarasi wa ndani wasipimwe kwa wingi wa vifaa walivyonavyo kwani vifaa vinaweza kupatikana kwa kukodi badala ya kuvimiliki. Aidha, iwe ni sheria kuwa wakandarasi wa nje wanapooomba kazi nchini walazimishwe kuwa na ubia na wakandarasi wa ndani ili kuwawezesha wakandarasi wa ndani kupata uzoefu na mitaji ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upatikanaji mdogo wa fedha kwa ajili ya kulipa madeni na hati za malipo zinazopokelewa kutoka kwa wakandarasi na Wahandisi Washauri wanaotekeleza kazi za kandarasi kuwekwe vipaumbele vichache vya barabara za kujengwa kutokana na umuhimu wake kiuchumi na kijamii ili kuleta tija kuweza kurejesha

gharama ya ujenzi wa barabara husika. Barabara za vipaumbele ziwe ni zile zinazounganisha nchi yetu na nchi za jirani na maeneo yenye uzalishaji kama vile maeneo yenye uzalishaji wa kilimo. Vipaumbele vitaifanya Serikali kutoelemewa na madeni yanayotokana na riba na adhabu zingine zinazotokana na Mikataba.

Hadi Machi, 2012, Serikali ilikuwa inadaiwa jumla ya shilingi bilioni 331.501 zikiwa fedha za ndani. Hali hii ilipelekea Wakandarasi tisa wanaojenga barabara za Mbeya–Makongorosi, Lwanjilo- Chunya, Isaka-Lusahunga, Isaka-Ushirombo, Kanazi-Kizi-Kibaoni, Sumbawanga-Kanazi, Mwigumbi-Maswa-Bariadi na *Jet-Corner-Vituka-Davis Corner*, kusimamisha kazi ya ujenzi, wakandarasi wanaojenga barabara mbili za Handeni-Mkata, Nyanguge-Musoma walitoa taarifa (*notice*) ya kusimamisha kazi na wengine 14 wanafanya kazi kwa kasi ndogo, baadhi yao ni wale wanaojenga barabara za Korogwe-Handeni, Kagoma-Lusahunga, Bagamoyo- Msata, Ubungo *Bus Terminal-Kigogo-Kawawa Roundabout*, Kigogo-Kawawa *Round about- Msimbazi Valley*, Tabora-Urambo, Tabora-Urambo, Sumbawanga-Matai-Kasanga *Port*. Mwenendo huu si mzuri kwa mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mpaka kufika mwezi Machi, 2012, Serikali imetoa kiasi cha shilingi bilioni 351.977 kati ya shilingi bilioni 609.743 zilizoko kwenye bajeti ya mwaka 2011/2012. Hata hivyo, sehemu ya fedha zilizotolewa imetumika kulipa madeni ya mwaka 2010/2011 ambayo yalikuwa ni shilingi bilioni 420. Tafsiri yake ni kwamba, sehemu kubwa ya miradi inayoendelea sasa inafanywa kwa mkopo kwani fedha iliyokasimiwa kuigharamia imetumika kulipa madeni yaliyopita. Kutokana na hali hii Kamati inashauri Serikali isianzishe miradi mipya mpaka itakapomaliza kulipa madeni ya miradi inayoendelea kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake haitoi upendeleo wa kutosha kuwezesha Wakandarasi na wahandisi washauri wa Kitanzania kupata kazi na kukua kibiashara. Kamati inashauri mapendekezo yaliyowasilishwa Serikalini kwa ajili ya kujumuishwa kwenye uandaaji wa kanuni mpya yazingatiwe kwani yanalenga kuboresha mazingira kwa ajili ya wahandisi wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Kamati inashauri Serikali itoe fedha za kutosha ili uweze kukamilika kwa muda uliopangwa.

Kamati inapongeza hatua ya Serikali kuamua kuhama kutoka kwenye mradi wa analogia kwenda Dijitali. Hata hivyo, ni ushauri wa Kamati kuwa kuwe na udhibiti wa ving'amuzi vinavyoingizwa nchini ili

20 APRILI, 2012

visiletwe ambavyo havina ubora. Aidha, elimu itolewe kwa wananchi juu ya matumizi ya ving'amuzi hivi pamoja na mfumo mzima wa dijitali.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya simu za mkononi yameongezeka sana na hivyo kuashiria kuwa mapato ya Makampuni ya Simu yameongezeka pia. Hata hivyo, ubora wa mawasiliano ni hafifu, simu zinakatika mara kwa mara, usikivu hafifu, gharama za kupiga juu, ni za juu na pia muda unaotumika kupima gharama ya malipo hauaminiki kwa mtumiaji anaweza kuongea muda mfupi lakini fedha zikakatwa tofauti na muda uliotumika. Kamati inashauri makampuni yaboreshie huduma zao, wateja wafurahie huduma za mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Spika, moja ya matatizo makubwa katika uendeshaji wa Mashirika ya Umma ni kuingiliwa katika utendaji na maamuzi yake na mamlaka za Serikali zilizo nje ya utendaji wa Mashirika hayo. Wakati umefika sasa Serikali iache mashirika yake yaendeshwe kitaalam na kwa mujibu wa sheria. Aidha, nafasi za Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma zitangazwe na kushindaniwa, ajira zao ziwe katika mikataba ya utendaji (*Performance Contract*) badala utaratibu wa sasa wa kuteuliwa. Utaratibu huu utaongeza uwajibikaji kwa watendaji hawa.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati yangu. Nawashukuru pia Mawaziri, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu, Maofisa wote na Taasisi zilizo chini ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati ya Bunge ya Miundombinu kwa ushirikiano, ushauri na utaalum wao ambao kwa kiwango kikubwa umeiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha taarifa hii leo katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi za jumla Wizara ya Uchukuzi haijafanya juhudi za kutosha kutatua kero ya usafiri nchini wakati sekta za reli, bandari na usafiri wa anga wanazosisimamia ndiyo moyo wa maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita pamoja na mafanikio yake makubwa ya kutekeleza majukumu yake, Kamati ilipata pigo kubwa la kuondokewa na wajumbe wake wawili ambao walikuwa makini sana. Wajumbe hao ni Mheshimiwa Regia Estelatus Mtema na Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari, ambao wameacha pengo kubwa sana kwenye Kamati yetu. Kwa hakika tutaendelea kuwakumbuka na kuwalilia. Mungu aendelee kuzilaza Roho za marehemu hawa mahali pema peponi. Amina.

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, pamoja na majonzi hayo natoa pongezi zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati hii kwa kunichagua kuwa Mwenyekiti wao na kwa umoja na ushirikiano mkubwa walionao katika kutekeleza majukumu yao. Aidha, umakini na weledi wao ndiyo ulioiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mwenyekiti; Mheshimiwa Anne K. Malecela, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Lolesia J.M. Bukwimba, Mjumbe; Mheshimiwa Herbert James Mtangi, Mjumbe; Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mjumbe; Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mjumbe; Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mjumbe; Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mjumbe; Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mjumbe; Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mjumbe; Mheshimiwa Engineer Ramo Matala Makani, Mjumbe; Mheshimiwa Mbarouk Rajab Mohamed, Mjumbe; Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, Mjumbe na Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mjumbe. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mjumbe; Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, Mjumbe; Mheshimiwa Haroub Mohammed Shamis, Mjumbe; Mheshimiwa Rukia Khassim Ahmed, Mjumbe; Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikila, Mjumbe; Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu, Mjumbe; Mheshimiwa Inocent Edward Kalogeresi, Mjumbe; Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mjumbe; Mheshimiwa Profesa Juma Athman Kapuya, Mjumbe; Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, Mjumbe; Mheshimiwa Saidi Amour Arfi, Mjumbe; Mheshimiwa Salvatory Naluyaga Macheemli, Mjumbe na Mheshimiwa Rita Louise Mlaki, Mjumbe.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Daktari Thomas Didimu Kasilillah, kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa na Katibu wa Kamati hii Ndugu Angumbwike Lameck Ng'wavi kwa kuihudumia Kamati ya Miundombinu kwa ufanisi mkubwa pamoja na kuiandaa Taarifa hii. Nawashukuru pia Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao mzuri wa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Ahsante sana, umetumia muda wako vizuri. Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge wa Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kwa niaba yake Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Zungu. *(Makofi)*

MHE. MUSSA A. ZUNGU – MAKAMU MWENYEKITI, KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa kazi za Kamati kuanzia Februari, 2011 hadi Aprili, 2012 kwa mujibu wa Kanuni ya 114(15), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati hii waliteuliwa kwa mujibu wa Kanuni ya 133, kwa barua yako ya tarehe 8 Februari, 2011. Naomba kuwataja kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mwenyekiti; Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mjumbe; Mheshimiwa Kapteni Mstaafu John Z. Chiligati, Mjumbe; Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mjumbe; Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mjumbe; Mheshimiwa Sadifa J. Khamis, Mjumbe; Mheshimiwa Daktari Muhamed S. Khatib, Mjumbe; Mheshimiwa Betty E. Machangu, Mjumbe; Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mjumbe; Mheshimiwa Mussa H. Mussa, Mjumbe; Mheshimiwa Eugen E. Mwaipasa, Mjumbe; Mheshimiwa Mchungaji Israel Y. Natse, Mjumbe; Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mjumbe; Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan A. Ngwilizi, Mjumbe; Mheshimiwa Rachel M. Robert, Mjumbe; Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mjumbe; Mheshimiwa Mohamed I. Sanya, Mjumbe; Mheshimiwa John M. Shibuda, Mjumbe; Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mjumbe na Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mjumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati hii yameainishwa katika Nyongeza ya Nane, Kifungu cha 8(4) na Kifungu cha 9(2) cha Kanuni za Kudumu za Bunge. Majukumu hayo ni kusimamia Shughuli za Wizara zifuatazo:-

- (i) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa;
- (ii) Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki;
- (iii) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; na
- (iv) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, mbali na majukumu ya kisekta niliyoyataja, Kifungu cha 9(2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kimetaja majukumu mengine kuwa ni:-

- (a) Kuimarisha ushirikiano na Mabunge ya nchi nyingine; na
- (b) Kushughulikia Taarifa za Wawakilishi wa *SADC-PF* na Bunge la Afrika.

Aidha, Kanuni ya 116 imetoa fursa kwa Kamati yoyote ya Kudumu ya Bunge kupendekeza kwa Spika ipewe majukumu ya Nyongeza na vile vile imempa Spika uwezo wa kukabidhi jambo lingine lolote kwa Kamati yoyote kadiri atakavyoona inafaa. Nalijulisha Bunge hili kuwa Kamati ilipendekeza jukumu la kupitia Taarifa ya Ofisi ya Rais kuhusu hali ya usalama nchini litamkwe kuwa la Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekelezwa, baada ya kuwateua Wajumbe wa Kamati hii, majukumu ya msingi yalipangiwa mpango kazi ambao mara zote yalizingatia masharti ya Kanuni ya 114(5), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007. Masharti hayo yalihusu vikao kuitishwa na Spika au Mwenyekiti kwa idhini ya Spika na kwamba Kamati inapaswa kuzingatia fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya shughuli hizo kwa mwaka. Ni kwa msingi huu kila mara Kamati ilijitahidi kufanya kazi zake bila kukiuka masharti hayo lakini kwa kuzingatia tija ya kazi zilizopaswa kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki Kamati ilitekeleza shughuli zake kwa njia ya semina, ziara za ndani na nje ya nchi, kukutana na Mabalizi na Wageni wengine wa Bunge kutoka nje ya nchi, kufuatilia utekelezaji wa Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati pamoja na kupokea na kujadili Taarifa za Hali ya Ulinzi na Usalama nchini. Aidha, Kamati ilizingatia Kanuni ya 114(8) iliyoruhusu Kamati kujiwekea utaratibu. Katika kutekeleza majukumu yake Kamati ilikuwa na utaratibu wa kupitia Taarifa ya Hali ya Ulinzi na Usalama wa raia, mali zao, mipaka na Taifa kwa ujumla ili kujiridhisha kuhusu mustakabali wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, Semina, katika kipindi cha 2011/2012, Kamati ilipata semina mbalimbali zilizolenga kuongeza uelewa katika maeneo inayosimamia. Mbali na semina zilioratibiwa na kuwezesha na Ofisi ya Bunge, Semina ya kwanza ilitolewa na *APRM* Tanzania tarehe 26 Machi, 2011 na ilihusu utaratibu wa *APRM* yaani *African Peer Review Mechanism*. Semina hii iliwawezesha wajumbe kupata uelewa kuhusu *APRM* na umuhimu wake. Semina nyingine ilifanyika tarehe 10 Agosti,

20 APRILI, 2012

2011 Mjini Dodoma ambayo ilihusu utii wa sheria bila shuruti kama ilivyoandaliwa na Jeshi la Polisi nchini. Napenda kutamka kuwa Semina hizi zilikuwa na manufaa katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kupitia na kujadili taarifa za hali ya Kidiplomasia na Ushirikiano. Kama unavyofahamu, Kamati hii ni mojawapo ya Kamati 10 za Kisekta kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane, 7(1), Kanuni za Kudumu za Bunge. Moja ya Sekta ambazo utekelezaji wa majukumu ya Serikali ulifuatiliwa kwa makini ni eneo la Diplomasia ya Uchumi na Ushirikiano wa Kimataifa. Katika kulisaidia Bunge lako Tukufu kufanya kazi yake vizuri, Kamati ilifuatilia sekta hii kwa kuangalia Taarifa za Wizara mbili zinazohusika na jambo hili. Wizara hizo ni Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia mojawapo iliyotumika ni kuzitaka Wizara hizo kuwasilisha Taarifa ya Robo ya Mwaka kuhusu hali ya Diplomasia Afrika Mashariki na Duniani kwa ujumla sanjari na kuonesha jinsi Serikali inavyojipanga na kuzingatia maslahi ya Watanzania na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati zilionyesha kuwa Tanzania ni nchi yenye ushawishi na kuheshimika sana Kikanda na Kimataifa katika uwanja wa Diplomasia. Hakuna ubishi katika hili kwamba Sera ya Mambo ya Nje ya Tanzania inaiweka vizuri nchi yetu Kidiplomasia. Hata hivyo, changamoto mbalimbali na kasoro zilizopo katika utekelezaji zinahitaji kufanyiwa kazi na kuboresha mwenendo wa utendaji.

Mheshimiwa Spika, iliripotiwa kuwa hali ya dunia imeendelea kuwa ya mashaka makubwa jambo linaloathiri nchi nyingi duniani. Hivi karibuni dunia ilishuhudia jinsi mambo ya Ndani ya Libya yalivyoingiliwa na baadhi ya nchi za Ulaya na kuiangusha Serikali ya Marehemu Kanali Muammar Gaddafi wa Libya. Serikali ya Tanzania na nyinginezo Barani Afrika zinatambua mchango wa Marehemu Kanali Muammar Gaddafi kwa nchi za Afrika na Umoja wa Afrika kwa ujumla. Hata hivyo, katika suala hili Umoja wa Afrika ulishindwa kuonesha umoja jambo ambalo lilidhihirisha udhaifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli ulio dhahiri kuwa Bara la Afrika, Tanzania ikiwa ni sehemu ya Bara hilo, limepoteza mwelekeo kutokana na kukosekana kwa uongozi makini. Taarifa zilizoifikia Kamati zinaonesha kuwa matukio ya Libya na Ivory Coast Mwaka 2011 yalionyesha ombwe lililopo katika Bara la Afrika. Ni wazi kuwa Kamisheni

20 APRILI, 2012

ya AU imepwaya katika utatuzi wa migogoro na badala yake Umoja wa Mataifa unaamua utakavyo kuhusu utatuzi wa Migogoro ya Ndani ya Afrika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Nchi za Ulaya na Marekani, Kamati ilijulishwa kuwa Nchi za Ulaya, Wanachama wa Sarafu ya Euro maarufu kama Euro Zone zimekumbwa na hali ya wasiwasi kutokana na mdororo wa uchumi ulioanzia nchi ya Ugiriki na kuendelea kusambaa katika nchi nyingine za Ulaya ikiwemo Italy, Spain na Portugal. Kamati inaitanabahisha Serikali kuhusu tafsiri ya hali hii kwa nchi za Afrika. Ni dhahiri kuwa kwa hali hiyo, misaada kutoka nchi za Ulaya kuja Afrika itapungua kutokana na ukweli kwamba nchi za Ulaya zinakabiliwa na jukumu la kulipa madeni ya ndani pamoja na kufufua uchumi wao sambamba na haja ya kusaidia nchi zilizoathiriwa ndani ya Jumuiya ya Ulaya.

Mheshimiwa Spika, Taarifa za Serikali zinaonesha kuwa tayari viashiria vya tafsiri hiyo vimeanza kujitokeza Tanzania, ikiwemo nchi Wahisani kutotimiza ahadi zao za kuchangia kwenye Bajeti ya Serikali yetu kwa wakati, hali iliyosababisha nakisi ya Bajeti ya Maendeleo. Kamati inasisitiza kwamba, kwa kuwa kuna dalili za hali hii kuchukua muda mrefu ni muhimu kwa Serikali kutahadhari na kujipanga ipasavyo ili kudhibiti mfumko wa bei na kupanda kwa gharama za maisha. Jambo muhimu kuzingatia ni kwamba matarajio ya Watanzania ni ufumbuzi wa matatizo yao kuhusu ugumu wa maisha.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya pili ambayo utekelezaji wa majukumu yake ulifuatiliwa ni Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Ili kujiridhisha na majukumu ya Wizara hii, Kamati ilijiwekea utaratibu wa kupokea Taarifa kuhusu Serikali inavyosimamia maslahi ya Tanzania katika utekelezaji wa Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, utekelezaji wa Itifaki zote chini ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ikiwemo itifaki ya Ushuru wa Forodha pamoja na Itifaki ya Soko la Pamoja. Katika kuendelea kufuatilia hatua za Mtangamano wa Afrika Mashariki, Kamati ilipenda kujua hatua iliyofikiwa kuelekea kwenye Shirikisho la Kisiaa la Afrika Mashariki na kama kila hatua imezingatia maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, hatua ya awali ya mtangamano wa Afrika Mashariki ni Umoja wa Forodha (*Custom Union*). Katika ufuatiliaji uliofanywa na Kamati ilibainika kuwa Wakuu wa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walipokuwa kwenye Mkutano wao wa tarehe 19 Aprili, 2011 waliagiza ufanyike utafiti juu ya namna ya kuanzisha Himaya moja ya Forodha (*Single Customs Territory*). Utafiti huo

ulianza mwezi Oktoba, 2011 na unatarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2012. Nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ilipokea Taarifa kwamba ili kujipanga vema kwa upande wetu Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilishirikiana na Wizara ya Fedha pamoja na Wadau wengine mbalimbali kufanya utafiti juu ya suala hilo. Kamati inakumbusha kuwa matokeo ya utafiti uliofanywa na Wizara zetu yatumike kujipanga vizuri kihoja na mkakati.

Mheshimiwa Spika, Soko la Pamoja ni hatua ya pili ya ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mujibu wa Ibara ya 76(2) inayosema kuwa hatua hii ni endelevu kutegemea majedwali yatakayopitishwa na Baraza la Mawaziri lililoanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya tisa (9) ya Mkataba wa kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ibara hiyo inasema:

Nanukuu: *"The establishment of the common market shall be progressive and in accordance with schedules approved by the council"*.
Mwisho wa kunukuu.

Katika utekelezaji wa itifaki ya soko la pamoja zipo Sheria zinazotakiwa kurekebishwa nchini Tanzania na pia katika nchi nyingine Wanachama. Kamati ilijulishwa kuwa kwa upande wa Tanzania Sheria hizo zimeanishwa kwa ajili ya mchakato wa marekebisho. Jambo muhimu linalosisitizwa na Kamati ni kuweka maslahi ya Taifa mbele katika mchakato huo.

Hatua ya tatu katika Mtangamano wa Afrika Mashariki ni umoja wa sarafu (*common currency*). Ni kweli tunafahamu kuwa kinadharia Umoja wa Sarafu unaweza kuwa na manufaa kwa nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania ikiwemo. Kwa mfano, hatua hii inaweza kupunguza gharama za miamala ya Kibiashara (*Transaction cost*) ndani ya nchi wanachama. Hata hivyo, ni vema mambo kadhaa yakawekwa sawa kabla ya kukamilisha itifaki ya Umoja wa Sarafu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kwa upande wetu tuna haja ya kujiridhisha ipasavyo kuhusu viwango vya ubadilishanaji wa fedha za kigeni (*exchange rate mechanism*); mfumo stahiki wa sera ya fedha katika umoja wa fedha (*Appropriate Monetary Policy Framework*) na vigezo vya kuoanisha uchumi mpana wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*Macro Economic Convergence Criteria*). Ni muhimu kuzingatia ushauri wa kitaalam ili kutetea vema maslahi ya Watanzania na Taifa kwa ujumla.

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, napenda pia kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Kamati imefuatilia kwa karibu mwenendo wa Mtangamano wa Afrika Mashariki kuelekea Shirikisho la Kisiasa (*Political Federation*). Tunafahamu kuwa wenzetu wa Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi wanaunga mkono hoja ya kuharakisha Shirikisho la Kisiasa. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri tulioutoa kuwa Mtangamano wa Afrika Mashariki uende hatua kwa hatua. Aidha, kila mara Kamati imekuwa ikisisitiza kuwa Watanzania walio wengi wana hofu kubwa na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Ni vema hofu iliyopo, kero na changamoto zinazodainishwa na wananchi zifanyiwe kazi na kushughulikiwa pamoja na kuwaelimisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, kushughulikia taarifa za Wawakilishi katika Bunge la Afrika na Bunge la Afrika Mashariki. Pamoja na majukumu ya jumla ya Kamati za Sekta kama yalivyoainishwa katika fasili ya (1) ya Kifungu cha (9) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati hii imepewa jukumu la kushughulikia Taarifa za Wawakilishi katika Bunge la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika. Ili kutekeleza jukumu hilo Kamati ilikutana na Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki mara mbili na Wabunge wa Bunge la Afrika mara moja. Katika vikao hivyo, Kamati ilipokea maelezo ya Wawakilishi hao kuhusu shughuli zao, changamoto na maoni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu taarifa ya Wawakilishi katika Bunge la Afrika, tarehe 9 Februari, 2012, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wawakilishi hao waliochaguliwa na Bunge lako Tukufu tangu tarehe 13 Aprili, 2011. Wakati walipotoa Taarifa yao Wawakilishi wetu katika Bunge la Afrika, walikuwa wamehudhuria Mikutano miwili. Kwa mujibu wa Taarifa ya Wawakilishi hao, Umoja wa Afrika na Bunge la Afrika wamelifanya suala la amani na usalama kuwa ajenda ya kudumu katika Mikutano yao.

Taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati inaonesha migogoro iliyofanyiwa kazi na hatua zilizochukuliwa kuikabili migogoro hiyo. Kamati iliendelea kuthibitisha kuwa suala la mgogoro wa Libya limepata maelezo na mtazamo unaotofautiana. Wapo wanaoamini kuwa sababu kubwa ya mgogoro huo ni kukosekana kwa mageuzi ya kidemokrasia na ukiukwaji wa haki za binadamu. Wapo pia wenye maoni kuwa mgogoro huu unatokana na ajenda isiyokwisha ya nchi za Magharibi kutaka kudhibiti rasilimali za Libya.

Mheshimiwa Spika, tukitafakari kwa kina na umakini, Serikali ya Tanzania na wananchi wake kama ilivyo kwa Serikali za nchi nyingine za Afrika na wananchi wake, tunayo mambo ya kujifunza na kuzingatia

20 APRILI, 2012

katika mgogoro huu. Kwa suala hili Kamati inabainisha kuwa ingawa Kanali Muammar Gaddafi ameondolewa madarakani na hayupo hai kwa sasa, Mustakabali wa nchi ya Libya upo matatani. Athari ya hali hiyo kama ilivyoripotiwa ni pamoja na kuzagaa kwa silaha ndogo ndogo na nyepesi jambo linaloathiri amani na usalama nchini humo. Ni jambo linalosikitisha kwa wenzetu wa Libya kuwa katika hali hiyo. Hata hivyo, nchi yetu ichukue tahadhari ya kutosha kutokana na matukio yaliyotokea huko na kuzagaa kwa silaha.

Mheshimiwa Spika, migogoro mingine iliyotolewa Taarifa ni:-

- (i) Mgogoro nchini Ivory Coast;
- (ii) Mgogoro nchini Tunisia;
- (iii) Mgogoro nchini Misri;
- (iv) Mgogoro wa watu wa Saharawi (*Western Sahara*); na
- (v) Mgogoro nchini Somalia;

Kwa mujibu wa Taarifa iliyotolewa kwenye kikao cha Kamati cha tarehe 7 Februari, 2012, Bunge la Afrika linaushauri Umoja wa Afrika kusimamia misingi ya utawala bora. Aidha, Umoja wa Afrika umeshauriwa kusimamia kwa dhati Mikataba, Itifaki na Protokali zinazohusu haki za binadamu; utawala bora na demokrasia ambazo nchi wanachama zilisaini na kuridhia.

Msisitizo uliwekwa kwamba Umoja wa Afrika uchukue hatua kali kadiri inavyopaswa dhidi ya Viongozi na Wakuu wa Nchi wanaokiuka Mikataba, Itifaki na Protokali walizosaini na nchi zao kuridhia. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Kamati inaafiki msimamo huo wa Bunge la Afrika na hasa kwa kuwa kinyume na hatua hiyo madhara yake yatakuwa makubwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu wa kujitathmini na kukosoana wenyewe, *African Peer Review Mechanism (APRM)* uliobuniwa na viongozi wa Afrika mwaka 2002, taasisi hiyo ilianza rasmi mwaka 2003 baada ya idadi ya wanachama iliyotakiwa kusaini mkataba huo kutimbia. Kwa upande wa Tanzania Kamati ilibaini kwamba Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) zinaonesha kuwa tarehe 1 Februari, 2005, katika Mkutano wake wa kumi na nne, kikao cha kumi, Bunge la Nane liliridhia mchakato huu kuanza hapa nchini kwa kupitisha *Azimio la kuridhia Mkataba wa Tanzania kujiunga na Utaratibu wa African Peer Review Mechanism*

20 APRILI, 2012

(APRM) chini ya Mpango wa Ushirikiano mpya ili kuleta Maendeleo Barani Afrika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mantiki ya utaratibu wa kujitathmini na kukosoana wenyewe kwa vigezo vya utawala bora, Kamati ina maoni kuwa Tanzania kama ilivyo kwa nchi nyingine za Afrika inapaswa kutilia maanani utaratibu huu wa APRM na kuboresha zaidi sera na taratibu za kiutendaji pale dosari zitakapojitokeza.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine muhimu kwa upande wa Umoja wa Afrika ni kuhusu Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Mahakama hii ilianzishwa kwa mujibu wa Ibara ya kwanza (1) ya Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na watu wa mwaka 2004. Ni heshima kubwa kwa Tanzania kutokana na uamuzi kwamba Makao Makuu ya Mahakama hiyo yawe Mjini Arusha. Ni wajibu wetu kuiendeleza heshima hiyo Kimataifa lakini kwa kuizingatia maslahi ya Watanzania na Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Taarifa za Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, Kamati ilipitia Taarifa zao na kubaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika utaratibu wao wa kuripoti kwenye Bunge lako Tukufu. Kwa mfano, pamoja na Kanuni za Bunge kuainisha jukumu la Kamati kushughulikia Taarifa zao, lakini wawakilishi hawa hawajawekewa utaratibu wa kupata mawazo ya Bunge letu kabla ya kwenda kwenye Bunge la Afrika Mashariki. Ingawa Kanuni zetu haziwazuii kufanya hivyo, bado kuna umuhimu wa Bunge letu kuweka utaratibu mzuri zaidi na madhubuti utakaowataka wawakilishi hao kuwajibika vema kwa Bunge na kufanya kazi ya uwakilishi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Kushughulikia Taarifa za Wawakilishi katika Chama cha Kibunge cha Jumuiya ya Madola (CPA) na SADC-PF. Kama unavyofahamu Bunge la Tanzania ni Mwanachama wa Chama cha Kibunge cha Jumuiya ya Madola (*Commonwealth Parliamentary Association - CPA*). Chama hiki kimehusisha nchi Wanachama wa Jumuiya ya Madola isipokuwa Brunei ambayo haina Bunge linalochaguliwa moja kwa moja na wananchi. Chama hiki ni muhimu kwa uimarishaji wa Diplomasia ya Kibunge pamoja na kujenga uwezo wa Mabunge Wanachama. Mambo haya hufanyika kwa njia ya machapisho, semina, warsha, makongamano na programu nyingine za kujenga uwezo. Bunge letu kama yalivyo Mabunge mengine ni Taasisi inayoimarika na kukua.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa ambazo Kamati imezipata Wawakilishi wetu katika CPA wamejielekeza kwenye mambo ya msingi

yanayoweza kuongeza uwezo wa Bunge letu ili kukuza tija kwa wananchi pamoja na kuwa chombo halisi cha uwakilishi wa watu. Ofisi ya Bunge na Serikali wametoa ushirikiano wa kutosha kwa Wawakilishi wetu kuwa na ushiriki mzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jukwaa la Kibunge la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC parliamentary forum*) lililoanzishwa Mwaka 1997, ushiriki wa Bunge letu unaendelea. Jukwaa hili lilianzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 9(2) ya Mkataba wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*The Southern African Development Community - SADC*). Ushiriki wa Wawakilishi wetu katika Jukwaa hilo umewezesha kubadilishana uzoefu na mawazo miongoni mwao na wawakilishi wa Mabunge ya Nchi Wanachama wa SADC.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine, Mkutano wa thelathini wa SADC - PF uliofanyika Victoria Falls Zimbabwe tarehe 5 hadi 12 Novemba, 2011 uliridhia chaguzi za Wenyeviti na Makamu wa Kamati za Kudumu kwa mujibu wa Katiba ya SADC-PF ambapo Mheshimiwa Mohamed H.J. Mnyaa, Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Biashara na Mahusiano (*Trade Development and Intergration Committee*). Tunampongeza kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, dhana ya Diplomasia na Uhusiano wa Kibunge haitumiki na Bunge la Tanzania tu, bali na Mabunge mengi duniani. Dhana hii inatumika kuboresha utendaji wa Mabunge katika kuzisimamia Serikali zao, kuwawakilisha watu na Majimbo ya Uchaguzi kwa ubora zaidi. Kwa maelezo ya aliyewahi kuwa Spika wa Bunge la Udachi, Mheshimiwa Frans W. Weiglas pamoja na Katibu wa Bunge Msaidizi wa Kamati ya Kudumu ya Ulinzi ya Bunge hilo, Ndugu Gonie de Boer, katika makala waliyoichapisha kwenye Jarida la *The Hague Journal of Diplomacy*, Toleo la Mwaka 2007, dhana ya Diplomasia ya Kibunge inaongeza uelewa wa pamoja na kusaidia kuboresha namna Bunge linavyoweza kuisimamia Serikali kwa Ufanisi.

Kwa mantiki hiyo, Kamati ina maoni kuwa Bunge letu liendeleo kujiweka sawa katika eneo hili na kuboresha zaidi utaratibu unaotumika kujiimarisha katika Diplomasia ya Kibunge. Aidha, Kanuni za Kudumu za Bunge zinahitaji kuboreshwa zaidi ili kuongeza tija ya diplomasia ya Kibunge na uhusiano wa Kimataifa katika muktadha wa Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya ulinzi na usalama kwa ujumla. Suala la ulinzi na usalama ni la msingi kwa ustawi na maisha ya watu. Ni

20 APRILI, 2012

jambo muhimu kwa demokrasia ya kweli. Ili kujiridhisha na hali ya ulinzi wa mipaka yetu na usalama wa Taifa, raia na mali zao, Kamati ilijiwekea utaratibu wa kupitia taarifa hizo kila ilipokutana. Mantiki ya kufanya hivyo ni kama ilivyoelezwa na Ushirikiano wa Kibunge Duniani (IPU) ambao wamesema:

Nanukuu: *“The executive may not be fully aware of the security issues which are priorities for citizens. Parliamentarians are in regular contact with the population and well – placed to ascertain their views. They can subsequently raise citizens’ concerns in Parliament and see to it that they are reflected in security laws.”* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, ili kuishauri vema Serikali na kuliwezesha Bunge kuisimamia Serikali ipasavyo, utaratibu huu wa kupokea na kujadili Taarifa za Hali ya Ulinzi na Usalama ulifaa sana na mara zote Serikali ilitoa majibu ya hoja mbalimbali zilizojitokeza kwenye taarifa hizo. Naomba kulijulisha Bunge hili kuwa kwa mujibu wa taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati, hali ya ulinzi kwa ujumla ni shwari, hali ya usalama wa raia na mali zao imeendelea kuimarishwa na Taifa kwa ujumla wake linaendelea vizuri. Serikali kupitia taasisi zake imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi ambazo zinawahakikishia usalama wao kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mlipuko wa mabomu katika kikosi cha 511-Gongo la Mboto. Tarehe 16 Februari, 2011 ilitokea mlipuko katika kikosi cha 511 na kusababisha maafa. Wananchi walitaharuki na kukimbilia vituo vya Daladala, vituo vya Mafuta, Uwanja wa Taifa na Sabasaba. Kutokana na hali hii, tarehe 27 Februari, 2011 Kamati ilitembelea Kikosi cha 511 eneo la Gongo la Mboto. Aidha, Tarehe 28 Februari, 2011 Kamati ilikutana na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Katika kikao hicho Mheshimiwa Waziri alitoa Taarifa ya Mlipuko wa Mabomu na utekelezaji wa mapendekezo ya Baraza la Uchunguzi wa Mlipuko ya Mbagala. Katika maelezo hayo, Kamati ilielezwa aina kuu mbili za mapendekezo. Kwanza mapendekezo ya muda mfupi na pili ni mapendekezo ya muda mrefu. Naomba kulijulisha Bunge kuwa Kamati ilipata fursa ya kushauri na kutoa maoni kuhusu eneo hili na kwamba Taarifa za Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa zinaonesha kuwa baadhi ya mapendekezo yamefanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usalama wa raia na mali zao, Kamati ilifuatilia jitihada zinazoendelea kuimarisha hali hiyo. Kila baada ya miezi mitatu, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya hali ya usalama wa raia na mali zao. Taarifa kutoka Serikalini zilionyesha kuwa kwa ujumla hali ya usalama wa raia na mali zao ni shwari. Hata hivyo, yapo matukio

mbalimbali kuhusu ujambazi, uporaji na makosa dhidi ya binadamu yaliyoripotiwa. Naomba kueleza kuwa kila mara Kamati ilipopokea na kujadili Taarifa hiyo ilijikita kwenye chanzo cha matukio hayo na kutoa ushauri kuhusu jinsi ya kuimarisha usalama.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ulinzi wa mipaka yetu, vyombo vya ulinzi na usalama vimejipanga imara na hali imeendelea kuwa shwari. Hata hivyo, Kamati inasisitiza kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuongeza juhudi za kutatua mgogoro wa Mpaka wa Malawi ili kuondoa hofu kubwa kwa wananchi wa maeneo ya mpaka huo na kuwafanya waishi kwa amani. Msimamo wa Tanzania ni kuwa mpaka baina ya Tanzania na Malawi unapita katikati ya Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba Serikali inatimiza wajibu wake wa kuliweka Taifa hili katika hali ya usalama, amani na utulivu tuliendelea kufuatilia taarifa kuhusu usalama wa Taifa hili. Taarifa zilizokuwa zikiwasilishwa kwenye vikao vya Kamati kila mara zilionyesha kuwepo kwa utulivu, amani na usalama kwa ujumla katika Taifa yetu. Hata hivyo, kutokea kwa ishara za uvunjifu na upotevu wa amani ni jambo lililowahi kuripotiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilichukua hatua madhubuti dhidi ya vyanzo vya uvunjifu wa amani, utulivu na usalama wa nchi. Mambo yaliyoripotiwa na kunasibishwa na hali ya utulivu, amani na usalama nchini ni pamoja na hali ya chakula, uchumi, tiba asililia, huduma za Wakimbizi, mabadiliko ya kisiasa duniani, upatikanaji na uhalali wa bidhaa katika uchumi pamoja na mambo mengine ya kiuchumi kama vile mfumko wa bei, gharama za maisha na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, mambo haya yalitolewa ufafanuzi sambamba na kueleza hatua zinazochukuliwa na Serikali. Katika kufuatilia Taarifa hizo Kamati ilihoji mambo mbalimbali ya msingi na kutoa maoni na ushauri kwa Serikali. Aidha, Kamati ilibaini kuwa tishio kubwa la uharamia linaathiri gharama za uingizaji bidhaa muhimu kutoka nje ya nchi. Kampuni za Bima zimeongeza gharama ya usafirishaji mizigo jambo linaloathiri bei ya bidhaa hizo zinapouzwa Tanzania. Ingawa tatizo hilo kimsingi lipo nchini Somalia lakini athari yake ni kubwa kwa nchi nyingine ikiwemo Tanzania na nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara. Katika kutekeleza jukumu la Kamati kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara zilizo chini yake kama zilivyoainishwa katika Nyongeza ya Nane, Kifungu cha 8(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, Kamati ilitekeleza jukumu hili mwezi Mei na Juni kwa kuchambua Makadirio ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la

20 APRILI, 2012

Kujenga Taifa, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kutekeleza jukumu hilo Kamati ilipokea maelezo kutoka Wizara zinazohusika na kutaka ufafanuzi katika maeneo mbalimbali pale ilipobidi. Baada ya kuridhika na ufafanuzi uliotolewa Kamati ilipitisha Makadirio ya Wizara zote na kuwasilisha maoni yake Bungeni ikiwa ni pamoja na kuliomba Bunge lipitisha makadirio ya Wizara hizo kama tulivyoshuhudia katika Mkutano wa Nne wa Bunge hili la Kumi. Aidha, Kamati ilipobaini jambo muhimu linalohitaji kuzingatiwa iliitumia fursa iliyotolewa na Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Kifungu cha 2(3)(b) kuwasilisha kwenye Kamati ya Uongozi, hoja zote zenye maslahi kwa Taifa na zikapelekwa Serikalini ili zifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ufuatiliaji wa utekelezaji wa Bajeti. Katika kuisimamia Serikali, Bunge lina wajibu wa kufuatilia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Kwa kuwa sehemu kubwa ya shughuli za Bunge hufanyika kupitia Kamati zake, Kamati hii ilitekeleza jukumu la Bunge kwa kufuatilia namna Wizara zilizo chini yake zilivyotekeleza Bajeti ya Mwaka 2011/2012 kwa kipindi cha nusu Mwaka. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa pamoja na ufinyu wa Bajeti kwa Wizara hizo, Kamati imebaini kuwepo kwa matatizo makubwa mawili: Moja ni fedha kutotolewa kama ilivyoidhinishwa na Bunge na pili ni kuchelewa upatikanaji wa fedha hizo kutoka Hazina. Hali hii inaathiri utekelezaji wa mipango iliyowekwa na hata kuathiri namna ya kuzingatia maoni na ushauri uliotolewa na Kamati pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine wakati wa majadiliano ya Bajeti husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ziara kutembelea Taasisi mbalimbali. Ziara ni mojawapo ya njia iliyotumika kutekeleza majukumu ya msingi ya Kamati hii. Ingawa Kanuni ya 114(4) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007 inatamka kuwa Mikutano ya Kawaida ya Kamati za Kudumu za Bunge itafanyika Dodoma, Dar es Salaam au Zanzibar, kazi ya Kamati ya Kudumu za Bunge iliyoainishwa katika Nyongeza ya Nane, Kifungu cha 9(1)(d) haiwezi kutekelezwa kwa ufanisi bila kufanya ziara pale inapobidi. Kwa kuzingatia hilo, baada ya kupata kibali chako Kamati ilifanya ziara kutembelea Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ziara nje ya nchi, tarehe 4 – 8 Julai, 2011 baadhi ya Wajumbe walikwenda nchini Malaysia na kuona jinsi utaratibu wa Vitambulisho vya Taifa, unavyotumika na kuisaidia nchi hiyo kuzingatia mambo muhimu. Ujumbe huo nchini Malaysia ulikuwa na

20 APRILI, 2012

Wajumbe wanane na Katibu. Aidha, katika kutekeleza jukumu la Kamati lililoainishwa katika Nyongeza ya Nane, Kifungu cha 9(2)(a), Wajumbe wanne walifanya ziara nchini Singapore, India na Malaysia. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ziara hizo ziliisaidia Kamati na Bunge kwa ujumla katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, wajumbe tisa na Katibu wa Kamati walikwenda Bunge la Umoja wa Nchi za Ulaya kwa ziara ya mafunzo na kujifunza mambo mengi ikiwemo kuona namna ya kuishauri Serikali katika eneo la diplomasia ya uchumi na namna ya kuwatuma Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri. Baada ya maelezo kuhusu kazi zilizotekelezwa, naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, pamoja na Diplomasia na Ushirikiano wa Kibunge.

Mheshimiwa Spika, kwanza, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kufuatia ziara za Kamati katika vyombo vya ulinzi pamoja na Taarifa za Wizara zilizokuwa zikitolewa mbele ya Kamati, yafuatayo ni maoni na ushauri kwa Wizara hii:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wizara ya Ulinzi na JKT – Fungu 57:-

(i) Serikali iendeleze juhudi za kuboresha mazingira ya kazi ya Askari wetu;

(ii) Madeni binafsi ya Askari wa Jeshi la wananchi yalipwe kwa wakati;

(iii) Kambi zote za JWTZ na JKT nchini zipatiwe Nyaraka za maeneo yao ili kuziwezesha kusimamia vema maeneo hayo. Vile vile Kambi hizo ziwekewe uzio sambamba na kuheshimu eneo la Wazi baina ya Kambi na raia;

(iv) Kasi ya kutatua mgogoro ya ardhi kwenye maeneo ya Kambi iongezeke kwa ushirikiano baina ya Wizara ya Ulinzi na JKT pamoja na Wizara na Mamlaka nyingine za Kiraia;

(v) Malipo kwa ajili ya Huduma muhimu kwenye Kambi za Jeshi yapewe umuhimu na kushugulikiwa kwa wakati;

20 APRILI, 2012

(vi) Utaratibu wa diplomasia katika Ulinzi (Defence Diplomacy) uimarishwe kulingana na mazingira yalivyo;

(vii) Ili kukuza uwezo wa Watendaji Serikalini wa kusimamia maslahi ya Taifa, Serikali iandae mpango wa Viongozi na Watendaji wake Waandamizi kupata mafunzo katika Chuo cha Ulinzi wa Taifa;

(viii) Serikali iongeze kasi katika mchakato wa kupitia Sheria ya Ulinzi wa Taifa (*National Defence Act*) na maandalizi ya Sera ya Ulinzi na usalama wa Taifa (*National Defence and Security Policy*) ili kukamilisha mambo hayo muhimu na kuondoa hisia za kuwapo kwa uzembe katika kuyashughulikia masuala hayo;

(ix) Jeshi la Wananchi wa Tanzania liimarisha Mipaka ya Maeneo yake na kudhibiti tabia ya watu wanaojenga katika maeneo hayo;

(x) Kuna umuhimu mkubwa wa Serikali kuwa na utamaduni wa kuwatumia Wanajeshi wastaafu wenye utalam adimu (*Rare- Profession*);

(xi) Inapotokea ulazima wa kuwapa Maafisa wa Jeshi waliostaafu Mkataba wa kuendelea na kazi, jambo hilo lifanyike sambamba na maandalizi ya kuwapata watakaochukua nafasi zao;

(xii) Serikali iwe na Kanuni, taratibu na utamaduni bora unaowaandaa vema Maafisa wa Jeshi na Askari kwa maisha yao baada ya kustaafu;

(xiii) Ili kuliinua Taifa kwa kupitia Sekta ya Kilimo ni vizuri Serikali iweke utaratibu wa kulitambua Jeshi la Kujenga Taifa kama Mkoa mmojawapo katika Masuala ya Kilimo. Aidha utaratibu huo utumike kuiwezesha Serikali kutekeleza juhudi za kiuwekezaji na uwezesaji kwenye Jeshi la Kujenga Taifa ili kuongeza uzalishaji;

(xiv) Utaratibu wa mafunzo ya Jeshi la kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria uharakishwe kutekelezwa sambamba na kuifanyia mapitio sheria ya Jeshi la kujenga Taifa;

(xv) Vyombo vya Habari vielimishwe na kuhamasishwa ili vizingatie vema maslahi ya Taifa na uzalendo vinaporipoti mambo yanayogusa masuala ya Ulinzi;

(xvi) Inapotokea wananchi wanajenga katika maeneo ya Kambi za Jeshi pamoja na ujenzi usiozingatia "buffer zone" hatua zichukuliwe mapema iwezekanavyo kusitisha hali hiyo;

20 APRILI, 2012

(xvii) Serikali ilianganalie kwa umakini mkubwa suala la mgogoro wa mpaka kati ya Tanzania na Malawi katika ziwa Nyasa ili kuepusha madhara makubwa yanayoweza kujitokeza;

(xviii) Ili kuimarisha ulinzi wa mipaka yetu Serikali ifanye juhudi ya kuboresha Barabara za mipakani; na

(xix) Pamoja na kuipongeza Serikali kwa kukamilisha ujenzi wa Chuo cha ulinzi wa Taifa (*National Defence College*) na kujipanga kwa kozi ya kwanza kuanza mwezi Septemba, 2012, Kamati inashauri kuwa Serikali itoe tamko la kuanzisha NDC na baadaye kuandaa utaratibu wa kuwa na Sheria ya NDC. Aidha, utaratibu mzuri wa kugharamia mafunzo katika NDC uandaliwe kwa kutenga fedha za mafunzo hayo katika Kasma ya Chuo hicho.

Mheshimiwa Spika, pili, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwa kuzingatia ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii na idara zake pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama vilivyo chini yake, Kamati ina maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(a) Jeshi la Polisi:-

(i) Maboresho yanayoendelea katika Jeshi la Polisi yaliwezeshe Jeshi hilo kuongeza Utaalamu na Matumizi Bora zaidi ya Vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuongeza ufanisi na kupunguza uhalifu;

(ii) Mpango mzima wa Maboresho ndani ya Jeshi la Polisi uzingatie umuhimu wa kuandaa vema hali za Askari watakapofikia umri wa kustaafu;

(iii) Jeshi la Polisi lijiimarisha zaidi katika utekelezaji wa jukumu la kusimamia Sheria za barabarani na matumizi ya alama za barabarani;

(iv) Ili kuliongezea uwezo Jeshi la Polisi, Halmashauri za Wilaya, Miji, Jiji na Manispaa zitoe msaada kwa kulisaidia Jeshi la Polisi kwa namna bora itakayowezezana kujenga vituo vya Polisi katika Halmashauri hizo;

(v) Jeshi la Polisi liboresheshe menejimenti na udhibiti wa usafiri wa Pikipiki ili kuzua ajali za Barabarani zinazosababishwa na Pikipiki;

20 APRILI, 2012

(vi) Ukiukwaji wa Sheria na Mauaji yanayofanywa na makundi ya watu ni mambo yanayopaswa kufanyiwa kazi na kusimamiwa ipasavyo na Jeshi la Polisi. Hali hii isipodhibitiwa itahatarisha maisha ya watu, usalama wa raia na mali zao. Tafiti zinaonesha kuwa hali hii inazidi kukua. Kwa mfano, Taarifa ya Haki za Binadamu iliyotolewa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Mwaka 2010 inaonesha kuwa Tatizo la makundi yanayokiuka haki za binadamu linakua:

Nanukuu: *"The LHRC's 2010 survey indicates that mob violence is still very rampant in country, especially in big cities, lake zones and Southern regions"*. Mwisho wa kunukuu.

Kamati inashauri kuwa Polisi iyafanyie kazi maelezo hayo ili kuimarisha hali ya amani, utulivu na usalama wa raia na mali zao;

(vii) Ili kupunguza mauaji yanayofanywa na watu kwa jina la wananchi wenye hasira kali ni vema Jeshi la Polisi lisimamie vituo vya Polisi ili kujenga imani kwa wananchi; na

(viii) Pamoja na jitihada kubwa za Serikali kuliwezesha Jeshi la Polisi bado kuna umuhimu mkubwa wa kuendelea kuliwezesha Jeshi hilo kifedha na vitendea kazi ili kuimarisha ipasavyo usalama wa raia na mali zao katika maeneo mbalimbali nchini.

(b) Jeshi la Magereza:-

(i) Serikali iongeze kasi ya kurekebisha Sheria zinazosababisha msongamano Magerezani;

(ii) Jeshi la Magereza liwezeshe zaidi kwa kulipa zana na fedha za kutosha ili liweze kuzalisha chakula chao na ziada kwa ajili ya soko. Aidha, Jeshi la Magereza wabainishe Magereza yanayoweza kujikita katika Kilimo na kuongoza uzalishaji wa mazao yanayowezekana kwa mazingira ya Magereza husika;

(iii) Muundo wa Kamati za kusukuma kesi (*Case flow Management Committee*) uangaliwe upya ili kuziwezesha Kamati hizo kukutana na kuwa na tija katika jitihada za kupunguza msongamano Magerezani; na

(iv) Ili kupunguza msongamano Magerezani, mojawapo ya njia za kufanya hivyo ni kupitia upya urefu wa muda wa kuchunguza tuhuma kisheria, kuongeza watumishi wa kutosha katika Mhimili wa Mahakama pamoja na kuboresha miundombinu ya chombo hicho.

(c) Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji:-

(i) Serikali iongeze juhudi ya kukiwezesha Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji kwa kukipatia vitendea kazi bora na vya kutosha ili kuimarisha utendaji kazi zao kwa mujibu wa Sheria;

(ii) Sheria na Kanuni zinazohusika na tahadhari ya matukio ya moto zisimamiwe vema;

(iii) Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji kiwe na ubunifu kuhusu utozaji wa gharama za huduma zake ili kukuza mapato na hatimaye kujitegemea katika utendaji kazi wake. Aidha, uwekwe utaratibu wa kima cha majengo kulazimika kulipiwa Kodi ya Hadhari ya moto na ukaguzi wake; na

(iv) Serikali iandae utaratibu wa mafunzo ya lazima ya Zimamoto na uokoaji kwa Taasisi ambazo Ofisi zake zinakuwa na mkusanyiko wa watu wengi.

(d) Huduma ya Wakimbizi:-

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu sasa Tanzania imekuwa na ukarimu kwa kupokea Wakimbizi. Taarifa zilizokuwa zikitolewa kwenye vikao vya Kamati, zinaonesha kuwa hali ya usalama katika nchi jirani imeendelea kuimarika na kwamba Wakimbizi waliokuwapo Tanzania wanaweza kurudi nchini kwao. Kwa hali hiyo Kamati inashauri kuwa:-

(i) Kambi zote za Wakimbizi nchini Tanzania zifungwe Rasmi; na

(ii) Maeneo yaliyokuwa yakitumiwa kama Kambi za Wakimbizi yaboreshwe kuwezesha matumizi mengine sambamba na kuzingatia taratibu zote zinazopaswa kufuatwa katika hatua hiyo.

(e) Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa:-

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa yanazingatia dira na dhima ya Mamlaka hiyo. Kamati inafahamu kuwa dhima ya Mamlaka ya vitambulisho vya Taifa ni kutoa vitambulisho kwa Watanzania, Wageni wakazi na kutunza Daftari la Utambuzi kwa lengo la kuimarisha usalama na amani, kiuchumi na kijamii na kwa Maendeleo ya Taifa. Kwa kuzingatia dhima hiyo Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa nchini iwezeshe zaidi kifedha na vifaa ili kuwa na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, idara na Taasisi za Serikali ambazo ni Wadau Wakubwa katika zoezi la utambuzi na utoaji vitambulisho zitoe ushirikiano wa kutosha;

(ii) Ili Mamlaka hii ifanye kazi kwa ufanisi na kuwa na tija, HAZINA ielekezwe kutoa pesa kwa Mamlaka hii kwa wakati na kuiwezesha kufanya kazi kwa kasi na kwa ubora wa kutosha;

(iii) Serikali iwe makini katika zoezi la utambuzi sambamba na kutumia vyombo mbalimbali kusaidia kubaini wasiostahili kupewa vitambulisho vya Taifa;

(iv) Viongozi wa Serikali za Mitaa waandaliwe vema na kutakiwa kutoa ushirikiano mkubwa katika ukusanyaji wa taarifa binafsi za watu wanaostahili kupewa vitambulisho vya Taifa; na

(v) Utaratibu wa kumbukumbu na usajili wa watoto mara tu wanapozaliwa uimarishwe na kuhusianishwa na mchakato wa mtoto huyo kupatiwa vitambulisho watakapofikia umri unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, tatu, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni jambo muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii iwapo Serikali zote za nchi wanachama zitakuwa makini. Kwa upande wa Tanzania, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ndiyo yenye dhima ya kuiwezesha Tanzania kunufaika kiuchumi, kijamii na kisiasa kutokana na kuwa mwanachama. Kwa kuzingatia maelezo hayo pamoja na taarifa mbalimbali zilizowasilishwa kwenye vikao vya Kamati, yafuatayo ni maoni na ushauri kuhusu Wizara hii:-

(i) Serikali iongeze kasi ya maandalizi ya Sera ya Taifa ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mkakati wa Sera hiyo; Katika Bajeti ya mwaka 2010/2011 na ile ya 2011/2012, Wizara ilipanga kukamilisha sera hiyo lakini hadi sasa Sera haijakamilika;

(ii) Ili kulinda heshima ya Taifa letu katika ushirikiano wa Afrika Mashariki ni vema Serikali iwe na utaratibu wa kulipa michango yake kwa wakati. Hadi kufikia mwezi Februari, 2012, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki haikuwa imelipa mchango uliokuwa unatakiwa kulipwa kabla ya tarehe 31 Desemba, 2011;

(iii) Kwa kuwa hati ya makubaliano (*Memorandum of Understanding – MOU*) ya ushirikiano wa ujenzi wa Reli ya Tanga – Arusha – Musoma – New Kampala imekamilika, ni vema Serikali ya Tanzania ikaongeze ushawishi na kupata juhudi ya pamoja katika kufanikisha mradi huu;

(iv) Katika utekelezaji wa makubaliano maalum ya ushirikiano katika nyanja za ulinzi (*Memorandum of Understanding of Cooperation in Defence*), Serikali iliwezeshe Jeshi letu kutumia fursa hiyo ipasavyo na kuimarisha zaidi utayari wa kukabiliana na changamoto yoyote ya kiulinzi, kiusalama pamoja na majanga mbalimbali;

(v) Ushirikiano wa Afrika Mashariki utumike kuhakikisha kuwa unapatikana msimamo madhubiti na wa pamoja kuhusu suala la kodi ya kusafirisha bidhaa nje (*Export Tax*) kuingizwa katika makubaliano ya ubia wa kiuchumi (*Economic Partnership Agreements*). Jambo hili ni miongoni mwa masuala yenye mvutano katika EPA na kama Jumuiya ya Afrika Mashariki haitakuwa na msimamo mmoja mustakabali wa Jumuiya hiyo kiuchumi utakuwa matatani;

(vi) Wizara ya ushirikiano wa Afrika Mashariki iimarishe mawasiliano na majadiliano baina yake na Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, Sura ya Tanzania, kabla na baada ya kila Mkutano wa Bunge la Afrika Mashariki. Aidha, utaratibu huo uonekane katika Bajeti ya Wizara, Fungu 97;

(vii) Ada ya Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki iondolewe kwenye Bajeti ya Wizara ya Afrika Mashariki na kuwekewa utaratibu mwingine;

(viii) Watumishi wa Serikali waliopo Wilaya mbalimbali nchini, watumike kutoa elimu kwa wananchi kuhusu ushirikiano wa Afrika Mashariki na fursa zake; na

(ix) Serikali iweke utaratibu mahususi wa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu Ushirikiano wa Afrika Mashariki na fursa zake.

Mheshimiwa Spika, nne, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Kutokana na taarifa mbalimbali zilizowasilishwa katika vikao, Kamati, ina maoni kama ifuatavyo:-

(a) Maoni kuhusu Wizara:-

(i) Kwa kuwa suala la fedha za uendeshaji wa shughuli za Balozzi zetu nje ya nchi ni muhimu kwa heshima ya Taifa letu na ufanisi

20 APRILI, 2012

katika diplomasia ya uchumi, fedha zinazotengwa kwa ajili ya Balozi hizo zipelekwe kwa wakati. Aidha, katika sehemu ambazo kuna upungufu wa watumishi kimuundo, ni vema Serikali ikashughulikia tatizo hilo mapema inavyowezekana;

(ii) Kanuni za Utumishi nje ya nchi (*Foreign Service Regulations*) zifanyiwe mapitio na kurekebishwa ili ziendane na wakati pamoja na kuboresha hali za maisha ya watumishi hao na familia zao;

(iii) Hali ya kiuchumi, kisiasa na kijamii inayoendelea duniani itumike kubaini mambo ya msingi ambayo Serikali yetu na Taifa kwa ujumla tutapaswa kuyafanyia kazi;

(iv) Ili kuendelea kunufaika kiuchumi Wizara iongeze kasi na juhudi katika kushughulikia masuala ya diplomasia ya uchumi sanjari na kuboresha mawasiliano na Wabia wa Maendeleo. Aidha, taarifa zinazotumwa Wizarani kutoka balozi zetu nje ya nchi zifanyiwe kazi kwa umakini na haraka inavyowezekana;

(v) Uhusiano na ushirikiano wa Kimataifa utumike kusaidia upatikanaji wa soko la bidhaa zinazozalishwa nchini kwa kuongeza juhudi ya kuzitangaza bidhaa hizo katika nchi za wenzetu;

(vi) Kwa kuwa umiliki wa majengo nje ya nchi kwa ajili ya matumizi ya Balozi zetu ni jambo lenye tija kiuchumi, Wizara iandae mpango mahususi wa ujenzi wa majengo hayo kwa njia ya kuweka rehani (*Mortgage*) au njia nyingine inayowezekana; na

(vii) Ili kuendeleza uhusiano wa kidiplomasia na uchumi baina yetu na Uholanzi, Serikali iharakishe mchakato wa kufungua Ubalozi wetu uliofungwa nchini Uholanzi.

(b) *APRM* Tanzania:-

(i) Kwa kuzingatia kuwa moja ya kazi zinazofuata baada ya kukamilika uhakiki ni kusimamia Mpango Kazi wa Kitaifa, Kamati inashauri kuwa Baraza la Usimamizi la Taifa la *APRM* na Sekretarieti yake viimarishwe ipasavyo. Aidha, ni vizuri kuwapatia wataalam katika *APRM* Tanzania fursa ya mafunzo kutoka nchi zilizotekeleza Mpangokazi kama vile Ghana, Rwanda na Uganda;

(ii) Ili kufanya vizuri zaidi Kimataifa katika eneo la utawala bora Serikali ifanye juhudi za kutoa elimu kwa umma hususan elimu ya uraia na kujenga uzalendo wa Watanzania wengi zaidi;

(iii) Katika kutekeleza vema Azimio la Bunge la Nane kuhusu *APRM* ni vema Taasisi hii itungiwe sheria na kuiwezesha kuwa Taasisi ya Serikali inayojitegemea (*Independent Government Department*); na

(iv) Kwa kuzingatia faida zinazopatikana kutokana na mchakato wa kujitathmini kwa vigezo vya utawala bora, utaratibu huu utumike katika Serikali za Mitaa nchini.

Mheshimiwa Spika, tano, Ushirikiano na Diplomasia ya Kibunge. Katika utaratibu wa Mataifa mengi, ushirikiano wa Kibunge na diplomasia ya Kibunge ni mambo ya msingi. Moja ya faida za ushirikiano wa Kibunge ni kuboresha utendaji wa Mabunge katika kusimamia Serikali za nchi husika. Aidha, ushirikiano na Diplomasia ya Kibunge unawezesha kuongezeka kwa uelewa na umakini kuhusu Taasisi za ushirikiano baina na miongoni mwa nchi tofauti ndani ya nchi husika. Utaratibu huu unaweza kuwa na tija zaidi kwa Taifa kama utaboreshwa kiutaratibu. Kamati inashauri kuwa:-

(i) Vyama vyote vya Kibunge viwekewe utaratibu madhubuti utakaowezesha Waheshimiwa Wabunge kuelewa kinachoendelea na kufuatilia mambo ya msingi;

(ii) Inapotokea Waheshimiwa Wabunge wametembelea Mabunge ya nchi nyingine, uwekwe utaratibu wa Wabunge hao kutoa Taarifa kwa namna itakayosaidia Bunge kubaini mambo ya kujifunza kutoka katika Taarifa hizo;

(iii) Uwekwe utaratibu mzuri zaidi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kuhusiana kikazi na Bunge la Tanzania. Kwa mfano, ili kuimarisha utekelezaji wa matakwa ya Kanuni za Bunge, Nyongeza ya Nane, Kifungu cha 9, Fasili ya 2(a), uandaliwe utaratibu wa kiutawala baina ya Wizara ya Afrika Mashariki na Ofisi ya Bunge ili kuwawezesha Wabunge hao kufika kwenye vikao vya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pale inapobidi;

(iv) Pendekezo la Wawakilishi wetu katika Bunge la Afrika, kwamba Bunge la Tanzania lishirikiane na Bunge la Afrika katika utatuzi wa migogoro barani Afrika kama lilivyoshiriki katika utatuzi wa migogoro ya nchi za Maziwa Makuu linahitaji kufanyiwa kazi na Bunge letu;

(v) Kutokana na taarifa mbalimbali zilizowasilishwa kwenye vikao vya Bunge la Afrika hususan kuhusu migogoro ya ndani ya nchi za Afrika,

20 APRILI, 2012

Serikali yetu ijifunze kwa kuimarisha uwekezaji katika Sekta zinazoweza kuibua ajira kwa vijana;

(vi) Serikali iainishe mikataba, itifaki na Makubaliano ya Kimataifa yaliyosainiwa ambayo hayajaridhiwa na Bunge na kueleza sababu za kutoridhia mikataba hiyo ili Bunge liweze kushauri ipasavyo; na

(vii) Kwa kuwa pendekezo la Bunge la Afrika kwa nchi wanachama kuhusu kutenga kiwango kisichopungua asilimia 25 ya Bajeti ya Taifa katika sekta ya Elimu linafaa kutekelezwa ni muhimu Serikali ikalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka 2011/2012. Tunaamini kuwa fursa hii inayotokana na masharti ya Kanuni ya 114(15), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, itasaidia kuliwezesha Bunge lako Tukufu kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuitambua kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya awamu ya Nne chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Daktari Jakaya Mrisho Kikwete, Mkuu wa Nchi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, kwa jinsi inavyosimamia masuala ya Ulinzi na Usalama wa Taifa, usalama wa raia na mali zao. Juhudi hiyo imewezesha hali ya ulinzi na usalama kwa ujumla kuwa shwari pamoja na amani na utulivu kustawi nchini.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Mheshimiwa Daktari Hussein A. Mwinyi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; Mheshimiwa Mathias Chikawe, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora; Mheshimiwa Samuel J. Sitta, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na Mheshimiwa Bernad K. Membe, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati. Aidha, nawashukuru Mheshimiwa Balozi Khamis S. Kagasheki, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; Mheshimiwa Daktari Abdulla J. A. Saadalla, Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Mheshimiwa Mahadh Juma kwa kuisaidia Kamati kila walipokuja kwenye vikao vya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua pia fursa hii kuwashukuru Makatibu Wakuu wote wa Wizara za Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Ulinzi na JKT, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa pamoja na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Ikulu kwa ushirikiano mkubwa walioipa Kamati kwa mwaka 2011/2012.

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, shukurani za pekee nazitoa kwa Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kuiongoza vema Kamati wakati wote nilipomwachia majukumu. Aidha, nawashukuru sana wajumbe wa Kamati hii kwa utendaji kazi wao na umakini pamoja na ushirikiano mkubwa waliouonesha kila mara tulipokuwa kwenye utekelezaji wa majukumu yetu. Kipekee kabisa nawashukuru na kuwapongeza Wakuu wote wa vyombo vya Ulinzi na Usalama nchini kwa kazi nzuri wanayoifanya na kuhakikisha kuwa ulinzi wa nchi yetu, usalama wa raia na mali zao na utulivu unaendelea kuimarika.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, lakini si kwa umuhimu, napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Daktari Thomas D. Kasilillah, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake kwa kipindi chote cha mwaka 2011/2012. Namshukuru Ndugu Athuman Hussein, Katibu wa Kamati hii akisaidiwa na Ndugu Gaitana Chima kwa kuratibu vema shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili taarifa hii na hatimaye kuyakubali maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kama kawaida yetu, Kamati yetu huwa haisemi maneno nyeti au mambo nyeti, mambo ya ulinzi wa nchi yetu, masuala hayo kuna ripoti maalum ambayo Mheshimiwa Spika anapewa na yeye anayafanyia kazi na ngazi ya mhimili mwingine wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

MHE. RACHEL M. ROBERT: Mheshimiwa Spika, naafiki!

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, Kamati zetu ambazo tutazijadili katika kipindi hiki ndiyo zimewasilisha taarifa zake. Kwa hiyo, nitamwita msemaji mmoja tu kabla ya kuahirisha, Mheshimiwa Selemani Zedi kama yupo. Kama hayupo...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, ameshakimbia, anawahi Dar es Salaam. Labda nimwakilishe!

SPIKA: Haya! Mheshimiwa Saidi Mtanda kama yuko tayari!

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, niko tayari! (*Kicheko*)

20 APRILI, 2012

SPIKA: Hapana! Mheshimiwa Grace Kiwelu kama uko tayari!

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza kuchangia hotuba za Kamati zetu zilizowasilishwa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wenzangu wa Chama cha Mapinduzi jana na juzi walisema wakutane kwenye vikao vya chama ili kwenda kuwawajibisha Mawaziri. Lakini kwa kuwa sitokani na Chama cha Mapinduzi, ningepomba niseme hapa hapa wale Mawaziri ambao tunaona hawaendani na taratibu za kazi zao.

SPIKA: Naomba jadili hoja hizi. Hapa hatuteti watu, tafadhali.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Spika, sawa. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya Miundombinu na katika Kamati yetu tunashughulikia Wizara tatu; Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Mawasiliano na Wizara ya Uchukuzi. Lakini, naomba zaidi nishughulike na Wizara ya Uchukuzi ambayo Mwenyekiti wangu wa Kamati, kwanza nimpongeze ameweza kuwasilisha hotuba yake vizuri sana ndani ya Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze na upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam, ujenzi wa Gati Na. 13 na Na.14. Tumekuwa na mkanganyiko mkubwa sana hasa Kamati yetu ya Miundombinu katika upanuzi wa Bandari yetu ya Dar es salaam. Sisi ni mashahidi, meli nyingi zimekuwa zinashindwa kutia nanga pale kwa sababu ya kina kifupi cha maji. Lakini pia msongamano mkubwa wa meli umeonekana na imesababisha wafanyabiashara wengi wameshindwa kutoa mizigo yao kwa wakati na kusababisha kukimbia bandari yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini kumekuwa na matatizo makubwa ambayo tumekuwa tukiyaona kwenye vyombo vya habari yakijitokeza na Kamati yetu chini ya Mwenyekiti tuliwaita Mamlaka ya Bandari, tukazungumza na Mamlaka hiyo na ilituonesha *documents* zote muhimu ambazo zimefikwa mpaka sasa ambapo ulitakiwa ujenzi huo uweze kuanza mwezi Juni mwaka huu. Mchakato huu umeanza tangu ilipokuwa Wizara ya Miundombinu chini ya Waziri Kawambwa.

Mheshimiwa Spika, lakini cha kushangaza Waziri Nundu ambaye ni Waziri wa Uchukuzi sasa hivi amekuwa ni kikwazo kikubwa sana kwa ujenzi huo wa hizo Gati Na. 13 na Na.14. (*Makofi*)

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, inatuwekea tatizo kubwa sana sisi Wajumbe wa Kamati, Serikali hii inafanyaje kazi! Mheshimiwa Kawambwa alishaanza zoezi hili na hata Wizara ya Fedha ilishatoa barua (*Government guarantee*) ya kuiruhusu Wizara ya Uchukuzi kuendelea na mkopo ambao ulikuwa unapatikana kupitia *Exim Bank* ya China. Lakini tumeona kabisa hapa kwamba kwenye taarifa tulizopewa, Waziri wa Uchukuzi amekuja na utaratibu mwingine ambao anadai huyu aliyepatikana kwa ajili ya ujenzi huu hamtambui, anataka uanze mchakato mwingine ambao utamleta mkandarasi binafsi ambaye tumeelezwa hapa kwamba utaratibu ambao anataka kuutumia hautalisaidia Taifa letu. Sana sana inaonesha kabisa hapa kwamba, viongozi tuliowaweka madarakani wanaangalia maslahi yao binafsi. Mwekezaji ambaye Waziri anamtaka, anataka baada ya kukamilisha ujenzi wa Gati hizo amiliki kwa miaka 45, ambapo atakapokuja kuirudishia Bandari, kwanza miundombinu itakuwa imechakaa, tuanze tena utaratibu mwingine wa kutafuta mwekezaji mwingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu ya Miundombinu tulikataa suala hilo na tatizo kubwa la Mheshimiwa Waziri amekuwa hakubali ushauri, anakuwa mkali na mbabe. Jana alisema hapa kwamba hata akizuiwa kuingia jikoni, ataingia chooni. Hizo ndiyo kauli za Mawaziri ambao leo wako mbele yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tungependa kuwaambia Mawaziri, dhamana waliyopewa na Mheshimiwa Rais wawatumikie wananchi, lakini siyo kutujibu tofauti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kuliomba Bunge lako na kumtaka Mheshimiwa Waziri kwamba yale makubaliano ambayo yamekwishaanza ya Kampuni ya CCC ipewe mradi huo, uendelee ili tuweze kulipatia Taifa letu fedha kwa sababu kila siku tunalia uchumi wetu unashuka, wananchi matatizo ni mengi. Lakini kwa ukiritimba wa watu wachache wanazuia mipango mizuri iliyokwishakupangwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kipekee nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara hii. Mheshimiwa Waziri aliondoka na watu wa Bandari kwenda China na kuwalazimisha wasaini mkataba ambao Katibu Mkuu alikataa, aliwakataza wajumbe wa Bodi ya Bandari. Kama wangesaini mkataba ule, leo Taifa tungekuwa na mkataba kama wa *Richmond*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa tuwatake viongozi wetu wawe wanalinda maslahi ya nchi yetu. Tunazo *documents* tulizopewa na Bandari, barua zote na vikao ambavyo walikutana, siyo kwamba tunatoa maneno ya

20 APRILI, 2012

barabarani. Kwa hiyo, niseme tu kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi amekuwa ni tatizo kubwa sana katika Wizara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni kuhusu reli zetu. Mheshimiwa Spika, tatizo limekuwa kwamba hatuna vipaumbele, tumeshika kila mahali, hatimaye hatuna cha kuonesha kwa wananchi. Leo tunaona wasafiri wa Reli ya Kati wanavyopata shida hususan akina mama na watoto. Wanakwenda kukata tiketi, matokeo yake safari hakuna, watoto wanahangaika, hawana chakula, wazazi wanateseka.

Mheshimiwa Spika, ningeiomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi, hebu tuwe na malengo maalum. Tunachotaka kufanya, tukifanye kimoja kwanza ili hatimaye tuwe na kitu cha kuonesha. Kama ni reli ya Kati, basi tuhakikishe miundombinu ya Reli ya Kati inakuwa mizuri ili wasafiri wa reli waweze kupata usafiri wa uhakika na ukizingatia usafiri wa reli ni usafiri wa watu wa kipato cha chini. Leo Serikali yetu haina usafiri ambao mtu akienda anaweza kuupata. Leo hatuna ndege, miaka 50 ya Uhuru hatuna ndege inayoruka angani. Hii ni aibu!

Mheshimiwa Spika, shirika letu tumesomewa kwenye taarifa yetu ya miundombinu kwamba miaka miwili leo halina Bodi. Je, shirika litaendeshwaje kama Bodi yenyewe hatuna? Tunategemea Shirika hili liende vipi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuna mambo mengi sana ya kusema, lakini kikubwa tunachoitaka Serikali ya Chama cha Mapinduzi, mtimize wajibu wenu kwa sababu wengi wamekuwa na maneno mazuri ya kusema lakini utendaji hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tuliombe Bunge lako liridhie yale maoni ya Kamati kwamba ujenzi wa Gati Na.13 na Na.14 uendelee na zile taratibu zote zilizokwishafanyika ziendelee na Waziri aache kuingilia Bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naunga mkono maoni ya Kamati yangu ya Miundombinu. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa hapa tulipofikia. Mchana tutaendelea na wafuatao...

Mtu anaweza kuchangia sekta yoyote anayoweza, Wenyeviti watakuwa wanachukua yale yanayowahusu na naamini kabisa na wasemaji wa upande wa Serikali katika sekta hizo mnasikiliza kwa sababu mtaitwa wakati wowote pale kufafanua baadhi ya mambo, kwa hiyo,

20 APRILI, 2012

mjiandae pia. Kwa hiyo, msije mkadhani hapa leo ni sisi, pamoja na ninyi leo mko upande wa pili, Wenyeviti ndiyo wanaoongoza mijadala yao. Kwa hiyo, tutarejea tena saa kumi na moja. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00.

(Saa 6.56 Mchana Bunge lillifungwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lillirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, vipi Mheshimiwa Makamba una nini?

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. JANUARY Y. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Spika, ulipopata nafasi hii ya Uspika ulitambua Wabunge kwamba unapenda kuwa na Bunge moja katika moja ya vipaumbele vyako na kweli umefanikiwa kuwa na Bunge moja hasa katika kuiwajibisha Serikali. Wabunge tunataka tuendelee kuwa hivyo, wamoja katika kuihoji Serikali, katika kuidhibiti Serikali na katika kuiwajibisha kama Wawakilishi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, tumesoma kwenye vyombo vya habari leo na tumesikia kwenye viwanja vya Bunge kwamba zinakusanywa saina 70 kwa ajili ya kupiga kura ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu. Kama unavyofahamu na kama ulivyosema tuendelee kuwa wamoja, kwa hiyo jambo hili tunataka tulifanye kwa pamoja tukiwa na umoja, kwa hiyo, nilikuwa nataka mwongozo wako kama jambo hili unalifahamu, kama limekufikia na kama ni la Kikanuni ama ni la kisiasa zaidi, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

SPIKA: Mimi nilifikiri tunajadili mambo ya Kamati kumbe uko huko, basi nitatoa maamuzi baadaye kidogo, kwanza tuendelee na kazi hii.

Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaondoka hapa mchana tulipata nafasi ya Mbunge mmoja kujadili lakini na muda pia ulikuwa umekwisha. Sasa nitamwita Mheshimiwa Said Mtanda, Mheshimiwa Mwijage, atafuatiwa na Dokta Peter Kafumu, nitakwenda kufuatana na orodha iliyopo hapa tu.

20 APRILI, 2012

MHE. SAIDI M. MTANDA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa tena fursa ya kuweza kutoa mchango wangu katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwapongeza sana wenzetu wa Kamati ya Nishati na Madini chini ya Mwenyekiti wake rafiki yangu Mheshimiwa January Makamba, kwa kazi kubwa aliyoifanya na hatimaye kuwasilisha taarifa nzuri mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, yapo baadhi ya mambo matatu, manne ambayo nadhani nitajielekeza kuyajadili kwa manufaa ya Watanzania lakini pia kwa manufaa ya wananchi wa Jimbo la Mchinga ambao ndiyo walionipa heshima na kunifikisha mbele ya Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, moja kati ya mambo ambayo nimeyaona katika taarifa hii na ninapenda niungane na Kamati, ni juu ya suala la gharama kubwa za uunganishwaji wa umeme, ni dhahiri kabisa kwamba Watanzania walio wengi hawana uwezo wa kumudu gharama kubwa ambayo hivi sasa ipo ya kuunganisha umeme. Mathalani ili uweze kuunganishiwa umeme na ukiwa na hitaji la nguzo moja tu, unalazimika kuwa na kiasi kisichopungua shilingi milioni moja na laki saba, shilingi milioni moja na laki saba ni fedha nyingi sana ambayo Mtanzania mlalahoi wa kawaida hawezi kuimudu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Wizara hii ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na *TANESCO* waliangalie kwa undani jambo hili ili hatimaye gharama ya kuunganisha umeme iweze kupungua na kuweza kuwasaidia Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, ninasema hivi kwa sababu pale kwangu Mchinga, wapo wananchi ambao wamejiandikisha kuletewa umeme, lakini wanakwama kwa sababu sasa wanashindwa kulipia gharama hiyo ya shilingi milioni moja na laki saba. Kwa hivyo, umeme umefika pale lakini wananchi walionufaika na mradi ule ni wananchi wachache sana. Kati ya nyumba 300 watu ambao wamevuta umeme pale hawafikii hata watu hamsini, kwa hiyo faida ya kuwepo na umeme katika eneo lile inakuwa ni ndogo. Kwa hiyo, hilo nadhani ni jambo la kwanza niweze kuwashawishi Wabunge wenzangu tufanye maamuzi na kuishawishi Wizara ione umuhimu wa kuliangalia jambo hili kwa kina.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili ni kuhusu mapendekezo ya Sheria mpya ya Gesi, ukusoma ukurasa wa 18 wa taarifa hii na mimi naomba nikubaliane kabisa na niwe sambamba na Kamati kwamba iko haja ya kuwa na sheria inayohusu masuala ya gesi. Kwa sababu

20 APRILI, 2012

tumepata matatizo makubwa sana katika nchi, sheria mbaya kuhusu madini, madini sasa hivi yanaisha, sasa wakati sekta hii ya gesi inaanza, ni vema tukaanza upya kwa kutofanya maamuzi ambayo yatapelekea gesi hii kutowanufaisha Watanzania na hususani wananchi ambao gesi hii ndiko inakotokea pale Mnazi Bay, Mtwara na Songosongo, Kilwa katika Mkoa wa Lindi. Tunadhani ni wakati muafaka sasa wa kupitia upya Sheria ya Gesi ili gesi iweze kuwanufaisha Watanzania badala ya mikataba ambayo haina uhakika na haina manufaa.

Mheshimiwa Spika, lakini nikubaliane na maoni ya Kamati kwamba, iko haja sasa ya kuwa na fidia kwa wananchi kwa wakati hasa wale ambao bomba la gesi litapita kutoka kule Mtwara kwenda Dar es Salaam hadi Tanga. Ninasema hivi kwa sababu lipo tatizo la kimsingi, wakati tunapanga mikakati hii mizuri ya maendeleo, lakini wananchi wetu wanaoguswa na maeneo ambayo mabomba haya ya mafuta ya gesi yatapita kimsingi huwa hawalipwi fidia inayostahili na hawalipwi kwa wakati. Kwa hivyo, hili ni tatizo kubwa, ninaiomba Wizara wakati wa kufanya *implementation* ya suala hili izingatie maslahi ya wananchi ambao wataathirika kutokana na maeneo yao hasa nyumba zao kubomolewa ili kupisha bomba hili la gesi kutoka Mtwara kwenda Dar es Salaam hadi Tanga kuweza kufanyiwa kazi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ninasema hivi kwa sababu kuna mkongo wa Taifa wa Mawasiliano umepita na katika eneo langu la Lindi Vijijini hususani Jimbo langu la Mchinga Mkongo huu umepita na wananchi wamewekewa X kwenye nyumba zao kuanzia pale Mchinga I, kufika Kilangala, kufika mpaka pale Mumbia inakwenda mpaka Kitomanga mpaka mwisho wa Jimbo pale Mkwajuni, wapo wananchi walioathirika, wamewekewa alama ya X lakini hadi leo hawaelewi kinachoendelea, hawaelewi fidia yao watapata wapi. Sasa na bomba hili la gesi litapita maeneo hayohayo, nina wasiwasi mkubwa kwamba wananchi wa maneo hayo hususani wa Mkoa wa Lindi na Mtwara bomba hili litakapopita kama watapata fidia yao maana inachelewa sana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia kuunga mkono hoja ya Kamati kwamba gesi inapozalishwa pale Mtwara ni lazima kuwe na gawio, kama inavyofanyika katika maeneo ya sekta nyingine kwamba wa kwanza kunufaika na rasilimali hiyo wawe ni wananchi wa pale Mtwara, wawe ni wananchi wa pale Lindi kwa sababu wao ndiyo rasilimali hii ipo maeneo yao. Kwa hiyo, mtani wangu Mwijage tunashukuru sana maoni ya Kamati yenu kwa sababu yamezingatia hali halisi, lakini pia yanajikita kutaka kuondoa umaskini katika Mikoa ya Lindi na Mtwara hasa ikizingatiwa kwamba Mikoa ya pembezoni haipewi vipaumbele katika sekta ya maendeleo, sasa tumepata gesi ni lazima gesi hii iwanufaishe wananchi

wa Lindi na Mtwara ndipo iende maeneo mengine. Hilo ilikuwa ni kuhusu gawio, lakini pia ni lazima tujue gawio hilo litakuwa ni kiasi gani, asilimia ngapi. Pia sisi watu wa Lindi na Mtwara tunadhani *production* ni lazima ifanywe Mtwara, kiwanda kiwe pale, ndipo sasa muweze kusafirisha gesi kwa ajili ya matumizi kwenda maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, lakini lipo tatizo lingine la Mnazi Bay, kwa sababu katika ile hatua za awali tuliambiwa Mnazi Bay ingetoa gesi, kwa hivyo umeme katika Mkoa wa Lindi na Mtwara ungezalishwa kupitia gesi hiyo, lakini hadi leo ni mashaka makubwa kwa watu wa Mkoa wa Lindi na Mtwara kwa sababu hatuna umeme wa uhakika na tunapoendelea kupiga kelele hapa bado Serikali haitusikii. Tunaomba kilio chetu kisikilizwe na wananchi wa Mkoa wa Lindi, Mtwara wapate fursa ya kupata umeme wa uhakika kwa sababu rasilimali hii ipo katika eneo lao.

Mheshimiwa Spika, mwisho nimalize kwa kuzungumzia ukurasa wa 25, kuhusu Wakala wa Umeme Vijijini (*REA*). Niliandika barua yangu pale *REA* na Waziri alituhakikishia kwamba *REA* wamepata fedha za kutosha kwa ajili ya usambazaji umeme Vijijini na kwa awamu na hatua ya kipindi cha mwaka huu ilikubalika kwamba umeme huo sasa usambazwe vijiji vya Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Mtwara. Kwa hiyo, naomba wakati Waziri atakapokuja hapa atueleze ni hatua gani zilizofikiwa hadi sasa ili maeneo ambayo tuliyataja kwenye barua yangu pale, maeneo ya Kijiji cha Rutamba, Kilolambwani, Mipingo yaweze kuzingatiwa na kuingizwa katika mpango huu wa umeme vijijini. Kwa sababu Watanzania wale sasa kwa kweli wanahitaji Nishati hii na kwa kuwa maeneo hayo ni vijiji vyenye watu wengi na endapo umeme utafika kule Kitwanga amenihakikishia ni rahisi sana minara ya simu ya *Vodacom*, *Zain* kuwekwa katika maeneo hayo. Naomba sasa Wizara izingatie na itupe taarifa humu ndani kwamba zile fedha za *REA* ambazo zimeshakwenda katika Mkoa wa Lindi na Mtwara, maeneo niliyoyataja ya Mipingo, Rutamba, Kilolambwani na Kitomanga ambako ndiko hospitali yetu ya Wilaya tunaiweka pale, yatapatiwa umeme kwa sababu hili ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, nadhani nikubaliane tena na taarifa hii ya Kamati, ninaunga mkono mapendekezo ambayo yamo ndani ya ripoti hii. Jambo la msingi ni kutekelezwa kwa haya yaliyoandikwa, maana nchi hii tuna mipango mingi na sisi ni mabingwa wa kupanga katika Afrika lakini sisi ni wavivu wa utekelezaji wa mipango hii tunayoizungumza.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kuunga mkono taarifa hii. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, katika kupitia vitabu vilivyopo hapa kuhusu mwongozo aliuomba Mheshimiwa Makamba, nimejaribu kupata taarifa zote, kwamba jana wakati Mwenyekiti wa Kamati ya Mashirika ya Umma anajibu hoja za Wabunge baada ya mjadala ule wa Kamati zile za *Watchdog*, moja ya mambo aliyoyasema mle ndani wakati wa hoja yake pamoja na mambo mengine alisema:-

“Mheshimiwa Naibu Spika, na mengine yote, bila kumwajibisha Waziri Mkuu, hawa Mawaziri waliotajwa hawatatoka na wasipotoka, madudu haya yatarudia. Kwa hiyo, akasema nampa taarifa kwamba kuanzia kesho, maana yake ilikuwa jana, kwa hiyo ni leo, tunakusanya saini za Wabunge 70 ili siku ya Jumatatu tutoe hoja hapa Bungeni ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu. Akaendelea na mengine halafu akasema, Naibu Spika, nawaomba Wabunge wote wenye uchungu, kuanzia kesho maana yake leo, tutakuwa pale mlangoni, saini zinazohitajika ni 70 tu kwa ajili ya kuleta hapa Bungeni na Wabunge wanaohitajika kupitisha Azimio hilo ni nusu tu ya Wabunge, hamsini *plus one*, tukifanya hivyo tutakuwa tumewapa heshima wananchi wetu, wataona kweli tumewatendea haki, mwisho wa kunukuu”.

Mheshimiwa anasema mnataka muungane lakini utaratibu ukoje?

Waheshimiwa Wabunge, siku zote ninawaambieni msome misaafu yetu. Bahati nzuri hii azma ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu, ni Kanuni ya 133 ya Kanuni zetu, *I hope* Waandishi wa Habari mnazo hizi Kanuni, maana ni lazima tuweke mambo vizuri, jambo hili siyo dogo. Ni Kanuni ya 133, hoja ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu, lakini hii Kanuni pia imepewa nguvu nadhani tulichukua moja kwa moja kwenye Katiba, Ibara ya 53A.-(3), ni maneno sawasawa na huku kwenye Kanuni. Kwa nini Mheshimiwa Zitto alisema vile, nafikiri ni kwa sababu kwa Mujibu wa Ibara ya 51 kifungu kidogo cha (2), inasema Waziri Mkuu atateuliwa na Rais lakini kabla hajakuwa Waziri Mkuu anathibitishwa na Bunge na inasema naye hatashika madaraka hayo mpaka kwanza uteuzi wake uwe umethibitishwa na Bunge kwa Azimio litakaloungwa mkono na kura za Wabunge walio wengi. Kwa hiyo, nadhani ndiyo msingi wa Mheshimiwa Zitto kwamba huyu ni mtu tuliyempitisha wenyewe kwa hiyo tuna mamlaka naye kwa sababu ndiye tuliyempitisha.

Wakati huohuo Katiba yetu inasema kwamba Waziri Mkuu ndiye atakayekuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, hii ni Katiba, Ibara ya 52(2). Ibara hizi zinafanana na Kanuni ya 53. Ibara ndogo ya (2) inasema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mamlaka ya Rais ndiyo itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya sera ya

20 APRILI, 2012

Serikali kwa ujumla. Kwa hiyo, nataka msikilize, na Mawaziri chini ya uongozi wa Waziri Mkuu watawajibika kwa pamoja Bungeni kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Kwa hiyo, hivi vifungu ndiyo vinatupa sisi nguvu kwamba tuna uwezo na Waziri Mkuu.

Ibara ya 53A.-(3), hoja ya kura ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu haitapitishwa na Bunge isipokuwa tu kama; taarifa ya Maandishi iliyotiwa sahihi na kuungwa mkono na Wabunge wasiopungua asilimia ishirini ya Wabunge wote itatolewa kwa Spika, naomba nirudie hapo, taarifa ya maandishi iliyotiwa sahihi na kuungwa mkono na Wabunge wasiopungua asilimia ishirini ya Wabunge wote itatolewa kwa Spika, siku angalau kumi na nne (14) kabla ya siku inayokusudiwa kuwasilishwa Bungeni. Spika atajiridhisha kuwa masharti ya Katiba kwa ajili ya kuleta hoja yametimizwa na masharti yenyewe yapo katika Ibara ya 53A, Kifungu kidogo cha (2). Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya Ibara hii, hoja yoyote ya kutaka kupitisha kura ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu haitatolewa Bungeni endapo:-

(a) haina uhusiano na utekelezaji wa majukumu ya Waziri Mkuu kwa mujibu wa Ibara ya 52 ya Katiba, wala hakuna madai kwamba Waziri Mkuu amevunja Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma; au

(b) haijapita miezi sita tangu alipoteuliwa;

(c) haijapita miezi tisa tangu hoja ya namna hiyo ilipotolewa Bungeni na Bunge likakataa kuipitisha.

Waheshimiwa Wabunge, haya siyo msingi wa *arguments* zetu, msingi hapa ni kwamba saina zile zinazotakiwa ziwepo, taarifa ipelekwe kwa Spika kwa maandishi katika siku angalau kumi na nne kabla ya siku inayokusudiwa kuwasilishwa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, sasa hii habari ya Mheshimiwa hapa alipokuwa akijibu akasema kwamba jamani njooni, huo siyo utaratibu, akiitumia hiyo haikubaliki kwa sababu mpaka sasa mimi sijapata hoja kabisa.

Pili, Bunge hili tunaahirisha tarehe 23 Aprili, maana yake ni Jumatatu, leo, kesho, Jumapili na Jumatatu ni siku nne, haikidhi siku kumi na nne, sanasana anaweza kukusanya hizo saina na akishakusanya labda aseme Bunge lijalo na zenyewe ziwe siku siyo chini ya kumi na nne. Kwa hiyo, zoezi linaloendelea kama linaendelea au linafanywa, kwa kweli ni batili kwa maana hiyo. (*Makofi*)

20 APRILI, 2012

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo si kwa sababu ya matakwa, ni matakwa ya Katiba na Kanuni zetu, msome vizuri tusiwe na tafsiri isiyokuwa na maana kwa sababu kazi kama hii ni kubwa kwa hiyo ni vizuri mkafuata hiyo. Kama ilivyosemwa hapa Bungeni kwamba nafikiri kesho, Jumatatu tuwe tumewasilisha, haiwezekani, Kanuni inakataa. Kwa hiyo, zoezi hili lote hata kama mkifanya labda m-*defer* mpaka Bunge lijalo na mkafanya kama mlikusanya wakati huo, hizi za leo siku mbili/tatu jazeni lakini haina msingi wowote.

Ninamshukuru Naibu Spika wakati anaahirisha alisema nawahoji mambo mengine yaliyoletwa hapa, haya mengine yalikuwa ni makandokando, hayakuhusika na uamuzi wetu hapa. Kwa hiyo, naomba ieleweke hivyo, kwamba tukifuata Katiba na Kanuni zetu, huo utaratibu uliotangazwa jana na Mheshimiwa Zitto hauwezekani kwa sababu ndiyo Katiba ilivyo. Nadhani nimeeleweka, someni Katiba na Kanuni zetu Ibara ya 133. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Mwijage atafuatiwa na Mheshimiwa Daktari Kafumu.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Taarifa za Kamati. Nitajitahidi kuanza na Wizara ya Nishati ambayo mimi ni mjumbe na nikijaliwa kupata nafasi nitaizungumzia Wizara inayohusika na bandari.

Mheshimiwa Spika, hakuna mtu mzuri kama mtu anayeshukuru. Napenda nimshukuru Mheshimiwa Mbunge wa Mchinga na Mjomba wangu Murtaza Mangungu kwa kuishukuru Kamati kwa kazi ambayo tumeifanya kwa ajili ya ukanda unaotoa gesi. Kama alivyozungumza Mwenyekiti wangu na kama inavyosomeka kwenye taarifa yetu, Taifa liko katika nafasi nzuri tunaposhuhudia upatikanaji wa gesi kwa wingi. Mwenyekiti amesema Serikali haijawajulisha wananchi sijui kama kuna kifungu cha Katiba kinachonizuia au Kanuni lakini niwaeleze gesi nyingi imepatikana mara kumi zaidi ya iliyoko Songosongo na kuna matumaini kwamba gesi nyingi itapatikana. Kwa hiyo, watu wa Kusini mkipata, msitusahau lakini tunaanzia Kusini na tunasambaa nchi nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Kamati yetu tulichopendekeza na tunachoendelea kuishauri Serikali ni kwamba shughuli kubwa zitakuwepo kule Kusini kwenye utafutaji na uchimbaji wa gesi, utitiri wa watu watakuwepo kule, wataalam wa kila namna, watakula vyakula, kama watu wa Kusini wakiweza kupata mafunzo ya kulima na kufuga na kuweza ku-*supply* kwenye *industry*, Machinga wataacha kuja Dar es Salaam watakwenda kule na mambo yataanza kupendeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, si kwa sababu nawapendelea Kusini kwa sababu ya Murtaza Mangungu au bwana wa Mchinga ni kwa sababu tunataka kujenga mazingira yatakayotofautisha nchi yetu na Nigeria. Matatizo ya Nigeria ni kwa sababu wananchi wa maeneo inakotoka malighafi walisahauliwa. Watu wanafyonza sheli, wanafyonza wanakwenda zao, watu wa Delta wanabaki watazamaji kwa sababu mimi masuala haya nayajua, imenilea miaka 28, tumehakikisha kwenye Kamati yetu tunaisema na tutaendelea kuipigia kelele Watanzania gesi inakuja ni kwa ajili yetu.

Mheshimiwa Spika, gesi inayokuja ni nyingi, kisima kilichogunduliwa juzi, kwa Kipemba kinaitwa Zafarani, kina gesi nyingi mno lakini ukiuliza kwenye taarifa za mafuta huko duniani, mimi nawasiliana na watu wa Ulaya, Wazungu wengi wanakuja, kampuni *competent* zinakuja kuchimba mafuta Tanzania. Kila watu ambao wanashughulika na uchimbaji wa mafuta wanakuja Tanzania mfano *Shevron, Meshen and big company*, inakuja tatizo, kilichoia Nigeria, Diwani wa Nigeria alikuwa na uwezo wa kugawa kitalu cha kuchimba mafuta, Mbunge wa Nigeria anagawa, *DC* wa Nigeria anagawa, ndio vurugu ya Nigeria, ndio maana wanauana. Tunachopendekeza sisi katika Kamati yetu, tumependekeza kitu kinaitwa Kilemba au mwali kamuona nani, tunachopendekeza sisi ni kwamba *tendering system* itumike, vitalu vyote vinafahamika, vitangazwe ijulikane hakuna Mwijage kuja na mtu wake kwenye koti kwa sababu alikuwa tajiri wake akampatia kiwanja. Hakuna bosi wake Mwijage kuja na mtu wake akampa, itangazwe. Yule atakayepata fursa kabla hajaanza kuchimba yule aliye mzuri tutamjua kwa umaarufu wake *plus* kitu kinachoitwa *signature bonus*. *Signature bonus* ni fedha ya zaidi anayoweka pamoja na *tender* ile yake au Kiswahili wanaita Kilemba au kwa kikwetu wanaita mwali kamuona nani. Bibi anayeona mwali lazima umpe chochote, hiyo fedha itaingia kwenye kapu letu na ndio namna ya kukusanya mapato, ndio kazi tuliyofanya kwenye Kamati yetu, mambo mazuri yanakuja.

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wangu hakupata nafasi ya kuzungumzia *site* ya Kijuweni, habari zinasema kwamba taarifa ya *tender* ya kugawa viwanja itakayofanyika mwezi wa nne, wa tano, wa sita, kuna madalali wameshaanza kudanganya Wazungu kwamba wao wana mamlaka ya kuwagawia viwanja, mimi simo lakini hiyo ikifanyika nitapiga kelele hapa, nitapiga kelele nje, hatutaki mambo ya Sarowiwa, hatutaki mambo ya *Delta*. Chonde chonde rafiki zangu, katika hili sina msamaha, tutatumia *tender system*, tutatumia *signature bonus*, hakuna kugawa viwanja. Fanyeni ujinga sehemu nyingine, hapa ni *transparent* na *openness*. Hilo nilitaka kulisema na ndio maana nilikuwa nahangaika

20 APRILI, 2012

niseme hilo, ndilo lilikuwa linanisukuma niweze kulisema. Tunataka tufaidi, tumehangaika sana, tuchume, tufaidi kwa ajili ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu wa Kusini, gesi inayokuja ni zaidi ya Songosongo, kuna mtambo mkubwa unaitwa LNG hautajengwa maji marefu utajengwa kwenye pwani ya Tanzania. Kwa hiyo, mtauona, mfanye vibarua na zaidi ya hapo tumependekeza kwenye Kamati kwamba vyuo vyote kikiwemo cha Mtwara, Watanzania wafundishwe, vijana wangu wa Kata wafundishwe mle ndani wajue kufunga va/ve za gesi, waweze kushiriki kusudi tuweze kufaidi namna hiyo. Hilo ndilo nalipendekeza.

Mheshimiwa Spika, suala la ushirikishwaji, tumejifunza kutokana na madini, kwenye madini nyanya hazitoki Tanzania, nyama haitoki Tanzania. Sasa tunasema nendeni Mchinga, nendeni Rufiji, teremka mpaka kule chini, ndugu zetu hawajui kulima mboga mnazotaka, leteni wataalam wa kilimo waje wawafundishe. Halafu kwenye Kamati tumekwenda mbele zaidi tumesema hatutaki ile *social corporate responsibility* ya kujengewa vyoo, mtu anakujengea choo anasema *the social corporate responsibility*, tunataka *social corporate responsibility* ya kutufundisha sisi kuwa wagavi, mtufundishe namna ya kutengeneza nyama na soseji wanazokula kusudi tuweze kuuza kwa bei za Ulaya, tuweze kupata fedha zaidi. Ndicho tulichopendekeza kwenye Kamati yetu na ndio maana nilikuwa nahangaika kama nilivyosema ili niweze kulisema hili. Nawashukuru sana watu wa Kusini kwa kutupa moyo tutaendelea kulisimamia hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la mafuta aina ya *petrol*. Nitangaze *interest*, mimi nimshauri au *consultancy* katika shughuli hizi, nina uzoefu wa miaka 28. Tulianzisha uagizaji wa pamoja, suala hilo mimi naliunga mkono lakini tumepata kasoro, *experience* ya miezi mitatu yametokea masaibu, mafuta machafu yameingia, nataka nizungumze moja. Mafuta machafu waliyokuwa wanasema Wabunge hayahusishi mafuta ya ndege. Mafuta ya ndege jamani hayategemei *certification* ya TBS, yanakuwa *satisfied abroad*, kwa hiyo, mafuta ya ndege yako safi lakini mafuta ya *petrol* yana kasoro, ndio maana hata Mkemia wa Serikali tangu yaingie nchini amekuwa na kigugumizi cha kueleza *oxygen content* kwenye mafuta yale. Mkemia wa Serikali anashindwa, TBS wana kigugumizi, nimesoma kwenye gazeti kwamba *sample* zimepelekwa *abroad*, Serikali tunapeleka *abroad* kwenda kupima *oxygen content* kwenye *gasoline*, siwezi kusema ni aibu lakini tunashauri na tuliwahi kushauri kwenye Kamati kwamba maabara ya Chuo Kikuu iwezeshwe, ipewe fedha zaidi kusudi iwe ni mbadala wa kupima vitu hivi. (Makofi)

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, niende kwa *REA*, *REA* tuliitengea fedha na fedha nyingi ya *REA* ilitokana na kuongeza kodi kwenye *kerosene*, Wabunge walilalamika, nilisimama nikasema watu wangu nawaombe sana umeme, tunaomba fedha ya *REA* iongezwe na iongezwe vipi, *TRA* sifa tunazowapa za kukusanya kodi, kodi imetokana na maamuzi magumu ya kuongeza ushuru kwenye mafuta ya taa, kwa hiyo, *TRA* waongeze fedha ili ipelekwa *REA* wapewe angalau bilioni 250. Mambo ni mazuri *REA* umeme unakwenda kusambaa, sasa asilimia 17 inaenda kwenye umeme lakini asilimia 17 lazima tuzingatie na vijijini.

Mheshimiwa Spika, nimelisema hilo na roho yangu imeridhika, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kwa mara ya kwanza na mimi nitoe mchango kwenye Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa mchango wangu, naomba nitoe shukrani kwa wananchi wa Igunga kwa kunichagua kuwa mwakilishi wao katika Bunge lako Tukufu lakini pia kwa kunichagua kuwa mshiriki wa maendeleo katika Wilaya yetu. Nakishukuru Chama cha Mapinduzi pia kwa kazi nzuri ya kuninadi na wananchi wakakubali. Mwisho naishukuru familia yangu, mke wangu Mariamagdalena kwa kazi nzuri aliyofanya na watoto wangu walinisindikiza mpaka mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba basi niwapongeze Wenyeviti wa Kamati zote kwa kazi nzuri waliyofanya ya kutuletea mapendekezo, uchambuzi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa mchango wangu hasa kwenye sekta ya madini ambako ninatoka, naomba niseme kwamba nchi yetu imegubikwa na utamaduni wa kutokuwa waadilifu. Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi tukienda Majimboni tunavyopata taabu kidogo, wananchi wetu tumewafundisha kuwa wapokea rushwa na sisi tumejifunza kuwa watoa rushwa. Ni utamaduni wa ajabu kabisa ambao tunatakiwa tuutafutie jibu. Ni kwa sababu gani imetokea? Ni kwa sababu sisi sote bila kubagua vyama, bila kubagua rika, bila kubagua jinsia, tunaiona rushwa kama siyo dhambi. Rushwa ni dhambi kubwa sana. Inasemwa kwenye vitabu, ni dhambi kubwa, sasa sisi tunaona kitu cha kawaida. Sasa tufanyeje ili rushwa hii itoke kwenye vichwa vyetu? (*Makofi*)

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani hatua za kuchukua ni kuwa na mkakati wa muda mrefu wa kujenga Taifa jipya ambalo litakuwa Taifa la waadilifu. Tutafanyaje? Mimi nafikiri tunatakiwa kubadili hata kuanzia mitaala yetu labda hata Shule za Msingi, Chekechea, Sekondari na Vyuo Vikuu tufundishe habari ya kuwa waadilifu. Sasa hivi siyo ajabu, mimi nilikuwa Mhadhiri wa Nje wa Chuo Kikuu cha Sokoine. Nilifundisha vijana wachache pale, lakini baada ya miezi mitatu, minne hivi unakutana na kijana wako amejiriwa sehemu fulani lakini anaendesha gari ya ajabu kabisa. Sasa unajiuliza hivi huyu kijana amepata wapi hela? Hii ni kwa sababu ya utamaduni huu. Lazima tutayarishe mkakati wa muda mrefu kwa ajili ya kulinusuru Taifa letu kuondokana na utamaduni huu. Sote kabisa tunahusika, tuione rushwa kama dhambi, ukiogopa rushwa utatenda dhambi kwa mbali sana. Sisi sote ni Wakristo na Waislam, kuna dhambi ambazo tunatenda lakini kwa woga. Sasa siku hizi rushwa si dhambi ambayo inaogopwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ambayo nafikiria ni muhimu ni hii hatua ya muda mfupi ambayo kila Mwenyekiti wa Kamati ameisema kwamba tujitahidi sasa hivi kuwa waadilifu, tujitahidi sasa hivi kuchukuliana hatua. Wabunge tokea juzi wanazungumza mambo haya. Kwenye Halmashauri zetu, kwenye Mawizara, kwenye Vyama huko tuchukuliane hatua, tutalinusuru Taifa letu vinginevyo tumeharibikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nichangie mambo mawili tu kwenye nishati na madini. Jambo la kwanza, sekta ya madini ni sekta ambayo inianza kukua vizuri. Tulianza kwa matatizo lakini inakua vizuri kwa sababu tunatakiwa na tunafanya sasa wananchi wetu washiriki zaidi na Serikali ishiriki zaidi. Sheria ya Madini tuliyoipitisha mwaka 2010 ina mambo mengi sana yanayozungumzia *local content* yaani wananchi washiriki, inazungumzia ushiriki wa makampuni ya Kitanzania. Sisi ni wazalishaji wa dhahabu labda namba tatu katika Afrika. Sasa niliwahi kupendekeza kwamba hii dhahabu tuliyoipata tuitunze kwenye Benki Kuu kwa sababu dhahabu inaonyesha utajiri wa nchi. Marekani ukubwa wake wote na umaarufu wake ni kwa sababu ina dhahabu nyingi kwenye Benki Kuu yao. Mpaka mwaka 2008 nchi ya Marekani walikuwa na dhahabu zaidi ya tani elfu nane dhahabu safi. *World Bank* wao ndio kabisa zaidi ya tani 34,000 wametunza kwenye benki ndio maana ni matajiri na nchi kama Libya, nchi kama Egypt wana dhahabu kwenye Benki Kuu zao. Kwa hiyo na sisi tunatakiwa kufanya jambo hili sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutafanyaje basi angalau tuanze kutunza dhahabu hii? Tunaweza kulipwa mrabaha wetu nusu katika dhahabu safi

20 APRILI, 2012

lakini pia Serikali inaweza kununua dhahabu hii kutoka kwa wachimbaji wadogo. Pia Serikali kwa sababu tumeamua kuwa wawekezaji kupitia STAMICO tunaweza tukawekeza kwenye dhahabu na dhahabu yetu yote tukaitunza kama dhahabu safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo napenda kuchangia ni kuhusu nishati. Gesi tumepata kama Wabunge walivyosema lakini tunahitaji tuitumie zaidi kwenye matumizi ya nyumbani, matumizi ya viwandani na matumizi kwenye magari lakini kwa sababu sasa tuna matatizo ya umeme tutumie sasa hivi kwa ajili ya kuzalisha umeme. Tuchimbe na tutumie rasilimali zingine za nishati kwa mfano makaa ya mawe, jotoardhi, hizi ni nishati ambazo zitatusaidia sana kutengeneza umeme ambao utakuwa unatutosha, utakaosaidia vyanzo vya umeme vinavyotokana na maji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, nawaomba pia na wananchi kwa ujumla kama alivyosema msemaji wa mwisho, gesi kwa sasa itatusaidia na tuitumie kwa ajili ya kuzalisha umeme lakini baadaye tutaiondoa kwenye suala la kuzalisha umeme tutakapokuwa na vyanzo vingine vya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kwa mara ya kwanza katika Bunge lako Tukufu. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa mawazo yangu juu ya ripoti ambazo zimeletwa na Kamati zetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nichangie kuhusiana na Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje. Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, ukurasa wa 19, kifungu cha 3.2, kifungu kidogo cha 6, kimeelezea kuhusiana na kulinda haki za binadamu pamoja na usalama wa raia na mali zao. Haki ni kitu cha msingi kwa mwanadamu yeyote na kiumbe chochote. Hata wanyama wana haki zao za kuishi. Wadudu vilevile kama utawaswaga kwa sababu ya udogo wao basi utabeba dhambi kwa sababu ya kuwadhulumu haki yao ya kuishi.

Mheshimiwa Spika, Mahakama zinasimamia haki, Jeshi la Polisi linatakiwa lilinde haki za raia na mali zao, lakini ni Jeshi hilo ambalo linatakiwa lisimamie haki za wafanyakazi wake. Hivi ikiwa mamlaka haiwezi kusimamia haki za wafanyakazi wake, itawezaje kusimamia haki za raia wengine na mali zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo, kwa sababu zifuatazo. Kuna vijana ambao walikuwa ni watumishi wa Jeshi la Polisi, wamesimamishwa kazi mwaka 2001, lakini kusimamishwa kazi huko hawakupewa barua mpaka leo 2012. Sasa mamlaka hii inasimamia vipi haki za raia na mali zao ikiwa imeshindwa kusimamia haki za wafanyakazi wake? Waliosimamishwa kazi mmoja ni D5657 Coplo Rashid Abbas Machano, mwingine ni D5713 PC Ramadhani Amani, mwingine ni Shaibu Hamis Makame E 4982 na mwingine ni Haroub Nassoro Hamadi E 3664 PC. Vijana walisimamishwa kazi mwaka 2001, lakini kusimamishwa kwao kazi hawakupewa barua. Sasa napenda niulize watu hawa kama hawakupewa barua na wamesimamishwa kazi, haki zao ziko wapi mpaka leo? Sasa hawa wanahesabiwa sio wafanyakazi lakini nina wasiwasi kama miongoni mwa wafanyakazi ambao wanapewa mishahara hewa na hawa wamo katika kundi hilo, lakini hawapewi mishahara kwa sababu wao hawahesabiwa kama ni wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, kuna mfanyakazi mmoja ambaye amefariki huyu anaitwa Amour Suleiman Amour mpaka karibuni mwezi wa pili mke wake alikwenda Makao Makuu ya Polisi Dar es Salaam kutafuta haki za marehemu mume wake pamoja na watoto wake watano, lakini alipofika akaambiwa Jeshi la Polisi halina mtumishi huyo. Sasa mambo mengine yanaliza. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, unaona huyu anavyoongea na mimi na wewe ulivyopita?

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba haki za wafanyakazi hawa wapatiwe wenyewe. Haki za Marehemu Amour Suleiman Amour zipewe familia yake na watoto wake.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la Kamati ya Uchumi na Fedha, kuhusiana na Kamati ya Uchumi na Fedha nachangia sehemu ya Kilimo Kwanza, ukurasa wa tano, kifungu cha 2.1.4.1. Suala la Kilimo Kwanza Tanzania linawezekana, lakini cha kusikitisha, sisi ni wataalam wazuri wa kuandika, ni wataalam wazuri wa kusema lakini tunayoyaandika na tunayoyasema yanatumiwa na nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania tokea uhuru mpaka leo, tuna karibu miaka 51, Zimbabwe nadhani wamejitawala mwaka 1980, lakini cha kusikitisha wenzetu ambao tuliwatangulia katika kutawala, kilimo chao ni kikubwa zaidi kuliko sisi Watanzania. Naamini wamechukua rekodi ya maandishi kutoka Tanzania wakaendeleza kwao. Rwanda, wamejitawala karibuni lakini kilimo chao ni kizuri kuliko sie Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Fedha na Uchumi ilipendekeza kwamba Tanzania tuna uwezo wa kuzalisha samaki kuliko nchi nyingine yoyote, lakini suala la uzalishaji wa samaki Tanzania halijapewa kipaumbele. Ukitajiwa maeneo ambayo yanazalisha samaki, unaambiwa hapa panazalisha samaki basi hayalingani na maeneo hayo wakati tuna Mito, tuna Maziwa, tuna Bahari tunaweza kuwekeza katika sehemu ya ufugaji wa samaki na ninaamini kwamba Tanzania inaweza ikaingiza mapato makubwa zaidi kuliko nchi nyingine yoyote katika uzalishaji wa samaki. Nchi kama Mauritius inajiendesha kwa sekta ya uzalishaji wa samaki. Kwa nini Mito, Maziwa na Bahari tulizonazo Tanzania tushindwe kuzalisha au kuwekeza katika ufugaji wa samaki? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la mfumuko wa bei. Wenzangu wamesema kwamba miongoni mwa mambo ambayo yamechangia mfumuko wa bei, ni suala zima la vyakula hasa mchele, sukari...

(*Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba za Kamati zote. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mimi nimetoka juzi Mauritius, sasa hivi wana tatizo la samaki. Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Arfi?

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi angalau kidogo niweze kuchangia japo kuwa leo sauti yangu sio nzuri lakini nitajaribu kidogokidogo niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nizipongeze na niwapongeze Wanakamati wa Kamati zote pamoja na Wenyeviti kwa namna walivyowasilisha mapendekezo, maono na mipangilio au mikakati ya Kamati kuwapelekea Wizara na Serikali ili iweze kuyatekeleza.

Mheshimiwa Spika, nataka kwanza ni-*declare interest*, mimi ni mmoja kati ya Wajumbe wanaounda Kamati ya Bunge ya Miundombinu. Kwa hiyo, nitajikita zaidi katika taasisi au Wizara ambazo Kamati yetu ya Miundombinu inazishughulikia. Nataka nianzie na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Mwaka jana tuliridhia Azimio ambalo lilihusiana na masuala ya utafiti. Nakumbuka nilitaka kuondoa shilingi kwa Waziri, kwamba Waziri umetuletea *Protocol* na tumeiridhia, *Protocol* ambayo ndani yake ilizungumza kwamba nchi wanachama ni lazima iwekeze

20 APRILI, 2012

certain amount ya pesa ambayo haipungui *1 billion* kwa ajili ya utafiti katika nchi husika. Bahati mbaya Waziri wetu akawekewa fedha kidogo na akaridhia. Hata hivyo, nataka nichukue nafasi hii, kwa sababu wanadamu wanasema mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni, nimshukuru Naibu Waziri wa Wizara hii ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia pamoja na Waziri wake kwa namna wanavyofanya kazi, *COSTECH* wameweza kwenda vizuri, sasa hivi wanaanza kufungua ofisi Zanzibar. Vilevile tumeona katika kipindi cha mwaka jana, wakati Kamati ilitoa mapendekezo yake kwamba hebu angalieni namna ya kusaidia wanafunzi, wameweza kutusaidia wanafunzi sita (6) ambao tayari wameshawapeleka katika vyuo. Kubwa zaidi ni kuweza kusaidia takribani shilingi milioni 650 kwa kituo chetu cha utafiti kilichoko kule Zanzibar Kizimbani, hilo tunawashukuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi ni kukubali kuweza kutujengea jengo la Shirika la Posta pale Chakechake ambalo tumeahidiwa kwamba katika sherehe hizi za Muungano litawekwa jiwe la msingi. Kwa hiyo, kwa upande wa Sayansi na Teknolojia kwa kweli tunashukuru kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Spika, niingie katika Wizara ya Uchukuzi na nianzie na suala la msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Kwa kweli suala la msongamano wa magari Dar es Salaam limekuwa ni tatizo, limekuwa ni gugumaji ambalo limetukabili au limewakabili hasa wakazi wa Dar es Salaam. Tatizo kubwa la msongamano wa Dar es Salaam ni kwamba viongozi wenyewe hawajawa na utashi wa kisiasa kuliondoa tatizo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina sababu ya kusema hivyo. Suala la Jiji la Dar es Salaam hasa katika masuala ya usafiri, linamilikiwa na maeneo yasiyopungua manne, pale kuna Wizara ya Uchukuzi, kuna TAMISEMI, kuna Manispaa, Polisi na wengine ambao wanashughulikia suala hili. Kwa kweli hawa kila mmoja anatafuta namna yake ya kuweza kupata mapato, hawana kitu ambacho ni kimoja ambacho kinaweza kushughulikia suala la usafiri wa Dar es Salaam. Kamati imependekeza mambo mengi, tunaangalia Serikali itafanya nini, imependekeza masuala ya *flyovers*, kuna mapendekezo ya mabasi yanayoenda kwa kasi ambayo imekuwa kama ni suala la *DARTS*, imekuwa kama ni lugha ya kawaida tu ileile, tumeweza, tumefanya hivi na tutaendelea kusonga mbele. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo hapohapo. Sasa *DARTS* linabakia huku, lakini ukweli wa *DARTS* haionekani kama Serikali ina dhamira ya kweli kuhusiana na mabasi yale yanayoenda kwa kasi. (*Makofi*)

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, lingine ni upungufu wa watendaji wa kushughulikia sheria zilizopo katika Jiji la Dar es Salaam. Kwa mfano, sheria zinasema kila ambaye atajenga jengo Dar es Salaam hususani la ghorofa basi aweke angalau *parking* na ramani zinapopasishwa kitu hicho kinaangaliwa kwamba je *parking* zipo? Ramani zinapitishwa kila siku, *parking* zinaonekana katika ramani, lakini wakati wa ujenzi hakuna *parking* inayowekwa matokeo yake sehemu zile zinageuzwa ma-*godown* au zinafunguliwa maduka ya biashara, msongamano uko palepale.

Mheshimiwa Spika, Kamati tumetoa mapendekezo, *at least* kuanzisha reli ambayo itatoka Stesheni hadi Ubungo Maziwa, haionekani kama kuna dhamira ya dhati Serikali inaweza kutekeleza. Nina wasiwasi kwamba tutakapofika katika bajeti haya yote ambayo tumeyazungumza kuhusu kuondoa msongamano wa Dar es Salaam yatashindwa kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, niende haraka haraka kwa sababu muda wangu uliobaki ni mdogo, nizungumzie suala la Bandari ya Dar es Salaam, hususani ujenzi wa gati Na.13 na 14. Nilimuuliza Waziri Mkuu Alhamisi iliyopita, najua alinjibu, kwamba, je, nchi hii imefilisika? Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu hakunielewa akaniambia kwamba kama imefilisika hata wewe usingekuwepo hapo, *Inna lillahi waina ilaih rajjuun. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi imefilisika kimawazo, viongozi wetu hawataki kufikiri, viongozi wetu hawataki kuelewa, ubinafsi umewajaa viongozi wetu. Hili ndilo tatizo tulilo nalo. Gati 13 na 14, tukubali kwamba ndiyo gati pekee ambayo itaisaidia uchumi wa Tanzania. Bandari ya Dar es Salaam ndiyo bandari pekee ambayo inasaidia bandari za Tanga, Mtwara na Bandari nyingine. Kufunguka kwa bandari ya Dar es Salaam, kutasaidia hata kufunguka kwa hii reli. Ikiwa leo Wazee wetu katika miaka mia iliyopita wameweza kufikiria suala la kuweka reli, leo sisi tunashindwa namna ya kuweka reli? Tutanue bandari, tutengeneze hii bandari ili tuweze kutengeneza na hizi reli.

Mheshimiwa Spika, mgogoro uliopo katika bandari ya Dar es Salaam baina ya Waziri na watu wake, sisi Kamati kwa kweli tumeufanyia kazi na tumetafuta nini kiini cha mgogoro ule na tatizo, jibu lilitoka juzi hapa kwa Waziri, anaulizwa swali lingine yeye anakwenda kuzungumza mambo ya *China Merchant*. Alisema yeye mbali ya kwamba ataingia jikoni tu, lakini atafika mpaka chooni, hatari kwa sababu chooni anaweza kukutana pengine na mkwe wake. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja hizi. *(Makofi)*

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni ya leo na mimi niweze kuchangia taarifa za Kamati mbalimbali za Bunge.

Mheshimiwa Spika, mimi leo nitachangia katika Kamati ya Nishati na Madini na napenda ku-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini. Kwanza kabisa, napenda niwapongeze Wenyekiti wote kwa ujumla wao na Wanakamati wote kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika Kamati zetu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe shukurani za kipekee kwa Kamati yangu ya Nishati na Madini kwa kazi kubwa wanayoifanya bila kujali muda lakini kwa kujali maslahi ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Nishati na Madini, mimi nitachangia katika mpango mzima wa umeme wa muda mrefu na umeme wa muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa umeme wa muda mfupi Serikali imeweza kujitahidi kuondoa tatizo la giza katika nchi yetu katika mpango huu wa umeme wa muda mfupi na tulifanikiwa. Lakini katika kununua mitambo kuna ile mitambo ya kukodisha, mitambo ya kukodisha ina gharama kubwa. Tuangalie sasa Serikali inafanya nini katika kununua mitambo yake yenyewe angalau katika kipindi cha muda wa miaka mitatu, pole pole tuwe na mitambo yetu wenyewe ambayo itatusaidia kuondoa *capacity charge* ile mitambo ya kukodisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* kumekuwa na matatizo. Tatizo la *TANESCO* linawachanganya hata wananchi na hasa wananchi wangu wa Mkoa wa Dar es Salaam wanashindwa kuelewa Serikali inatangaza hakuna mgao wa umeme. Lakini hapo hapo utakuta maeneo ya Mbagala, Temeke, Sinza, kuna kukatika katika kwa umeme kwa mara zote. Wananchi kwa kweli hali hii iliwashangaza sana. Lakini mimi napenda niwaambie wananchi wangu nikiwa kama Mjumbe wa Kamati hii si tatizo la mgao na wala kweli hakuna mgao wa umeme, tatizo ni miundombinu ya *TANESCO*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali kulipozibwa na giza nene, ilijitahidi kununua mitambo mingi na mingine kukodisha ili kuondoa tatizo kwa wananchi wangu. Lakini mitambo ile iwapo itawashwa yote tunaweza kupata *megawatts 1,270* au na zaidi. Lakini uwezo wa kuingia kwenye Gridi ya Taifa umeme huo ni *megawatts 972* yaani haizidi hata 1,000; hilo ni tatizo tena ni tatizo kubwa. Kwa maana hiyo tumejitahidi sana katika

20 APRILI, 2012

kununua mitambo na kukodisha lakini miundombinu iliyopo haitoshelezi hali ambayo inasababisha tuzime mitambo mingine.

Sasa nawaomba hawa watu wa *TANESCO* wanapokaa kujadili mipango yao mikakati, wawe wa kweli na waseme nini kianze, nini kiishie. Tunapoletewa kwenye Serikali kwamba kuna tatizo la maji kwa hiyo, Serikali inaelekeza akili zote kwenda kutatua juu ya kununua mitambo ya umeme wa dharura. (*Makofi*)

Lakini huku nyuma kuna tatizo lingine nalo ni la miundombinu. Sasa jamani kila siku nchi hii wataiweka hivyo yaani linatatuliwa hili, hili linaanza. Hili linatatuliwa, mimi nilombe sasa Serikali tuwe makini na Shirika hili la *TANESCO*, tuhakikishe mipango yake, wanayotenda na wanayosema yawe ya kweli vinginevyo inatuchangia hata kuyumba sisi kama Wabunge na Serikali nzima, haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kuchangia ni kupendekeza hii miradi ya maendeleo ambayo *TANESCO* waliisema katika bajeti yetu iliyokuja kwamba kutakuwa na ule mradi wa kupeleka umeme Kibwegele - Kibamba, Kibwegele - Mbezi Juu, Mbande, Chamazi, Kibada mpaka Mji Mwema na pia Pemba Mnazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mipango ile tuliambiwa kwamba ikifika Julai itakuwa imekamilika pamoja na urekebishaji wa umeme kuzuia au kupungua kwa ile hali ya kukatika, umeme kupungua nguvu zake katika maeneo ya Mbagala na Kinondoni, hali ambayo Serikali ilisema itajenga vituo vya umeme viwili, kimoja Mbagala na kimoja Ubungo ili kurekebisha hali hiyo ambayo inasababisha wananchi wengi kuharibikiwa na mali zao. Naiomba Serikali yale ambayo wameyapanga wayatekeleze sasa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo pia naomba sasa niliombe Shirika langu la *TANESCO* katika kuwasaidia wananchi wake kuwawekea umeme wao kama Shirika ambalo linaangalia mapato na inatoa huduma kwa wananchi wake, waangalie uwezekano wa kuwaunganishia wananchi wake umeme na wao kuwakata hizo gharama katika *tariff* zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wameelekeza suala la umeme kwenye *Akiba Bank*. *Akiba Bank* ni benki ya biashara ambayo kwa wananchi kweli itatoa huduma, lakini huduma ile mbele inaweza ikaleta madhara kwa sababu wao watawapa ile huduma kibiashara zaidi na watawalipisha riba kubwa kiasi ambacho wengine wataanza kutuletea matatizo na inawezekana yakaleta matatizo baina ya benki na *TANESCO*. Ni vyema sasa Shirika langu la *TANESCO* likaangalia jinsi gani kwa wananchi hawa

20 APRILI, 2012

kuweza kuwaunganishia wao kama biashara na hata kuwaongezea riba kidogo ili iwaongezee kama *TANESCO*, kama shirika na wala si kumpa mfanyabiashara au benki ya biashara ambayo italeta matatizo.

Mheshimiwa Spika, nayaona matatizo ya Mkoa wa Dar es Salaam katika mikopo. Watu wengi wananyang'anywa mali zao, kina mama wananyang'anywa mpaka vyombo vya nyumbani kwa matatizo ya mikopo. Sasa niombe Serikali iwalinde wananchi wake kwa kuwakopesha wao na walipe kupitia *tariff* zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nichangie katika suala zima la wasimamizi wa mafuta na hasa *EWURA*. Serikali katika mpango wake wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja kweli imesaidia kupunguza baadhi ya kodi ambazo wafanyabiashara walikuwa wanatozwa kwa kulimbiliza kwa kujaa kwa meli pale bandarini, hali ambayo imewapa nafuu wenye matenki ya mafuta, wale matajiri wakubwa. Lakini haikumpa nafuu Mtanzania wa kawaida yule wa chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo, *EWURA* katika mtazamo wake inaishia kwenye kituo cha mafuta (*Petrol Station*), haishii kwenye duka la mlaji. Wananchi wananunua mafuta ya taa kwa lita mpaka shilingi 3,000, wale wanaonunua katika vikoroboi. *EWURA* haimwangalii yule mwananchi, inawaangalia matajiri wakubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapa watu ndipo wanapojiuliza kuna nini kwa hawa watendaji wetu? Lengo la Serikali wanaweka hizi mamlaka kumsaidia Mtanzania na hasa yule wa chini aweze kupata nafuu ya maisha yake. Lakini badala yake unakuta vyombo vinasimamia maeneo ya juu, uagizaji mkubwa, yule mwananchi wa chini nafuu haioni. Naomba sasa hili Shirika langu la *EWURA* lirudi kwa wananchi nao kuhakikisha yale wanayoyasema kwenye redio na kwenye TV ni kweli yako sahihi? Wananchi wanakaa, wanalaumu Serikali, wanatulaumu Wabunge wao, lakini mambo sivyo yalivyo. Utakuta watu wanaongea *research* wanafanyia kwenye meza, hii hali siyo nzuri. Hebu shukeni kwanza, shukeni kwanza kwa wananchi, hebu piteni kwa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa muwaulize hali ikoje? Watakuelezeni nini kinachoendelea. Mnakaa kwenye meza, *EWURA* leo imefanya hivi, imesaidia mwananchi. Inapita kwenye *Petrol Station* mnachukua bei. Mnachukua bei za wa chini wanatumiaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naiomba sana *EWURA*, hiki kitu kishughulikiwe vizuri kwa sababu mara nyingi imekuwa ikileta matatizo na hata utata baina ya wananchi na Serikali yao kumbe mambo sivyo yalivyo. (*Makofi*)

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, sasa nakuja katika upande wa miundombinu. Kwenye miundombinu mimi nitachangia katika upande wa Bandari ya Dar es Salaam. Bandari ya Dar es Salaam...

(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Namwita Mheshimiwa Freeman Mbowe hayupo. Mheshimiwa Moshi Sulemani Kakoso, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga pia ajiandae.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja za Kamati.

Kwanza niwashukuru watoa hoja wote watatu wamechangia mawazo mazuri ambayo naamini yakifuatwa yanaweza yakaleta tija kwa maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi najikita kwenye miundombinu. Miundombinu Kamati imewasilisha taarifa nzuri, lakini bahati mbaya karibu miradi mingi inayohusu miundombinu haijakamilika. Taarifa zinapoletwa za bajeti tunadanganywa Wabunge. Tunapitisha hapa taarifa na bajeti yetu inapitishwa tukiwa na matumaini na wananchi wetu wanakuwa na matumaini makubwa sana kwamba miradi itakamilika. Lakini bahati mbaya karibu miradi mingi ya barabara haijakamilika. Nina mifano, barabara ya ujenzi ya kutoka Sumbawanga kuja Mpanda kwa kiwango cha lami imesinzia mpaka leo hii, lakini wananchi wanaangalia sasa nini matokeo yake.

Mheshimiwa Spika, kuna barabara iliyoahidiwa na Serikali ya ujenzi wa kutoka Mpanda kwenda Uvinza bado hakuna lolote lililofanyika. Tunaiomba sana Serikali ijaribu kuangalia yale ambayo inaahidi yaweze kutekelezwa. Bahati mbaya Mkoa ya Kusini ina hali mbaya ya miundombinu kwa maana ya Mkoa wa Rukwa, Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba sana Serikali ielekeze nguvu katika maeneo hayo ili yaweze kufanana na mazingira ya sehemu nyingine ya nchi yetu. Tuna mradi wa ujenzi wa bandari kule katika Ziwa Tanganyika eneo la Karema. Ukifika katika mradi huo utashangaa ni kama mchezo wa kuigiza unaofanywa. Kuna hali mbaya na nashangaa

20 APRILI, 2012

ni kwa nini wakandarasi ambao hawana sifa wanapewa miradi kama ile mikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye ujenzi wa bandari ukweli kilichofanyika wameenda kujenga choo tu. Lakini taarifa kila siku Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri husika wanaripoti kitu ambacho kwa kweli bado hakijafanyiwa kazi. Niwaombe sana watafute wakandarasi ambao watakuwa na sifa za kufanya hiyo kazi ili wananchi waweze kuangalia kile ambacho kinaahidiwa na Serikali na kuona kwamba kinatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Mpanda, naishukuru sana Serikali kwani tuna kiwanja kizuri sana. Lakini bahati mbaya hakina ndege yoyote inayoruka pale. Kile kiwanja kimejengwa kama maonyesho tu. Tunaomba sana Serikali iweze kuleta huduma ya mafuta ili kiwanja kile kiweze kutumika vizuri na kiwanufaishe wananchi kuliko ilivyo sasa tutaishia tu kuangalia kiwanja kilivyo kizuri. Hali halisi ya kile kinachotarajiwa na wananchi hakitakuwa sahihi na hakitakuwa na tija kwa manufaa ya wananchi wa Mpanda na kwa manufaa ya Taifa zima.

Mheshimiwa Spika, juu ya miundombinu ya reli. Tuna reli ya Mpanda inayounganisha na mkoa wa Tabora. Reli ile imechakaa kwa kiwango kikubwa sana na bahati mbaya sasa hivi hata watumishi wa reli wamekuwa sasa wanatumia kama shamba la bibi, ile reli hasa kwa usafiri ule wa treni inayokuja Mpanda.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tabia na sasa hivi wananchi wanaposafiri kwenda Tabora lazima awe amechukua posho ya kutosha. Kuna uhuni unaofanyika na watumishi wa treni hiyo, imefikia hatua wanauza mafuta, treni inasimama mahala popote pale njiani jambo ambalo ni la hatari kubwa, wasafiri na wajawazito, wanapata shida, tuna watoto wanaokuwa wanasafiri katika treni ile lakini hawana uhakika wa kufika katika safari ambayo wamekuwa wameazimia kwenda.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali iangalie kwa kina na itafute mbinu gani ya kuwachukulia hatua wale wazembe wanaofanya hujuma katika reli ya Mpanda na watumishi wanaohujumu treni inayokwenda Mpanda. Lakini haitoshi bado hatuna behewa za kutosha. Wananchi wengi wangependa sana kusafiri kwa treni na ukizingatia barabara karibu zote zimeharibika kitu ambacho walikuwa wanategemea sana ni reli ile lakini bado nayo ina matatizo makubwa sana. Behewa zenyewe ni za shida.

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, pia tuna mizigo mingi ya Mpanda hasa mahindi na mpunga unaotegemewa kusafirishwa kwenda katika mikoa ile yenye uhaba wa chakula, lakini bado mahindi hayo yanakuwa na shida ya kusafirishwa kiasi kwamba hata wafanyabiashara wanakosa imani ya kutumia reli hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa sana kuiomba Serikali iweze kufuatilia yale ambayo Kamati imeshauri ili yaweze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ninaomba tuna wakandarasi ambao hawana sifa katika Mkoa wa Rukwa, Serikali ijaribu kuleta walau kituo katika Ukanda huo kwa makandarasi ili tuwe tunapata vifaa vya kukodi katika maeneo ambayo yako kule. Vinginevyo hatutapata watu ambao wataweza kusaidia shughuli za uendelezaji wa ujenzi wa barabara na ujenzi wowote ule unaohitaji makandarasi ambao watakuwa na sifa imara ili tuweze kupata huduma iliyo safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja ya Kamati na ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante, sasa nimwite Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Haji Kombo ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Christina Mughwai. *(Makofi)*

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uzima kwa siku hii ya leo nikasimama mbele ya Bunge lako Tukufu nami kuchangia hoja za Kamati. *(Makofi)*

Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, pia napenda kuwashukuru Wenyeviti wote waliowasilisha maoni ya Kamati leo na kwa kuweza kuyawasilisha nasi kuweza kuyachangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kuanza na reli, naiomba Serikali ifanye juhudi za makusudi za kuweza kuboresha reli iliyopo wakati wakijipanga kubadilisha na kuweka reli yenye geji kubwa, waboreshe kwanza hii reli iliyopo kwani wananchi wanaoishi katika Mikoa ya Kigoma, Mwanza, Shinyanga, wanapata shida sana. Wananunua vitu kwa bei ghali sana kwa mfano, mfuko wa *cement* mmoja unapofika Mwanza au Kigoma unauzwa mpaka shilingi 20,000 au 22,000; hii haiwezi ikamjengea Mtanzania maisha bora bali inazidi kumdhoofisha na kumpa umaskini. *(Makofi)*

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, vilevile barabara zetu nyingine zinaharibika kwa sababu ya kuchukua mizigo mizito kwenye malori. Lakini kama reli ingeweza kufanya kazi, ninafikiri pamoja na barabara hizi kujengwa chini ya kiwango lakini zingeweza kuhimili kama hazingeweza kupitisha mizigo mizito sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iweze kulifikiria hili, wakati wanasubiri kubadilisha mataruma ya reli waweze kuboresha kwanza reli iliyopo, akinamama na watoto wanaosafiri hasa kwa treni ya kwenda Kigoma na Mpanda waweze kwenda bila matatizo wala usumbufu. Si reli peke yake, waboreshe na mabehewa, kwa sababu mabehewa yamekuwa na matatizo chungu mzima wanayosafiria binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili na mimi ningependa nigusie kidogo kwa upande wa Bandari ya Dar es Salaam. Inasemekana Bandari ya Dar es Salaam ndiyo inayotengeneza faida. Bandari zote ambazo zipo katika nchi yetu hazitengenezi faida, zinategemea kuendeshwa na Bandari ya Dar es Salaam. Hivi tujiulize ni kwa nini Bandari ya Dar es Salaam peke yake iweze kuhudumia bandari zingine zote? Kwa sababu kwanza kama vile Bandari ya Mwanza ilikuwa inaweza kupokea mzigo mkubwa wa Uganda ikapeleka mzigo ule Uganda, kukosekana kwa reli ya uhakika sasa hivi inapokea mizigo michache sana na kuweza kuisafirisha. Ni lazima kwa sasa bandari hii isitengeneze faida na iweze kulishwa na Bandari ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi ningeomba, ndiyo maana nimeongea kwamba reli ni kitu cha muhimu, kama reli itatengenezwa, matatizo ya Watanzania yatapungua. Nikirudi pale pale kwenye Bandari ya Dar es Salaam, kwenye gati 13 na 14 kama walivyoongea wenzangu, gati hii imekuwa na matatizo ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kwanza imeanza kushughulikiwa kwa muda tangu mwaka 2008 wapo katika kushughulikia gati, mwaka 2009/2010 mpaka leo mwaka 2012 na mambo yameelekea kunyooka. Lakini sasa hivi limekuja tatizo na tatizo kubwa ni Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Uchukuzi hashauriki, haambiliki na wala hawezi kuiheshimu Kamati hata siku moja. Kwanza napenda kumshukuru Mwenyekiti wangu, Mheshimiwa Peter Serukamba, ni Mwenyekiti asiye na hasira, ameweza kwenda na Mheshimiwa Waziri taratibu, lakini majibu yake hayaridhishi. Ni kama juzi amejibu mbele ya hadhara hapa kwamba atawafuata watu mpaka chooni. *(Kicheko)*

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, Waziri huyu huyu ndani ya Kamati anang'ang'ania Bandari ya Dar es Salaam pamoja na kwamba tumekwishapata uelekeo wa mkopo anang'ang'ania itangazwe; tunauliza, kulikoni? Anachong'ang'ania Bandari hii iingie kwenye PPP wakati tayari imeshapata mkopo, ni kitu gani? Yeye anafaidika na nini kwa PPP wakati Bandari wameshapata mkopo? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini ni Waziri huyu huyu ameweza kumchukua mtu mtaani akampeleka ATCL, Mkurugenzi Mtendaji bila kutangaza. Sasa ananufaika nini na Mkurugenzi Mtendaji hakutangaza nafasi hii? Na leo anang'ang'ania ujenzi wa gati 13 na 14 utangazwe? Kuna nini katikati? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ninaona hii ni zaidi ya RICHMOND kwa sababu, ametayarisha mkataba ambao unasema; "Mkataba huu ni siri na hautakiwi kuonwa na mtu yeyote isipokuwa mwekezaji." Hii ni mali ya Watanzania, wanapopewa dhamana Mawaziri, wajue kwamba wamepewa kulinda mali za Watanzania na sio mali yao wao kama wao, kuna nini hapa? Kwanza unamng'ang'ania mwekezaji huyu, pili unasema mkataba huu uwe siri; kuna nini hapa katikati? Sisi tunajiuliza kama Kamati, kuna nini? Ameshikwa na nini huyu Mheshimiwa Waziri? Hii ni hatari kwa Watanzania, huku ni kupoteza mali ya Watanzania na pia huku ni kuweza kuwaweka Watanzania katika hali mbaya ambayo kila siku tunaipigia kelele humu ndani ya jengo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, mkataba wa mwekezaji wake aliyemleta ni miaka 45 aendeshe gati hilo 13 na 14 tena bila kuingiliwa na mtu. Kitu cha ajabu, mkopo ambao unatoka Exim Bank China, utakwenda miaka 12; miaka 45 kwa miaka 12, hata hesabu hii ukimpa mtoto wa chekechea, atakwambia kipi kina maana kati ya hivi vitu viwili, kuna nini hapa katikati? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sisi tungewaomba Mawaziri, nchi hii ni yetu sote, tungewaomba walichopewa ni dhamana na wakati wowote walichopewa sio chao, mtu yeyote anaweza akakaa kwenye nafasi ile kwa manufaa ya Watanzania wote. Mbaya zaidi na ni kwa nini nilimshukuru sana Mwenyekiti wangu wa Kamati, ameweza kumtetea Mkurugenzi Mtendaji aliyemuweka ATCL, akisema yuko tayari kuacha Uwaziri wake, lakini Chizi awe Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL. Huyu ndio Waziri ambaye tunamtarajia kulinda maslahi ya Watanzania na mali za Watanzania.

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu binafsi, nasema Waziri huyu hafai kuwa Waziri na wala hafai kuiongoza nchi hii na wala hafai kuiongoza Wizara hiyo kwa sababu, Wizara ya Uchukuzi ndio Wizara mama nchi hii. Wizara ya Uchukuzi, ndio Wizara inayoweza ikatatua matatizo ya Watanzania. Wizara ya Uchukuzi ndio Wizara ambayo, inaweza ikamneemesha Mtanzania au kumuangusha Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umefika wakati Mawaziri ambao hawawezi kulinda mali za nchi, waachie ngazi na wawaachie wengine waweze kuondoka hapo walipo ili waweze kutuondoa Watanzania, lakini sio kuweka mikataba ambayo inamfilisi Mtanzania. Miaka 45 gati litakuwa limekwishachoka, ina maana watu hawa ambao hataki waulizwe wala mikataba yao haionekani kwa mtu yeyote, watakuwa wamekwishaondoka na itabidi tutafute mwekezaji mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi yangu ni hayo kwa ufupi. Napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hoja iliyoko mezani. *(Makofi)*

Nazipongeza Kamati zote kwa taarifa nzuri na hususan Kamati yangu ya Fedha na Uchumi chini ya Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Daktari Abdallah Kigoda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaongelea ukuaji wa Pato la Taifa na nitaongelea suala la Mapato na Matumizi ya Serikali kama ambavyo ni sehemu ya taarifa ya Kamati yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu na taarifa ya Serikali inatuambia kwamba Pato la Taifa kwa mwaka 2010/2011 limekuwa kwa 6.3% na mwaka uliotangulia Pato la Taifa lilikuwa kwa 7%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali ambalo tunajjuliza kila siku, haiingii masikioni kwa Watanzania walio wengi kuwaeleza kwamba Pato la Taifa linakuwa kila mwaka ilhali hali ya maisha ya Watanzania ikizidi kuwa ngumu na duni kila siku. Wananchi wanajjuliza hili Pato la Taifa linakuwa kuelekea upande upi, mbona haliwaelekei wao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Pato la Taifa limechangiwa kama ambavyo tunaambiwa na sekta ambayo haijumuishi au haiajiri Watanzania walio wengi kama vile huduma, viwanda na ujenzi. Lakini kila mara Kamati yetu imekuwa ikiishauri Serikali juu ya kuongeza ufanisi katika sekta ambayo

inaajiri Watanzania wengi ambayo ni sekta ya kilimo. Ikifanya vizuri sekta hii hapo Pato la Taifa litakuwa na manufaa na litaonekana moja kwa moja kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikijinasibu na Sera yake ya Kilimo Kwanza, sera hii ya Kilimo Kwanza kwa vitendo haionekani; kwani ukuaji katika sekta ya kilimo umepungua, mwaka 2011 ukuaji wa sekta ya kilimo umepungua na kuwa 3.6% kutoka 4.2% mwaka 2010. Sasa je, ni kweli tupo katika sera ya Kilimo Kwanza wakati ukuaji wa sekta husika unashuka?

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ambayo mengine ni rahisi tu kuyazingatia; hivi ni kwa nini Idara ya Uwezeshaji na Uwekezaji imeshindwa kuwekeza tu katika maeneo ya kilimo ambayo ni rahisi wananchi wanalima kwa mfano matunda? Tumeshindwa kuwa na viwanda vikubwa vya kusindika matunda ambavyo tungeweza kuinua kipato cha wakulima, tungeweza kuajiri vijana walio wengi katika viwanda hivyo, lakini matokeo yake tumekuwa tukiagiza maji ya matunda kutoka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule kwetu tunalima alizeti, Mkoa wa Singida unalima alizeti na una viwanda vidogo vya kienyeji vingi vinavyosindika mafuta ya alizeti. Naitaka Serikali, iongeze ufanisi katika usindikaji wa mbegu ili kuongeza mafuta ya kula na kuongeza kodi katika mafuta ya kula yanayoagizwa kutoka nje ya nchi ili kuinua vipato vya wakulima wanaolima mbegu za mafuta katika nchi hii na pia kuboresha afya za Watanzania. *(Makofi)*

Kuhusu Mapato na Matumizi ya Serikali, takwimu za TRA zinasema kwamba nusu ya kwanza ya mwaka 2011/2012 TRA walikusanya mapato yanayotokana na kodi kwa 101.4% na matumizi ya Serikali kwa kipindi hicho yalikuwa ni 87.7%. Sasa cha kushangaza, iwapo TRA walivuka malengo na kukusanya kwa 101% inakuwaje basi fedha za maendeleo hazijaenda katika maeneo ambayo yalibajetiwa? Tumeona Waheshimiwa Wabunge, hapa wakilia kwamba fedha hazijaenda katika Halmashauri na mipango mingi ya maendeleo imekwama, ilhali Serikali inasema kwamba makusanyo hayana matatizo? Fedha zinazokusanywa je, zinaenda kweli kwenye maeneo yaliyobajetiwa na Bunge lako Tukufu?

Mheshimiwa Spika, lakini katika moja ya taarifa zilizowasilishwa na Kamati hapa Bungeni inasema kwamba Serikali ilitumia trilioni 1.3 kwa matumizi ambayo yalikuwa nje ya bajeti. Inashangaza, ikiwa Bunge hili lilikaa likapitisha bajeti, ni nani huyo mwenye mamlaka nje ya Bunge, anayeweza ku-diverge trilioni 1.3 bila idhini ya Bunge na bila hata

kuishirikisha Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi? Mimi naona hii ni dharau kubwa ya Serikali kwa Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, pamoja na mapato kuwa kidogo, tumeshuhudia wigo wa mapato ukiwa hauongezeki. Kuna makampuni ambayo yangeweza kuchangia kutoa kodi, hasa makampuni ya simu, sekta isiyo rasmi ambayo kama ikirasimishwa, inaweza ikachangia katika kuongeza Pato la Taifa, lakini Serikali haijafanya vya kutosha katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi imeendelea kuwa tatizo; nchi majirani zetu, nchi za Afrika Mashariki ambayo na sisi ni wanachama tena wakongwe, wanatoza au wanaruhusu misamaha ya kodi ya 1% tu, lakini sisi Watanzania tunatoza misamaha ya kodi kwa 2.3% ya Pato la Taifa na kwa bahati mbaya misamaha ya kodi inatozwa kwa makampuni binafsi ambayo ndio yana uwezo wa kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi namna hii kweli Pato la Taifa litaongezeka? Naishauri Serikali, kama ambavyo Kamati yangu imekuwa ikipendekeza siku zote, ifute na au ipunguze, haiwezi ikafuta najua misamaha ya kodi ni muhimu katika maeneo fulani, lakini misamaha ya kodi isizidi 1% ya Pato la Taifa ili tuendane sawa na wenzetu katika soko la Afrika Mashariki na ili pia tuweze kuhimili ushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naitaka Serikali izingatie masuala yote yaliyoainishwa na Taarifa za Kamati, Taarifa ya Mdhidhi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, juu ya ubadhirifu mkubwa ulioaibisha Serikali katika Mkutano huu wa Bunge, kwa kuwachukulia hatua wote waliopatikana na ubadhirifu huo. Wachuliwe hatua ili kuwatendea wananchi wa Tanzania haki na kuokoa mabilioni ya Watanzania yasiendeleo kupotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii na ninaunga hoja mkono, hoja ya taarifa ya Kamati yangu ya Fedha na Uchumi. *(Makofi)*

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuwa mmojawao katika kuchangia hoja hizi zilizo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naanza kwa kuzishukuru Kamati hizi kuleta na kubainisha yale ambayo dhahiri yana ukweli usiopingika kwa 100%. Katika haya, mimi nataka nianze na hii Wizara ya Miundombinu. *(Makofi)*

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, mengi yamesemwa na hata tukisema mpaka kesho bado tunayarudia yale yaliyosemwa, lakini ni dhahiri ujumbe umefika hususan kwa wale Mawaziri ambao wanachukulia Wizara zao na maamuzi yao kama vile wanaongoza mashamba yao binafsi na wanasahau kwamba hapa walichokabidhiwa ni dhamana ya kuwaongoza Watanzania na kusimamia mali za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna msiba; huu ni msiba kwa Taifa. Si la kujivunia kuamka vyombo vyote vya habari, kuna picha za Mawaziri wetu zimetandazwa pale, kila mmoja akipewa jina la aina yake, aibu. Hii ni aibu na si la kulifurahia hata kidogo, watoto wetu wanayaona, wanajua na wanayasikia haya na kwa kweli sio mambo ya kufurahia hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninaposema msiba, msiba sio kufa mtu tu, leo wakati na mimi nasema nitakuwa mmoja wa kuchangia na nilisema wazi kwamba kwa kweli sikufurahishwa na kilichomo katika ripoti ya Kamati hii ya Miundombinu. Kitendo cha Waziri wa Miundombinu kutaka kuiingiza nchi hii katika mkenge mwingine, hii ni aibu. Ni juzi, hatujasahau machungu ya *RICHMOND* ya nchi hii yaani nyumba inatoa maiti, yeye anataka kutuletea mgonjwa, atapona? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, lilipotolewa tangazo la kwamba Wabunge 70 hapa waweke saini zao ili kuonesha hisia zao za kutokuwa na imani na Waziri Mkuu, mimi nina hakika hakuna ambaye kwamba haelewi kama Waziri Mkuu ni mtu safi kabisa. Nasema kutoka ndani ya moyo wangu kwamba Waziri Mkuu wetu ni mtu safi kabisa. Mimi sitasema chungwa nikaliita embe, hata siku moja; hatanishinikiza yeyote wala hakuna atakayenipa amri juu ya kuukataa ukweli ninaoamini, na ninaamini hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Mawaziri ambao wanamzunguka Waziri Mkuu, wenzangu wamesema wezi, wenzangu wamesema kila aina ya majina wamewapa; lakini nasema ni vizuri kwa sababu haya yanayotokea hapa hawataanza wao wa kwanza, yameshafanyika, yameshawakuta na wengine tunao humu tunasalimiana nao. Iweje wao wang'ang'anie viti hivi ilhali maozo yao yanaonekana? Hivi wao wanaona raha sisi badala ya kukaa hapa tukajadili mambo mengine ya maendeleo ya nchi hii, kila siku tujadili watu wa aina hii? Wanachong'ang'ania hasa ni nini? Kututoa roho zetu? Watakufa wao, sisi watatuona hivi hivi. *(Makofi)*

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, kwa hili halina u-CCM, halina u-CHADEMA, halina u-CUF, oneni aibu jamani. Kila siku mnatuangalia tukiwaambia jamani, hee, mmezidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa nakumbuka tumeshaalika wageni wengi wengi, *Coastal Union*, Simba, Yanga, sasa kama Kanuni haitakuwa ngumu, naomba tuwaalike Mapadri na Masheikh waje watuombee. Tuna mapepo mabaya humu yameingia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, au niruhusu niombe mimi leo Wabunge waitikie. *(Makofi/Kicheko)*

SPIKA: Utatumia lugha gani? *(Kicheko)*

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, umeniruhusu? *(Makofi/Kicheko)*

SPIKA: Utatumia lugha gani? *(Kicheko)*

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, hoja hiyo kwenye Kanuni haimo, lakini kama hairuhusiki basi. Ila lakini, ee Bwana wetu utunusuru na mafisadi hawa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tuliache hilo, lakini nadhani ujumbe umefika na mwenye macho ndiye anayeambiwa tazama, kiswahili kile cha mwenye macho haambiwi tazama mimi sikubaliani nacho. Mna macho, tunawaambia angalieni; hamuwi wa mwanzo kuachia madaraka wala hamtakuwa wa mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala lingine la miundombinu, kuhusu barabara na msongamano wa Dar es Salaam. Ie hali iliyopo Dar es Salaam, tuna wataalamu wengi tu wa Mipango ya Miji, lakini sasa mimi nataka kusema hatuna wataalamu wa Mipango ya Miji, tuna wataalamu wa Mipango ya Wizi.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani tunatunga Sheria, kama mtu yeyote anataka kujenga jengo kubwa Dar es Salaam, ni lazima aweke eneo la *parking*, lakini leo majumba yanaota kama uyoga. Ukienda na gari lako Dar es Salaam, ukipaki gari wanakuja mgambo, wanalitia lile dubwasha; wewe kosa lako ni nini? *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, mnyororo.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, mnyororo. Pana mnyororo utafikiri wa watumwa, wanatembea nao. Sasa mtu a-park wapi, juu ya vichwa? Mnaruhusu ujenzi holela na kila mtu anakimbilia Kariakoo na Dar es Salaam. Serikali, kila Ofisi yake inajenga Dar es Salaam katikati ya mji, kuna maeneo huko Tegeta na kwingi tu; Dodoma mliyoichagua kuwa Makao Makuu ya nchi, leo kila mtu anang'ang'ania Dar es Salaam, kuna nini Dar es Salaam? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hali inatisha. Mimi binafsi ninakaa Dar es Salaam eneo la Mbezi Juu, lakini nimeiacha nyumba yangu, ndani ina mpaka uwanja wa *tennis* nimekaa Kariakoo kijumba cha *National Housing* vyumba viwili, nashindwa kukaa kwa sababu kutoka Mbezi mpaka mjini Dar es Salaam kwa shughuli zangu inachukua saa tatu. Saa tatu kwenda na saa tatu kurudi, wewe utatumia saa ngapi kufanya nini kuna siku natahadharisha Watanzania Dar es Salaam itasimama ita-jam, itakuwa hakuna kiendacho wala kirudicho, hakuna kiingiacho wala kitokacho kama mtakujasema kama kweli yametokea, mimi si mjukuu wa Yahaya wala si mtabiri wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Lakini hili lipo wazi nawaambia wenye macho tazameni yaoneni ya Dar es Salaam yanatishia na Dar es Salaam ndiyo mji unaotegemewa kwa kila kitu. Tusiogope kuvunja na maeneo ambayo watu wataweza kuifika Dar es Salaam, hakuna uzuri, ukitaka uzuri lazima uzurike kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nashangaa Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu alipotaka kubomoa ile barabara na kuongeza upande huu njia nne na huu njia nne ilizuka sokomoko na ikaingiliwa kati akazuiwa, lakini haikuwa na mantiki hata kidogo kuzuia lile suala lingetusaidia jamani Dar es Salaam, haifikiki mwisho sasa tutaunguzana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ilikuwa nitangulize, nimeona nitoe mwisho napenda kwa dhati kabisa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)

MHE. KHATIB SAID HAJI: Aah!, ahsante sana Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati zote tatu kwa kazi nzuri ambayo wameifanya wao binafsi pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwenye Kamati hizo. Nasema hongereni sana. *(Makofi)*

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, nitakuwa na machache sana kwa leo kwa sababu mengi yamesemwa. La kwanza kabisa niungane pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Januari Makamba katika suala zima la kuhusiana na mpango wa gesi, gesi hii ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu kama Serikali itakuwa makini sana katika suala hili inaweza ikamkomboa Mtanzania na pengine inaweza ikawa ni rasilimali kuliko rasilimali zote ambazo tunazo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja tu ambalo nilikuwa niombe Serikali na nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ni kwamba Serikali iwe makini katika suala hili, tunahitaji sheria madhubuti ya gesi iletwe hapa Bungeni tuweze kuipitisha na gesi yetu iweze kuwafaidisha Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi natokea kule Karagwe, natokea Jimbo la Karagwe mkoa wa Kagera, kama gesi ingeweza kugundulika katika jimbo langu la Karagwe ningemshukuru sana Mwenyezi Mungu. Nawaonea wivu ndugu zangu wa Mtwara kwa gesi hii kugundulika kwao, lakini wakati huo huo nawasikitikia kwa sababu gesi wanaiona tu na wanaisoma kwenye gazeti, hawana faida nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe sana Serikali iwaangalie sana hawa ndugu zetu wa Mtwara ambao gesi imegundulika kwao iwafaidishe. Huu mrahaba ambao tunauzungumzia hapa unatakiwa ubadilishe maisha ya wananchi wa Mtwara ili wafaidike kutokana na mauzo ya gesi, wasiwe watazamaji, wasiwe washangiliaji wakati wengine wanafaidi gesi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nigusie mfumuko wa bei, amezungumza hapa Mheshimiwa Kigoda. Ukienda mitaani Dar es Salaam, hata Dodoma, Kagera, Kigoma na sehemu nyingine unakutana na nyuso zenye huzuni kubwa sana, siyo kwamba hawana mapenzi na wewe unayekutana nao, lakini tatizo ni kwamba wananchi hawa utakuta wengi wanapata mlo mmoja kwa siku na hii ni kutokana na mfumuko wa bei jinsi ambavyo umekuja kwa kasi ya kutisha.

Mheshimiwa Spika, sukari inazalishwa *Kagera Sugar* ambako ni mkoani Kagera ni kilomita chache sana kama 55 kutoka kiwanda cha sukari kuja jimboni kwangu Karagwe. Lakini utakuta sukari ile inavyouzwa wilayani Karagwe katika miji ya Omurushaka, miji ya Kayanga, miji ya Nyakaiga, miji ya Nyaishozi, Ihembe na sehemu zingine, kilo moja ni zaidi ya shilingi 3,000/=. Mwanachi wa kawaida sasa hivi kunywa kikombe cha

20 APRILI, 2012

chai ni mpaka aandikiwe na daktari kwamba unahitaji kupata kikombe cha chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hawezi kunywa chai yeye mwenyewe kwa mapenzi yake kwa sababu hawezi kumudu bei hiyo ya sukari. Mimi nasema hali hii ikiendelea kuna hatari kubwa sana tukapoteza ndugu zetu kwa sababu ya njaa. Mchele sehemu zote kilo moja shilingi 2,000/= na kuendelea, maharage shilingi 1,000/= na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, katika hali kama hii Serikali naiomba iwe makini sana hasa Benki Kuu, wachumi wetu wakae waangalie namna gani mfumko huu wa bei unaweza kudhibitiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamezungumza kuhusiana na Mfuko wa Umeme Vijijini (*REA*), mimi kwanza niwapongeze sana *REA*, wanajitahidi sana na wanafanya kazi nzuri. Nawapongeza jimboni kwangu wanapeleka umeme katika maeneo ya Nyaishozi, wanafanya kazi nzuri nawaomba waharakishe, lakini pia wahakikishe kwamba umeme unafika karibu kila nyumba, siyo umeme upite barabarani, wananchi wanataka umeme na wananchi wangu wana mashamba makubwa kwa hiyo kila nyumba zinapishana kwa umbali mrefu mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia hawa ndugu wa *REA* wanapata matatizo makubwa sana, mimi namuonea huruma rafiki yangu Mheshimiwa Ngeleja, akija hapa Bungeni wakati wa bajeti na najua sasa hivi atakuwa anajiandaa kuleta bajeti nzuri sana. Alisoma bajeti ilikuwa ni bajeti nzuri sana na yenye matumaini makubwa. Akimaliza kusoma unadhani kwamba Tanzania nzima itawaka umeme vijijini kote. *(Makofi/Kicheko)*

Lakini utekelezaji sasa unakuja kuwa mgumu sana, kuna ahadi nyingi hapa tumepewa Bungeni kwamba umeme utawaka vijijini lakini utekelezaji umekuwa ni mgumu, ni mgumu kweli. Nilikuwa naomba katika bajeti ijayo, Mheshimiwa Ngeleja na Serikali kwa ujumla wajiandae kujibu matakwa yetu kuhusiana na umeme vijijini. Tunataka bajeti ambayo inatekelezeka siyo bajeti ya matumaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilitaka nizungumzie leo ni kuhusiana na Wizara yetu ya Miundombinu. Wizara hii imeanzisha miradi mikubwa ya barabara na kwa kweli halikuwa jambo baya. Lakini kama ulivyoona kwenye taarifa Kamati ya Miundombinu, barabara nyingi ambazo zimeanzishwa hazitaweza kuisha katika muda ambao

20 APRILI, 2012

umepangwa na Serikali. Barabara nyingi wakandarasi wanaanza kusimama wanakata tamaa, haziishi, hazitekelezeki kwa sababu ya ukosefu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashauri Wizara ya Miundombinu, niombe sana sasa ijikite katika kumaliza miradi ambayo tayari imeshaanza na iishe kwa wakati. Ni vizuri tukafanya jambo moja zuri na kwa haraka kuliko kugusa huku na tukashindwa kutekeleza mambo yote kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili nilikuwa naomba nitoe angalizo katika barabara inayojengwa ya kutoka Kyaka mpaka Bugene katika jimbo la Karagwe ambako ndiyo jimbo langu, barabara hii ilikusudiwa iwe imeisha mapema sana lakini kwa bahati mbaya naona inakwenda taratibu mno na yule mkandarasi ambaye yupo hapo kampuni ya Kichina naona hana dalili kabisa za kuanza hata kumwaga lami. Wananchi wameanza kumtukana hata Mbunge utadhani mimi ndiyo nimeingia mkataba, kwa hiyo naomba Serikali iliangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine kuhusiana na Shirika letu la *TANESCO*, wanajitahidi kufanya kazi nzuri mno tofauti wanavyowafikiria. Tatizo la *TANESCO* ni kwamba fedha wanayopewa ni ndogo sana, *TANESCO* wanatakiwa kusambaza umeme nchi nzima, lakini utakuta miundombinu yao ni ya muda mrefu, imechakaa na mingine kwa kweli ni kama imekufa na *transforma* waliyonayo nyingine hazina ubora zinalipuka asubuhi, zinaleta tishio kwa wananchi. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri *TANESCO* liangaliwe vizuri liweze kupewa fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunahitaji kabisa kuwa na sheria nzuri ya madini, hivi karibuni tuliambiwa kwamba kuna madini ya *Uranium* yamegundulika na inawezekana muda wowote yakaanza kuchimbwa lakini tusingetaka kuona madini haya ambayo ni muhimu na yenyewe yanaingia katika mtego wa madini mengine ambayo tumeshuhudia Taifa likipata hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashauri kwamba kabla mradi huu wa *uranium* haujaanza kuchimbwa basi angalau Watanzania waelimishiwe kiasi cha kutosha, Wabunge tuelimishwe kiasi cha kutosha, semina zipite za kutosha na mabadiliko ya sheria mazuri ya kufaidisha nchi yetu yaletwe hapa tuyafanyie kazi. *(Makofi)*

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema wenzangu wamezungumza mengi mimi kwe leo nilikuwa na machache, mimi niendeleo kupongeza Kamati zilizofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho tu nigusie kuhusiana na Waheshimiwa Mawaziri ambao wamezungumzwa na wenzetu hapa Bungeni siyo jambo zuri sana kuona Mheshimiwa Waziri unanyooshewa kidole, hata mimi hainifurahishi, ningekuwa labda kwenye nafasi yako ningejisikia vibaya sana. Lakini mimi nipende kusema kwamba Serikali ichukue jambo hili *seriously i-take note* kwamba kwa nini kwa mara ya kwanza Mawaziri wetu wananyooshewa kidole namna hiyo?

Mimi ni mwanasheria, ninaamini kwa mtu kupewa nafasi ya kujieleza kwa sababu naweza nikasimama nikamsema Waziri ninavyotaka kwa sababu hana nafasi ya kujieleza pengine naweza nikamuonea. Lakini ninasema mtu mzima hawezi kusimama hovyo hovyo akasema bila sababu za msingi. Kwa hiyo, nilikuwa nasema Mawaziri...

(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Ni kengele ya pili Mheshimiwa?

SPIKA: Ya pili.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Spika, naunga mkono. *(Makofi)*

SPIKA: Niliona yale uliyokuwa unayasema nilitaka uyamalize vizuri. Nasikitika kule nyuma umeme umezimika najaribu kupata taarifa kwa nini. Mheshimiwa Mahenge.

MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE: Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuwa mchangiaji kwenye hoja hizi zilizotolewa na Kamati zetu na nianze na taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukiongelea miradi ya MCC ambayo inafadhiliwa na Marekani (*Millenium Challenge Cooperation*) na sasa karibu tunaenda kwenye bajeti mwezi wa sita, lakini tuliambiwa vilevile kwamba miradi hii itakamilika mwishoni mwa mwaka huu wa 2012. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani kwa sababu nimeangalia kwenye taarifa ya wenzetu sikuliona hili limeongelewa mahali fulani. Sasa nilikuwa nadhani ni muda muafaka basi Serikali itakapokuwa inatoa ufafanuzi kwenye masuala haya basi ielezee utekelezaji wa miradi hii hasa usambazaji

umeme kwenye maeneo yaliyokuwa yameainishwa ikiwemo yale ya Jimbo la Makete.

Mheshimiwa Spika, tuliambiwa tulipofuatilia kwa Mkurugenzi Mkuu wa MCC Ndugu Mchomvu alituahidi kwamba Makete wataanza kuweka ile miundombinu ya ule umeme Tandala na maeneo mengine mwezi wa tano yaani baada ya siku chache na kwamba natarajia mwezi wa tisa wawe wameshakamilisha wawashe ule umeme na mwezi wa kumi na mbili watakuwa wamekamilisha suala la umeme kwenye mradi huu katika Tanzania nzima. Sasa nimuombe Mheshimiwa Ngeleja atakapokuwa anatoa taarifa basi aelezee utekelezaji wa miradi hii...

SPIKA: Sema Waziri wa Nishati na Madini...

MHE. DKT. BINLITH S. MAHENGE: Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini atupe basi taarifa vizuri kama ni kweli hiyo ratiba itafikiwa na itatekelezwa kama ilivyokuwa imeahidiwa nadhani wananchi wangu na wananchi mahali pengine watafurahi sana kulisikia hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu usambazaji wa umeme vijijini, wote tunafahamu kwamba ili kuleta maendeleo vijijini kuna mambo muhimu ambayo yanatakiwa yatekelezwe ikiwemo umeme, maji, barabara za vijijini, huduma za afya, elimu na kadhalika. Kwa hiyo, umeme ni suala ambalo ni muhimu sana. Sasa tunachokiomba hapa ni kwamba ili kuonyesha mgawanyo wa rasilimali za Tanzania kwamba zinamfikia kila Mtanzania au kila wilaya au kila kijiji au kila kata basi ni vizuri wenzetu wa Wizara ya Nishati na Madini waandae mpango mkakati unaoonesha jinsi walivyojipanga kupeleka umeme vijijini ili kila wilaya ijionee, kila kata ionekane kwamba hata kama hakuna fedha za kupata umeme mwaka huu lakini tumekadiriwa pengine ndani ya miaka minne au mitano kwamba itakuwa ni zamu yetu. Nadhani hili litakuwa ni jambo la wazi ambalo linaweza likavutia hisia za watu wote kwamba na sisi tupo kwenye mpango wa kuletewa umeme vijijini kama inavyoonyesha mpango wa muda mfupi, kati na muda mrefu wa kuzalisha umeme ambao tuliupitisha ndani ya Bunge hili. (*Makofi*)

La pili, ni kuhusu hii REA, kwanza tunawapongeza kwani wanafanya kazi vizuri sana, lakini ni mfano pia kwamba kumbe kukiwa na agency inaweza ikafanya kazi vizuri sana kuliko ilivyo kwenye maeneo mengine. Sasa REA wanahitaji kuwezeshwa waweze kuwa na fedha zinazotosha kwa ajili ya kusambaza umeme vijijini. Baada ya kuwa na mkakati unaoeleweka na ratiba inayoeleweka ya kupeleka umeme vijijini kulingana na watakavyokuwa wamejipangia.

20 APRILI, 2012

Sasa hizi fedha nakumbuka tulikubaliana kwenye Bunge lililopita kwamba moja ya chanzo cha kuchangia fedha hizi ni kupitia simu za mikononi kwamba kila anayetumia simu basi atachangia shilingi 40 kwa kila anapoongea. Sasa agizo hili limetekelezwa mpaka wapi kwa sababu hiki ni chanzo kizuri ambacho kingeweza kuwapa wenzetu wa *REA* chanzo cha kutosha na hivyo kuweza kutekeleza miradi mingi ambayo ingeweza kufikia wilaya nyingi, kata nyingi na vijiji vingi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, niombe hili pengine maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini afafanue hili kama kwake limekwama au ni kwenye Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia basi tujue ni namna gani linaweza likaeendelea. (*Makofi*)

La tatu kwenye sehemu hii ya umeme ni kuhusu kupunguza gharama za vifaa vya umeme, tunafahamu kwamba yapo maeneo ambayo yamepitiwa na nguzo za umeme kwa mfano Makete, umeme unatoka Mbeya kwenda Makete Mjini na umepita kwenye vijiji na baadhi ya kata. Lakini vile vijiji havina umeme na kila tunapopeleka maombi tunaambiwa kwamba fedha za kununulia *transforma* hazitoshi kwa maana kwamba *transforma* bei juu sana. Lakini tunafahamu kwamba vipo viwanda ndani ya nchi vinavyozalisha au vinavyotengeneza *transforma* na viwanda vinavyotengeneza nyaya kama *East African Cables*.

Sasa ni vizuri Serikali ikaona namna ya kuviwezesha hivi viwanda kama *TANALEC* au kuweka ruzuku ili bei za *transforma* zishuke na hivyo ziweze kuharakisha zoezi la kusambaza umeme vijijini na hasa kwenye maeneo ambayo yalipitiwa na nguzo ambapo wananchi wamekuwa walenzi na mimi nina mfano kwa Makete, juzi juzi amekuja Makamu wa Rais wananchi wametanda barabarani wakimuomba, wao wamechoka kulinda zile nguzo wangehitaji wapate umeme. Sasa utatuzi mmojawapo ni Serikali kuwekeza kwenye vifaa ili bei yake ishuke na viweze kuwafikia walio wengi.

Mheshimiwa Spika, lingine bado kwenye umeme vijijini kwamba tumekuwa tukitegemea umeme wa gridi lakini vipo vyanzo vingine ambavyo vinaweza vikasaidia sana hasa vyanzo vya maji. Ukiangalia jiografia kama ya Wilaya ya Makete kijiji ambacho kiko mbali kweli kutoka kwenye *line* ya umeme wa gridi kama kilomita 70 hivi. Sasa ili upeleke umeme wa gridi kule utakuwa bei ya juu sana, kwa hiyo, tunashauri kwamba kwa kuwa yale maeneo ya mito yenye maporomoko makubwa na madogo ni vizuri Serikali ikajipanga kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko madogo yaliyopo kwenye vile vijiji ambavyo itakuwa bei ndogo kuliko kupeleka umeme wa gridi.

Mheshimiwa Spika, kwenye taarifa ya miundombinu, hapa tumekuwa tukishauri na niendeleo kushauri kwamba ili tuboresha uchumi wetu, ni muhimu sana barabara za vijijini zikaboreshwa na njia pekee ya kuboresha barabara hizi hebu tuige mfano wa utendaji bora wa REA ambayo ni *agency*, mfano wa utendaji bora wa TANROADS ambayo ni *agency*. Kwa hiyo, ipo haja ya Serikali kuona umuhimu wa kuanzisha *Rural Roads Agency*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tumeiongelea sana tena sana, hii itafungua hizi barabara na mazao yatafika kwenye barabara kubwa zinazotengenezwa na TANROADS na hivyo kufika makao makuu ambako kuna masoko ya yale mazao. Kwa hiyo, hili ni pendekezo tu kwamba wenzetu walione hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kuhusu taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi, kule kuna matatizo kwenye suala la uchumi, ni kwamba tatizo letu kubwa ni kwamba tunakubaliana tunapanga bajeti, tunapitisha humu ndani, lakini hakuna anayesimamia ile bajeti utekelezaji wake ukoje. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hakuna anayesimamia nidhamu ya matumizi ya zile fedha ambazo tumekubaliana, hakuna anayesimamia uchumi. Ndiyo maana pale Kilombero sukari inazalishwa kwa shilingi 1,300/= kwa kilo, lakini inamfikia mtumiaji mpaka kwa shilingi 2,500/= kwa kilo, hapa katikati kuna watu wengi wamejiingiza, ambapo pengine Serikali ingewaangalia vizuri bei ingewafikia wanunuzi kwa bei ambayo ni nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashauri kwamba leo ni mwaka 2012 tuache tabia za mwaka 1960, 1970, 1980, 1990; hebu tubadilike tuwe na nidhamu na tuweze kusimamia uchumi vizuri badala ya kuingiza mambo mengine ambayo hayakuweza kupangwa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, iko miradi ya umeme tuliyokuwa tumeiweka ambayo ni miradi ya kati kama Luhuji na Rumakaria. Lakini leo kwa sababu limejitokeza suala la gesi na makaa ya mawe, ile miradi ni kama hatuiongelei kabisa. Lakini naamini kwamba kuendeleza ile miradi ni pamoja na kulinda vyanzo vya maji. Kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini aelezee utekelezaji wa ile miradi. Wananchi wanadhani pengine imeachwa baada ya kuongelewa gesi na makaa ya mawe. Hebu atueleze ipo au haipo? Tujue kama ipo iko kwenye ratiba ile ile au vipi?

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, namuunga mkono Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Fedha na Uchumi - Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda kwamba, tunahitaji *Budget Committee* ambayo itakaa na Serikali mapema zaidi kuangalia bajeti kabla, tunapoletewa kwenye Kamati hizi ambapo muda unakuwa mdogo sana, hautoshi kuweka *inputs* na mwono wa nchi nzima wa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hizi taarifa na ninashukuru sana. (*Makofi*)

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Spika, nami nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi nichangie angalau Kamati hizi tatu; Nishati na Madini, Miundombinu, na Kamati ya Mambo ya Nje.

Kwa kweli suala la umeme ukitoka Dar es Salaam unaelekea Kaskazini ukifika njia ya kwenda Moshi, hata nyumba za mbavu za mbwa kuna umeme kule, inakwenda moja kwa moja mpaka Moshi, mpaka Turwa wapi huko mpaka kwenye mbuga za Wanyama, unakuta na wanyama nao wana umeme kule. Lakini ukitoka hapa unaelekea Songea, unaelekea Kusini sisi tunaongoza katika ujenzi wa nyumba bora katika nchi hii. Wananchi wote wa Ruvuma wana nyumba za matofali ya kuchoma na wengi wameweka mabati, nyuma kubwa zenye madirisha makubwa, hewa nzuri, lakini tatizo lao kubwa ni umeme.

Ukitoka Njombe unaelekea Songea, ukiuacha Njombe hupambani na umeme tena mpaka unapita! Hata ukipita kwa Mheshimiwa mama Makinda ambaye ndiye Spika wetu humu ndani hakuna umeme. Ni giza tupu! Giza tupu mpaka unafika kuona umeme, ni Songea kilomita 240. ukitoka hapo sasa unaelekea Mbinga kilomita 100 hupati umeme tena mpaka unafika Mbinga ndiyo unaona umeme. Sasa utoke Mbinga uende Mbamba Bay, Wilaya mpya ya Nyasa hakuna umeme kabisa. Wilaya nzima hii haina umeme hata kijiji kimoja, wala mji mmoja wa Makao Makuu ya Wilaya, hamna umeme.

Mheshimiwa Spika, lakini mara nyingi naongea na Waziri wa Nishati na Madini na Naibu wake, nawaambia jamani sisi ni matajiri, tunalima Kahawa, tunavua Samaki, tuna nyumba nzuri na bahati nzuri tuna jenereta la umeme katika *Council* ya Mbinga ipeleke ikawashe umeme Mbamba Bay, tupelekee tu waya hizi mkaziweke kule *network* hii ya umeme mkaifanye kule ili angalau mji mmoja katika vile vijiji vya kule na miji ya kule Nyasa vipate umeme. Hicho kitu nimeongea zaidi ya miaka mitano iliyopita mpaka leo jenereta lile linaanza kuoza. Kama mnaona hatufai, basi njooni tuwauzie lile jenereta. Kaskazini kuna maeneo

20 APRILI, 2012

machache sana wanaweza kupelekewa wakaongezewa kwa sababu tunaona halina faida yoyote sasa!

Mimi nakwambia kabisa, Mheshimiwa Ngeleja ni rafiki yangu, wewe Kigoma Malima, ni rafiki yangu, tunafanya mambo yetu pamoja, lakini mnanichekea jino pembe. Muache kunichekea bwana! Tutachekeana, lakini mwende *Mbamba Bay* mkaweke jenereta la umeme. Tuna hali mbaya sana! Bahati mbaya ziwa lile ukisimama kwenye milima ya *Livingstone* ya huku, maana Ziwa Nyasa liko katika *Riff Valley*, katikati kuna ziwa, kuna milima ya Livingstone upande wa Tanzania na *Livingstone* upande wa Malawi.

Ukisimama pale kwenye milima ya *Livingstone* unaona umeme ziwa lile la Malawi tangu chini mpaka mwisho. Umeme mtupu! Lakini ukiwa Malawi kule ukaangalia huku ni giza totoro, yaani utafikiri wale wako Mbinguni, sisi tuko tohorani au motoni, sijui. Tuna hali mbaya kweli! Nimesema mara nyingi labda mnafikiri sisi akina Komba, Tembo, akina Nguruwe, akina Miti, sio watu. Sisi ni watu kama ninyi, tunahitaji kumulikiwa umeme kama ninyi! Tuna jenereta letu, njooni mchukue jenereta, tulateeni waya tufanye kazi angalau na sisi tuanze kuona kwamba haya ni matunda ya uhuru. Baada ya miaka 50 ya uhuru, hatuna umeme! Naomba mfanye kazi hiyo. Mkifanya hivyo mtaendelea kuwa marafiki zangu. Msipofanya hivyo msinichekee tena! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuna bahati nyingine nzuri. Mungu hamtupi kiumbe wake, tuna makaa ya mawe. Mbinga hiyo hiyo makaa ya mawe; kule Ngaka wako Wazungu wamewekeza pale, nao wamesema tunaomba *TANESCO* mturuhusu au Serikali mturuhusu tujenge *power station*, tunaweza kuzalisha umeme wa *MW 400* tukapeleka mpaka Songea wenyewe tukawauzia umeme. Sharti wanalotupa wanasema mkitaka mtuuzie umeme mpaka muwe na mashine mpya. Wewe unataka mashine mpya, za kwako? Wewe unataka umeme uingie kwenye *grid* ya Taifa. Ametumia jenereta la zamani, jipya, wewe linakuhusu nini? Unawaambia kwamba mpaka walete jenereta jipya ndipo mtakubali wajenge hiyo *power station*. Hapo ni kutuonea sisi! Mimi nafikiri kama wangewekeza kule Kilimanjaro, Arusha, Mwanza, wapi msingetoa masharti haya. Lakini kwa sababu kule tunaishi wenye majina ya akina ngedere, akina Komba, wamezoea kukaa kwenye giza ndiyo maana hamtaki kutusaidia. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye miundombinu, sisi tuna Bandari, Kuna *Mtwara Corridor*. Ni kweli Serikali inajenga lami kutoka Masasi – Tunduru kwa Vita Kawawa pale Namtumbo – Songea – Mbinga na baadaye Mbinga – *Mbamba Bay*, lakini hii barabara lengo lake ni

20 APRILI, 2012

kwamba iweze ku-*service* Mtwara *Corridor*, isaidie kutoa bidhaa kule iende mpaka *Mbamba Bay*, kisha ivushe iende Malawi, Zimbabwe iende Zambia, *South Africa*, Botswana, Congo na kuendelea. Lakini ukienda kuona Bandari ya *Mbamba Bay* ni kichekesho kabisa. Yaani hata mimi naweza nikatengeneza Bandari.

Kama ndiyo ile Bandari hata mimi Komba mshahara huu wa Ubunge naweza nikatengeneza Bandari kama ile. Ni mbaya, haina uwezo wowote, haivutii! Sasa tafadhali, tengenezeni bandari ile, maana yake mkitengeneza barabara bila kutengeneza Bandari ile mnatwanga maji kwenye kinu. Mtaleta mizigo mpaka *Mbamba Bay* haiwezi kwenda kule mnakotaka iende. Kwa hiyo, uchumi utakuwa bado unadorora.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ni Wizara ya Mambo ya Nje. Tangu nimeingia katika Bunge hili, ninazungumza kila wakati kuhusu mpaka kati ya Tanzania na Malawi. Tangu mwaka 2005 ninazungumza jambo hilo. Wako wawekezaji wengine na wengine kadhaa nimewapeleka kwa Mheshimiwa Membe.

Mheshimiwa Membe na mimi ni majirani kule kwetu, na ndiye Waziri wa Mambo ya nchi za Nje. Nimewapeleka mpaka kwake, bwana unaona Mzungu huyu? Anataka kufungua hoteli. Mheshimiwa Membe anasema afungue hoteli. Lakini Wazungu wanajua wanapokuja wanapata elimu kuanzia alikotoka, akienda upande wa pili anaambiwa pale unapotaka kujenga Bandari, lile eneo ni la Malawi. Maana Malawi wanajua mpaka wao ni kando kando ya Ziwa Nyasa na kilomita 10 kutoka kando kando ya Ziwa Nyasa kuingia ndani. Kwa hiyo, wakiwekeza, maana yake siyo ardhi ya Tanzania, ni ardhi ya Malawi. Wengine sijawapeleka, wanakuja wanazungumza hilo hilo, kwamba siwezi kuwekeza kwa sababu hamjatatua *protocol* hii kati ya Malawi na Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sasa imekuwa mbaya zaidi. Sasa hivi wanakuja Wamalawi kusudi tu, wamefanya utafiti wamegundua kwamba katika Ziwa lile *deep sea* iko huku upande wetu, kule kwao ni kwepesi. Kwa hiyo, kuna uwezekano kabisa wa kupata mafuta. Sasa wanakuja na ndege, inaitwa ndege boti, inatua kwenye maji wanapiga picha, baadaye inaondoka tena pale kwenye maji inaruka tena inakuja ardhini kwenye mchanga, wanapiga picha katika kijiji hivi, wanaendelea kila siku. Tumeshatoa ripoti kwa Serikali. Sasa kama wanafika mpaka huku na hawaogopi wanajua kwamba ile ni ardhi yao. Sasa sisi Watanzania tunafikiri kweli ule mpaka uko *secured* kweli?

20 APRILI, 2012

Kwa hiyo, nina wasiwasi sana, mpaka wetu wa Tanzania na Malawi hauko *secured*. Naomba sana Waziri atakaposimama au yeyote kuja kueleza habari ya jambo hili la mpaka wa Tanzania na Malawi atueleze hii harassment tunayopata kila siku kutoka Malawi itakwisha lini, na *protocol* hii itakwisha lini?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja hizi za Kamati. (*Makofi*)

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Kamati ya Nishati na Madini.

Nianze kwanza kwa kuipongeza Kamati, imefanya kazi nzuri na kilichokuwa kizuri huna sababu ya kumwuliza jirani, maana kinaonekana ni kizuri. Baada ya kuipongeza Kamati, naomba nijielekeze iliko *REA*.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi sana nimekuwa nikisikia Waheshimiwa Wabunge wakielezea vijiji vyao vipatiwe umeme. Napata taabu kweli kweli! Wengine wanalalamikia vijiji, mimi na mtani wangu Komba Wilaya nzima yenye Kata 17 hakuna umeme hata sehemu moja, na bado tunasema raslimali za nchi hii zinagawanywa kwa usawa. Huo usawa uko wapi? (*Makofi*)

Bahati nzuri sana Mheshimiwa Naibu Waziri amefika kwangu. Yeye mwenyewe kwa macho kajionea jinsi ambavyo tuna vigezo vyote, tunakidhi kupatiwa umeme, lakini hakuna. Natarajia pale ambapo itapatikana nafasi ya yeye kuchangia hoja hii atatueleza sisi wananchi wa Kalambo tutapa lini umeme, maana vigezo vyote tunakidhi. Kama kuna sababu ambayo inasababisha tusipate umeme, tuelezwe ili tukatekeleze hilo.

Ukienda Kata ya Kasanga ambako Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu anajua kwamba kuna upanuzi wa Bandari kule, tumefanikiwa kujenga soko la Samaki la Kimataifa, lakini soko hilo bila umeme tunafanyaje? Tunakwenda kufyeka miti tuje tukausha Samaki? Tunasindika vipi hao Samaki? Halafu la kushangaza zaidi ni pale ambapo itafika zamu yetu ya kuunganishiwa umeme, tutaambiwa gharama ya kuunganisha imepanda. Sisi kosa letu nini mpaka tuje tulipie gharama kubwa? Mimi nadhani kwa *logic* ya kawaida, wale ambao waliunganishiwa miaka ya 1980 na sisi ambao hatukupata nafasi hiyo tuunganishiwe kwa bei iliyokuwa inatumika miaka ya 1980. Kwa sababu sisi tulikuwa tuko tayari tupewe umeme, lakini nyie hamtuletei. Inakuja

wakati wa kuunganisha, mnasema gharama imepanda. Imepanda, kosa letu nini? (*Makofi*)

Maana kama kuna kile ambacho kimesababisha sisi katika kuongeza gharama ya kupanda, mtuambie kwamba mmepandisha gharama kwa sababu moja, mbili, tatu. Lakini sisi tunasema tuko tayari, mtuletee umeme, mnakuja wakati wa kutuunganishia mnatuambia bei imepanda. Hatutakubali.

Mheshimiwa Spika, wakati tunakubaliana kwenye Bunge lako la mwaka jana hapa kwamba bei ya mafuta ipande kwa maana ya kuhakikisha kwamba uchakachuaji unakomeshwa, ndiyo *motive* ya Wabunge wengi hapa na kwamba tukishakomesha hili suala la kuchakachua na pesa ile itakayopatikana iende kwa Watanzania wote ndiyo maana nadhani tulikubaliana. Lakini imekuja hadithi kwamba pamoja na kupandisha bei ya mafuta ya taa ili ilingane sawa na bei ya petroli, *almost* tofauti ni ndogo sana, uchakachuaji unaendelea. Mnakuja kutueleza nini katika Bunge hili? Mwananchi wa kipato cha chini ambaye imebidi alipie bei kubwa ya mafuta leo hii uchakachuaji unaendelea. (*Makofi*)

Je, mnataka kutuaminisha kwamba ilikuwa ni namna tu ya kuweza kuwaibia wananchi au ni namna gani mliyokuwa mnalenga? Naomba majibu yapatikane ili wananchi wetu waelewe kwamba kweli bei ilipandishwa kwa nia njema.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kuhusiana na miundombinu. Miundombinu yetu imekuwa ya taabu kweli kweli, lakini ndiyo hiyo hiyo hadithi ya Mikoa ya pembezoni. Hadithi hii tunaomba iishe kwa sababu sisi ni makosa gani ambayo tumefanya kwa kuwa pembezoni? Leo hii unaweza usishangae kwamba, mwaka jana ndiyo Mheshimiwa Waziri wa Maliasili amebaini kwamba maporomoko ya Kalambo ni ya pili kwa Afrika. Wabunge wengi hawalijui hilo. Tatizo ni nini? Wanakwambia tutafikafikaje huko? (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba sana miundombinu iboreshwe ili hata hii hadithi tunapolalamika kwamba Mheshimiwa Waziri tunahitaji mawasiliano usiwe na yale maneno kwamba, hakuna umeme, miundombinu haifikiki, maneno haya hatuyafurahi tena, yanatusononesha sana. Kwa sababu mngokuwa mnaweza ku-*point* kwamba sisi ni makosa yetu, *then* ingekuwa ni rahisi sisi ku-*confess*. Lakini sisi hakuna makosa tuliyofanya, ni wajibu wenu kuhakikisha kwamba mnatutendea haki na sisi tusije tukajisikia unyonge.

20 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, nadhani niseme machache ili yachukuliwe kwa uzito mkubwa nisije nikayaharibu. Naamini wakati wanahitimisha nitapata majibu ambayo wananchi wa Kalambo walionituma watayasikia.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naunga mkono hoja. Ahsante.
(Makofi)

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya pekee kabisa kwa saa hii. Lakini naomba nianze kwa kuzishukuru Kamati zote zilizotoa taarifa hizi. Taarifa ni nyingi, lakini mimi naomba nichangie zaidi eneo la Kamati ya Kilimo. Nataka nizungumzie hasa kwenye zao la Pareto.

Mheshimiwa Spika, mwaka juzi katika Bunge lako nilikuwa nimeuliza swali kuhusu kuwaruhusu wanunuzi wa Pareto kuwa wengi kule Mbeya na maeneo mengine ambako wanalima Pareto. Lakini Waziri wakati huo alikuwa Mheshimiwa Wasira, alinijibu kwamba Pareto ambayo inanunuliwa na watu holela wanapeleka Pareto hiyo huko Kenya na Rwanda.

Kwa hiyo, tunamruhusu mnunuzi wa Pareto awe na kiwanda. Lakini mwaka jana kule kwangu kukatokea vurugu kubwa sana kwa sababu huyu mnunuzi wa Pareto ambaye ana kiwanda pale Mafinga akawa ananunua Pareto kwa bei ya chini ya Sh. 1,800/= kwa kilo. Lakini baadaye wale wanunuzi wengine walikuwa wanaweza kununua Pareto ile kwa Sh. 2,000/= mpaka Sh. 2,200/=. Kwa hiyo, baadaye Wilaya wakakutana na kuwaruhusu wale wanunuzi wengine waweze kununua ile Pareto.

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa naiomba Serikali ,sijui kama watakuwa na mpango gani, lakini nilikuwa nafikiri kwamba mnunuzi huyu wa Pareto ambaye ana kiwanda pale Mafinga ingekuwa ni vizuri awaruhusu hao jamaa ambao wananunua Pareto wamwuzie. Wanunue Pareto, wamwuzie ile Pareto, kuliko yeye anunue Pareto na huku tena atengeneze hapo hapo. Hilo ndilo lilikuwa ombi langu kwa Serikali. Sijui kama Waziri yuko hapa, nafikiri atanisikia na bila shaka atanipa majibu. Kwa sababu hata hivyo, bado wanunuzi hao wengine wananunua hiyo Pareto kwa bei kubwa kuliko hata hii ya kiwanda. Nilikuwa naomba kuliweka hilo sawa.

Mheshimiwa Spika, lingine ilikuwa ni suala la maji vijijini. Kwa kweli miradi mingi ambayo inafadhiliwa na Benki ya Dunia imekuwa ni kero, imekuwa ni balaa kwa sababu badala ya kuwa baraka kwa watu imekuwa ni balaa kwa sababu miradi hii imeahidiwa kwa siku nyingi sana.

20 APRILI, 2012

Kuna miradi ambayo kabla sijawa Mbunge hapa, watu walihidiwa kwamba mtapata maji mwaka huu. Lakini mpaka leo hii, nasema wala hakuna dalili kwamba maji yatakuja. Sasa nafikiri labda Serikali ingetafuta njia nyingine ya kupata fedha za kufadhili miradi hii. Lakini tukitegemea fedha za kutoka Benki ya Dunia nawaambieni kwa kweli tunawababaisha wananchi na tunawaletea kero kubwa sana. (*Makofi*)

Nilikuwa naomba kitafutwe chanzo kingine cha kupata fedha hizi ili miradi hii ambayo imesimama, Wahandisi wamehangaika pale kusanifu ile miradi, lakini haitekelezwi, hakuna fedha. Bunge lililopita, niliuliza swali hili hili hapa na Waziri akaniambia, mwaka jana tulikuwa tumetenga Shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kueneza maji Mbeya Vijijini lakini hata senti tano hatukupata na mwaka huu, naambiwa tumetengewa Shilingi bilioni 1.5 na mpaka dakika hii nasema hakuna hata senti tano imefika. Sasa kweli tutafika hapo?

Ninaomba miradi hii yote ya maji, maji jamani ni muhimu sana na ndiyo maana wakati mwingine tunazungumzia kwamba elimu imeshuka na kuwa chini. Hapana! Hao walimu wanaoletwa vijijini wakishaona kwamba maji hakuna wanaondoka saa hiyo hiyo, huku mijini walizoea kunywa maji kule, waende wakachote maji mtoni, tena usafiri ni kilomita tano au sita; huyo mtu atakaa? Hawezi kukaa.

Kwa hiyo, naomba hii miradi ikiboreshwa, yaani barabara, maji na umeme vikiwepo, nawaambia kabisa, hata hiyo elimu mnayoisema itaboreshwa na watu wengi watafaulu. Lakini sasa hivi vijana wengi wanaofaulu ni wale ambao wako mijini ambao wana uwezo wa kujisomea, sasa vijijini utasoma na koroboi? Kwa hiyo, naomba miradi ya maji, umeme na barabara vikitengenezwa na Serikali ikiwa makini kuhakikisha kwamba vitu hivyo vinapelekwa vijijini kama alivyosema Mbunge fulani hapa, ni vizuri tuweke mawakala maalum kama ilivyo kwa REA.

Nawashukuru watu wa REA kwa sababu kwa kweli wanajitahidi pamoja na kuwa na fedha ndogo, lakini bado wanajitahidi kuhakikisha kwamba wanasambaza umeme. Kule kwangu nawashukuru, kwani sasa hivi wanapeleka umeme katika Tarafa ya Irembo na Tarafa nyingine. Kwa hiyo, nawashukuru kwamba wamefanya kazi hiyo nzuri sana lakini tuwaongezee nguvu pia.

Kwa hiyo, hata suala la maji, ni lazima litafutiwe fedha nyingine, siyo za *World Bank*. Hawa Wazungu wanatutania tu hapa, miaka mitano inakwenda hawatupatii hata senti tano. Kuna nini hapo? Kwa hiyo,

naomba tujitahidi kuhakikisha kwamba vyanzo vingine vya kukamilisha miradi hii ya maji Tanzania nzima inafanyika.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni suala la barabara kama nilivyosema. Barabara za Vijijini kwa kweli fedha zake zimekuwa ni ndogo mno na kama kuna fedha, basi zinatolewa kiasi kidogo ambacho hakikidhi hata kuweza kutengeneza barabara. Kama alivyosema msemaji mwingine, ni vizuri tungeweka Wakala Maalum ambaye atashughulikia barabara za vijijini. Lakini tukisema tutapeleka fedha Halmashauri, tutakuwa tunapoteza muda tu. Barabara ni kidogo sana zinazotengenezwa, na kama zinatengenezwa lakini kwa viwango ambavyo siyo vizuri kwa sababu ya ufinyu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, fikiria mpaka dakika hii hakuna hata senti tano ya maendeleo ambayo imefika katika Halmashauri na walikuwa wanategemea kwamba fedha hizo ndiyo zitasaidia kuboresha barabara za vijijini, lakini mpaka leo hii nasema hakuna hata senti tano iliyokwenda kule. Sasa tutafika kweli? Tutawaletea wananchi maendeleo?

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge kila tukipita, tunaahidi kwamba Serikali itawajengea barabara na kadhalika, wakati wa kampeni, lakini mwisho wake tunajikaanga wenyewe kwa sababu Serikali yetu wakati mwingine imeshindwa kutusaidia. Hakuna pesa! Nina imani kwamba vyanzo vya pesa bado vipo, utamaduni wa kulipa kodi kwa Mtanzania uko chini sana. Kwa hiyo, ni muhimu kabisa hata TRA wawe na vitengo ambavyo vinashughulikia kubuni na kutafuta vyanzo vingine vya mapato, lakini tukitegemea kwamba *system* iliyopo pale inatosha, nawaambia kwa kweli hatutafika mahali.

Wenzetu Ulaya wako makini, wana hakika ya kulipa kodi na kulipa ni haki yake, ni lazima alipe kodi kama anaruhusiwa kulipa. Lakini sisi hapa ulipaji kodi, bado ni tatizo. Unatakiwa kufanyika utafiti wa hali ya juu kabisa kuhakikisha kwamba njia nyingine za kupata kodi hiyo au mapato hayo zinatafutwa, siyo hivi tulivyo sasa hivi, milioni 40 na zaidi ya Watanzania, watu wengi na mambo mengi. Mbunge mmoja alieleza katika Bunge lililopita akasema kuna vyanzo vingi kama majumba ambayo watu wanajenga, kwa nini yasitafutiwe fedha ili ziletwe kusaidia maendeleo ya wananchi hapa? Mtu anakuwa na nyumba 10!

Mheshimiwa Spika, mimi nimekaa Uswisi, kule hata mtu kuwa na nyumba anatafakari mara mbili au tatu kwamba je, niwe na nyumba ngapi? Maana akiwa na nyumba nyingi, kodi ni nyingi atalipa. Kwa hiyo, wengi wao wanaona ni afadhali wapange kuliko kujenga nyumba. Lakini

20 APRILI, 2012

sisi hapa kuna watu wana majumba wanapata mamilioni ya pesa, lakini hakuna hata senti tano anayolipa kwa Serikali.

Ninaomba Serikali ijaribu kutafuta na kubuni mbinu, ni namna gani tutapata vyanzo hivi. Fedha zipo, siyo madini tu, kuna mambo mengi. Madini ni sawa yapo, lakini kuna vitu vingine vingi ambavyo nafikiri Serikali ingekuwa makini tungeweza kupata fedha nyingi sana na kuwasaidia wananchi wetu waliopo vijijini. Leo unawatuma Walimu, wanakwenda vijijini wote, wanarudi, unawapeleka 30 wanabaki 10, lakini 20 wote wameshatoroka kwa sababu wanaona mazingira ni magumu vijijini.

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Spika, nashukuru na ninaunga mkono taarifa zote ambazo zimetolewa. Ahsante sana.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nashukuru. Kama nilivyotangaza, kesho tutaendelea na wachangiaji, kama baadaye mkikubaliana na hoja hiyo.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mwongozo wa Spika!

SPIKA: Ndiyo, nilikuona Mheshimiwa Tundu Lissu.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kuhusu jambo ambalo limetokea mapema leo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa January Makamba aliomba mwongozo juu ya sahihi ambazo zinakusanywa kwa lengo la kuleta hoja ya kupiga kura ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu, na hoja hii bado haijalletwa kwenye Kiti chako. Kwa hiyo, matakwa ya kanuni ya 133(3)(a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge letu ilikuwa haijafikiwa kwa maana kwamba kanuni hiyo inahitaji hoja ya maandishi iletwe mbele ya Spika siyo chini ya siku 14 kabla ya siku inayotarajiwa kujadiliwa. Kama nimeelewa sawa sawa, Mheshimiwa Zitto alisema kwamba tutaleta hii hoja siku ya Jumatatu siyo kwa lengo la kujadiliwa, katika Mkutano huu wa Bunge ila kwa lengo la kutoa taarifa ili ipangiwe kwa siku nyingine za baadaye.

Mheshimiwa Spika, sasa umeshasema kwamba kinachoendelea kufanyika cha kutafuta hizi sahihi ni batili na kadhalika, mwongozo ninaoomba ni kwamba: Je, ni sahihi kutoa maamuzi ya uhalali wa kitu

20 APRILI, 2012

ambacho hakijafika katika Meza yako kwa ajili ya kuangaliwa kama kiko sahihi ama la? Nafikiri *it was a bit pre-mature* kutoa hiyo *determination* kwamba ukusanyaji wa hizi saini ni batili.

Mheshimiwa Spika, kingine cha mwisho ni kidogo sana. Kuna mwelekeo kama wa *collusion* hivi ambao nafikiri siyo mzuri sana kwa kweli kwa heshima na hadhi ya Bunge hili Tukufu na kwa Kiti chako. Hoja inaletwa, tayari majibu yameshaandaliwa, *it looks bad! It just looks bad.*

Mheshimiwa Spika, naomba utupe mwongozo kama ilikuwa ni sahihi kutoa maamuzi juu ya uhalali wa hiki kinachofanyika kabla hakijafika kwenye Meza yako.

Mheshimiwa Spika, nashukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante.

Mheshimiwa Lissu, kama nilivyotoa mwongozo kwa mwenzako na wewe nakutolea sasa hivi. Kwa sababu nilichosema alivyo-*present* Mheshimiwa Zitto nimesona na *Hansard* yake, na bahati nzuri Naibu Spika jana alieleza kwamba siwezi kuwahoji kwa suala hili na lile lingine la Kamati Teule kwa sababu hayo hayakuwa sehemu ya taarifa zilizowekwa, zina taratibu zake za kuleta. Alisema *very clear!* Kwa hiyo, ndiyo maana nikasona *exactly*, alichokisema kwamba jamani tukutane kesho asubuhi tutakuwa mlangoni, tutakusanya *signature* na halafu Jumatatu tuwasilishe. Ndivyo alivyosema.

Kwa hiyo, watu wanauliza, huu ni utaratibu? Ndiyo maana nikasema kwamba ngoja kwanza nijipange vizuri, nikachukua kanuni, nikachukua Katiba na kukusomea, siyo kwamba kuna kitu chochote kile. Kwa hiyo, wewe pia umedhalilisha Kiti changu kwamba ninajibu kitu *collusion*. *What collusion?* Ni kweli kwamba nimesoma *Hansard*, *according to* huyu mtu kwamba sawa anaweza kukusanya, lakini kwamba *lita-fit* Bunge hili, haitawezekana, kwa sababu siku 14 hazitapatikana. Ndivyo nilivyosema.

Mheshimiwa Mnyika!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa hata baada ya kutoa mwongozo wako wa awali, Waheshimiwa Wabunge wa vyama mbalimbali ikiwemo CCM wameendelea kuja kusaini na mpaka sasa kuna idadi ya watu 66 na zimebaki nafasi chache kuweza kutimia: Naomba mwongozo wako kwa mujibu wa kanuni ya 133 (1) inayosema; "Mbunge yeyote anaweza kutoa taarifa kwa maandishi

20 APRILI, 2012

kwa Spika kutaka kuleta hoja ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu kwa mujibu wa Ibara ya 53(a) ya Katiba.”

Mheshimiwa Spika, noamba mwongozo wako ikiwa Waheshimiwa Wabunge wakiendelea kusaini kama hivi, idadi ikatimia: Je, Jumatatu uko tayari kupokea taarifa ya hoja ili hatua nyingine zifuatwe?

SPIKA: Jamani msipende kupoteza wakati. Nilipokuwa natoa mwongozo nilisema hivi, kwa Bunge hili haiwezekani kwa sababu tunategemea kufunga Bunge hili siku ya Jumatatu. Kwa hiyo, siku 14 hazipatikani. Maana yake ni kwamba, kama mtaandika hizo hoja zenu kwa ajili ya Bunge lijalo, hiyo barua itaniambia kwamba tunataka kufanya hivyo Bunge lijalo. *This is what I am saying.* Sidhani kama kuna *complication* hapa, *it is very crystal clear* na ninaomba msome kanuni zetu vizuri msitafsiri watu visivyo. Hizi ni tafsiri za kanuni zilizoandikwa na *Hansard* zenu, mnapozungumza hapa, tunawa-*quote* kila kitu. Bahati nzuri siku hizi *Hansard* zetu hakuna namna ya kubadilisha maneno. Maana yake zamani ilikuwa *very old fashion*, kwa hiyo, inabidi upewe tena usahihishe wewe mwenyewe, kwa hiyo, unavyosahihisha, ukikuta ulisema vibaya, unabadilisha, lakini siku hizi hapana. Sasa hivi nikikwambia *Hansard* aliyozungumza mtu nitapata sasa hivi.

Kwa hiyo, ninaomba mwelewe hivyo kwamba wale wanaoweka *signature*, mimi sikatai kuweka *signature*, kwanza *I don't know* kwa sababu sijaandikiwa. Kama wataniandikia siyo kwa Bunge hili, kwa sababu siku 14 hazitafika, maana yake ni keshokutwa. Kama watasema kwamba tunataka hoja hiyo tutaleta Bunge lijalo, tutapokea na kuweka lakini tutakapofika Bunge lijalo tutaangalia wanasema nini. Kwa hiyo, huo ndiyo utaratibu.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo. Kwanza kabisa, namwomba Mheshimiwa Waziri anayekaimu nafasi ya kuendesha Bunge aweze kutoa hoja ya kutengua kifungu kinachofuata.

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje kwa niaba ya Waziri!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge - Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, naomba kutoa hoja ya kutengua kanuni ya Bunge chini ya kanuni namba 150(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la mwaka 2007.

Kwa kuwa, chini ya masharti ya kanuni ya 28(15), Bunge hukutana siku zote za juma isipokuwa siku za Jumamosi, Jumapili na siku za

20 APRILI, 2012

mapumziko, na kwa kuwa mjadala unaoendelea sasa wa hoja za Kamati za Bunge zimevutia Wabunge wengi kuomba nafasi ya kuchangia na hivyo kuwepo kwa ulazima wa kuongeza muda wa mjadala huu, hivyo basi ili kuliwezesha Bunge kukamilisha mjadala wa hoja za Kamati na kuweza kuendelea na shughuli nyingine zilizopangwa kwenye ratiba ya Mkutano huu, Bunge linaazimia kwamba:

Kanuni ya 28(15) itenguliwe na kwamba Bunge likutane kesho Jumamosi tarehe 21 Aprili, 2012 kwa ajili ya kuendelea na mjadala wa hoja za Kamati ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI):
Naafiki!

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Bunge liliafiki Hoja ya Kutengua Kanuni iliyotajwa)

SPIKA: Ahsante. Hoja hiyo imeungwa mkono. Nashukuru wote mmeafiki.

Kwa hiyo, kama nilivyosema kesho tukianza saa tatu, nina wazungumzaji waliobaki hapa kama 60, na wakati huo huo itabidi nitoe nafasi kwa Wenyeviti wangu wajibu, halafu itabidi nitoe nafasi kwa Wizara ambazo zinatakiwa kujibu. Lakini tutafanya kazi nzuri kwa sababu tutaanza bila maswali. Kwa hiyo, itawezekana kabisa.

Kwa wale walioomba isipokuwa waliochangia mara moja, naomba wala wasihangaiki. Lakini wale ambao hawakuchangia, wajiandae tu.

Nina matangazo. Kwanza kabisa, nina tangazo la ofisini kwangu, nawatangazia Wabunge wote kuwa kuna nyaraka muhimu zimewekwa kwenye masanduku yenu ya nyaraka, yaani *pigeon holes*, mnaombwa kuzichukua. Nyaraka hizo ni kama zifuatavyo: -

Kuna masuala ya msingi juu ya uendeshaji wa Serikali za Mitaa kwa sababu ninyi nyote ni Madiwani; halafu kuna *The Tanzania Long Term Perspective Plan LTPP 2011/2012 mpaka 2025/2026*, hii inaitwa *the Road Map to a Middle Income Country*.

20 APRILI, 2012

Pia kuna nyaraka ya tatu, ni taarifa tano za CAG kwa lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, ni *document* muhimu, msiziache zikabakia pale.

Tangazo lingine ni Waheshimiwa Wabunge wote wanaotoka Majimbo yanayolima Pamba wataendelea na kikao chao Jumapili saa 8.30 mchana katika Ukumbi wa Msekwa B. Katika kikao hicho wanasema wamewaalika pia Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Bodi ya Pamba, Chama cha Wakulima wa Pamba (TACOGA) na Chama cha Wanunuzi wa Pamba (TCA). Wajumbe wote mnaombwa kufika kwa wakati ili kupata muda wa kutosha wa kujadili na kufanya maamuzi muhimu kwa mustakabali wa zao la Pamba ambao msimu wa ununuzi unakaribia. Kwa hiyo, hawa walikuwa na kikao chao, leo wanasema wataendelea tena siku ya Jumapili saa 8.30 mchana.

Katibu wa *caucus* ya Chama cha Mapinduzi anaomba niwatangazie Wabunge wote wa CCM kuwa watakuwa na kikao leo jioni baada ya kikao hiki kuahirishwa. Kwa hiyo, wakitoka hapa waende katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge tukiacha hayo, sina matangazo mengine, naomba niwatakie jioni njema na mapumziko mema mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.38 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumamosi,
Tarehe 21 Aprili, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*